NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 17 Mei, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MHE. OMARI A. KIGODA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kigoda. Katibu

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu nimwite sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kujibu maswali hayo. Tutaanza na Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul, Mbunge wa CHADEMA.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi ni Mbunge wa Babati Mjini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Sera ya Serikali ya mwaka 1996 ya kushusha madaraka katika Halmashauri zetu *(Decentralization by Devolution)*. Lengo la sera hii ni kuzipa Halmashauri zetu majukumu mbalimbali. Jukumu mojawapo ni kubuni vyanzo vya mapato, kukusanya lakini kwa kutumia fedha hizo kwa maslahi ya wananchi. Pale ambapo majukumu haya ya Halmashauri zetu au vyanzo hivi vinakuwa vinapokonywa kutokufuata taratibu na sheria na jambo hili linasababisha Halmashauri zetu ku-*perform* na pale zinaposhindwa ku-*perform* wewe ulitoa kauli kwamba Halmashauri ambayo haitafikisha asilimia 80 ya makusanyo Halmashauri hiyo itafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limetokea katika Halmashauri ya Mji wa Babati ambako chanzo kikubwa cha stendi ya mabasi ilipokonywa ikidaiwa ni kauli ya Mheshimiwa Rais na bahati nzuri Mheshimiwa Rais ameliweka vizuri kwamba yeye hahusiki bali ni viongozi wa Manyara na tulimalize wenyewe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli ya Serikali na nini kauli yako juu ya tatizo hili ambalo Mheshimiwa Rais ameshaliweka wazi kwamba yeye hahusiki kuchukua Stendi ya Mji wa Babati kuikabidhi CCM?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul najua kwamba unafahamu ni maswali gani Mheshimiwa Waziri Mkuu anaulizwa. Anaulizwa maswali gani, yako kwenye

Kanuni ya kisera, ukimuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kuhusu Babati utajibiwa na Waziri anayehusika. Mheshimiwa Waziri Mkuu anaulizwa maswali ya kisera. Nitakupa nafasi tena baadaye tafuta swali la kisera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amina Saleh Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Azimio la Wakuu wa Mikoa la Novemba, 2014 lililofanyika hapa Mjini Dodoma ilisisitiza kwa Wakuu hawa wa Mikoa kupitia Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo kwa ajili ya vijana ili vijana hawa waweze kujikita katika shughuli mbalimbali kwa mfano kwenye kilimo, ujasiriamali, uvuvi, madini pamoja na shughuli nyingine ambazo zingeweza kuwaletea kipato.

Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kufahamu juu ya kauli hii, Serikali imefikia wapi tukizingatia kwamba vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa na itihada zinazofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Mollel natambua kuwa leo ni siku ya kwanza kwa Waislam wote duniani na hapa nchini kufunga Ramadhani, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla tunawatakia mfungo mwema Waislamu wote duniani na hapa kwetu Tanzania na kuwatakia kheri kwenye mfungo huu wa Ramadhani na tunawaombea sana Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu kuumaliza mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo, sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mollel, Mbunge wa Mkoa wa Arusha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa ujumla wake inayo mipango ya kuendeleza makundi mbalimbali ikiwemo na hao vijana. Kwa kuwa, Serikali imetoa mwelekeo huo Wakuu wa Mikoa kama ambavyo mmesema nao pia waliweka maazimio kila mmoja kwenye Mkoa wake kuandaa fursa zitakazowawezesha vijana kufanya shughuli za kujipatia kipato, kuongeza uchumi wao kwenye maeneo mbalimbali ya kilimo, uvuvi kama ulivyosema madini na maeneo mengine yote ambayo yanaweza kumletea tija kijana huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linaendelea kila Mkoa wameendelea kutenga ardhi na maeneo yote yanayogusa kutokana na eneo ambalo linaweza kuboresha kiuchumi ili kuwapa fursa kila mmoja kushiriki kikamilifu katika kujiletea kipato na kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaishia tu kwenye maazimio hayo, hata ofisi yangu pia Ofisi ya Waziri Mkuu nayo pia tuna Kitengo cha Ukuzaji Uchumi, uwekezaji ambacho pia na chenyewe kimeongeza nguvu kwenye Azimio hilo la Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba vijana wote wanaongezewa ujuzi katika sekta mbalimbali ili ziwasaidie katika kusimamia shughuli zao. Kwa hiyo, mkakati wote wa Serikali pamoja na maazimio hayo ya Wakuu wa Mikoa mpango thabiti wa ukuzaji uchumi ulioko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu inalenga kuwawezesha vijana kujipatia kipato na kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nitoe wito kwamba mipango hii ya Serikali ni fursa nzuri kwa vijana wote nchini kushiriki kikamilifu kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kila mmoja atumie fursa aliyonayo mahali alipo na miongozo inayotolewa na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa hata ile ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuitumia vizuri ili kuweza kuongeza pato hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia jambo hili na kuongeza mkakati wa kupanua wigo siyo tu kwa vijana lakini pia hata kwa watu wa umri wa kati na wazee kila mmoja aweze kushiriki kikamilifu kujiletea maendeleo popote alipo na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Swali langu linahusu swali la kisera, kwamba ni Sera ya Serikali....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul kama unarudi tena kwenye hilo swali naomba ukae. Mheshimiwa Waitara Mwita Mwikabe.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ninaitwa Mwita Mwikwabe Waitara siyo Mwikabe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba raia wa Tanzania wanakuwa salama katika mazingira mbalimbali na kwa sababu hiyo imeanzisha Mfuko wa Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo yeye mwenyewe ndiyo msimamizi mkuu. Tunatambua sasa mvua zinanyesha karibu kila mahali nchi nzima, miundombinu imekatika madaraja, barabara, sehemu kubwa ya nchi hii hakuna mawasiliano. Vilevile tunatambua kwamba baadhi ya Mikoa wameshafanya tathmini zaidi ya miezi miwili sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nipate kauli ya Serikali sasa, maeneo ambayo yamepata maafa makubwa kwa maana kukatika kwa mawasiliano ya barabara nchi nzima, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hatua gani Serikali imeshachukua mpaka sasa ili kuweza kurejesha mawasiliano watu waweze kwenda makazini kwao na shughuli mbalimbali za kijamii ziweze kuendelea ili uchumi usiendelee kushuka kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba nchi yetu imepata athari kubwa kutokana na kuwepo kwa mvua nyingi ambazo pia zimesababisha maeneo mengi barabara, nyumba na miundombinu mingine kuharibika. Ni kweli pia kwamba tunazo Kamati za Maafa kutoka ngazi ya Halmashauri lakini ngazi ya Mkoa pia hata ofisini kwangu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ngazi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kubwa ambalo tumelifanya mpaka sasa baada ya mvua kubwa ambazo zimeharibu miundombinu mingi ni kuhakikisha kwamba tunaratibu vizuri kwa kuanza kufanya tathmini na tathmini inafanywa kutoka ngazi ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue mfano kwenye Halmashauri yako ya Manispaa ya Ilala ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zimepata madhara makubwa tunajua na tumeona pia hata kwenye *television* miundombinu mingi, barabara zimeharibika na nyumba na watu wameshindwa kufika eneo jingine kwa sababu ya kuharibika miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi ya kwanza ni Halmashauri yenyewe kufanya tathmini na tathmini ile sasa wataona ni maeneo gani wao wenyewe kwa ngazi ya Wilaya wanaweza wakayaondoa wakayaratibu vizuri na kuyatekeleza ili kurudisha hali ya kawaida na wananchi waendelee kufanya kazi. Lile ambalo linawashinda linaenda kwa ngazi ya juu ambayo ni ngazi ya Mkoa na ngazi ya Mkoa nayo wanaratibu pia wakishindwa nao wanavileta sasa Ofisi

ya Waziri Mkuu kwa ajili ya uratibu wa Kitaifa kama uharibifu huo unakidhi viwango na vigezo vya ngazi ya Taifa kuja kushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata taarifa mbalimbali kwenye maeneo yote na kwenye Halmashauri yako tumepata taarifa pia kwamba miundombinu ya barabara iliyoharibika imeendelea kufanyiwa tathmini na *TARURA* kwa pamoja na *TANROAD* kwa *nature* ya Halmashauri yako wameanza kufanyia kazi na wametenga fedha kwa ajili ya kurudishia miundombinu ya barabara ili wahakikishe kwamba kila kitu kinarudi kama kawaida ili wananchi waweze kutembea kwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati za Maafa kwenye maeneo yenu yale yote yaliyoharibika na wiki iliyopita tuliulizwa swali la Kaliua kule, wanaendelea kuratibu na pale ambako inashindikana kwenye ngazi ya Wilaya wataenda Mkoa na Mkoa watakuja Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tutaendelea kuwapa taarifa kadri tathmini zinavyofanywa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata fursa hii kumuuliza Waziri Mkuu swali. Nafahamu kwamba hivi karibuni Serikali imefanya mabadiliko makubwa sana kwenye sera ya elimu na kama unavyofahamu mabadiliko hayo yametoa fursa kubwa kwa sekta binafsi kuwekeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kujua ni hatua gani ambazo zinachukuliwa na Serikali kwanza kudhibiti ubora wa elimu hapa nchini na pia nidhamu na malezi kwenye hizi shule binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ukweli kwamba kwenye sekta ya elimu nako tumetoa fursa kwa taasisi binafsi kuwekeza na kuendesha shule, vyuo na taasisi yoyote ambayo inatoa elimu hapa nchini. Taasisi hizi Serikali inaziratibu kwa ukaribu sana, kwanza tunaanza na miundombinu yake kuona kwamba miundombinu hiyo inakidhi mahitaji ya taasisi kusudiwa ili iweze kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, tukishajiridhisha miundombinu kuwa inatosha lazima tusajili na usajili unatokana na ukaguzi wa kina kama eneo hilo linafaa kwa namna yoyote ile kwa usalama, lakini pia mazingira ya kitaaluma kuwa yanaweza kutosha na yanaruhusu kutolea taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu; kama mwekezaji huyu amekubali kuwekeza kwenye sekta ya kielimu kama ni shule za msingi, sekondari au vyuo atalazimika kufuata mitaala ya kiserikali ili afundishe mtaala ambao unafundishwa pia na kwenye shule za Serikali. Wanafunzi wote ili mradi Watanzania wapate elimu inayofanana. Pia, tunao utaratibu wa ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo haya ili kubaini kama elimu inayotolewa ina kiwango sawa na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Idara ya Ukaguzi nayo itakuwa inalazimika kwenda kukagua shule binafsi zote nchini ili zitoe elimu inayofanana na shule nyingine kwa sababu mwishoni kutakuwa na mitihani, kutakuwa na kupima vijana wanaopata elimu ile na kipimo ni kimoja tu kitakachotokana na Baraza la Mitihani ili kuweza kuona kama wote wamefundishwa kwa mtaala mmoja na elimu iliyotolewa ina viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huo sasa tunaangalia pia hata na lile jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge umelieleza la malezi na nidhamu. Suala la malezi na nidhamu tumeliwekea msisitizo kwenye taasisi zetu kwa sababu ndiyo zinajenga vijana hawa kuwa viongozi wa baadaye, kuwa Watanzania wema hapo baadaye ili sasa nchi iweze kujengwa na maadili yanayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea kusimamia shule hizi kupitia *machinery* zetu au vyombo vyetu ili Serikali ijiridhishe kuwa elimu inayotolewa nchini kote inafanana na kila mmoja aweze kunufaika na elimu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania mmeshuhudia sasa elimu yetu ilivyokuwa na mabadiliko yote yanaenda pande zote mbili, Serikali na Sekta Binafsi na namna ambavyo elimu inapata mafanikio makubwa na Watanzania wengi tumeanza kuona namna ambavyo wamenufaika na elimu zote kwa kutoka pande zote mbili. Kwa hiyo, malengo yetu ni kuhakikisha kwamba elimu yetu nchini inaboreshwa na elimu yetu nchini inatolewa kwa vijana wetu wote Watanzania na Serikali imefungua mianya kwa upande wa Serikali elimu kutolewa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hawa watu binafsi wanao utaratibu ambao tumewawekea ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaotamani kupata elimu kwenye taasisi hizo wanapata elimu hiyo kamilifu lakini maadili yataendelewa kusimamiwa, nidhamu itaendelea kusimamiwa na walimu wanaofundisha ni walimu waliofundishwa na taasisi zetu za elimu nchini na wana viwango vinavyofanana pande zote mbili, Serikali pia Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutaendelea kusimamia elimu kote nchini upande wa Serikali na Sekta binafsi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la migogoro katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini kati ya ma-*DC* na ma-*RC* na kumekuwa na migogoro katika Halmashauri mfano Halmashauri ya Gairo, Halmashauri ya Malinyi, Halmashauri Mbeya Vijijini na Halmashauri ya Mwanga pia kati ya *DC* na Waheshimiwa Madiwani, lakini migogoro hii imekuwa ikitatuliwa na Viongozi wa Serikali, Waziri mwenye dhamana wa TAMISEMI pia migogoro mingine umeitatua mwenyewe kama Waziri Mkuu katika maeneo ambayo umefanya ziara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma kumekuwa na mgogoro kati ya *DC* na Baraza la Madiwani. Mgogoro huu umedumu kuanzia Agosti mwaka 2017 na mpaka sasa hivi hakuna kikao chochote cha Baraza la Madiwani kilichofanyika. Pamoja na juhudi kubwa zilizofanyika na Wizara ya TAMISEMI ya kuandika barua za kuamrisha Baraza lifanyike haraka lakini *RC* na *DC* wamekuwa wakizigomea barua za Waziri wa TAMISEMI na kuhakikisha kwamba jambo hilo lisifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na Halmashauri ya Mji wa Tunduma ili Madiwani wale waanze kufanya kazi na kuwalatea maendeleo wananchi wa Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka swali lako litajibiwa na Waziri anayehusika, ulipeleke kwenye ofisi mahsusi.

Mheshimiwa Leah Komanya, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na wimbi la wageni kuingia katika soko la ajira nchini, kwa sasa viashiria vinaonyesha kuwa wageni hawa wakifanya kazi katika sehemu nyeti kama viwanja vya ndege, bandarini na mipaka ya nchi yetu, hii inaweza kuwa ni hatari na siyo salama kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi na kuchukua hatua? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu ya swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Mwanza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia suala la ajira lakini pia tumeona ameweka suala la usalama kwenye maeneo nyeti. Naweza kusema kwa ujumla wake kwamba Serikali imeratibu vizuri sana suala la ajira nchini na imetoa kipaumbele kwa Watanzania kupata ajira kwenye sekta zote nchini, wageni wanayo fursa lakini kwa masharti. Ajira zote za wageni nchini Tanzania ni kwa nafasi zile za kitaalam tu ambazo Watanzania hawana uwezo nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaacha wazi, tumeweka ukomo ni wageni watano tu kwa taasisi ndiyo wanapata fursa ya kuajiriwa ndani ya nchi kuitumikia taasisi hiyo na ni kwa nafasi ambazo Watanzania hawana uwezo nazo. Jambo hili linasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na tutaendelea kulisimamia kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa nambari moja ya kuajiriwa kwenye sekta zote ndani ya nchi. Pale ambapo inalazimika Taifa la nje

kupata ajira kama ambavyo nimeeleza tunaendelea kusimamia kama nafasi hiyo kweli kama ambavyo nimeeleza kuwa ni nafasi nyeti yenye utaalam ambao Mtanzania hana ndiyo tunaajiri na idadi ni waajiriwa watano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo Mheshimiwa ameyataja kwamba wapo wageni wanaweza kufanya kazi, tumeendelea kudhibiti vilevile kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya viwanja vya ndege, bandari na maeneo ya mipaka kule kwenye *boarder* zetu hakuna mgeni anayeweza kufanya kazi kwa sababu ni lazima tuweke Watanzania ambao kweli wanakerwa na nchi yao na wanaweza kulinda nchi yao kuanzia kwenye mipaka ili kuhakikisha kwamba hakuna jambo lolote linaloashiria kuvunjika kwa amani na kuingizwa ndani ya nchi na mtu yeyote ambaye tunaweza kumwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba ajira hizi ukikuta mtu yeyote wa Taifa la nje anafanya kazi kwenye maeneo hayo ya viwanja vya ndege, bandari na mipaka labda kama kampuni inafanya shughuli maalum kwenye eneo hilo na kwa masharti yale kwamba watapata nafasi kufanya kazi kwenye kampuni hiyo kama nafasi hiyo hatuna Mtanzania mwenye uwezo nayo, vinginevyo tunaendelea kusimamia kwamba kazi zote mpaka mipakani na maeneo nyeti Watanzania ndiyo wanapata fursa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania msisitizo huu tunausimamia na ofisi yangu inayo Idara inasimamia jambo hili na tunafanya ukaguzi wa mara kwa mara kujiridhisha kwamba hakuna ujanja ujanja unaoletwa iwe na mwekezaji au mtu yeyote ambaye amepata nafasi ya kuingia nchini na siyo Mtanzania kupata ajira kwenye sekta zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kusimamia maeneo haya ili yaendelee kuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa ajili ya kuwekeza katika miundombinu mbalimbali nchini, lakini kwa muda mrefu sasa wapo wachache ambao wanaharibu kwa kuchukua vyuma hivi kwa ajili ya vyuma chakavu. Je, Serikali ipo tayari kuwachukulia hatua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia uharibifu wa miundombinu mbalimbali lakini ametaja na vyuma, sasa inaonekana miundombinu anayoizungumzia yeye ni ile yote iliyowekwa vyuma. Kama hivyo ndivyo nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali kwanza inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuboresha miundombinu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya barabara, ujenzi wa nyumba maalum, ujenzi wa majengo mbalimbali ambayo tunaamua kuyajenga ili kutolea huduma na kama miundombinu hiyo inatumia vyuma vizuri lakini tunachoweza kusema kwamba miundombinu hii tunao wajibu wa kuilinda Watanzania wote na endapo itatokea yupo miongoni mwa Watanzania wenye nia mbaya wanaihujumu miundombinu hii, Serikali hatuwezi kukaa kimya, lazima tuchukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza Serikali maana yake jukumu hili la Watanzania wote, kila Mtanzania anayo dhamana ya kulinda, ulinzi na usalama wa ndani ya nchi ikiwemo na kuilinda miundombinu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimeona kwenye *television* Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo kule Mkoani Shinyanga akishirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wamekamata lori la fuso lilijazwa vyuma vilivyong'olewa kwenye barabara vile ambavyo vinawekwa kwenye daraja na kingo za barabara, huu ni uharibifu ambao hatuwezi kuuvumilia, nadhani hili Watanzania lazima tuungane pamoja tukemee tabia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatumia fedha nyingi kujenga kingo za barabara kuashiria maeneo yenye hatari lakini Watanzania wengine wanakuja kung'oa kwa matumizi yao. Mimi naamini Mkoa wa Shinyanga utakuwa umechukua hatua kali dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaambia Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Kiswaga hivyo vyuma ulivyoeleza vitalindwa. Pia siyo vyuma tu, kila miundombinu ambayo imejengwa na tumetumia fedha za Serikali, tutaendelea kuilinda na Watanzania tuendelee kuilinda pale ambapo tunaona kuna Mtanzania anaenda kuharibu lazima tumkamate na tumchukulie hatua kumpeleka kwenye vyombo vya sheria ili iwe funzo kwa wengine na kwamba kila mmoja lazima alinde miundombinu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nusu saa na naona saa yetu imeshafika. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Waheshimiwa Wabunge sasa ni Maswali ya kawaida, tunaanza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 261

**Ugonjwa wa *Hepatitis***

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

*Hepatitis* ni ugonjwa hatari usiofahamika vizuri kwa wananchi walio wengi:-

(a) Je, dalili za ugonjwa huo ni nini;

(b) Je, ugonjwa huo una chanjo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maambukizi ya Homa ya Ini husababishwa na virusi ambavyo vinapoingia mwilini mwa binadamu hushambulia ini pekee na hivyo kulifanya kushindwa kufanya kazi vizuri. Katika hatua za mwisho mwathirika wa ugonjwa huu anaweza kupata saratani ya ini. Virusi vya homa ya ini vipo katika makundi matano, yaani (A), (B), (C), (D) na (E).

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za homa ya ini ni pamoja na ngozi na macho kuwa na rangi ya njano, kukojoa

mkojo wenye rangi nyeusi, joto la mwili kupanda, kuwa na mafua, kichwa kuuma, kukosa nguvu, kupata kichefuchefu, kutapika, tumbo kuuma upande wa juu kulia na kupungua uzito.

Mheshimiwa Spika, maambukizi ya homa ya ini yanategemeana na kundi la Virusi. Kundi la B, C na D huambukizwa kwa niia ya kuongezewa damu yenye virusi vya ugonjwa huo, kujamiiana, utumiaji usio salama wa sindano na vitu vingine vyenye ncha kali, utumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga sindano yenye virusi vya ugonjwa huo, majimaji ya mgonjwa kumpata mtu mwingine ambaye ana kidonda, pia mama anaweza kumwambukiza mtoto wake wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina ya homa ya aina ya ini inayosababishwa na virusi vya kundi (B) *Hepatitis* B *(HBV)* ndiyo inayoongoza kwa maambukizi nchini. Aina ya Kirusi cha A na E huambukizwa kwa njia ya kinyesi na kutokuwa na majisafi na salama *(faecal oral)* ambazo hufanana kwa kiasi kikubwa na uambukizwaji wa magonjwa ya kuhara.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa *Hepatitis B* unaweza kukingwa kwa kutumia chanjo na chanjo hii hutolewa kwa mtu asiye na maambukizi ya virusi hivyo na hutoa kinga kwa kipindi chote cha maisha yake. Hapa nchini chanjo hii inapatikana kwa watu wazima na watoto wachanga. Kwa watoto wachanga, chanjo hii ipo katika mchanganyiko wa chanjo ya *pentavalent* ambayo watoto wachanga hupatiwa, katika mwaka 2017, asilimia 98 ya watoto walipata chanjo hii. Kwa wenye maambukizi ya virusi aina (C), kwa sasa hakuna chanjo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayoelimisha umma juu ya ugonjwa wa Ini, ugonjwa ambao ni hatari kama alivyoeleza mwenyewe Naibu Waziri kwamba, ugonjwa huu unaweza ukaambukizwa kwa kujamiiana, kwa mama kumuambukiza mtoto wake mchanga, kudungwa au kujidunga sindano na mama kumwambukiza mtoto anapojifungua. Ni ugonjwa hatari sana ambao wananchi wengi hawaujui na hawajui namna ya kujikinga. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kutoa elimu kama inavyotoa juu ya ugonjwa wa malaria, kifua kikuu na maradhi mengine ili wananchi wajiepushe na wawe na elimu juu ya ugonjwa huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua wigo kwa zahanati na vituo vya afya kuwa na uwezo wa kupima ugonjwa wa Ini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Moja, ametaka kujua Serikali tunafanya nini katika kuelimisha jamii. Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii kupitia vitengo vyake vya elimu kwa umma imekuwa inaandaa majarida na machapisho mbalimbali ambayo tumekuwa tunayatoa kwa umma na kwa kupitia katika Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumekuwa tunatoa elimu hii katika kliniki mbalimbali lakini kutokana na umuhimu wa ugonjwa huu, tutajaribu kuongeza juhudi zaidi kuhakikisha kwamba wigo wa elimu hii unapanuka na kuweza kuwafikia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili alitaka kujua wigo wa upimaji. Kwa sasa upimaji wa ugonjwa huu unafanyika katika ngazi ya Wilaya kwenda juu kwa aina ya vipimo ambavyo tulikuwa navyo, lakini kwa sababu

teknolojia imekua sasa hivi na vipimo vya haraka *(rapid test)* zimeweza kupatikana, Serikali inatafakari sasa upatikanaji wa vipimo hivi katika ngazi nyingine za chini ili upimaji wa ugonjwa huu uweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitoe rai kwamba maambukizi ya *Hepatitis B* yanafanana na maambukizi ya UKIMWI na nawaomba sana wananchi tuwe tunajenga tabia ya kupima ili tuweze kutunza maini yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kwamba kuna aina tofauti za maradhi ya ini lakini amesema kuna (A), (B) na (C) lakini ukipata aina ya A, B na C zinaathiri vipi ili tuweze kujielewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nipate ufafanuzi huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ufafanuzi kwa Mheshimiwa Fakharia.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba tunapozungumzia virusi vya ugonjwa wa *Hepatitis* maana yake ni kwamba ni virusi ambavyo vinashambulia Ini. Katika jibu langu la msingi nilisema kwamba kuna makundi matano, kinachotofautiana pale ni jinsi gani ya virusi hivi vinaambukizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, virusi vya *type* B, C na D maambukizi yake yanafanana na yanafanaa vilevile kama mtu ambaye anaambukizwa virusi vya UKIMWI kwa maana kuongezewa damu, kujitoga ama kwa kujamiiana. Virusi vya *type* A na E uambukizwaji wake mara nyingi ni kwa njia ya maji, mtu anapokunywa maji yasiyo safi na salama anaweza kuambukizwa virusi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu virusi hivi vyote *type* A, B, C, D na E vinashambulia ini dalili zake zote huwa zinafanana kwa maana mgonjwa kuwa na macho na ngozi kuwa manjano, mkojo kuwa mweusi, kupata homa, kuumwa tumbo na wengine kuweza kuhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwa *Hepatitis B* tuna chanjo ambayo sasa hivi tunaitoa kwa watoto lakini *Hepatitis C* hii haina chanjo mpaka sasa, hizi nyingine kwa mfano *Hepatitis* A na E ni magonjwa ambayo athari zake sio kubwa sana kama zilivyo za *Hepatitis* B.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 262

**Hitaji la Kituo cha Polisi Tarafa ya Kipatimu - Kilwa**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE** aliuliza:-

Moja ya majukumu makubwa ya Serikali ni kulinda raia na mali zao kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama ikiwemo Polisi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukirejesha Kituo cha Polisi katika Tarafa ya Kipatimu Wilayani Kilwa ambacho kilihamishwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Kituo cha Polisi cha Kipatimu kilifungwa mwaka 1998 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu wa miundombinu na mahusiano mabaya kati ya raia na Askari kiasi cha kutishia usalama wa Askari na mali za Serikali zilizoko kituoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wananchi wameona umuhimu wa kurejesha huduma za Polisi katika eneo husika ambapo wameanza ujenzi wa kituo kipya cha Polisi. Aidha, nimshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Lindi ili kuona namna bora ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedasto Ngombale, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nimeyasikia na naomba anisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba eneo hilo la Tarafa ya Kipatimu lina zaidi ya wakazi 60,000, hatuna kituo cha Polisi, jitihada hizo zimefanywa na wananchi, nikiwemo na Mbunge, nimetoa mifuko 100 ya saruji ku-*support* na wananchi tayari wamefyatua matofali, tunayo matofali, lakini shida kubwa tunayopata ni ushirikiano kutoka kwa ofisi yake ya Mkoa ambayo mpaka sasa tumehitaji kupata ramani imekuwa shida, tumehitaji kupata mchanganuo imekuwa shida. Je, sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kunipatia ramani na mchanganuo wa ujenzi ule ili ujenzi uweze kuendelea kwa sababu wananchi wana ari kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa mchango wake katika kufanikisha ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ramani na ushirikiano mwingine nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba atapata. Naomba tu baada ya maswali tukutane ili niweze kumpa utaratibu huo namna gani ambavyo anaweza akapata ushirikiano huo, naamini kabisa inawezekana tu tatizo ni mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida Vyombo vyetu vya Dola, kwa maana ya Jeshi la Polisi, vimekuwa vikipenda sana kufanya kazi karibu na wadau mbalimbali ikiwemo Wabunge na wamekuwa wakitoa ushirikiano wa haraka. Kwa hiyo, nadhani kama kulikuwa na changamoto ya mawasiliano, basi baada ya maswali nitakuwa tayari kumsaidia kufanikisha hilo kwa haraka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na Kituo cha Kipatimo ambacho amesema Mbunge mwenzangu wa Kilwa Kaskazini, Mbunge wa Kilwa Kusini kuna kituo cha Polisi ambacho kimejengwa na wananchi lakini bado kumalizika kule Kijiji cha Nanjilinji. Je, Mheshimiwa Waziri, unaweza kutusaidia ili kituo hicho kimalizike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Nanjilinji ni miongoni mwa vituo vingi ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi ambavyo vinahitaji kukamilika. Hiyo ni dhamira ya Serikali, kuhakikisha kwamba vituo vyote hivyo nchi nzima ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi vinakamilika, siyo tu kwa sababu ya faida na manufaa ya matumizi ya vituo hivyo, lakini pia kwa kuweza kutokuwavunja moyo wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kituo cha Nanjilinji, pale ambapo hali ya kifedha itakaa vizuri, tutakimaliza pamoja na vituo vingine, lakini Mheshimiwa Mbunge vilevile anaweza akatumia fursa hiyo kusaidia kuweza kufanikisha ujenzi huo kwa kuhamasisha wananchi wake ama wadau kuendeleza jitihada hizi za Serikali na Serikali pale ambapo uwezo utakuwa tayari basi tutavimaliza.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Ujenzi wa Kituo cha Polisi Keza, Wilaya ya Ngara, kilichojengwa kwa nguvu za wananchi, kitakamilika lini maana kina zaidi ya miaka saba kimeezekwa bado *finishing.* Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Keza nacho ni miongoni mwa vituo ambavyo havijakamilika. Bahati njema ni kwamba mwaka huu wa fedha katika Mkoa wa Kagera tumetenga takribani bilioni 1.56 kwa ajili ya kumaliza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo haijakamilika, ikiwemo nyumba pamoja na vituo vya Polisi. Hiyo inaonesha azma ya Serikali ya kuweza kukabiliana na changamoto ya kumaliza vituo hivi ambavyo havijakamilika pamoja na nyumba za Askari nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ipo na pale ambapo hali ya kifedha itakaa vizuri basi tutakamilisha kituo hicho pamoja na vituo vingine ambavyo kama alivyosema mwanzo kwamba viko sehemu mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Oliver Semuguruka amesema, ni kweli tuna vituo vingi ambavyo vimeshafikia hatua hiyo, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wamechangia kwa kiwango kikubwa sana. Kwa sababu ni wengi tu siwezi kuwataja wote, lakini natambua Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Oran Njeza na wengine wengi ambao mmechangia ujenzi wa vituo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kilichoulizwa, Mheshimiwa Ulega hapa ndiye aliyekianzisha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wameongelea sana masuala haya ya vituo ambavyo vimeshafikia hatua ya kukamilishwa pamoja na nyumba za vijana wetu ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi, kwa sababu bado tuko hapa na bajeti tumeshapitisha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wanipenyezee maeneo ambayo yana vituo hivyo ili tunavyomaliza Bunge twende tukae ngazi ya Wizara tuweze kuweka vipaumbele ili tusiharibu nguvu kazi za wananchi ambazo zimeshafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joseph Selasini ameliongelea sana jambo hili, leteni hivyo vituo ili tutakapokwenda kukaa kwenye ofisi tuweze kuona kile tulichonacho na kuweza kumalizia vile ambavyo vimeshafikia hatua za kumaliziwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naamini huko kupenyeza maana yake tukuletee, maana sasa kila mtu akipenyeza hapa, nadhani utaanza na kituo cha Mheshimiwa Ngombale kabisa maana ndiye mwenye swali lake. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 263

**Wavuvi Wadogo Kutokuwa na Teknolojia Rafiki ya Kuvulia Samaki**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Wavuvi wadogowadogo hawana teknolojia rafiki inayowawezesha kuvua kwenye maeneo yenye samaki wengi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maeneo ya uvuvi kwa kutumia teknolojia rafiki kuweka vifaa vya kuvulia samaki *(Fish Aggregating Devices)* ili kuongeza upatikanaji wa samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* imeandaa programu ya kuweka vifaa maalum vya kuvutia samaki *(Fish Aggregating Devices – FADs)* kwenye bahari kwa kushirikiana na wavuvi. Kwa kuanzia programu hii inatekelezwa katika Wilaya ya Bagamoyo kwa upande wa Tanzania Bara na Nungwi, Tanzania Visiwani, ambapo vikundi viwili vya wavuvi kila upande vinafundishwa jinsi ya kutengeneza *FADs* na kuziweka baharini ili kuwasaidia wavuvi kupata samaki wengi na kutumia muda mfupi katika kuvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu inafadhili programu hii ambapo jumla

ya *FADs* 70 zimekwishatengenezwa na kuwekwa baharini katika maeneo ya Bagamoyo, Mafia na Visiwa vya Unguja na Pemba. Vilevile, wavuvi wameweka *FADs* za asili ambazo hutengenezwa kwa kutumia magogo ya minazi na magari chakavu katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Aidha, Serikali inaandaa mpango wa kufuatilia upatikanaji wa samaki baada ya *FADs* hizo kuwekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itahakikisha programu hii inafanikiwa na teknolojia hii inasambazwa katika maeneo mengine ili wavuvi waweze kufaidika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na jitihada za Serikali za kuongeza zana za uvuvi katika sekta hii ya uvuvi na pamoja na kupongeza jitihada zinazoendelea. Ningependa kujua, pamoja na mwanzo huu mzuri uliofanywa na Serikali, je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuongeza wigo zaidi ili zana hizi zipatikane katika bahari yote ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta ambazo zinaweza zikaleta tija katika Taifa letu na kuongeza Pato la Taifa, tumeshuhudia miaka iliyopita wakati Mheshimiwa Rais, Dkt. Joseph Magufuli, akiwa Waziri wa Uvuvi, alikamata meli moja tu na ikaleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza meli za kutosha ili ziweze kwenda kuvua katika kina kirefu na kuongeza Pato la Taifa katika Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kazi nzuri anayoifanya wakati wote ya kuwapambania wavuvi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, anataka kujua juu ya mkakati wa Serikali wa kusambaza teknolojia hii. Katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba Taasisi yetu ya Utafiti ya *TAFIRI* inafanya utafiti wa kujiridhisha juu ya ufanisi wa teknolojia hii katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mara tu baada ya kuwa tumefanikiwa na kujiridhisha kwamba teknolojia hii inaweza kutupatia tija, naomba nimhakikishie tutaisambaza kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo katika maeneo mengine ya bahari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, anataka kujua juu ya mkakati wa Serikali wa kupata meli kubwa kwa ajili ya kuweza kuvua na kupata faida kubwa kwa ajili ya nchi yetu. Naomba nimhakikishie kwamba Serikali tumejipanga vizuri na tupo katika programu ya kuhakikisha tunapata meli hiyo, hivi sasa tupo katika hatua kabla ya kwenda katika ununuzi wa meli hiyo, tuanzishe na kulifufua Shirika letu la *TAFICO* ambalo hili ndilo litakalokwenda kuwa msimamizi mkuu wa hata hiyo meli ambayo tunatarajia kuinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba aendelee kuvuta subira na kutuunga mkono ilimradi tuweze kufikia katika hatua hii tunayoifikiria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi lakini nafahamu kwamba mnajua hoja yao ndiyo iko mbele, kwa hiyo mengine tuyatunze kwa ajili ya michango baadaye. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ziwa Victoria lina samaki wa aina nyingi, ukiacha sangara tuna samaki aina ya gogogo, nembe

na furu, lakini aina ya nyavu ambazo Wizara na Serikali inaruhusu kuvua ni nyavu ambazo zinavua sangara peke yake. Nataka Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie hawa samaki wengine wanavuliwa kwa zana za aina gani, ikizingatiwa kwamba wanapatikana kwenye maji marefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ni kweli Ziwa Victoria lina aina nyingi ya samaki wakiwemo hawa aliowataja samaki aina ya gogogo, nembe na furu. Samaki hawa upo wakati ambapo hawakuwepo na ni kweli kanuni na sheria zetu haziwataji moja kwa moja samaki hawa. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tupo katika hatua sasa ya kuhakikisha kwamba samaki hawa nao wanatajwa na sheria na kanuni zetu ilimradi waweze kuingizwa katika hata vifaa vya kuweza kuwavulia na wananchi na wavuvi waweze kupata faida ya rasilimali hizi za nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa muda tulionao tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 264

**Kukamilika kwa Matengenezo ya MV. Victoria na MV. Serengeti**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Kufuatia kuzama kwa Meli ya *MV* Bukoba, kuharibika kwa Meli za *MV* Victoria na *MV* Serengeti ambazo zilikuwa zikitoa huduma ya usafirishaji abiria na mizigo kati ya Mwanza na Bukoba kwa gharama nafuu katika Mkoa wa Kagera:-

(a) Je, ni lini Meli za *MV* Victoria na *MV* Serengeti zitamalizika kufanyiwa matengenezo yenye viwango vya uhakika ili zianze kutoa huduma?

(b) Je, ni lini ahadi ambazo zilianza kutolewa na Serikali ya Awamu ya Tatu tangu kuzama kwa *MV* Bukoba za kununuliwa kwa meli mpya zitatelekezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua adha ya usafiri kwa njia ya maji wanayoipata wananchi wa Mwambao wa Ziwa Victoria, hususani wakazi wa Mwanza na Bukoba kutokana na Meli za *MV* Victoria na *MV* Serengeti kusitisha kutoa huduma kwa maeneo hayo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo uchakavu hasa kwa Meli ya *MV* Victoria na hitilafu ya mitambo kwa *MV* Serengeti ilivyovipata vyombo hivyo vya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilitenga fedha katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 ya shilingi bilioni 24.496 kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya mbili na ukarabati wa meli tano za Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* ikiwemo Meli za *MV* Victoria na *MV* Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Meli za *MV* Victoria na *MV* Butiama, unatarajiwa kutekelezwa na Kampuni ya *KTMI* kutoka nchini Korea ikishirikiana na *Yuko's Enterprises Company Limited* wakati wowote kuanzia sasa baada ya kusainiwa kwa mkataba wa utekelezaji wa mradi huo. Matengenezo haya yanatarajiwa kuchukua miezi kumi tangu kusainiwa kwa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, zabuni ya ukarabati wa *MV* Serengeti ilitangazwa tarehe 25 Aprili, 2018 na inatarajiwa kufunguliwa tarehe 24 Mei, 2018. Uchambuzi wa kina utafuata mara baada ya ufunguzi wa zabuni hiyo ili tuweze kumpata mzabuni sahihi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa meli moja mpya katika Ziwa Victoria, zabuni za kumpata Mkandarasi wa kujenga meli hiyo ziligawanywa kwa makampuni makubwa mbalimbali ya ujenzi wa meli duniani ambapo kampuni zenye uwezo zilionesha nia ya kujenga meli katika Ziwa Victoria kwa vigezo vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wa kumpata mzabuni, tarehe 10 Aprili, 2018, Kampuni ya *STX Engine Company Limited* na *STX Offshore & Shipbuilding Company Limited Joint Venture* zilishinda zabuni ya ujenzi wa meli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, Serikali na kampuni hizi hazikufikia makubaliano ya mwisho na hivyo kushindwa kutia saini mkataba wa utekelezaji wa mradi na hivyo kulazimika kusitisha zabuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitangaza tena zabuni hiyo tarehe 24 Aprili, 2018 na inatarajiwa kufunguliwa tarehe 24 Mei, 2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare swali la nyongeza.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.La kwanza, kwa wananchi wa Bukoba *Town* na Kagera kwa ujumla usafiri wa meli ni ajira, usafiri wa meli ni usafiri wenye nafuu na wenye kuaminika na usafiri wa meli unatoa unafuu wa bidhaa mbalimbali zinazokwenda Mkoa wa Kagera kuliko ilivyo sasa. Sasa miaka 22 tangu *MV* Bukoba izame na ahadi za kupata meli mpya zianze kutolewa tangu awamu ya

Mheshimiwa Mkapa ni miaka mingi; je, wananchi wa Bukoba na Kagera kwa ujumla wakijenga hisia kuwa wanatengwa watakuwa wanakosea?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nini kimekuwa chanzo cha mazungumzo baina ya Serikali na makampuni kutofikia makubaliano ili meli mpya ijengwe na wananchi wa Kagera ambao wanaadhimisha mwezi Mei huu kukumbuka waliotwaliwa ili waweze kuwa na matumaini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi wananchi watakuwa wanafanya kosa kubwa sana kuona kwamba wanatengwa kwa sababu hatua mbalimbali za Serikali zimekwishaanza kuchukuliwa na nimeeleza wazi kwamba tayari kuna Mkandarasi ambaye amekuja kwa ajili ya kuingia mkataba wa kujenga meli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu mbalimbali za kiufundi hasa tumeshindwa kuingia nao mkataba kwa sababu hatupendi tuwadanganye wananchi na vilevile hatupendi Serikali yetu iingie kwenye gharama zisizokuwa na sababu kutokana na kuingia mikataba ambayo siyo ya uhakika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili tumeshindwa kuingia mkataba nao kwa sababu kuna vigezo mbalimbali vya kiufundi na kiutaalam ambavyo walitakiwa waviingize katika mkataba wao, wao walivisahau. Sasa hivi nimhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wameviingiza na wao tena wameomba *tender* katika kuhakikisha kwamba wanatengeza hiyo meli mpya, tunahakikisha kwamba tukishapatana nao vizuri meli itajenga na inawezekana wakapata wao au wakapata watu wengine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge naona mmesimama hadi ambao kwenu hamna meli, lakini muda wetu umekwenda, tutamalizia swali la mwisho. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Na. 265

**Kuhusu Fidia kwa Wananchi wa Kata ya Matogolo na Seed Farm Songea Mjini**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO (K.n.y MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO)** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Matogoro na Kata ya *Seedfarm* wanaidai Serikali fidia inayotokana na Serikali kutwaa ardhi yao katika Bonde la Mto Ruhira na mpaka sasa bado hawajalipwa fidia ili wapate ardhi mbadala:-

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao fidia stahiki?

(b) Je, Serikali ipo tayari kulipa riba inayotokana na ucheleweshaji wa kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi hao?

**NAIBU WA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Daniel, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wananchi 803 ambao walikuwa ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha Mto Ruhira walipisha maeneo yao ambapo maeneo hayo kwa sasa yanatumika kama chanzo cha maji kwa wananchi wa Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Songea ilifanya tathmini ambapo jumla ya kiasi cha Sh.1,477,475,000 zilihitajika kwa ajili kulipa fidia kwa wananchi hao. Mwaka 2018 Serikali ilifanya mapitio ya tathmini ya fidia hiyo ili kuendana na thamani halisi ambapo kwa sasa fidia hiyo imefikia kiasi cha Sh.1,913,832,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha taratibu za kulipa fidia hiyo kwa kulipa shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi kilichobakia kitalipwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa kwenye swali la msingi kwamba wananchi 803 wa Kata za Matogoro na *Seedfarm* wanadai fidia ya kiasi cha shilingi bilioni 1.9, lakini majibu ya Serikali wamesema katika mwaka wa fedha 2017/2018 watalipa, mimi nafahamu mwaka wa fedha 2017/2018 unaishia hivi karibuni watalipa milioni 500. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kiasi hiki kilichobaki kinalipwa kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa malipo haya yamechelewa; Je Serikali haioni kwamba iko haja ya kuwalipa wananchi hawa pamoja na fidia kwa kuwa jambo hili limekuwa la muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie nafasi kumpongeza dada yangu Sikudhani Chikambo pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Songea Mjini kwa namna wanavo wapigania wananchi wa Majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji kwa kuona wananchi wale wametoa eneo kwa ajili ya chanzo cha maji, Wizara yetu ikaona haja ya kulipa. Nadhani kabla ya bajeti hii kuisha tutawalipa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiasi kilichobakia nitumie nafasi hii kwanza kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kutuidhinishia Bajeti yetu ya Maji na katika fedha zile kiasi ambacho kilibakia tumeshawatengea fedha wananchi wa Songea. Kikubwa nimwombe Mheshimiwa Mbunge akawasimamie wananchi wake waende kuzitumia fedha zile vizuri, badala ya kwenda kuongeza familia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji hatuko kwa ajili ya kuwadhulumu, kikubwa fedha hizi zitatoka kwa wakati katika kuhakikisha tunawalipa fidia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha nitaleta matangazo kwenu kabla hatujaendelea, nitaanza na matangazo ya wageni walionifikia Bunge siku la leo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni walio jukwa la Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Mheshimiwa Paul Sherlock ambaye ni Balozi wa Ireland nchini ambaye ameongozana na Mheshimiwa Robert Aylward ambaye ni Mbunge wa Bunge la Ireland; Mheshimiwa Catherine Connolly ambaye ni Mbunge wa Bunge la Ireland; *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa John Conlon ambaye pia ni Mbunge wa Bunge la Ireland;, wameongozana pia na Ndugu Allan Farrel ambaye ni Mkurugenzi wa Fedha wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ireland;, Ndugu Ruairi De Burca ambaye ni Mkuu wa Irish Aid Ireland na nchi zinazosaidiwa na Ireland. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Ndugu Josephine Maguire ambaye ni Afisa Mwandamizi wa Ofisi ya CAG - Ireland; wameongozana na Ndugu Collete Drinnan ambaye ni Afisa Mwanadamizi Ofisi ya CAG – Ireland; Ndugu Ciaran Lenillah ambaye ni Katibu Kamati ya *PAC* Ireland; *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia Ndugu Broangh Carry ambaye ni Mkuu wa Shirika la Irish Aid Tanzania; wameongozana pia na Ndugu Aran Corrigan ambaye Mshauri Mwandamizi Ubalozi wa Ireland; Ndugu Peter Nyella ambaye Afisa Afya Ubalozi wa Ireland; Ndugu Oliva Kinabo Mshauri Maendeleo ya Wanawake Ubalozi wa Ireland; Ndugu Joseph Kapinga ambaye ni Afisa Wizara ya Mambo ya Nje ya Tanzania. Karibuni sana Waheshimiwa wageni wetu, wageni wa Mheshimiwa Spika karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika jukwaa la Spika katika jukwaa la Spika pia tunao wageni wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tutaanza na Dkt. Yohana Budeba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi, tunaye pia Dkt. Mary Mashingo ambaye ni Katibu Mkuu Mifugo.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wenyeviti wa Bodi wa Taasisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tutaanza na Profesa Salome Mutayoba ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo *(TALIRI);* yupo pia Ndugu Lucas Malunde ambaye anatoka Bodi ya Maziwa; tunaye pia Profesa Faustine P. Lekule, Bodi ya Nyama; tunaye pia Profesa Ludovick Kazwala, Baraza la Vetenari; tunaye pia Profesa William Semuguruka ambaye anatoka *LITA;* tunaye pia Profesa Uswege Minga ambaye anatoka *TVLA*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao Wakurugenzi wa Idara, Taasisi na Wakuu wa Vitengo vilivyopo chini ya Wizara hii na wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Luhaga Mpina ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Naibu Spika ambao hawa ni wageni mahsusi kabisa wa Mheshimiwa Abdallah Ulega na mimi kwa sababu Abdallah Ulega ni baba yangu kwa hiyo hawa ni wageni mahsusi. Tutaanza na Mama Tulia ambaye ni ndugu Mariam Ulega Mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ahsanteni kwa makofi hayo kwa mama yangu mpendwa. Waheshimiwa Wabunge pia leo tumetembelewa na Tulia mwenyewe, Tulia Abdallah Ulega, karibu sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao pia wageni 85 ambayo ni wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita kutoka shule ya sekondari Patric *Mission* ya Jiji Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Ndele Mwaselela ambaye ni Mkurugenzi wa shule hiyo na Mwalimu Ndugu Kiletus Kilamba ambaye ni Mkuu wa Shule, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, naye ni Mwanamitindo wa Kimataifa anaefanya kazi zake nchini Marekani vilevile ni Muasisi wa Flaviana Matata *Foundation* pamoja na kampuni ya bidhaa. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa mlikuwa mnapiga makofi ngoja nisome tangazo lake vizuri ili tuwe tumeelewana sawasawa. Huyu ni Mwanamitindo wa Kimataifa ambaye ni Mtanzania anayefanya kazi zake nchini Marekani pia ni Muasisi wa Flaviana Matata *Foundation* pamoja na kampuni ya bidhaa za urembo ya *Lavy* na huyu ni Ndugu Flaviana Matata, karibu sana Flaviana, unafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 14 wa Constantine J. Kanyasu ambao ni Viongozi wa Chama cha Wavuvi Tanzania *(TAFU)* kutoka Kanda ya Ziwa, Kanda ya Pwani na Zanzibar, wakiongozwa na Mwenyekiti wa *TAFU* Ndugu Jephta Machandaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 25 wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma waliotoka Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga wakiongozwa Ndugu Adolvine Munisi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 44 wa Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge vile vile tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Augustino Masele ambao ni viongozi wa Geita *Co-operative Union* kutoka Mkoani Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambao ni Viongozi wa Chama kutoka Wilayani Kaliua Mkoani Tabora, Waheshimiwa Wabunge hawa ni Viongozi wa Chama cha Wananchi *(CUF)*, maana ukisema tu Chama inaweza ikatafsiriwa ni chama kingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni Mchungaji wa *Assemblies of God* Mchungaji Lameck Ngobito ambae ameambatana na mkewe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni Viongozi wa Shirikisho la Mashine Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Ernest Matondo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni Wanne wa Mheshimiwa Jitu V. Soni ambao ni Viongozi wa Vyama vya Wafugaji kutoka Mikoa mbalimbali, wageni wa Mheshimiwa Jitu Soni karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine ambayo nimeletewa hapa ni tangazo la mgeni mwingine

wa Mheshimiwa Waziri Luhaga Mpina ni Ndugu Ganeshan Vedagiri ambaye ni mmiliki wa viwanda vya samaki, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naleta matangazo mengine kwenu, kwanza ni tangazo linalotoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, anawatangazia Wabunge wote Wanawake kwamba leo tarehe 17 Mei, 2018, kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote, semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kuahirishwa Kikao ha Bunge saa saba mchana. Waheshimiwa Wabunge wanawake mnasisitizwa kuhudhulia semina hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka maeneo yanayolima kahawa, kutakuwa na kikao leo saa saba Ukumbi wa Waziri Mkuu mnaombwa msikose kwenye kikao hiki muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge wote mnaotoka maeneo yanayolima kahawa tafadhali mwende kwenye ukumbi wa Mheshimiwa Waziri mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Dustan Kitandula ambaye ni Mwenyekiti wa Vinara wa Lishe. Mheshimiwa Dustan Kitandula anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tarehe 17 mwezi wa tano 2018 kutakuwa na maonesho ya viazi, maharage na mahindi lishe katika viwanja vya sherehe vya Bunge mkabala na jengo la Idara ya Habari.

Maonesho hayo yameandaliwa kwa pamoja na kikundi cha Wabunge Vinara wa Lishe kwa kushirikiana na Taasisi za Lishe, *PANITA* na *CIP*, maonesho yataanza saa saba Mchana baada ya kuahirishwa Bunge, Waheshimiwa mnaombwa kwenda kujionea wenyewe vyakula lishe hivyo muhimu na pia kujipatia mbegu. Hii itatusaidia

kwenye Majimbo kusaidia watu wetu kuondokana na utapiamlo. Kwa hiyo, wote nashauri tupite pale tukaangalie maonesho hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa John Kadutu ambaye ni Meneja wa Bunge *Sports Club,* anapenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kuwa timu yetu ya watoto waishio katika mazingira magumu Tanzania *Street Children* ambayo inatokea Mwanza ilishiriki michezo ya Dunia kule Urusi, jana ilicheza fainali na Brazil matokeo Brazil ilikuwa moja, Tanzania hatukupata. Hivyo, tumechukua nafasi ya pili. Hata hivyo timu yetu hii imetoa mchezaji bora wa kiungo. Kwa hiyo Mheshimiwa Kadutu alikuwa anatujulisha hili lakini kwa niaba ya Bunge tunawashukuru sana watoto hao kwa heshima waliyotupa kama nchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine nimeletewa hapa kwamba wafugaji hawakutangazwa mwanzo, majina yao hakuletwa hapa, lakini niwatangaze kwa pamoja wafugaji wote karibuni sana, sijui wamekaa upande gani, karibuni sana. Pamoja na mambo mengine tunawaheshimu sana, maana bila ninyi hatuwezi kupata kitoweo nchi hii, karibuni wafugaji wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Juliana Shonza, anaomba mtu yeyote ama Mbunge yeyote ambaye alipita hapo kwenye kiti chake majira ya jioni halafu pengine akaondoka na simu ambayo inafanana na ya kwake anaomba amrejeshee tafadhali. Kwa hiyo kama kuna mtu ameiona ama amemwona aliye nayo tafadhali amrejeshee Mheshimiwa Juliana Shonza simu yake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Mimi naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na naomba nisisome. Mwongozo ambao naomba kwako ni kuhusu maswali kwa Waziri Mkuu ambayo yanaongozwa kwa mujibu wa Kanuni zetu lakini kwa Nyongeza ya Sita ya Kanuni zetu na naomba ikikupendeza niisome.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, kwa sababu unahitaji mwongozo wangu mimi nilishaisoma, kwa hiyo, wewe endelea ili tusipoteze muda.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, fasili ambayo nilikuwa nahitaji uzingatie ni ya (2) kwa Nyongeza ya Sita kwamba maswali kwa Waziri Mkuu siyo suala tu la kisera, inasema hivi, ni Sera za Serikali au jambo lolote lenye manufaa na maslahi kwa jamii na Taifa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba kuna masuala ya kisera, Kanuni zetu zime-*provide* maeneo mawili; jambo la kisera au jambo lolote lenye maslahi kwa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ambalo asubuhi nilikuwa namuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu ni suala la kisera lakini ni suala ambalo pia lina maslahi kwa umma wa Watanzania wa Babati. Kama kuna jambo ambalo napenda kukufahamisha ni kwamba suala hili lilishafika kwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa Kanuni zetu hili suala siyo la kitakwimu, maana lingekuwa la kitakwimu Waziri Mkuu asingeweza kulijibu, lakini hili lilishafikishwa kwake na Madiwani wa Babati wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri na Wazee wa Babati na nyaraka zote tulishampatia Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala hili pia limekuwa likisingiziwa kwamba ni kauli ya Rais na hili jambo limemchafua sana Mheshimiwa Rais Babati lakini Mheshimiwa Rais amesema yeye hahusiki ni masuala ya uongozi wa Mkoa wa Manyara walimalize. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali, Mheshimiwa Rais amejivua kuhusu stendi ya Babati kwamba hafahamu. Sasa mimi ninapouliza kama Mbunge linagusa wananchi wangu wa Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunashindwa kuelewa kwa sababu kuna Wabunge wengine wanauliza maswali ya moja kwa moja ya jimboni yanajibiwa, sitaki kutaja Wabunge wengine. Mheshimiwa Sakaya nyakati zilizopita aliuliza suala la mafuriko jimboni kwake moja kwa moja likajibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe tu mwongozo wako, ni mpaka lini suala la Babati litapigwa danadana wakati kwa hali ya kawaida limekuwa likiichafua Serikali, likimchafua Mheshimiwa Rais moja kwa moja na kwa bahati mbaya ukimfanyia mtu dhuluma inakurudia. Mwanzoni CCM - Babati walifurahia wakijua zile pesa watazipata, leo wamenyang'anywa na CCM wako nyuma yetu Babati wakidai hii stendi irudishwe Halmashauri kwa sababu hata zile pesa wao hawafaidi zinakwenda...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, naomba umalize tafadhali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako, ni kwa nini meza isimuache Waziri Mkuu awe anajibu maswali yetu yawe ya kisera au yasiyo ya kisera badala ya kumchagulia maswali yapi ajibu wakati haya mambo yako wazi na wanayajua kama Serikali, kwa nini asijibu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati likijibiwa swali la 263 lililoulizwa na Mheshimiwa Makilagi, muuliza swali alitoa maelezo akisema kwamba Serikali ilipata tija kutokana na kukamatwa kwa Meli ya Wachina maarufu kama Meli ya M.V. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni tunatakiwa kusema ukweli na ni kosa kusema uongo. Huu ni mwezi wa Ramadhani, mimi nataka kuwarudisha katika ukweli ili tusimame katika mstari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Serikali ilishindwa kesi na ilitakiwa kulipa shilingi trilioni 1.3. Kwa hiyo, maelezo aliyoyatoa amelipotosha Bunge na amesema uongo na Watanzania waliokuwa wanatusikiliza *live* wamesikia maelezo ambayo hayakuwa sahihi. Naomba mwongozo wako, ni sahihi Mbunge kutoa taarifa ambazo siyo za ukweli?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), kutokana na muda nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 3 Aprili, 2018 niliomba mwongozo na bahati nzuri kwenye Kiti ulikuwa Naibu Spika kuhusu kukosewa kwa Wimbo wa Taifa unaoimbwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Nataka tu kujua mwongozo wako, huwa inachukua muda gani kujua wimbo umekosewa, unahitaji miezi mitatu au minne maana yake mwongozo wangu tokea tarehe 3 Aprili, 2018 haujajibiwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, miongozo niliyochukua kwa leo inatosha.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na mwongozo nilioombwa na Mheshimiwa Pauline Gekul. Yeye anaomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu maswali. Katika maelezo yake marefu ambayo sitayarudia ametoa mifano michache kwamba kuna Wabunge ambao wanauliza maswali ya majimbo yao na wanajibiwa, lakini pia ameuliza kwamba jambo hili litapigwa danadana mpaka lini na mwisho akasema anaomba mwongozo kwa nini Mheshimiwa Waziri Mkuu asiachwe ajibu maswali yote ya kisera na mengineyo.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu tuliojiwekea kwenye Kanuni zetu wenyewe kwamba maswali yataulizwa kwa nani na wakati gani, tunafahamu yapo maswali anayotakiwa kuulizwa Waziri Mkuu ndiyo maana amewekewa utaratibu mahsusi, maswali wanayoweza kuulizwa Mawaziri wengine nayo yana utaratibu wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maelezo marefu aliyotoa Mheshimiwa Gekul kwamba jambo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu analifahamu, mimi si katika mamlaka yangu kujua Waziri Mkuu analijua ama halijui, suala ni kwamba Kanuni zetu namna tulivyoziweka, Waziri Mkuu hawezi kuwa anaulizwa maswali ambayo yako mahsusi na eneo fulani kwa sababu hatarajiwi kwamba kila jambo yeye analijua kwa kuwa ni Waziri Mkuu, hiyo ni moja.

La pili, maswali ya majimbo yanaulizwa kwa Mawaziri na ndicho ambacho tunakifanya kila siku. Maswali ya kisera ambayo tunaona kwamba Waziri hawezi kujibu ndiyo tunamwekea Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kila Mbunge humu akisimama akiuliza swali linalohusu Jimbo lake tunatarajia Waziri Mkuu atakuwa anajibu kwa namna gani halafu tutaanza kusema hajajibu kikamilifu. Kwa hiyo, kila Mbunge

hapa akiuliza jambo la mahali kwake Waziri Mkuu asimame ajibu siyo sawasawa, Kanuni zetu zimesema wazi swali la kisera au la kijamii, kijamii haimaanishi kwenye jimbo lako wewe barabara imekatika unataka Waziri Mkuu ajibu, hapana. Kama barabara zimekatika kote unamtaka aseme Serikali ina mpango gani kwenye barabara zote siyo kwenye barabara ya jimbo lako.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Gekul siyo peke yake ambaye swali lake limezuiwa leo, hata la Mheshimiwa Mwakajoka limezuiwa ni kwa sababu walianza kueleza kama tatizo la maeneo mengi nchini baadaye anauliza la Halmashauri yake peke yake. Sasa Halmashauri ya Tunduma peke yake Waziri Mkuu taarifa hizo anazo au hata kama anazo kama linahusu Tunduma peke yake utamuulizaje yeye hapa, unataka akujibu nini wakati Mheshimiwa Jafo yupo na hiyo ndiyo kazi yake? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwasihi kwa sababu kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kinaendelea na tuko hapa kwa muda, tujielekeze kwenye yale maswali ambayo tunataka kuwasemea siyo tu watu wetu wa jimbo kwa sababu hayo Mawaziri wapo kwa ajili ya kazi hiyo lakini yale ambayo tunayaona ni ya jumla ndiyo ambayo tunatakiwa kumuuliza Waziri Mkuu ambayo Mawaziri hawana uwezo wa kuyajibia yote kwa ujumla, wanajibu kwenye eneo lao peke yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gekul huo ndiyo mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, nieleze jambo lingine kwa ujumla. Kiti hiki kikishatoa maamuzi unarudi kwenye Kanuni ya tano (5), hukirudii Kiti tena. Leo niseme kwa sababu imeshawahi kutokea siku za nyuma, Mheshimiwa Mbunge mimi leo natoa maamuzi, kesho anakuja mtu mwingine anakaa hapa unaomba mwongozo juu ya kile kilichoamuliwa jana, kikanuni siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mbunge unatakiwa utumie Kanuni ya tano (5) kuandika malalamiko yako, usiulize tena Kiti kuhusu jambo ambalo aliamua mtu mwingine aliyekaa hapa, ndiyo

utaratibu ulivyo. Tumejiwekea utaratibu huo kwa ajili ya kulinda heshima, kwa sababu tusipofanya hivyo tutashindwa wenyewe kuendeshana humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Khatib Haji kuhusu swali namba 263 la Mheshimiwa Makilagi. Ametoa maelezo kuhusu namna ambavyo wakati akiuliza swali la nyongeza kwamba kuna maelezo aliyatoa na kwa mujibu wa yeye Mheshimiwa Khatib anavyoona maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Makilagi yamelipotosha Bunge. Kwa hiyo, anaomba mwongozo kujua kama ni sahihi kwa Mbunge kulipotosha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili. La kwanza, kama ni jambo lililoulizwa kwenye swali la nyongeza, nitatafuta kwenye Taarifa Rasmi za Bunge Mheshimiwa Makilagi alisemaje na nitatoa maelezo.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili, kanuni kuhusu kupotosha Bunge tunazifahamu. Kanuni ya mwongozo inataka kujua kama jambo hilo linaruhusiwa ama hapana. Mheshimiwa Khatib mwongozo wako kuhusu Mheshimiwa Makilagi kutoa hayo maelezo na kwamba amelipotosha Bunge nitafuatilia Taarifa Rasmi za Bunge nijue Mheshimiwa Makilagi alisemaje na wewe maelezo yako namna ulivyoyatoa. Kwa hiyo, wakati huo nitaweza kutoa mwongozo kuhusu jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine nilioombwa nimeombwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda akieleza kuhusu mwongozo alioomba mnamo Aprili na kwamba mpaka leo hajapewa majibu. Japokuwa ameeleza jambo la msingi lakini huu siyo mwongozo ambao unaweza kutolewa na Kiti na Katibu yuko hapa, jambo hili linahitaji majibu. Katibu kama wimbo haujakosewa basi tuambiwe haujakosewa na kama umekosewa uletwe wimbo mahsusi kwa ajili ya kuimba ili tusikosee.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI –KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu wetu. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu la 99 - Maendeleo ya Mifugo na Fungu la 64 - Maendeleo ya Uvuvi, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa heshima kubwa, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za mifugo na uvuvi zinasimamiwa na kulindwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi yetu kwa umahiri na falsafa ya Hapa Kazi Tu, mapinduzi ya viwanda hapa nchini na utekelezaji makini wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naishukuru familia yangu kwa dhati, kwa upendo na kwa ushirikiano wanaonipa wakati natekeleza majukumu yangu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuhimiza masuala ya utunzaji wa mazingira ambayo ni muhimu katika utekelezaji wa kusimamia sekta ya mifugo na uvuvi. Nichukue fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Makamu wa Rais kuwa nitasimamia kikamilifu sekta ya mifugo na uvuvi katika usimamizi na utunzaji wa mazingira ili kuwa na ufugaji na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kwa hotuba yake nzuri sana ambayo kwa ufasaha imetoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali na kazi zitakazotekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza kwa busara Bunge hili Tukufu. Niwapongeze Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum wa Morogoro kwa ushirikiano na ushauri mzuri sana ambao wamekuwa wakiipatia Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo, hali ya mifugo. Katika mwaka 2017, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 2.8 ikilinganishwa na asilimia 2.6 ya mwaka 2016 na ikichangia asilimia 6.0 katika pato la Taifa ikilinganishwa na

asilimia 7.7 mwaka 2016. Aidha, kulingana na takwimu za mpango kabambe wa mifugo-Tanzania za mwaka 2017, idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kufikia ng'ombe milioni 30.5; mbuzi milioni 18.8; kondoo milioni 5.3; kuku wa asili milioni 38.2; kuku wa kisasa milioni 36.6; nguruwe milioni 1.9; na punda wapatao 595,160.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2017 uzalishaji wa maziwa umefikia lita bilioni 2.4 ikilinganishwa na lita bilioni 2.2 zilizozalishwa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017. Aidha, katika kipindi hiki usindikaji wa maziwa umeongezeka na kufikia lita milioni 56.2 ikilinganishwa na maziwa lita milioni 40.2 zilizosindikwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi Aprili, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kipindi hiki, jumla ya mitamba 590 ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na ya kampuni ya Ranchi ya Taifa *(NARCO).* Vilevile sekta binafsi ilizalisha na kuuza kwa wafugaji wadogo nchini jumla ya mitamba 13,145.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2018 uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kufikia tani 679,992 ikilinganishwa na tani 558,164 zilizozalishwa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi kufikia Aprili, 2018. Aidha, katika kipindi hicho cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 jumla ya tani 2,608.93 za nyama ziliuzwa nje ya nchi na jumla ya tani 1,224.5 za nyama ziliingizwa nchini. Pia uzalishaji wa mayai uliongezeka nchini kutoka mayai bilioni 2.76 mwaka wa 2016/2017 hadi bilioni 3.6 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018. Makadirio ya Mapato ya mwaka 2018/2019. Makusanyo ya mwaka 2017/2018 na makadirio ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu kupitia Fungu la 99 - Maendeleo ya Mifugo ilipangiwa kukusanya Sh.16,404,739,500. Hadi kufikia tarehe

30 Aprili, 2018 kiasi cha Sh.13,677,333,381.24 zimekusanywa sawa na 84.3% ikilinganishwa na Sh.10,952,827,500 zilizokusanywa katika mwaka 2017/2018. Mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Fungu la 99 inatarajia kukusanya jumla ya Sh.18,467,945,100. Vyanzo vya fedha hizo vimeanishwa katika aya 17 katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele katika mpango wa bajeti wa mwaka 2017/2018. Maeneo ya kipaumbele katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018 na katika mpango wa 2018/2019 kupitia Idara Kuu ya Mifugo yameainishwa katika aya ya 21 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu katika sekta ya mifugo mwaka 2017 na mpango wa fedha wa 2018/2019. Uzalishaji wa mashamba ya mifugo. Wizara itaendelea kuboresha mashamba ya Serikali ili kuzalisha mitamba katika mashamba ya Sao Hill, Kituro, Ngerengere, Mabuki na Nangaramo kwa kuwapitia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki, jumla ya mitamba 590 ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na *NARCO* ikilinganishwa na mitamba 634 iliyozalishwa na kusambazwa katika mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, sekta binafsi ilizalisha na kusambaza kwa wafugaji wadogo nchini jumla ya mitamba 13,145 ikilinganishwa na mitamba 11,454 mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini katika sekta ya mifugo. Biashara ya mazao ya mifugo na pembejeo. Sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upotevu wa mapato unaotokana na biashara ya mifugo na mazao yake kufanyika kinyume cha sheria na taratibu pia uuzaji wa dawa bandia ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto za ukusanyaji wa kiasi kidogo cha mapato ambapo kwa mwaka 2016/2017, Wizara ilikusanya shilingi bilioni 10.95 tu

na kutochangia ipasavyo katika pato la Taifa. Mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu iliunda timu ndogo ya wataalam kufanya tathmini ya biashara ya mazao ya pembejeo na mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu imebaini uwepo wa mianya ya utoroshaji wa mazao ya mifugo; ushindani usio sawa wa mazao ya mifugo kutoka nje ya nchini; kusuasua kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda hali ambayo imesababisha baadhi ya viwanda ndani kutelekezwa na vingine kubadilishiwa matumizi. Pia upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali na wimbi kubwa la uingizaji wa bidhaa za mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi bila kujali uhitaji halisi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yaliyoibuliwa na Kamati ya Tathimini ni pamoja na uwepo wa utoroshaji mkubwa wa mifugo kwenda nje ya nchi ambapo zaidi ya ng'ombe 1,614,035 sawa na kilo 201,754,335 zinapotea kila mwaka kutokana na ng'ombe hao kutoroshwa ambapo wangeliingizia Taifa takribani Sh.32,280,700,000 kutokana ushuru wa ng'ombe na nyama tu pamoja na Sh.24,210,525,000 kutokana na kodi ya mapato ambayo inafanya upotevu wa mapato kufikia takribani shilingi bilioni 56.49.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yamefafanuliwa vizuri sana katika aya ya 10 ya hotuba yangu. Kutokana na utoroshaji mkubwa wa rasilimali za mifugo na biashara ya magendo ya mazao ya mifugo, Serikali inapoteza zaidi ya shilingi bilioni 263.95 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi, Wizara yangu iliamua kufanya operesheni ambayo itadumu kwa kipindi cha miezi miwili (siku 60). Lengo la operesheni hii ni kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali unaosababishwa na utoroshaji wa rasilimali za mifugo nje ya nchi; uingizaji wa bidhaa ya mifugo bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo na biashara holela ya mazao ya mifugo na pembejeo. Operesheni hii inaitwa Operesheni

Nzagamba. Hadi kufikia tarehe 8 Mei, 2018 jumla ya Sh.1,992,804,200 zimekusanywa kama ushuru, tozo na faini mbalimbali katika operesheni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mikakati ya kulinda rasilimali za mifugo na mazao yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi inafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni zinazosimamia sketa ya mifugo nchini pamoja na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya uendeshaji wa Shirika la *NARCO* na mashamba ya uzalishaji wa mifugo. Utata wa umiliki wa Kampuni ya *NARCO*. *NARCO* imeanzishwa kwa Sheria ya Makampuni, Sura 212, kuna utata kwenye usajili wa Kampuni ya *NARCO* ambapo *Memorandum and Articles of Association (MEMARTS)* za *NARCO* zinaonyesha kuwa wanahisa ambao walisaini kwa vyeo vyao walipokuwa Mameneja wakuu, Katibu wa Shirika la Maendeleo la Taifa *NDC* wakati *NARCO* ilipoanzishwa mwaka 1968 *MEMARTS* hizi zimeendelea kusomeka hivyo mpaka sasa na hivyo kuifanya kampuni kuonekana kuwa ni mali ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mkanganyiko huo, Wizara yangu imeandaa pendekezo la kuibadilisha *NARCO* kutoka kampuni kuwa shirika la umma (*public corporation*) ili kuondoa utata uliopo na kupanua wigo wa utekelezaji wa majukumu yake. Faida za kuibadilisha *NARCO* kuwa shirika la umma ni pamoja na kuondoa mkanganyiko wa kisheria uliokuwepo katika muundo wa uendeshaji wa kampuni na kuwa shirika lenye uwezo, mamlaka na uwanda mpana zaidi wa kuleta tija kwenye sekta ya mifugo hapo nchini na kuwa na dira, malengo na majukumu yanayopimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya uwekezaji kati ya *NARCO* na wawekezaji wadogo waliokodishwa vitalu vya kuanzia hekta 2,000 hadi hekta 4,000. Maelezo ya awali yanaelezwa lakini niseme kwamba vitalu 23 vya wawekezaji

ambao wameshindwa kuwekeza zaidi ya 50% ya mikataba yao, mikataba yao itavunjwa kabla ya Juni, 2018. Vitalu 24 vya wawekezaji ambao wameshindwa kulipa pango la ukodishaji wa ranchi, mikataba yao itavujwa kabla ya Juni 2018. Wawekezaji waliokidhi masharti na matakwa ambao wamewekeza zaidi ya 50% na kulipa ada ya pango mikataba yao itahusishwa kabla ya Juni, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa Serikali kati ya Kiwanda cha Sukari cha Kagera na Mtibwa. Timu ilibaini mambo muhimu ambayo ni pamoja na makampuni haya kumilikishwa ardhi yenye ukubwa wa hekta 75,000 sawa na hekari 887,500 bure bila kulipia fidia ya ardhi kwa *NARCO.* Pia hakuna uwekezaji wowote wa mifugo, majengo na miundombinu uliofanyika katika mashamba ya Dakawa ambapo Kampuni ya Sukari ya Mtibwa ilimilikishwa jumla ya hekta 30,000 kwa ajili ya ufugaji wa kisasa kwa muda wa zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kitengule Misenyi, kampuni imewekeza ng'ombe 5,307, mbuzi 125, kondoo 35 ingawa hakuna uwekezaji wowote wa majengo katika miundombinu kinyume na makubaliano ya mikataba. Kufuatia changamoto hiyo, Wizara yangu inaandaa madai kwa makampuni haya ili waweze kuilipa *NARCO* fedha wanayodaiwa (mapunjo) na pia nimeagiza makampuni hayo kuwasilisha mpango kazi wa uwekezaji wa miaka mitatu katika maeneo hayo na endapo watashindwa kufanya hivyo tutawaondoa kwenye ranchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba kati ya *NARCO* na Kampuni ya *OVERLAND Livestock Multiplication Unit and Embryo Transplant* (Ranchi ya Mzeri na Mkata). Timu ya tathmini ilibaini kuwa katika mkataba huu *NARCO* na Serikali kwa ujumla hapakuwa na maslahi ambapo uwekezaji ulikuwa hisa 70% na *NARCO* 30% tu wakati *NARCO* inamiliki ardhi hekta 40,447.3 yenye thamani ya shilingi bilioni 27.6 pamoja na majengo ya miundombinu yenye thamani ya shilingi bilioni tatu ikilinganishwa na uwezo wa mwekezaji. *NARCO* inakamilisha utaratibu wa kuvunja mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba baina ya *NARCO* na A*gri-ranch*. Ranchi hii imegawanyika katika maeneo hayo yaliyotajwa na tayari *NARCO* imevunja mkataba huo na hatua za kupata mwekezaji mpya zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Kiwanda cha Nyama cha Dodoma *Meat Company Limited*. Wizara yangu iliunda kamati ya wataalam na kuchambua mkataba huu. Nimeonyesha katika aya ya 55 ya hotuba yangu ambapo Serikali haijapata gawio kwa miaka 10 sasa tangu kuingia mkataba huo mwaka 2008. Hivyo, ili kukamilisha taarifa za uchambuzi wa mkataba wa kuiwezesha Serikali kufanya uamuzi, Msajili wa Hazina ameelekezwa kufanya ukaguzi maalum (*special financial audit*) katika Kampuni ya Nyama iliyoko Dodoma ili baadaye hatua za kuvunja mkataba zifuate.

Mheshimiwa Naibu Spika,tathmini ya Viwanda vya Mazao ya Mifugo (nyama, maziwa na ngozi) vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi. Wizara inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa viwanda vya nyama vinajengwa na ambavyo havizalishi vinaanza usindikaji. Wizara kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina inafanya tathmini ya viwanda vya nyama vilivyokuwa vinamilikiwa na *Tanganyika Packers Limited* vya Mbeya na Shinyanga; Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza kinachomilikiwa na Serikali, Kiwanda cha Maziwa cha Utegi kilichokuwa kinamilikiwa na *Tanzania Dairies Limited,*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo ya uthamini inakamilika Mei, 2018. Uthamini huo utaiwezesha Serikali kutafuta mwekezaji mahiri ifikapo tarehe 30 Juni, 2018. Aidha, kutokana na changamoto zilizojitokeza, ubinafsishaji wa viwanda hivi vya Serikali baadhi ya hisa zitabaki Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Kiwanda cha Shinyanga kilikuwa na kizuizi cha kuendelea na uwekezaji kutokana na kutokuwa na hati ya kiwanda na mashamba ya kuhifadhi mifugo kushikiliwa na mwekezaji baada ya Serikali kutaifisha kiwanda hicho kutoka kwa mwekezaji

*Tripple S. Limited* ambaye alikuwa amekiuza kinyemela kwa *Abuward Investment Group Limited*. Wizara yangu ilifanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba hati hii inarejeshwa ambapo Aprili, 2018 hati hii ilikabidhiwa rasmi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile juhudi zinaendelea za kufufua Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Sumbawanga SAAFI, ambacho kilisimamisha usindikaji kutokana na deni na changamoto za uendeshaji. Ili uzalishaji katika kiwanda hicho uanze *NARCO* na SAAFI wanaandaa makubaliano ya kuanza biashara na ili kiwanda hicho kiweze kufufuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro baina ya wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Maelezo ya awali yametajwa katika aya 64; moja, Serikali kuwekeza kikamilifu katika mashamba yake na maeneo mengine. Aidha, Wizara yangu ilipokea mapendekezo ya namna ya kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Mapendekezo hayo yamefanyiwa kazi na hadi kufikia Desemba, 2018 kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Serikali kuwekeza kikamilifu katika mashamba yake na maeneo mengine yaliyokodishwa kwa wafugaji ili kupunguza tatizo la malisho kwa mifugo. Mashamba hayo ya Serikali ni pamoja na *NARCO, TALIRI, LMUs* na vituo vya kupumzishia mifugo.

(ii) Kutenga maeneo kwa ajili ya kuchunga hususan wakati wa uhaba wa malisho kwa kutoa mkataba maalum na mwongozo wa matumizi ya ardhi bila kuathiri kazi zilizoelekezwa na taasisi hizo ikiwemo utafiti na utunzaji wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga hekta 7,000 kutoka katika ranchi zake nne za *NARCO* kwa ajili ya matumizi ya wafugaji wa vijiji 29 katika Wilaya ya Kongwa kwa Spika, Bagamoyo, Siha, Loliondo, Arumeru na Karagwe kama ilivyoainishwa katika kiambatisho namba tisa (9). Jumla ya hekta 1,370 kutoka *TALIRI* zimetengwa kwa matumizi kwa ajili ya wafugaji wa

vijiji 14 katika Wilaya za Mpwapwa, Misungwi, Kongwa, Tanga na Siha kama ilivyoonyeshwa katika kiambatisho cha 10. *(Makofi)*

(iii) Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itasimamia kikamilifu migogoro ya ardhi katika mashamba na minada kote nchini na kutoa elimu na kusimamia uhifadhi wa malisho kwa ajili ya matumizi wakati wa ukame na kiangazi.

(iv) Kuwaondoa wawekezaji katika ranchi na vitalu vya *NARCO* walioshindwa kuwekeza kwa mujibu wa mkataba na kupangisha wafugaji wenye mifugo mingi wasio na maeneo ya kutosha kwa malisho. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, *NARCO* imetoa *notice* na kuwaondoa wawekezaji katika vitalu 24 vyenye eneo la ukubwa wa hekta 65,879.51. Ni imani yangu kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itatekeleza mapendekezo ya timu hii ya wataalam na kuyakabidhi maeneo tengefu yenye jumla ya hekta 96,501 ambayo yamekosa sifa ili waweze kupatiwa wafugaji.

(v) Sheria ya Malisho ya Mifugo, Na.13 ya mwaka 2010 itaboreshwa ili kuwezesha sasa haya mashamba ambayo yanatolewa kwa ajili ya wafugaji kulindwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi na Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na.12 wa mwaka 2010. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa tathmini ya utekelezaji wa zoezi la kupiga chapa ya moto ng'ombe na punda limefanyika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia Aprili, 2018 jumla ya ng'ombe 17,045,944 wamepigwa chapa ikiwa ni asilimia 98 ya lengo la kupiga chapa ng'ombe 17,390,090. Vilevile ng'ombe wa maziwa 58,214 wamevishwa hereni ambapo ni 7.4% kati ya ng'ombe wa maziwa 782,995 wanaotakiwa

kuvishwa hereni nchini. Punda 57,799 wamepigwa chapa ikiwa ni 10.1% ya lengo la kupiga chapa punda 571,351.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sekta ya uvivu. Katika mwaka 2017, sekta ya uvuvi ilichangia 2.5% katika pato la Taifa ikilinganishwa na 2% kwa mwaka 2016. Wavuvi na wafugaji wa samaki wapatao 230,977 walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uvuvi. Aidha, zaidi ya Watanzania milioni nne wanaendelea kupata kipato cha kila siku kwa kushiriki shughuli zinazotegemea kuwepo kwa sekta ya uvuvi ikiwemo kutengeneza maboti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao yake, wachuuzi na mamalishe. Pia katika mwaka 2017, sekta ya uvuvi imekua kwa 2.7% ikilinganishwa na 4.2% kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za tafiti za Taasisi za Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*) na Baraza la Kilimo Tanzania zinazofanyika kwa kipindi tofauti zinaonesha kwamba kiasi cha samaki kilichopo katika maji yetu ya Tanzania ni tani 2,736,248 kwa mtawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria tani 2,143,248; Ziwa Tanganyika tani 295,000; na Ziwa Nyasa tani 168,000; maji madogo na maji kati, mito na mabwawa ni tani 30,000 na maji ya kitaifa ya Bahari ya Hindi ni tani 100,000. Kiambatisho Na.16 kinaonesha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wavuvi na vyombo vya uvuvi imeendelea kuongezeka kutoka wavuvi 183,800 waliotumia vyombo vya uvuvi 57,291 mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2018 wavuvi 203,529 walitumia vyombo vya uvuvi 59,338. Kiasi kikubwa cha nguvu ya uvuvi kikiwa katika Ukanda wa Ziwa Viktoria ikifuatiwa na Ukanda wa Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na nguvu hiyo ya uvuvi, uzalishaji wa samaki kwenye maji ya asili umeongezeka kutoka tani 362,645 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.48 mwaka wa 2015 hadi tani 387,543 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.74 kwa mwaka wa 2017/2018, sawa na ongezeko la asilimia 6.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini kuhusu utendaji wa kazi ya sekta ya uvuvi katika Ziwa Viktoria ilifanyika kuanzia tarehe 12 Desemba, 2017 hadi 27 Desemba, 2017. Uamuzi wa kuendesha tathmini hii ulitokana na Wizara kwa miaka mingi mfululizo kushindwa kufikia malengo ya kukusanya maduhuli, viwanda vya kuchakata minofu ya samaki kukosa malighafi na samaki wachanga kuuzwa katika masoko mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Wizara yangu iliamua kuunda timu ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali za sekta binafsi ili kufanya tathmini kuhusu utendaji wa sekta ya uvuvi katika Ziwa Viktoria ambapo mambo makubwa yaliyoibuliwa katika tathmini hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Viwanda vya kuchakata samaki na mazao yake kupungua kutoka viwanda 13 vilivyokuwepo mwaka 1998 hadi kufikia viwanda vitatu tu vinavyofanya kazi kwa sasa;

(ii) Wastani wa uzalishaji wa samaki viwandani kupungua kutoka tani 1,065 kwa siku hadi tani 171 kwa siku hivi sasa ambapo pia ajira zimepungua kutoka 4,088 na kubaki 2,179 kwa sasa katika viwanda hivyo.

(iii) Samaki aina ya sangara wanaoruhusiwa kuvuliwa wenye urefu wa sentimita 50 hadi 85 wamepungua wamebaki asilimia tatu tu katika ziwa letu ambapo wale wachanga ni asilimia 96.6 na samaki wazazi wamebaki asilimia 0.4 tu.

(iv) Kupungua kwa mauzo ya sangara kutoka tani 53,675 kwa mwaka wa 2005 hadi 26,045 kwa mwaka 2016 sawa na upungufu wa takribani asilimia 50 katika kipindi cha miaka 10.

(v) Samaki aina ya sangara wanaovuliwa katika maeneo ya mipakani wanatoroshwa kwa njia za magendo na kupelekwa katika viwanda vya nchi jirani.

(vi) Wapo raia wa kigeni ambao wanajihusisha na biashara ya samaki ambapo wanakwenda hadi visiwani kukusanya mazao ya uvuvi kinyume cha sheria na mara nyingine kutumia leseni na vibali vya Watanzania, pia leseni moja imekuwa ikitumiwa na wafanyabiashara zaidi ya mmoja.

(vii) Imebainika kuwa mawakala wa samaki viwandani na wasafirishaji wa samaki nje ya nchi hukwepa kufanyiwa makadirio na *TRA* na kutokutaja thamani halisi ya mauzo na udanganyifu wa mapato yatokanayo na biashara zao. Aidha, imebainika kuwa mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 581.5 hayakufanyiwa makadirio ya kodi na *TRA* katika mwaka wa fedha 2016/2017 na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

(viii) Kutokana na kushamiri kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Viktoria, mapato ya Serikali yanayokusanywa kutokana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA)* na Mamlaka ya Serikali za Mitaa inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 25 kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizi, Wizara yangu iliamua kufanya operesheni ya kupambana na uvuvi haramu pamoja na kudhibiti upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Operesheni hiyo kwa jina maarufu inaitwa Operesheni Sangara ya mwaka wa 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya mifugo na Uvuvi imeendesha Operesheni Sangara 2018 ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Viktoria. Matokeo ya operesheni tangu ianze yameainishwa katika aya ya 134 ya hotuba yangu ambapo kwa uchache ni pamoja na:-

(i) Wavuvi na wafanyabiashara mbalimbali wapatao 2,610 wamefanyiwa ukaguzi na kupatikana na makosa. Aidha, samaki wachanga waliovuliwa kwa njia haramu wapatao kilo 136,031 walitaifishwa na kugawiwa

taasisi za umma na wananchi. Vilevile mazao ya uvuvi yakiwemo kayabo kilo 178,244 na mabondo kilo 5,052 yalikamatwa yakitoroshwa kwenda nchi jirani ambapo yalitaifishwa na kupigwa mnada;

(ii) Jumla ya dhana haramu zilizokamatwa ni vipande 539,128 pamoja na kamba za kuvutia makokoro mita 511,698 zilikamatwa na kuondolewa ziwani na kisha kuteketezwa kwa moto baada ya kupata kibali cha Mahakama;

(iii) Kiasi cha shilingi bilioni saba zimekusanywa kutokana na mauzo ya samaki, kayabo na mabondo pamoja na faini katika operesheni hii; na

(iv) Viongozi na watumishi wa umma wapatao 35 wamepatikana kujihusisha na uvuvi haramu kwa njia moja au nyingine wakiwemo Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Maafisa Uvuvi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na watendaji wengine wa Serikali. Mfano katika Kisiwa cha Lubiri Wilayani Muleba kilo 65,000 za kayabo zilizokuwa zimevuliwa kwa njia haramu zilikamatwa na huku wakiwemo watendaji na viongozi katika eneo hilo na hawakuwahi kuchukua hatua yoyote. Hii ni kinyume cha Katiba yetu, kinyume cha sheria na Kiapo cha Maadili ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo nilizoziainisha hapo juu kuhusu uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, Wizara yangu imeamua kufanya mambo yafuatayo na mengine yameainishwa katika aya ya 135.

(i) Kuanzisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Rasilimali za Uvuvi hapa nchini;

(ii) Kuweka ulinzi imara wa kudhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato ambayo itapelekea kuongezeka kwa mapato ya Serikali zaidi ya mara 10 yanayokusanywa hivi sasa kutokana na shughuli za uvuvi;

(iii) Kuendelea kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ya kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za uvuvi; na

(iv) Kuishauri *TRA* ifanye makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi waliokwepa kulipa mapato ya Serikali mwaka 2016/2017 ambapo inakadiriwa kuwa mapato ya kiasi cha bilioni 581.5 hayakufanyiwa makadirio na *TRA* na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Operesheni Jodari. Matokeo ya Operesheni Jodari ambao ukaguzi wake ulianza tarehe 25 Septemba, 2017 hadi Novemba, 2017 jumla ya meli 24 zilizopewa leseni ya uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu Tanzania zilikaguliwa. Meli hizo zilishusha tani 12.3 za samaki wasiolengwa ambao ni *by catch* kwenye bandari ya hapa nchini, kuuzwa na kuingiza mapato ya jumla ya shilingi bilioni 41.4. Kati ya meli tano zilizokaguliwa meli mbili zilipatikana na makosa, meli tatu ziliruhusiwa baada ya kuonekana hazina makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya Bwana Buah ya Malaysia ilikamatwa kwa makosa ya kukutwa na mapezi ya mikia ya papa 30 bila miili, yakiwa na uzito wa kilo 90, meli haikuwa na cheti cha usalama wa meli na Nahodha alikutwa na bastola aina ya bereta pamoja na risasi 10 ambapo hakuwa na kibali chochote. Hivyo, iliamuliwa kulipa faini ya Dola za Kimarekani 350,000 sawa na shilingi milioni 770 ambapo alitakiwa kulipa faini hiyo ndani ya siku saba. Hata hivyo, alishindwa kulipa faini hiyo na alipelekwa Mahakama Kuu ya Mtwara na kesi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya *Tai Hong One* ya china ilikutwa makosa ya kuwa na mikia ya papa 44 bila miili, uchafu wa mazingira, mabaharia kupewa chakula kilichokwisha muda wake, kufanya njama za kufaulisha na kutorosha meli zingine zaidi ya tano. Pia meli hii ilifanikiwa kutoroshwa bandarini lakini Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Kuu ilifanikiwa kuwapiga faini ya shilingi bilioni moja kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli 19 zilitoroshwa bila kukaguliwa. Hata hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu iliwatoza faini ya kiasi cha shilingi bilioni moja kwa kila moja kwa hiyo kwa jumla zote ni shilingi bilioni 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, Operesheni *MATT*. Katika Ukanda wa Pwani uvuvi haramu wa kutumia mabomu umeshamiri ambapo mabomu yalikuwa yakilipuliwa kila kona. Kutokana na hali hiyo, rasilimali za uvuvi zilipungua sana katika maeneo hayo ya Pwani, mabomu yakilipuliwa huuwa viumbe wote mayai, vifaranga na mazalia na kuharibu mfumo mzima wa ikolojia na mazingira ya bahari. Bomu moja likilipuliwa lina uwezo wa kuharibu eneo la mzunguko wa mita 15 mpaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki waliovuliwa kwa mabomu asilimia 75 mpaka 90 hupotelea kwenye maji, watu wengi wamepoteza maisha na wengine kupata vilema vya maisha, kutishia usalama wa maisha ya wananchi na watalii kuogopa kuja nchini kwetu kwa kuhofia usalama wao. Tumeendesha operesheni hiyo na vifaa mbalimbali vimekamatwa. Kutokana na operesheni hii milipuko imepungua sasa kwa asilimia 88 hadi Machi, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa ufanisi wa kazi katika Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na maeneo tengefu *MPRU*. Katika mwaka wa 2017/2018, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa utendaji kazi (*performance audit)* wa Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa 2013/2014 hadi 2016/2017. Katika vigezo 24 vya kiukaguzi vilivyowekwa, vyote vilionekana na udhaifu mkubwa wa kiutendaji na kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi huo yalibaini upungufu mbalimbali ukiwemo utoaji wa vibali kiholela, doria hafifu, utaratibu na usimamizi dhaifu wa hifadhi ya bahari na maeneo tengefu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ametoa mapendekezo ya kuboresha utendaji kazi katika kitengo hicho. Katika kutekeleza mapendekezo hayo,

niliamua kuvunja Bodi ya Wadhamini na kumsimamisha kazi Meneja wa Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu huku mapendekezo mengine yakiendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa Jumuiya za Afrika Mashariki kupitia taasisi yetu ya *LVFO* kuendesha operesheni ya kuondoa uvuvi haramu katika Ziwa Viktoria. Katika ombi la Wizara yangu, nchi hizo zimekubaliana kuchangia fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni sita kwa ajili ya nchi hizi kuendesha Operesheni Okoa Sangara katika Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa 2017/2018 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2018/2019. Makusanyo ya maduhuli katika mwaka wa 2017/2018; Wizara kupitia Fungu la 64 ilipangiwa kukusanya Sh.19,700,628,051 hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2018 kiasi cha Sh.21,280,222,364.68 zimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia 108.2 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 16 zilizokusanywa katika kipindi hicho cha Aprili, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018, Wizara kupitia Fungu la 64 inatarajia kukusanya jumla ya Sh.21,534,305,600. Vyanzo vya fedha hizo ni kama ilivyoainishwa katika aya ya 147 katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya vipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2018/2019; Wizara kupitia Fungu la 64 imeendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni, mikakati na programu mbalimbali za kuendesha sekta ya uvuvi kwa lengo la kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinalindwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa njia ambayo ni endelevu kwa faida ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo kama ilivyoainishwa katika aya ya 152 hadi 154.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uvuvi katika bahari kuu; katika mwaka wa 2017/2018, Mamlaka imeboresha ukusanyaji wa takwimu na meli za uvuvi za samaki na

kuanzisha kanzidata za kuendeleza kukusanya takwimu za uvuvi na samaki aina ya jodari na jamii zake unaofanyika katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu *(EEZ).* Aidha, Mamlaka inaendelea kukusanya takwimu za uvuvi wa jodari kwa wavuvi wadogo ambapo jumla ya tani tisa za jodari zilivuliwa katika Wilaya ya Mtwara, Kilwa, Mafia, Kinondoni na Tanga kwa upande wa Tanzania Bara na tani 10 za jodari zilivuliwa upande wa Wete Pemba na Kaskazini A Unguja kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mamlaka iliweka waangalizi wa shughuli za uvuvi katika meli wa tatu (3) katika meli zilizopewa leseni ili kukusanya takwimu na kufanya ulinganifu wa takwimu hizo na zile zinazotumwa na meli hizo ambapo jumla ya tani 2,247.4 za jodari kutoka katika *EEZ* ziliripotiwa kuvuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji wa viumbe kwenye maji; katika mwaka 2017/2018, Wizara ilikuwa na jukumu la kuendelea kutekeleza Mkakati wa Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji kwa kuimarisha na kuendeleza vituo vitano (5) vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Ruhila (Songea), Mwamapuli (Tabora), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi) na Nyamirembe (Chato) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni 10. Aidha, jumla ya vifaranga vya samaki na kambamiti 15,119,757 vimezalishwa na vituo vya Serikali ikilinganishwa na vifaranga 14,119,272 vilivyozalishwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sekta binafsi imezalisha vifaranga 14,924,569 na kusambazwa kwa wafugaji katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani na Tanga. Vilevile, jumla ya vifaranga 12,080,000 vya kambamiti vimezalishwa na Kampuni ya *Alphakrust* (12,000,000) na Kampuni ya *Prawnto Limited* iliyopo Mkuranga (80,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuimarisha na kuendeleza vituo vitano (5) vya ufugaji samaki wa maji baridi kwa ajili ya kuzalisha

vifaranga milioni 10. Pia, itaendeleza vituo vya ufugaji samaki wa maji bahari vya Machui (Tanga) na Mbegani (Pwani) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni tatu. Vilevile, Wizara itawezesha vituo vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Bukoba, Kilimanjaro, Mwanza na Mara kutoa huduma za ugani na itazalisha na kupandikiza vifaranga vya samaki milioni tano katika malambo na mabwawa ya asili 10 na kwenye skimu tano (5) za umwagiliaji miwa na mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uratibu wa Masuala ya Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Uvuvi; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Norway, *NORAD* na *FAO*, mwezi Aprili, 2018 nchi yetu ilipata fursa ya kushiriki katika utafiti wa uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kutumia meli ya Utafiti ya *Dr. Fridtjof Nansen* kutoka Norway. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kupatikana baada ya uchambuzi wa takwimu na yatawezesha kufahamu aina, wingi na mtawanyiko wa samaki ambao utasaidia katika kusimamia uvuvi endelevu na kuvutia fursa za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupitia Benki ya Dunia, nchi yetu imewezeshwa kutekeleza mradi wa *SWIOFish* ambao unalenga kuimarisha usimamizi wa uvuvi katika ngazi ya kijamii; kujenga uwezo wa taasisi katika kusimamia rasilimali za uvuvi; na kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi hususan uvuvi wa Bahari kuu. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba utafiti wa namna hii wa bahari kuu haujawahi kufanyika toka Tanzania ipatikane na dunia iumbwe lakini umefanyika kwa mara ya kwanza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika sekta ya uvuvi; Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya vibali 2,751 vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi vilitolewa na tani 36,063 za samaki na mazao yake na samaki hai wa mapambo 101,110 walisafirishwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 10.52 kama ushuru. Aidha, sekta binafsi zimeendelea kuwekeza katika

viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, kutengeneza zana za uvuvi na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, jumla ya viwanda vikubwa 15 na vidogo 34 vya kuchakata mazao ya uvuvi, vitatu (3) vya kutengeneza vyavu, vitatu (3) vya kutengeneza boti na maghala 56 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi vimeanzishwa. Pia, vibali 199 vya kuingiza samaki kutoka nje ya nchi vilitolewa na tani 22,961 zenye thamani ya shilingi bilioni 56 ziliingizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi wa bahari zimekamilika ambapo Kampuni ya *Sering Ingegneria* ya Italy kwa kushirikiana na Kampuni ya Kitanzania inayoitwa Doch *Tanzania Limited* zimefanikiwa katika hatua za awali za kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa makubaliano unategemewa kuwekwa saini mwisho wa mwezi Mei, 2018 na kazi hii itatekelezwa kwa muda wa miezi nane (8). Hivyo, Tanzania itaanza sasa jukumu la kujenga Bandari ya Uvuvi kama Wabunge walivyoomba kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imewezesha uwekezaji katika ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ambapo jumla ya vizimba 315 vimewekwa katika maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika ikilinganishwa na vizimba 109 mwaka 2016/2017. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni kwamba Shirika la *TAFICO* na lenyewe linafufuliwa, Julai litaanza kazi na taratibu nyingine zitafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa

ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza mifugo na uvuvi. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Israel, Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswis. Nashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa mbalimbali ambazo zimetuunga mkono sana ikiwemo *FAO* na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Makatibu Wakuu, Dkt. Mary Mashingo, Katibu Mkuu - Mifugo; na Dkt. Yohana Budeba, Katibu Mkuu - Uvuvi; pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kutekeleza majukumu kwa bidiii, juhudi na uhodari wa hali ya juu. Endeleeni kuchapa kazi napenda na nafurahishwa sana na jinsi mnavyofanya kazi kwa bidii, *"Leadership is action not position". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati na pekee kwa wananchi wangu wa Kisesa ambao baadhi yao wako hapa, kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa. Nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kipaji nilichopewa na Mwenyezi Mungu kama nilivyowaahidi kuwa 'sitapumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawashukuru sana wafugaji, ambao wengine wako hapa na wavuvi wa nchi

nzima kwa kazi kubwa wanayofanya katika kutekeleza majukumu ya ufugaji na uvuvi na hivyo kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba kusisitiza mambo yafuatayo:-

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imejipanga kuleta mageuzi makubwa katika sekta za mifugo na uvuvi, tumeamua, tumejipanga na hatutashindwa "hakika penye nia pana njia". Hatutakubali kuona rasilimali za uvuvi na mifugo zikitoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulinufaisha Taifa. Aidha, uvuvi na biashara haramu ya mazao ya mifugo na uvuvi havitapata nafasi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia, katika Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tumejipanga kuleta mageuzi makubwa katika sekta za mifugo na uvuvi, tumeamua, tumejipanga na hatutashindwa "hakika penye nia pana njia". Hatutakubali kuona rasilimali za uvuvi na mifugo zikitoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulinufaisha Taifa. Aidha, uvuvi na biashara haramu ya mazao ya mifugo na uvuvi havitapata nafasi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha; mkulima hodari huacha jembe shamba. Nakuja kwenye Bunge lako Tukufu sasa ili waniwahishe mimi na Wizara yangu kwenda kutekeleza majukumu kwa kunipitishia fedha ninazoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Sh.56,455,749,000.00 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Maendeleo ya Mifugo; Wizara inaomba kutumia jumla ya

Sh.35,362,663,000.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 99. Kati ya Fedha hizo; Sh.30,362,663,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.5,000,000,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 64: Maendeleo ya Uvuv; katika mwaka 2018/2019, Wizara inaomba jumla ya Sh.21,093,086,000.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 64. Kati ya fedha hizo; Sh.13,966,406,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.7,126,680,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii, niombe kabisa kwa sababu hapa nimesoma kwa muhtasari iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyoainishwa katika kitabu changu cha hotuba. Pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: *www.mifugouvuvi.go.tz*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa tutaendelea na utaratibu wetu.

Mheshimiwa Waziri kabla hujatoka hapo, hebu tusomee jumla ya shilingi unazoziomba kutoka Bunge ili Taarifa Rasmi ya Bunge ikae vizuri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Sh.56,455,749,000.00 kwa mchanganuo kama ifuatavyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

# HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A: UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99: Maendeleo ya Mifugo na Fungu 64: Maendeleo ya Uvuvi), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa heshima kubwa namshukuru Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais nitatumia uwezo wangu wote kuwa nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali za mifugo na uvuvi zinasimamiwa na kulindwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi yetu kwa umahiri kwa **falsafa ya hapa kazi tu**, Mapinduzi ya viwanda hapa nchini na utekelezaji makini wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa dhati kwa upendo na ushirikiano wanaonipatia ninapotekeleza majukumu yangu.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuhimiza masuala ya utunzaji wa mazingira ambayo ni muhimu katika kuendeleza na kusimamia sekta za mifugo na uvuvi. Nichukue fursa hii kumwahidi Mhe. Makamu wa Rais kuwa nitasimamia kikamilifu sekta za mifugo na uvuvi katika usimamizi na utunzaji wa mazingira ili kuwa na ufugaji na uvuvi endelevu.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**, Mbunge wa Ruangwa kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa ufasaha imetoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi zitakazotekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe na Naibu Spika, kwa kuliongoza kwa busara na hekima Bunge letu Tukufu. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuongoza Bunge letu Tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Mahamoud Hassan Mgimwa**, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake **Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro kwa ushirikiano na ushauri mzuri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mhe. Damas Daniel Ndumbalo, Mbunge wa Songea Mjini, Mhe. Justine Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, Mhe. Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, Mhe. Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha, Mhe. Stephen Lemomo Kirushwa, Mbunge wa Longido kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili wawatumikie wananchi waliowachagua. Pia, nitumie fursa

hii kumpongeza Mhe. Janeth Maurice Massaburi kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge. Waheshimiwa Wabungeni hongereni sana.

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mhe. Mbunge mwenzetu; Hayati Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa jimbo alilokuwa analiwakilisha. Mwenyezi Mungu aweke roho ya marehemu mahali pema peponi Amina. Aidha, naomba pia, nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali na waliogua katika kipindi cha mwaka 2017/2018.

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba niwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kisesa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha hapa Bungeni.

## B: SEKTA YA MIFUGO

### I: HALI YA MIFUGO

10. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 2.8 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2016 na kuchangia asilimia 6.9 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2016. Kulingana na takwimu zilizokokotolewa katika Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania 2017, katika mwaka 2017 idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kufikia ng'ombe milioni 30.5, mbuzi milioni 18.8 na kondoo milioni 5.3, kuku wa asili milioni 38.2, kuku wa kisasa milioni 36.6, nguruwe milioni 1.9 na punda wapatao 595,160 (Chanzo: Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2017).

11. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 uzalishaji wa maziwa umefikia lita bilioni

2.4 ukilinganishwa na lita bilioni 2.1 zilizozalishwa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 usindikaji wa maziwa umeongezeka na kufikia lita milioni 56.2 ikilinganishwa na maziwa lita milioni 40.1 zilizoshindikwa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2018. Pia, katika kipindi hicho, jumla ya mitamba 590 ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO). Vilevile, Sekta Binafsi ilizalisha na kuuza kwa wafugaji wadogo nchini jumla ya mitamba 13,145.

12. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kufikia tani 679,992 ikilinganishwa tani 558,164 zilizozalishwa katika kipindi Julai, 2016 hadi Aprili, 2017. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, jumla ya tani 2,608.93 za nyama (mbuzi tani 1,248.14, ng'ombe tani 1,030.79, kondoo tani 50 na punda tani 280) ziliuzwa nje ya nchi na jumla ya tani 1,224.55 za nyama (nguruwe tani 506.05 nguruwe, ng'ombe tani 711.03 na kondoo tani 7.47) ziliingizwa nchini. Pia, uzalishaji wa mayai uliongezeka nchini kutoka mayai bilioni 2.76 mwaka 2016/2017 hadi bilioni 3.16 mwaka 2017/2018.

13. **Mheshimiwa Spika,** ulaji wa nyama kwa mwaka 2017/2018 ni wastani wa kilo 15, lita 47 za maziwa na mayai 106 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ambavyo ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, vipande vya ngozi zilizosindikwa hatua ya *wet blue* vimepungua kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,215,030 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7 mwaka 2016/2017 hadi vipande 292,394 vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.255 na viliuzwa katika nchi za China, India, Pakistani, Italia, Uturuki, Ghana, Nigeria, Ethiopia, Thailand, Oman - UAE na Kenya**.** Pia, idadi ya ngozi ghafi za ng'ombe vipande 482,752 vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.176 vimeuzwa nchi za China,

Nigeria, Ghana, Misri, Pakistan, India, Malawi na Italia vimeongezeka ikilinganishwa na vipande 241,773 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.89 vilivyouzwa mwaka 2016/2017.

15. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na hali halisi iliyoelezwa hapo juu, sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; upotevu wa mapato unaotokana na biashara ya mifugo na mazao yake kufanyika kinyume na sheria na taratibu, migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uvamizi wa maeneo ya minada ya mifugo, ranchi za Taifa, mashamba ya mifugo pamoja na vituo vya kupumzishia mifugo, uingizwaji holela wa mazao ya mifugo toka nje ya nchi,Tanzania kugeuzwa kuwa maeneo ya kuchungia mifugo ya nchi jirani pia uuzaji wa madawa bandia ya mifugo.

## II: MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2018/2019

### Makusanyo ya Maduhuli

16. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Fungu 99 (Maendeleo ya Mifugo) ilipangiwa kukusanya kiasi cha shilingi 16,404,739,500.00. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2018 kiasi cha shilingi 13,677,333,381.24 kimekusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 83.4, ikilinganishwa na shilingi 10,952,827,50 zilizokusanywa mwaka 2016/2017 kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi tarehe 30 Aprili, 2017.

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli mwaka 2018/2019

17. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 99 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 18,467,945,100.00. Vyanzo vya fedha hizo vimetokana na marekebisho katika ada, tozo na kodi mbalimbali zinazotozwa katika sekta ya mifugo. Vyanzo vikuu vya fedha

hizo ni pamoja na leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi (export duty license fees); Ada ya kutoa vibali vya kusafirisha wanyama, nyama, ngozi na mazao mengine nje ya nchi; Ada ya huduma ya vibali vya kusafirisha mifugo ndani ya nchi (Movement Permits); Ushuru wa soko (Market fee); Mauzo ya chanjo za mifugo, mifugo, mitamba, mazao ya mifugo; Kodi ya pango la nyumba za Serikali na mauzo ya zabuni Tender documents) mbalimbali.

**Fedha Zilizoidhinishwa**

18. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi 35,645,980,426.30. Kati ya Fedha hizo, shilingi 31,645,980,426.30 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 4,000,000,000.00 ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida**

19. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Fungu 99 lilitengewa jumla ya shilingi 31,645,980,426.30 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi, shilingi 18,232,921,600.00 ni mishahara na shilingi 13,413,058,826.3 ni Matumizi Mengine. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, jumla ya shilingi 26,214,758,881.87 zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia 82.84 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 14,387,998,700.00 ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na shilingi 11,826,760,181.87 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

20. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya shilingi 4,000,000,000.00 za matumizi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Mpango wa Bajeti ya Maendeleo kwa Fungu 99 ulihusisha utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 hakuna fedha iliyokuwa imetolewa.

## III: MAENEO YA KIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA KATIKA MPANGO WA 2018/2019

21. **Mheshimiwa Spika,** maeneo ya kipaumbele katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na katika mpango wa 2018/2019 kupitia Idara Kuu ya Mifugo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kutenga maeneo ya malisho;
(ii) Kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo;
(iii) Kuimarisha huduma za utafiti, ugani na mafunzo ya uzalishaji bora wa mifugo ili kupata bidhaa za mifugo zenye ubora (nyama, maziwa na ngozi);
(iv) Kuimarisha vituo vya uhimilishaji Kitaifa na Kikanda;
(v) Kuboresha masoko na miundombinu ya uzalishaji mifugo na kuongeza thamani bidhaa za mifugo;
(vi) Kuimarisha tasnia ya nyama na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa;
(vii) Kuimarisha tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo; na
(viii) Kufanya sensa ya mifugo
(ix) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mazao ya mifugo na pembejeo pamoja na kuvifufua viwanda vya zamani.

## IV: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SEKTA YA MIFUGO KATIKA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### SERA, SHERIA, MIKAKATI NA PROGRAMU

22. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo wa mwaka 2011. Jumla ya wadau 2,600 walipata elimu hiyo kupitia Maonyesho ya Sabasaba, Nanenane na

Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imesambaza kwa wadau nakala 350 za Sera ya Taifa ya Mifugo na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Pia, Wizara ilisambaza kwa wadau nakala za vijitabu 100 vya Fursa za Uwekezaji katika sekta ya mifugo.

23. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kupitia sheria za sekta ya mifugo ili ziendane na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka na kuboresha mazingira ya kibiashara. Aidha, Wizara imeandaa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Mbari Bora za Wanyama (Animal Breeding Act) na kufanya Mapitio ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya mwaka 2010. Vilevile, kanuni zifuatazo zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni:

(i) Kanuni za Fedha na Utumishi za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, 2017;

(ii) Kanuni tano (5) za Tasnia ya Mifugo zinazohusiana na tozo;

(iii) Kanuni tatu (3) chini ya Sheria ya Nyama tayari zimeshafanyiwa mapitio ya kina na upekuzi (*scrutinization and vetting;)*

(iv) Kanuni mbili (2) za Vyakula vya Wanyama (Import and Export of Animal Feed Resources, Regulations na Detention, Treatment, Disposal and Distruction of Animal Feed Resources, Regulations); na

(v) Rasimu mpya nne (4) za kanuni zimeandaliwa ambazo ni: *Packing, Branding, Labeling and Sealing of Animal Feed Resources, Regulations*; *Animal Feed Resources Product Registration Regulations*; *Fees and Charges of Animal Feed Resources, Regulations*; na *Varietal Purity Certification of Pasture Seeds, Regulations*.

Katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea kukamilisha mapitio ya Sheria na Kanuni zote za mifugo kwa lengo la kuziboresha ili ziweze kuboresha huduma za biashara za mifugo na mazao yake.

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo pamoja na wadau wengine imeanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini Awamu ya Pili (ASDP II). Lengo la ASDP II ni kufanya mageuzi ya sekta ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya uhakika wa chakula, kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na Taifa kwa ujumla. Aidha, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza kutekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan - TLMP) wa mwaka 2017 ambao unatekelezwa kupitia Programu pana ya sekta ya kilimo ASDP II. Mpango huu unaolenga kuboresha sekta ya mifugo inayotegemewa na watanzania zaidi ya milioni 50 na itatekelezwa kwa miaka 15 ambapo itatekelezwa kwa awamu tatu za miaka mitano na itawezesha kuwaongoza wadau wa sekta ya mifugo kuhusu maeneo ya uwekezaji.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuendeleza sekta ya mifugo kupitia Pogramu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (Agricultural Sector Development Programme - ASDP II). Utekelezaji wa miradi hii utaimarisha usimamizi wa rasilimali za mifugo kwa maendeleo ya sekta. Pia, Wizara itafanya mapitio ya Sera na Miongozo mbalimbali ya sekta za mifugo ili kuboresha mazingira ya biashara na kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan - TLMP) kupitia mfumo wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili (Agriculture Sector Development Programme - ASDP II).

## UZALISHAJI NA BIASHARA YA MIFUGO NA MAZAO YAKE

26. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, vituo 184 vya kukusanya maziwa vimeanzishwa kwenye maeneo yenye mfumo wa masoko unaounganisha viwanda vya kusindika maziwa. Kutokana na hali hiyo, usindikaji wa maziwa katika viwanda vya

kusindika maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 40.1 mwaka 2016/2017 na kufikia lita milioni 56.2 mwaka 2017/ 2018. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa kutoka viwanda 65 vilivyokuwepo mwaka 2016/2017 hadi viwanda 76 vinavyofanya kazi kufikia mwezi Aprili 2018 (Kiambatisho Na. 1).

Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kwa lengo la kuimarisha uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa kufikia lita 200,000 kutoka lita 154,000 kwa siku.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imeendelea kuratibu Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Njombe na Tanga katika shule 40, ambapo takriban wanafunzi 34,561 walikunywa jumla ya lita za maziwa 631,860. Mikoa iliyohusika ni Arusha (Arusha mjini) Shule 3 wanafuzi 3,047 ambao walikunywa lita 60,940 za maziwa; mikoa ya Mbeya na Njombe shule 15 ambapo wanafunzi 10,000 walikunywa lita 200,305.5 za maziwa; na mkoa wa Tanga (Tanga Mjini) Shule 4 ambapo wanafunzi 3,606 walikunywa lita 57,600 za maziwa. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wa mifugo itaendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa katika shule za msingi katika Halmshauri 50 nchini.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea kuboresha mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill, Kitulo, Ngerengere, Mabuki na Nangaramo kwa kuyapatia vitendea kazi. Katika kipindi hiki jumla ya mitamba 590 ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na NARCO kama ilivyoanishwa kwenye Kiambatisho Na. 2 ikilinganishwa na mitamba 634 iliyozalishwa na kusambazwa katika mwaka 2016/2017. Kupungua kwa uzalishaji katika mashamba ya Serikali na NARCO kumeendelea kutokana na ubinafsishaji uliofanywa katika ranchi za NARCO ambapo mitamba mingi ya maziwa hivi sasa inazalishwa na ranchi (vitalu) za NARCO zilizobinafsishwa na wafugaji wadogo wa ngombe wa

maziwa. Aidha, Sekta Binafsi ilizalisha na kusambaza kwa wafugaji wadogo nchini jumla ya mitamba 13,145 ikilinganishwa na mitamba 11,454 mwaka 2016/2017.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaimarisha mashamba matano (5) ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill, Kitulo, Ngerengere, Nangaramo na Mabuki kwa kununua mitamba 1,000 aina ya boran, madume bora aina ya Friesian 100 na aina ya boran 100 ili kuongeza idadi ya ng'ombe wazazi na kuboresha malisho na miundombinu ya maji. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuongeza uzalishaji wa mitamba na kusambaza kwa wafugaji. Pia, Wizara imeanzisha Programu ya Uzalishaji wa Mitamba 1,000,000 kwa mwaka kutokana na makundi ya ng'ombe wa asili kwa kufanya uhimilishaji (Artificial Insermination -AI) katika ng'ombe milioni 3.0 (massive AI) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji maziwa ili kukidhi mahitaji. Programu hii ni mojawapo ya kazi zilizoainishwa kutekelezwa kupitia Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania ambao umeainisha kuwa ifikapo mwaka 2021/2022 idadi ya ng'ombe wa maziwa wataongezeka mara 3.8 kutoka 789,000 mpaka 2,985,000.

30. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Mradi wa Ushirikano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kuboresha Uhimilishaji (Public Private Partinership for Artificial Insermination Delivery - PAID) kwa ufadhili wa taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation imeendelea kuimarisha Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (NAIC) Usa River - Arusha kwa kununua madume bora ya mbegu 11 kutoka Afrika Kusini (5) na New Zealand (6) na kununua vifaa vya maabara, kununua *bailer*, mtungi wa lita 2,000 wa kusafirishia kimiminika baridi cha nitrogeni, na mitungi mitano (5) ya lita 50 kila moja ya kuhifadhia mbegu pamoja na kimiminika cha nitrojeni. Gharama ya mradi huu ni Dola za Kimarekani 8,365,494 kwa miaka mitano (5) kuanzia mwezi Mei, 2016 hadi mwezi Oktoba, 2020. Vilevile, jumla ya dozi 140,000 zilizalishwa ikilinganishwa na dozi 100,000 mwaka 2016/2017.

31. **Mheshimiwa Spika**, vituo vya kanda vya uhimilishaji vimeendelea kuimarishwa, ambapo mtambo wa kuzalisha kimiminika baridi cha nitrojeni cha Kanda ya Mashariki Kibaha umefanyiwa matengenezo. Ng'ombe waliohimilishwa wameongezeka kutoka 457,557 mwaka 2016/2017 hadi ng'ombe 508,200 mwaka 2017/2018. Wataalamu 204 wa uhimilishaji kutoka maeneo mbalimbali nchini walijengewa uwezo kwa kupewa mafunzo. Serikali imetoa mafunzo ya unenepeshaji wa mifugo kwa wafugaji 2,199 kutoka katika Halmashauri za Wilaya 17 katika mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Mwanza, Singida na Shinyanga.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC Usa River, Arusha kwa kununua vitendea kazi kama vile *semen analyzer* (CASA), minibus, *disc plough, pump* ya umwagiliaji, vifaa vya ofisi, kukarabati mabanda ya madume na kuendeleza malisho. Pia, Wizara itajenga kituo cha NAIC Sao Hill Iringa, itanunua trekta na vifaa vyake na kutoa mafunzo kwa wahimilishaji 200 kutoka mikoa 10 ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Katavi na Geita. Aidha, itaimarisha vituo sita (6) vya Kanda vya uhimilishaji vya Dodoma, Kibaha, Lindi, Mbeya, Mpanda na Mwanza kwa kufanya matengenezo ya mitambo ya kuzalisha kimiminika baridi cha Naitrojeni, pamoja na vituo vidogo vya uhimilishaji vya Tanga na Tabora. Pia, itatoa mafunzo ya awali ya uhimilishaji kwa washiriki 50, mafunzo rejea kwa wahimilishaji 50, kutoa mafunzo kwa wataalam watano (5) wa kukarabati mitambo na kuandaa mwongozo wa matumizi ya huduma ya uhimilishaji.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, Mradi wa Uendelezaji wa Sekta ya Maziwa Afrika Mashariki na Kati (Eastern Africa Dairy Development - EADD II) kupitia taasisi ya Heifer International umetoa mafunzo kwa wafugaji 25,659 (wanaume 14,159 na wanawake 11,500) kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa katika nyanja za uzalishaji mifugo, ulishaji, tiba na afya ya mifugo. Wafugaji hao walitoka katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe. Aidha, Mradi huu umeunda

jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi 37 na kuunda vitovu vya biashara ya maziwa (Dairy Hubs) ambapo vimeweza kuwa na mapato ya takriban shilingi bilioni 2 kwa mwaka. Aidha, Heifer International imewawezesha wafugaji kuanzisha vituo 11 vya kisasa vya kukusanya maziwa (Milk Collection Centres) vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.4. Fedha hizi zilizotolewa kama ruzuku kwa wafugaji zitagharamia ununuzi wa matenki 11 ya maziwa, jenereta 11, vyombo na vifaa vya kusafirishia maziwa na ujenzi wa vituo. Ununuzi wa vifaa hivi umeshafanyika na matenki yataingia nchini tarehe 20 Mei, 2018. Aidha, ili kupanua wigo wa masoko ya maziwa ya wafugaji, EADD inashiriki katika kukiboresha Kiwanda cha Wafugaji Njombe kuwa cha kisasa na kukipanua kutoka uwezo wa kusindika lita 6,000 hadi 20,000 kwa siku. Gharama zitakazotumika ni takriban shilingi bilioni 1.6, fedha zote hizi ni msaada kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha Njombe na vituo vya kukusanyia maziwa.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, mradi wa EADD II umeanzisha program ya unywaji maziwa shuleni kwa lengo la kuwafikia wanafunzi wa shule za awali na msingi 10,000 ambao watakunywa maziwa mls 200 kwa kila mtoto kwa siku za shule. Hadi kufikia Machi 2018, wanafunzi wapatao 11,398 wamenufaika na mradi huu kwa siku 4 kati ya siku 5 za shule katika shule 17 za wilaya za Rungwe (shule 6; wanafunzi 4,874), Njombe (shule 8; wanafunzi 4,522) na Wanging'ombe (shule 3; wanafunzi 2,002). Aidha, kutokana na utekelezaji wa mradi huu, masoko ya maziwa ghafi yameongezeka ambapo kwa kiwanda cha Njombe kutoka lita 3,200 hadi kufikia lita 5,600 kwa siku; udahili, mahudhurio na umakini wa kujifunza miongoni mwa wanafunzi katika shule husika umeongezeka.

35. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Heifer International kupitia mradi wa EADD II inatarajia kupanua wigo wa mradi huu ili kufikia maeneo mengi ya mradi kadiri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, EADD II itaendelea kushirikiana na wadau wa Sekta Binafsi na Serikali kuwasaidia wafugaji kupanua wigo wa masoko ya maziwa na ujenzi wa viwanda vya maziwa. Vilevile, itaendelea

kushirikiana na Serikali, wafugaji na wadau wengine katika kuanzisha vituo vya kisasa vya kukusanya maziwa (Milk Collection Centres) ili wafugaji wengi zaidi waweze kuvifikia kwa karibu zaidi. Pia, mradi utaendelea na programu ya unywaji wa maziwa shuleni kwa kuwafikia wanafunzi wengi zaidi katika maeneo ya mradi.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 558,164 mwaka 2016/17 hadi kufikia tani 679,992 mwaka 2017/2018 (Kiambatisho Na. 3). Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha na kuboresha mfumo wa unenepeshaji mifugo kwa kulisha mifugo ya nyama yenye umri mdogo chakula chenye lishe ya protini na nishati nyingi ili wakue haraka na kufikia uzito wa kuchinjwa ndani ya miezi 3 hadi 4 ili kutoa nyama nyingi na bora inayokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kwa asilimia 14 kutoka 280,000 mwaka 2016/2017 na kufikia ng'ombe 320,000 mwaka 2017/2018. Serikali imetoa mafunzo ya unenepeshaji wa mifugo kwa wafugaji 2,199 kutoka katika Halmashauri za Wilaya 17. Pia, uzalishaji wa mayai uliongezeka nchini kutoka mayai bilioni 2.76 mwaka 2016/2017 hadi bilioni 3.16 mwaka 2017/2018.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa nyama na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji wa mifugo ili kufikia ng'ombe 450,000 kwa mwaka.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwezeshaji imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya ng'ombe 1,614,321, mbuzi 1,340,222 na kondoo 315,636 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.1 waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe 1,618,047 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.34, mbuzi 1,278,182 na kondoo 278,595 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.02 mwaka 2016/2017. Pia, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kufuatilia

biashara ya nyama ndani na nje ya nchi ambapo hadi kufikia Aprili, 2018 jumla ya tani 2,608.93 za nyama (tani 1,248.14 za nyama ya mbuzi, tani 1,030.79 za nyama ya ng'ombe, tani 50 za nyama ya kondoo na tani 280 za nyama ya punda) zenye thamani ya Dola za Kimarekani 5,679,217.28 ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Dubai, Iraq, Oman, Comoro, Hongkong na Vietnam ikiwa ni pungufu kwa asilimia 17.5 ikilinganishwa na kiasi cha tani 3,162.65 zilizouzwa nje ya nchi katika mwaka 2016/2017. Upungufu huo umetokana na kuzuiliwa kwa muda kwa biashara ya uuzaji wa nyama ya Punda nje ya nchi.

38. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, jumla ya tani 1,401.96 za nyama (tani 548.87 za nyama ya nguruwe, tani 843.02 za nyama ya ng'ombe na tani 10.07 za nyama ya kondoo) zenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,368,858.07 ziliingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini, Ireland, Ubelgiji na Uingereza ikiwa ni ongezeko la asilimia 57.4 ikilinganishwa na kiasi cha tani 890.66 zilizoingizwa ndani ya nchi mwaka 2016/2017. Ongezeko hili limetokana na kuimarishwa kwa ushirikiano baina ya Wizara, Bodi ya Nyama, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), TFDA katika kusimamia na kudhibiti mianya ya uingizaji nyama na bidhaa za nyama kwa njia zisizo rasmi na hivyo, kupata takwimu sahihi za nyama zinazoingia nchini.

Katika kukabiliana na hali hii Serikali imejipanga kuboresha mifugo ili kuzalisha nyama na mazao yake yatakayokidhi soko lenye mahitaji maalum ya walaji (niche market) kama vile kwenye migodi ikiwa ni pamoja kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mifugo bora na ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika nyama. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kufuatilia biashara ya nyama ndani na nje ya nchi.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuchinja jumla ya ng'ombe 2,488 walionenepeshwa kwa thamani ya shilingi bilioni 2.24. Aidha, NARCO imezalisha na kukuza ndama 4,269

kutokana na ng'ombe wazazi 5,242. Pia, jumla ya ng'ombe 1,412 wenye thamani ya shilingi milioni 800 waliuzwa katika soko la ndani. Vilevile, NARCO kwa kutumia mapato yake imenunua ng'ombe 1,175 wenye thamani ya shilingi milioni 508 kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kuendeleza Programu ya Unenepeshaji. Vilevile, NARCO imetoa ushauri wa ufugaji bora kwa wawekezaji katika ranchi ndogo waliowekeza jumla ya ng'ombe 87,601, mbuzi 12,432 na kondoo 9,537.

40. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia NARCO kwa kushirikiana na wadau wengine itakamilisha mipango ya kibiashara (business plans) katika ranchi zake pamoja na kutekeleza Mpango Kazi ulioandaliwa kutokana na tathmini iliyofanyika ya muundo, uendeshaji, uzalishaji wa mapato, matumizi na usimamizi wa rasilimali wa Kampuni ya Ranchi za Taifa, Mashamba ya Mifugo ya Wizara na Vituo vya Kupumzisha Mifugo kwa majukumu yaliyoainishwa hapo juu. Aidha, NARCO inatarajia kuzalisha jumla ya ndama 4,356 kutokana na ng'ombe wazazi 5,414. Pia, NARCO inatarajia kununua ng'ombe 1,115 kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato na itauza ng'ombe 3,298 walionenepeshwa wanaotarajiwa kufikia thamani ya takriban shillingi bilioni 2.3. Vilevile, NARCO itanunua ng'ombe wazazi 100 na itaendelea na ujenzi wa Machinjio ya Ruvu, kuongeza idadi ya mifugo na kujenga viwanda kwenye eneo la Ranchi ya Ruvu kwa kutengeneza bidhaa za ngozi kwa ajili ya kuongeza ajira ya wanawake na vijana kutokana na mkopo wa riba nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Ushirikiano wa Kiuchumi kwa Serikali ya Korea (EDCF).

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa kuku kibiashara ili kuongeza mapato ya kaya pamoja na Taifa kwa ujumla. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya vifaranga 85,565 vya kuku wa nyama na mayai ya kutotolesha vifaranga 46,080 vya kuku chotara aina ya *SASSO* na vifaranga 120,000 vya kuku wa nyama viliuzwa nje katika nchi za Kenya, Comoro, Zanzibar na Uganda. Aidha, jumla ya vifaranga vya

kuku wazazi 86,837 wa nyama, 4,480, 110 wa mayai na 6,216 wa chotara wa aina ya *Kuroiler* pamoja na mayai ya kutotolesha vifaranga vya kuku wazazi 86,837 wa nyama, 4,480 wa mayai na 41,400 chotara wa *kuroiler* waliingizwa nchini kutoka katika nchi za Kenya, Malawi, Zambia, Uingereza, Uholanzi, Mauritius na India ili kuongeza uzalishaji wa mayai ya kutotolesha vifaranga wa biashara kutoka kwenye mashamba ya kuku wazazi ikilinganishwa na mayai 2,825,480 ya kutotolesha vifaranga yaliyoingizwa nchini kutoka nje mwaka 2016/2017.

42. **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mayai katika mwaka 2016/2017 umeongezeka kutoka mayai bilioni 2.76 hadi mayai bilioni 3.16 mwaka 2017/2018. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali imesajiri vituo saba (7) vya kutotolesha vifaranga vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga bora 350,000 vya kuku wa nyama, 29,000 vya kuku wa mayai, 18,200 vya kuku wa asili na 86,000 vya kuku aina ya *Kuroiler* kila wiki. Aidha, mashamba ya kuku wazazi saba (7) yenye uwezo wa kutunza idadi ya kuku wazazi 149,121 yameanzishwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Pwani.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) itaendelea kutekeleza Mradi wa Kuboresha Mbari za Kuku wa Asili Afrika (African Chicken Genetic Gains - ACGG) kwa ufadhili Taasisi ya Bill & Mellinda Gates Foundation ambao unatekelezwa kwa pamoja na nchi tatu za Ethiopia, Tanzania na Nigeria kwa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2015 hadi 2019. Lengo kuu la mradi ni kuongeza tija katika uzalishaji wa kuku wa asili kwa ushirikishwaji wa sekta ya umma na sekta binafsi (Public-Private Partnerships), hivyo kuongeza upatikanaji wa kuku bora na kuongeza tija; kipato na uhakika wa lishe. Mradi huu pia unatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Kimataifa (ILRI) na wadau wengine. Aidha, mradi wa kusambaza vijijini vifaranga aina ya *Kuroiler* katika mikoa 25 nchini utaboreshwa. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha

sekta binafsi kuongeza uzalishaji wa vifaranga ili kukidhi uzalishaji.

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji, usindikaji na biashara ya nguruwe hai. Biashara ya nyama ya nguruwe imeongezeka kutoka tani 18,899 mwaka 2016/2017 hadi tani 37,191 katika mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo limetokana na kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever) katika mikoa ya Rukwa, Morogoro, Mbeya, Songwe na Iringa na wafugaji kuanza kuwekeza tena. Aidha, Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini (Tanzania Association of Pig Farmers -TAPIFA) kimeendelea kukua.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuimarisha shamba lake la nguruwe la Ngerengere ili liweze kuendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na biashara ya nguruwe. Pia, Wizara itahimiza sekta binafsi kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa nguruwe, nyama na mazao yake. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini TAPIFA kwa lengo la kuboresha kosaafu za nguruwe nchini.

46. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika ngozi ambapo hadi sasa kuna viwanda sita (6) ambavyo ni: (i) Lake Trading Co. Ltd. (Kibaha), (ii) Himo Tanners and Planters (Moshi Vijijini), (iii) SAK International Ltd (Arusha), (iv) ACE Leather (T) Ltd. (Morogoro), (v) Salex Tannery Ltd. (Arusha Jiji); na (vi) Moshi Leather Industries Ltd. (Moshi). Viwanda hivi kwa sasa vina uwezo wa kusindika ngozi jumla ya futi za mraba 71,520,000 za ng'ombe (2,634,008) na mbuzi (520,000) kama inavyoonekana katika (Kiambatisho Na. 4.) Katika mwaka 2016/2017, vipande vya ngozi zilizosindikwa hatua ya *wet blue* vimepungua kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,215,030 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7

hadi vipande 292,394 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 3.255 mwaka 2017/18 vilivyouzwa nchi za China, India, Pakistan, Italia, Uturuki, Ghana, Nigeria, Ethiopia, Thailand, Oman – UAE na Kenya.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, idadi ya ngozi ghafi za ng'ombe vipande 482,752 vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.176 vimeuzwa nchi za China, Nigeria, Ghana, Misri, Pakistan, India, Malawi na Italia vimeongezeka ikilinganishwa na vipande 241,773 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.89 vilivyouzwa mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo limetokana na kupanuka kwa soko la ngozi ghafi zilizouzwa katika nchi za Nigeria na Ghana. Hata hivyo, vipande vya ngozi za mbuzi/kondoo 1,009,101 vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.76 vilivyouzwa nchi za China, Falme za Nchi za Kiarabu, Pakistani, Nigeria na Ethiopia zilizosindikwa hadi hatua ya wet blue, vimepungua ikilinganishwa na vipande 1,124,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.2 katika mwaka 2016/2017. Upungufu huo umetokana na kudorora kwa biashara ya ngozi katika soko la kimataifa na hivyo kusababisha kuendelea kurundikana kwa ngozi ghafi na wet blue zilizopo viwandani kutokana na ufinyu wa soko la ndani. Vilevile jumla ya vipande 43,000 vya ngozi za ng'ombe vyenye thamani ya shilingi 1,820,939.00 vilivyosindikwa hadi hatua ya mwisho (finished leather) vimeuzwa nchi za Pakistani, China na India. Aidha, jumla ya vipande vya ngozi za punda 9,933 vyenye thamani shilingi 112,758,508.72 vimeuzwa nchi za Vietnam na China.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Viwanda Biashara na Uwekezaji, na Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi (DTI - Mwanza) iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy 2016 - 2020). Jumla ya wataalam 17 wa ngozi kutoka mikoa ya Arusha, Geita, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Mwanza, Njombe na Simiyu walipatiwa mafunzo juu ya Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria ya Ngozi, Kanuni na Mkakati wa kuendeleza zao la ngozi. Aidha, vikao viwili (2)

vya Kamati za Kisheria za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo - Kamati ya Kitaifa ya Ushauri na Kamati ya Usimamizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo vilifanyika.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kutoa mafunzo kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi nchini katika Halmashauri za Wilaya 15. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Wizara ya Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi (DTI - Mwanza) itafuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy 2016 - 2020). Pia, Wizara itawajengea uwezo wakaguzi wa ngozi (Hides, Skins and leather Inspectors) wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini 187 na kuwaelimisha wafugaji, wazalishaji, wasambazaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi kupitia vipindi 12 vya radio na luninga.

## TATHMINI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

### Biashara ya Mazao ya Mifugo na Pembejeo

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kubaini changamoto zinazoifanya Sekta ya Mifugo kukusanya kiasi kidogo cha mapato ambapo katika mwaka 2016/2017, Wizara ilikusanya shilingi bilioni 10.95 tu na kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa, katika mwaka wa fedha 2017/ 2018, Wizara yangu iliamua kuunda timu ndogo ya wataalam kufanya tathmini ya biashara ya mazao na pembejeo za mifugo hapa nchini. Timu hii ilifanya kazi na kuwasilisha taarifa ambayo imebaini uwepo wa mianya ya utoroshaji wa mazao ya mifugo, ushindani usio sawa wa bidhaa na mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, kusuasua kwa uwekezaji katika sekta na viwanda hali ambayo imesababisha baadhi ya viwanda vya ndani kutelekezwa na vingine kubadilishwa matumizi. Pia, upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali na wimbi kubwa la uingizaji wa bidhaa na mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi bila kujali mahitaji halisi ya nchi.

Aidha, baadhi ya mambo mengine yaliyoibuliwa na kamati ya tathmini ni kama ifuatavyo:-

(i) Uwepo kwa utoroshwaji mkubwa wa mifugo kwenda nje ya nchi ambapo zaidi ya ng'ombe 1,614,035 sawa na nyama takribani kilo 201,754,375 zinapotea kila mwaka kutokana na ng'ombe hawa kutoroshwa ambao wangeliingizia Taifa takribani shilingi 32,280,700,000 kutokana na ushuru kwa ng'ombe na nyama tu pamoja na shilingi 24,210,525,000 kutokana na kodi ya mapato ambayo inafanya upotevu wa mapato kufikia takribani shilingi bilioni 56.49;

(ii) Kiasi cha nyama kilichoombewa vibali kutoka Bodi ya Nyama (TMB), TFDA na Idara ya Huduma za Mifugo (Directorate of Veterinary Services - DVS) ni chini ya kile kilichoingizwa nchini kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mfano, katika mwaka 2017 nyama iliyoingizwa nchini kwa mujibu wa TRA ni tani 3,700 wakati takwimu za DVS ni tani 700, TMB tani 1,700 na TFDA tani 2,500, hivyo kati ya DVS na TRA kuna tofauti ya tani 3,000 zenye thamani ya shilingi bilioni moja. Tofauti hii inatokana na baadhi ya waagizaji wa nyama kulipia vibali vya kilo chache ikilinganishwa na kiasi halisi cha nyama kilichoingizwa na hivyo kuikosesha Serikali mapato;

(iii) Uuzaji holela wa maziwa ghafi bila usajili wala vibali vyovyote kumepelekea Serikali kupoteza mapato mengi. Aidha, maziwa lita bilioni 2.03 huuzwa katika soko lisilo rasmi na Serikali imekuwa ikipoteza takribani shilingi bilioni 120 kila mwaka;

(iv) Kupishana kwa taarifa za TRA na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) ambapo katika mwaka 2016/2017, maziwa yaliyoingia nchini kwa takwimu za TDB ni kilo 17,025,921.91 wakati takwimu za TRA zinaonyesha kilo 9,286,307. Hii ina maana kuwa kiasi cha kilo 7,739,614.94 zimepita bila kulipiwa kodi TRA;

(v) Zaidi ya asilimi 20 ya maziwa yaliyopo sokoni huingia kwa njia za magendo kupitia bandari bubu na mipakani;

(vi) Uuzaji na usafirishaji holela wa ngozi ndani na nje ya nchi na kupelekea Serikali kukosa mapato kiasi cha shilingi bilioni 87.46 kwa mwaka;

(vii) Uingizaji mkubwa wa bidhaa za ngozi kuzidi mahitaji ya bidhaa hizo na hivyo kutumia fedha nyingi za kigeni ambapo mwaka 2017 kiasi cha Dola za Kimarekani 57,216,732 sawa na shilingi bilioni 128.7 zilitumika kuagiza bidhaa za ngozi;

(viii) Kuwepo kwa dawa bandia za mifugo na zisizokidhi viwango ambazo zimeendelea kuathiri mifugo kutokana na matumizi ya dawa hizo na hivyo kuathiri ukuaji na wakati mwingine vifo kwa mifugo na binadamu; na

(ix) Uwepo wa dawa zilizoingizwa nchini bila kufuata taratibu ambapo mikoa maarufu kwa uingizaji wa dawa na chanjo kwa njia zisizohalali ni pamoja na Arusha, Mwanza na Mbeya.

**Kutokana na utoroshaji mkubwa wa rasilimali za mifugo na biashara za magendo ya mazao ya mifugo Serikali inapoteza zaidi ya shilingi bilioni 263.95 kwa mwaka**.

51. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo Wizara yangu imeamua kufanya operesheni ambayo itadumu kwa kipindi cha miezi miwili (siku 60). Malengo ya operesheni ni kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali unaosababishwa na utoroshaji wa rasilimali za mifugo nje ya nchi, uingizaji wa bidhaa za mifugo bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo na biashara holela ya mazao ya mifugo na pembejeo (operesheni hii inaitwa "Operesheni Nzagamba").

**Operesheni Nzagamba**

52. **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za mifugo na mazao yake, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali zikiwemo Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Ofisi ya Rais-Usalama wa Taifa, Baraza

la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Jeshi la Polisi zimeendesha Operesheni Nzagamba kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato na usimamizi wa biashara ya mifugo na mazao yake pamoja na pembejeo za mifugo. Awamu ya kwanza ya operesheni hii inatekelezwa katika maeneo mbalimbali kuanzia mwezi Machi, 2018 na itamalizika mwezi Juni, 2018 ambapo katika awamu ya kwanza imebainika kuwa mifugo mingi, hususan ng'ombe, kondoo, mbuzi na punda inatoroshwa na kuuzwa nje ya nchi bila kibali wala kulipia ushuru wa Serikali hivyo kuikosesha Serikali mapato. Aidha, imebainika kuwa maduka mengi ya pembejeo za mifugo yanauza dawa bandia na zilizopita muda wa matumizi yake. Vilevile, baadhi ya viwanda vya vyakula vya mifugo hutengeneza vyakula vilivyo chini ya viwango. Hadi kufikia tarehe 08 mwezi Mei**,** 2018 jumla ya shilingi 1,992,804,200 zimekusanywa kama ushuru, tozo na faini mbalimbali katika operesheni hii (Kiambatisho Na. 5).

53. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mikakati ya kulinda rasilimali za mifugo na mazao yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi inafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya mifugo nchini pamoja na sheria nyingine za nchi. Pia, Wizara itaimarisha minada ya upili na ya mipakani kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kukarabati minada mitatu (3) ya mifugo ya upili ya Murusagamba (Ngara), Mutukula (Missenyi) na Buhigwe (Buhigwe);

(ii) Kutoa mafunzo kwa wakusanyaji maduhuli 20 na wafanyabiashara wa mifugo 200 ili kuimarisha ufanisi katika soko la mifugo;

(iii) Kujenga minada mipya miwili (2) ya mipakani ya Longido na Kirumi na kukarabati minada ya upili ya Nyamatala na Kasesya; na

(iv) Kuwezesha operesheni ya kudhibiti biashara haramu ya mifugo kwenye minada na masoko ili kuhakikisha mifugo inafikishwa machinjioni.

## TATHMINI YA UENDESHAJI WA NARCO, MASHAMBA YA KUZALISHA MIFUGO NA VITUO VYA KUPUMZISHIA MIFUGO

54. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na ufanisi usioridhirisha wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (Livestock Multiplication Units -LMUs) na Vituo vya Kupumzishia Mifugo (Holding Grounds - HGs), Wizara ilifanya tathmini ya uendeshaji, uzalishaji, mapato na matumizi pamoja na usimamizi wa rasilimali katika maeneo hayo. Tathmini hii ilifanyika kati ya tarehe 01 Januari hadi 06 Februari, 2018 na matokeo yake ni kama ifuatavyo:-

### Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)

#### (i) Utata wa Umiliki wa Kampuni ya NARCO

NARCO imeanzishwa kwa Sheria ya Makampuni SURA Na. 212, kuna utata kwenye usajiri wa Kampuni ya NARCO ambapo *Memorandum and Articles of Association* (MEMARTS) za NARCO zinaonesha kuwa wanahisa ni Clement George Kahama na Hippolitus Pamfili Njau ambao walisaini kwa vyeo vyao walipokuwa Meneja Mkuu na Katibu wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) mtawalia, wakati NARCO ilipoanzishwa mwaka 1968. MEMARTS hizi zimeendelea kusomeka hivyo mpaka sasa na hivyo kuifanya Kampuni kuonekana kuwa ni mali ya watu binafsi. Kutokana na mkanganyiko huo, Wizara yangu imeandaa pendekezo la kuibadilisha NARCO kutoka Kampuni kuwa Shirika la Umma (Public Corporation) ili kuondoa utata uliopo na kupanua wigo wa kutekeleza majukumu yake.

Faida za kubadilisha NARCO kuwa Shirika la Umma ni:-

(a) Kuondoa mkanganyiko wa kisheria uliokuwepo katika muundo na uendeshaji wa Kampuni na kuwa na shirika lenye uwezo, mamlaka na uwanda mpana zaidi wa kuleta tija kwenye sekta ya mifugo hapa nchini na kuwa na dira, malengo na majukumu yanayotekelezeka na kupimika;

(b) Kuvutia wabia wa maendeeleo kuchangia uendeshaji wa Shirika kwa kutekeleza Sera ambazo zinalenga kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo ina mchango mkubwa katika ustawi wa umma tofauti na Kampuni ambayo inafanya biashara kwa lengo la kutengeneza faida;

(c) Kutoa fursa ya kuanzisha Kampuni Tanzu kwa ajili ya majukumu maaalum kama vile viwanda vya maziwa, nyama na ngozi hivyo kuongeza wigo katika kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo kwa ujumla wake kunalifanya Shirika kuongeza mapato (Benefits from economies of Scale);

(d) Kutekeleza majukumu yanayolenga kulinda na kusimamia maslahi ya Umma ambayo hayawezi kutekelezeka kupitia Kampuni za Kibiashara; na

(e) Kuwa na Shirika kubwa la Umma linaloshughulikia maendeleo ya mifugo litakaloweza kujiendesha kwa faida na kuongeza pato la Taifa.

**(ii) Mikataba ya uwekezaji kati ya NARCO na wawekezaji wadogo waliokodishiwa vitalu kuanzia hekta 2,500 hadi hekta 4,000**

NARCO ilifanya tathmini ya vitalu vya wawekezaji wadogo kuanzia mwezi Februari, 2018 hadi Machi, 2018. Lengo la tathmini ilikuwa kupitia vitalu vya wawekezaji ili kubaini hali halisi ya uwekezaji iliyofikiwa kulingana na mpango wa biashara na makubaliano ya uwekezaji baina ya mwekezaji na NARCO ambapo jumla ya vitalu 107 vyenye eneo la ukubwa wa hekta 289,068 vilifanyiwa tathmini. Tathmini ilibaini changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoendelezwa kikamilifu kwa baadhi ya vitalu kulingana na masharti ya mikataba ya uwekezaji na kutolipa kodi ya pango. Aidha, kulingana na vigezo vilivyowekwa, vitalu 38 vilipata alama kati ya 0 - 49, vitalu 69 viilipata zaidi ya asilimia 50. Vilevile, kati ya vitalu 38 ambavyo havikukidhi vigezo, vitalu 15 vina migogoro (Kiambatisho Na. 6a hadi Na. 6d).

NARCO kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina na Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(a) Vitalu 23 vya wawekezaji ambao wameshindwa kuwekeza zaidi ya asilimia 50 mikataba yao itavunjwa kabla ya Juni 2018;

(b) Vitalu 24 vya wawekezaji ambao wameshindwa kulipa pango la ukodishaji ranchi mikataba yao itavunjwa kabla ya Juni 2018; na

(c) Wawekezaji waliokidhi masharti na matakwa yaani kuwekeza zaidi ya asilimia 50 na kulipa ada za panog mikataba yao itahuishwa Juni, 2018.

**(iii) Mkataba kati ya Serikali na Viwanda vya Sukari vya Kagera na Mtibwa**

Timu ilibaini mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Makampuni haya yalimilikishwa ardhi yenye ukubwa wa hekta 75,000 (sawa na ekari 187,500) bure bila kulipia fidia ya ardhi kwa NARCO;

(b) Fidia iliyolipwa kwa majengo na miundombinu iliyokuwepo ambapo tathmini ilifanywa na Mthamini wa kujitegemea ambapo malipo yalifanyika bila kuthibitishwa na Mthamini wa Serikali na kwamba fedha zilizolipwa ni kidogo na hazilingani na thamani halisi ya majengo na miundombinu hiyo, ambapo Ranchi ya Dakawa zililipwa jumla ya shilingi milioni 47.1 na Ranchi za Kitengule na Missenyi shilingi milioni 290 tu;

(c) Hakuna uwekezaji wowote wa mifugo, majengo na miundombinu uliofanyika katika shamba la Dakawa ambapo Kampuni ya Sukari ya Mtibwa ilimilikishwa jumla ya hekta 20,000 kwa ajili ya ufugaji wa kisasa kwa muda wa zaidi ya miaka 15; na

(d) Kwa upande wa Kitengule na Missenyi kampuni imewekeza ng'ombe 5,307, mbuzi 125 na kondoo 31 ingawa

hakuna uwekezaji wowote wa majengo wala miundombinu kinyume na makubaliano ya mkataba.

Kufuatia changamoto hizo, Wizara yangu inaandaa madai kwa makampuni hayo ili yaweze kulipa NARCO fedha yote wanayodaiwa (mapunjo) na pia nimeagiza makampuni hayo kuwasilisha mpango kazi wa uwekezaji wa miaka mitatu katika maeneo hayo.

**(iv) Mkataba kati ya NARCO na Kampuni ya OVERLAND Livestock Multiplication Unit and Embryo Transplant (Ranchi ya Mzeri na Mkata)**

Timu ya tathmini ilibaini kuwa katika mkataba huu, NARCO na Serikali kwa ujumla hapakuwa na maslahi, ambapo mwekezaji alikuwa na hisa asilimia 70 na NARCO asilimia 30 tu licha ya NARCO kuwa mmiliki wa ardhi ya jumla ya hekta 40,446.28 yenye thamani ya shilingi 27,688,396,750 pamoja na majengo na miundombinu yenye thamani ya shilingi 3,031,619,296 ikilinganishwa na uwezo wa mwekezaji.

Kutokana na mkanganyiko huo wa umiliki wa hisa, NARCO inakamilisha utaratibu wa kuvunja na kuandaa mkataba mpya wenye masilahi kwa pande zote mbili kwa eneo lenye jumla ya hekta 40,446.28 ambapo Mzeri ni hekta 21,000 na Mkata ni hekta 19,446.28.

**(v) Mkataba baina ya NARCO na Agri Ranch Company Limited**

Ranchi hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3) ambazo ni Kikulula, Kagoma na Mabale zenye jumla ya hekta 37,470, licha ya mwekezaji kukodishwa eneo hilo tangu miaka sita (6) iliyopita ameshindwa kuwekeza kwa mujibu wa mkataba. Katika kipindi cha Novemba 2017 NARCO imevunja mkataba huo na hatua za kupata wawekezaji wapya zinakamilishwa.

**(vi) Kuboresha uendeshaji na usimamizi wa Ranchi /Vitalu:-**

(a) **Ranchi/vitalu vya NARCO**. Changamoto kubwa ni wananchi kuvamia na kuanzisha vijiji ndani ya ranchi. Kazi itakayofanyika ni pamoja na kuondoa wavamizi katika maeneo ya Ranchi; kutumia ardhi ya NARCO yote kikamilifu kwa kufuga, kulima malisho na kukodisha kwa wafugaji; kwa sasa ranchi za Missenyi, Kikulula na Mabale zinalindwa na JKT. Aidha, NARCO inaendelea kukamilisha taratibu za kutumia JKT na Jeshi la Mgambo ili kulinda Ranchi zote kwa lengo la kuzuia uvamizi;

(b) **Mipango ya kibiashara ya ranchi za Taifa (core ranches) kuwa na upungufu**. Wizara kupitia NARCO inafanya mapitio ya Mipango ya Biashara ya ranchi zote za kitaifa kulingana na mapendekezo ya tathmini iliyofanyika;

(c) **Tozo ndogo ya ardhi ya vitalu vilivyokodishwa.** Tozo ya ardhi ya vitalu vya uwekezaji shilingi 500 kwa ekari kwa mwaka ni ndogo na hivyo NARCO imehuisha tozo za mikataba ya ukodishaji ardhi. Hivyo, ukodishaji wa ardhi ya vitalu itakuwa shilingi 5,500 kwa ranchi zenye ukubwa wa ekari 1 hadi 4,999.75, shilingi 7,500 kwa ekari 5,000 hadi 12,499.75 na shilingi 10,500 kwa ekari 12,500 na kuendelea; na

(d) **Vyanzo vichache vya mapato vya NARCO.** Vyanzo vikuu vya mapato vya NARCO ni uuzaji wa mifugo na mazao yake yanayozalishwa katika ranchi hizo. Kutokana na idadi ndogo ya mifugo iliyopo, vyanzo vinachangia kiasi kisichotosheleza mahitaji ya kuendesha Kampuni. NARCO itafanya yafuatayo ili kuongeza mapato yake:-

- Kuongeza aina ya mifugo inayofugwa na miradi ya ufugaji;
- Kushirikiana na sekta binafsi kujenga viwanda vya mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi); na
- Kutangaza machinjio zote ambazo hazina wawekezaji ili ziweze kupata wawekezaji makini kwa utaratibu wa ubia.

**(vii) Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs) na Vituo Vikubwa vya Kupumzisha Mifugo (Holding Grounds)**

Tathmini vilevile ilibaini uwepo wa uzalishaji mdogo katika mashamba ya kuzalisha mifugo (LMUs) na pia hayaendeshwi kibiashara kwa vile lengo la uanzishwaji wake ni kusambaza mitamba kwa wananchi kwa bei nafuu. Wizara kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina itahamisha umiliki wa mashamba kutoka Wizara kwenda Shirika la Maendeleo ya Mifugo linalopendekezwa kuanzishwa na kuandaa Mipango ya Biashara (Business Plans) ya kila shamba. Katika vituo vya kupumzisha mifugo, tathmini imebaini uwepo wa uvamizi unaofanywa na wananchi pamoja na taasisi za Serikali katika vituo hivyo mfano, Igawa (Mbeya) imevamiwa na Pori la Akiba la Mpanga Kipengere, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na wananchi. Pia, baadhi ya vituo vya kupumzisha mifugo havitumiki ipasavyo. Ili kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinatumika kikamilifu, Wizara imeandaa mkakati wa kuyatumia kikamilifu maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuwaondoa wavamizi wote, kuhakiki vituo vyote, kuweka alama za kudumu (nguzo) na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali.

**Ukusanyaji wa Madeni kutoka kwa Wawekezaji katika Vitalu vya NARCO**

Kampuni ya Ranchi za Taifa ilikuwa na wadaiwa sugu wa jumla ya shilingi 3,641,385,250, hata hivyo baada ya Wizara kuingilia kati kufikia Machi 2018 kampuni imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 1,852,664,078. Aidha, kiasi cha shilingi 1,788,721,172 bado zinadaiwa kwa wawekezaji ambapo NARCO imeteua kampuni ya udalali ya *Yono Auction Mart* kukusanya madeni hayo.

**(a) Tathmini ya Kiwanda cha Nyama Dodoma (Tanzania Meat Company Limited - TMCL)**

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu, iliunda Kamati ya Wataalam kuchambua Mkataba wa ubia kati ya NARCO na *National Investiment Company Ltd* (NICOL).

Mkataba huo uliingiwa mwaka 2008 kufuatia Serikali kuuza hisa zake asilimia 51 za Machinjio ya Dodoma na kubaki na asilimia 49 kupitia NARCO.

Katika uchambuzi Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Serikali haijawahi kupata gawio lolote yapata miaka 10 sasa tangu kuingiwa kwa Mkataba huo mwaka 2008;

(ii) Mpango Biashara (Business Plan) ambao ulikuwa ni hitaji na sharti la msingi katika Mkataba wa Mauzo Ibara ya 7 na 13 haukutekelezwa;

(iii) Baadhi ya miamala ilikuwa ikifanyika bila kufuata taratibu za fedha (Financial Regulations) za TMCL ikiwemo uhamishaji wa fedha (Inter Company Transfer) kwa NICOL, miamala hiyo haikuwa na mahusiano na ubia. Aidha, katika Taarifa ya Uchunguzi Maalum, (Forensic Investigation Report) uliofanywa na Kampuni ya KPMG ilibaini kuwa, taarifa za hesabu za kila mwaka za Kampuni ya TMCL zilizoandaliwa kwa kutumia makampuni yenye sifa zilionesha kuwa TMCL ilikuwa inapata faida kinyume na uhalisia. Katika uchunguzi huo, KPMG ilithibitisha udanganyifu katika uandaaji wa hesabu za TMCL na matumizi mabaya ya rasilimali zake;

(iv) Kuwepo kwa mgongano wa masilahi kwa kuwa aliyekuwa mwenyekiti wa Bodi ya NARCO alikuwa pia mjumbe wa Bodi ya NICOL;

(v) Mkataba haukuwa umefanyiwa rejea (Review) kwa muda wa miaka tisa (9) wakati matakwa ya mkataba yalitaka kurejewa kila baada ya miaka mitano (5); na

(vi) Hakuna tathmini wala uhakiki uliokwishafanyika ili kuona na kujiridhisha kama uendeshaji wa biashara hiyo ya ubia ina maslahi kwa Serikali.

Kutokana na changamoto na kasoro za utekelezaji wa mkataba na uendeshaji wa biashara hapo juu, na kwa

kuwa NARCO haikupata gawio lolote kwa kipindi cha miaka 10 na kwa kuwa hakuna maendeleo yoyote yaliyofanyika kwa mujibu wa mkataba na Mpango Biashara, machinjio imeendelea kuchinja mifugo ya wateja badala ya mifugo yake na hivyo kutofikia malengo na matarajio ya Serikali. Hivyo, ili kukamilisha taarifa ya uchambuzi wa mkataba na kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi, Msajili wa Hazina ameelekezwa kufanya ukaguzi maalum (Special Financial Audit) katika Kampuni ya Nyama iliyopo Dodoma.

### (b) Tathmini ya Uvamizi wa Mnada wa Pugu

56. **Mheshimiwa Spika**, mnada wa Pugu ni moja kati ya minada 12 ya upili inayosimamiwa na Wizara na ulianzishwa Kisheria ukiwa na Hati Miliki Na.4873 iliyotolewa tarehe 9 Julai, 1939. Aidha, kumekuwa na changamoto ya uvamizi wa wananchi kwenye eneo hili kwa kujenga makazi ya kudumu, kulima na shughuli nyinginezo hali inayopelekea kuwepo kwa migogoro ya mara kwa mara kati ya wavamizi na watumishi wa mnada. Kutokana na changamoto hizi, Wizara iliunda timu ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali ambazo ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam na Manispaa ya Ilala. Timu hiyo ilifanya zoezi la tathmini ya hali ya uvamizi kuanzia tarehe 07 Machi 2018 hadi mwezi Aprili 2018 ambapo ilibainika kuwa sehemu kubwa ya eneo limevamiwa na kubaki eneo dogo tu la ekari 108 sawa na asilimia 5.7 ya eneo lote. Pia, kuna jumla ya nyumba 5,391 ambazo watu wanaishi. Wenye nyumba 5,148 sawa na asilimia 96 walipata maeneo yao kwa kununua, asilimia 4 walisema kuwa wao ni wenyeji wa eneo hilo toka mwaka 1976. Kutokana na hali hiyo Serikali itachukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kulilinda ipasavyo eneo la ekari 108 lisivamiwe, kuhamisha hati miliki kutoka Tanganyika Packers Limited kwenda Wizara yenye dhamana ya mifugo, kuwachukulia hatua za kisheria waliohusika kuuza maeneo ya mnada, kushauriana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhusu namna bora ya kumaliza mgogoro huo.

**(c) Tathmini ya Viwanda vya Mazao ya Mifugo (nyama, maziwa na ngozi) vilivyo binafsishwa ambavyo havifanyi Kazi**

57. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa viwanda vya nyama vinajengwa na vilivyopo ambavyo havizalishi vinaanza usindikaji. Wizara kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina inafanya uthamini wa Viwanda vya nyama vilivyokuwa vinamilikiwa na *Tanganyika Packers Limited (TPL)* vya Mbeya na Shinyanga, kiwanda cha ngozi cha Mwanza kinachomilikiwa na Serikali na kiwanda cha maziwa cha Utegi kilichokuwa kinamilikiwa na *Tanzania Dairies Limited (TDL).* Kazi hiyo ya uthamini itakamilika mwezi Mei, 2018. Uthamini huo utaiwezesha Serikali kutafuta wawekezaji mahiri ifikapo tarehe 30 Juni, 2018. Aidha, kutokana na changamoto zilizojitokeza za ubinafsishaji wa viwanda hivi Serikali itabaki na sehemu ya hisa.

Awali kiwanda cha Shinyanga kilikuwa na kizuizi cha kuendelea na uwekezaji kutokana na hati za kiwanda na mashamba ya kuhifadhia mifugo kushikiliwa na mwekezaji baada ya Serikali kutaifisha kiwanda kutoka kwa mwekezaji Tripple S Limited ambaye alikuwa amekiuza kinyemela kwa Abuward Investment Group Limited, Wizara yangu ilifanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba hati hii inarejeshwa ambapo mwezi Aprili 2018 hati hii ilikabidhiwa rasmi Serikalini. Vilevile, juhudi zinaendelea za kufufua kiwanda cha kusindika nyama cha Sumbawanga cha SAAFI ambacho kilisimamisha usindikaji kutokana na deni na changamoto za uendeshaji. Ili uzalishaji katika kiwanda hicho uanze, NARCO na SAAFI wanaandaa makubaliano ya kibiashara.

58. **Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuhamasisha usindikaji wa maziwa, Kiwanda cha Tanga Fresh kilisaidiwa kupata hati ambayo ilitumika kupata mkopo ambao ulikiwezesha kuwekeza katika ununuzi wa miundombinu ya usindikaji wa maziwa yanayodumu kwa muda mrefu bila kutumia jokofu (Ultra Heat Treated - UHT). Kutokana na uwekezaji huu kiwanda kimeanza usindikaji wa maziwa ya UHT yatokanayo na maziwa yanayokusanywa

moja kwa moja kutoka kwa wafugaji. Mafanikio haya yametokana na Wizara kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa hati ya umiliki ya Tanga Fresh imepatikana. Baada ya maboresho ya kiwanda, uzalishaji utaongezeka kutoka lita 50,000 kwa siku hadi lita 120,000 kwa siku.

**MATUMIZI YA RASILIMALI ZA ARDHI, MAJI NA MALISHO KWA MIFUGO**

59. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta 10,378.53 kwa ajili ya maeneo ya ufugaji kwenye vijiji 13 katika Wilaya za Makete, Kilolo, Tanganyika, Mpanda na Kalambo (Kiambatisho Na. 7) na kufanya jumla ya eneo lililotengwa kwa ajili ya ufugaji hadi sasa kufikia hekta milioni 2.545 katika vijiji 741**.**

60. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi katika uandaaji wa mipango ya matumizi na usimamizi wa ardhi katika vijiji 25, kuyatambua maeneo yaliyotengwa kwa ufugaji katika vijiji 25, kuyaweka na kuyasajili katika mpango. Pia, kumilikishwa maeneo hayo 25 kwa wafugaji na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali. Vilevile, itashirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi na Halmashauri za Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Iramba, Kiteto, Hanang na Rufiji kuainisha na kutenga maeneo ya ufugaji katika vijiji 10.

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya mifugo ambao unafanywa na sekta binafsi. Katika mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea kuhamasisha wafugaji na wawekezaji kuzalisha na uhifadhi wa malisho kwa njia ya kitaalam. Aidha, Wizara imeongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho katika mashamba ya Serikali na sekta binafsi. Tani 10 za mbegu bora

za malisho zilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na Sekta Binafsi ikilinganishwa na tani 3.717 zilizozalishwa mwaka 2016/2017. Vilevile, elimu ya uzalishaji na hifadhi ya malisho ilitolewa kwa wananchi katika vijiji vya Wilaya ya Mvomero (Mkindo, Hembeti, Dihombo Kigugu), Kilosa (Rudewa, Gongoni na Pepea) na Wilaya ya Babati (Mawemairo, Matufa, Seloti, Singu na Gichameda). Pia, elimu hii pamoja na elimu ya unenepeshaji mifugo imetolewa kupitia luninga.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, jumla ya marobota 1,141,946 yalizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na marobota 1,130,246 yaliyozalishwa mwaka 2016/2017. Kati ya hayo, marobota 482,246 yalizalishwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali na marobota 659,700 yalizalishwa kutoka mashamba ya sekta binafsi (Kiambatisho Na. 8a na 8b). Pia, Wizara ilifanya ukaguzi wa maeneo 72 ya kuzalisha, kuhifadhi na kuuza vyakula vya mifugo. Kati ya hayo, Wizara ilisajili viwanda 26 vya kutengeneza vyakula vya mifugo na maeneo matano (5) ya kuhifadhi na kuuza vyakula hivyo. Aidha, mafunzo kwa wakaguzi tisa (9) na watengenezaji 10 wa vyakula vya mifugo yalitolewa ili kuwajengea uwezo.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora katika uzalishaji na usindikaji wa vyakula vya mifugo nchini kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo 50 na watengenezaji wa vyakula vya mifugo 40 na kuendelea kukagua maeneo na viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo. Aidha, itahamasisha na kuelimisha wafugaji na wawekezaji kuhusu mfumo wa kuzalisha, kuhifadhi, kusindika malisho na vyakula vya mifugo kwa kuanzisha mashamba darasa katika Wilaya 10 katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Tabora, Simiyu, Mara, Geita, Mbeya na Kagera. Pia, Wizara itahamasisha na kuanzisha kilimo cha malisho ya mifugo pamoja na kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuendeleza Malisho Nchini. Vilevile, Wizara itaongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho kwa kuimarisha mashamba saba (7) ya Serikali pamoja na kuanzisha mashamba darasa 25 ya kuboresha malisho katika

Halmashauri 25 katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Arusha, Manyara, Dodoma, Shinyanga, Simiyu, Geita, Mwanza, Kagera, na Mara. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu bora za malisho na kuandaa mashamba darasa; na kusimamia urasimishaji wa mbegu bora za malisho kwa ushirikiano wa vituo vya Utafiti na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI).

**Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi**

64. **Mheshimiwa Spika,** migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imekuwepo hapa nchini kwa muda mrefu. Aina ya migogoro hiyo ni kama ifuatavyo:- (i) Migogoro baina ya wafugaji na wakulima; (ii) Migogoro ya wafugaji na Mamlaka za Hifadhi; (iii) Migogoro baina ya wafugaji na wawekezaji; (iv) Migogoro baina ya wafugaji na Mamlaka za Mapori Tengefu; (v) Migogoro baina ya wafugaji na Hifadhi ya Misitu. Hivyo, kutokana na hali hii, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutatua migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi ni kama ifuatavyo:-

(i) **Kutoa elimu juu ya matumizi bora ya ardhi**

Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Kiserikali na wadau wengine imeendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa ardhi kuhusu mipango ya matumizi bora ya ardhi kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Nyanda za Malisho (Sustainable Range Management Project) kwa ufadhili wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Elimu imetolewa kwa wafugaji wa vijiji vya Leluku, Ngapapa na Olkitkit katika Wilaya ya Kiteto. Aidha, mafunzo kuhusu utatuzi wa migogoro kati ya wafugaji na wakulima yalitolewa kwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Kilindi, Handeni, Bagamoyo, Chalinze, Chamwino, Chemba, Kiteto, Kondoa na Morogoro. Pia, wananchi 753 katika vijiji 48 vya Wilaya za Handeni, Chalinze, Kilindi, Mvomero, Kiteto na Morogoro

walipata mafunzo kuhusu sheria za matumizi bora ya ardhi na utatuzi wa migogoro.

(ii) **Kupima, kutenga na kumilikisha ardhi kwa ajili ya ufugaji**

Hadi kufikia mwezi Juni, 2017, jumla ya vijiji 1,695 vilikuwa vimepimwa na kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kati ya vijiji 12,545 vilivyopo nchini. Jumla ya hekta milioni 2.545 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika vijiji 741 vilivyoko katika mikoa 22.

(iii) **Kujenga na kukarabati miundombinu**

Wizara iliwezesha ujenzi wa mabwawa mawili ya Olyapasei (Kiteto) na Kwamaligwa (Kilindi) pamoja na lambo la Masusu katika Wilaya ya Ngorongoro. Ujenzi wa miundombinu hii inafanya kuwa na jumla ya miundombinu iliyojengwa na kukarabatiwa kwa mabwawa matatu (3), malambo 1,378, visima virefu 101, minada ya upili 12, minada ya mipakani 11 na minada ya awali 445.

(iv) **Kutekeleza mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo**

Kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010, Mfumo wa Utambuzi kwa njia ya chapa ya moto umefanyika na unaendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote nchini. Mfumo huu utaimarisha usimamizi wa mifugo nchini ambapo utachangia kwa kiasi kikubwa kumaliza migogoro kwa wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

(v) **Kufanyika kwa zoezi la kutambua idadi halisi ya mifugo na wamiliki wake ndani ya maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba na kuwaondoa**

Kufuatia Agizo la Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Mei, 2016 kuhusu kutokuondoa mifugo iliyopo kwenye

maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba kabla ya kutenga maeneo itakapopelekwa mifugo hiyo, Wizara ilifanya yafuatayo:-

(a) Kuitisha mkutano wa Wakuu wa Mikoa 25 tarehe 20 – 21 Julai, 2016 kwa ajili ya kutenga maeneo ya malisho kwa mifugo kwenye maeneo ya Hifadhi na Mapori ya Akiba. Hadi mwezi Julai, 2017 jumla ya hekta 772,244 zilitengwa katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora, Kagera, Singida, Manyara na Morogoro; na

(b) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanya tathmini katika mikoa ya Kagera, Geita na Simiyu kuhusu mifugo iliyopo kwenye Hifadhi na Mapori ya Akiba.

(vi) **Kuongeza uzalishaji wa malisho na uboreshaji wa maeneo ya machunga**

Ili kukabiliana na ukame unaoathiri mifugo, hususan katika maeneo kame na athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji na wawekezaji kuzalisha na kuhifadhi malisho kwa njia ya kitaalam. Vilevile, elimu ya uzalishaji na uhifadhi wa malisho imetolewa kwa wananchi katika Wilaya za Mvomero, Kilosa na Babati.

(vii) **Kuunda Kikosi Kazi cha Wataalam**

Serikali iliunda kikosi kazi cha Wataalam 14 kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maliasili na Utalii; Kilimo; Mifugo na Uvuvi; Mambo ya Ndani; TANAPA, TAWA, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa lengo la kupitia migogoro ya ardhi, sera na sheria za mifugo na maliasili na kutoa mapendekezo ya namna ya kuipunguza/kuiondoa migogoro. Mapendekezo ya Timu hiyo yaliwasilishwa na yanaendelea kufanyiwa kazi na Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali ili kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi hapa nchini.

Aidha, Wizara yangu ilipokea mapendekezo ya namna ya kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kwamba mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi na kufikia Desemba 2018 kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Serikali itahahakikisha inawekeza kikamilifu katika mashamba yake na maeneo mengine yatakodishwa kwa wafugaji ili kupunguza tatizo la malisho kwa mifugo. Mashamba hayo ya Serikali ni pamoja na NARCO, TALIRI, LMUs na vituo vya kupumzisha mifugo;

(b) Serikali itatenga maeneo kwa ajili ya kuchunga hususan wakati wa uhaba wa malisho kwa kutoa Mkataba maalum na mwongozo wa matumizi ya ardhi hiyo bila kuathiri kazi zinazotekelezwa na Taasisi hizo ikiwemo utafiti na utunzaji wa mifugo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itatenga hekta 7,000 kutoka katika ranchi nne (4) za NARCO kwa ajili ya matumizi ya ufugaji kwa vijiji 29 vya wilaya za Kongwa (13), Bagamoyo (10), Longido (2), Arumeru (1) na Karagwe (3) kama ilivyoainishwa kwenye Kiambatisho Na. 9. Aidha, jumla ya hekta 1,370 kutoka TALIRI zitatengwa kwa matumizi ya ufugaji kwa vijiji 14 vya wilaya za Mpwapwa (1), Misungwi (4), Kongwa (2), Tanga Jiji (1) na Siha (6) (Kiambatisho Na. 10);

(c) Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itasimamia kumaliza migogoro ya ardhi katika mashamba na minada kote nchini, kutoa elimu na kusimamia uhifadhi wa malisho kwa ajili ya matumizi wakati wa ukame/kiangazi;

(d) Kuwaondoa wawekezaji katika ranchi na vitalu vya NARCO walioshindwa kuwekeza kwa mujibu wa mkataba na kupangisha wafugaji wenye mifugo mingi wasio na maeneo ya kutosha kwa malisho. Katika mwaka 2017/2018 NARCO imetoa notisi ya kuwaondoa wawekezaji katika vitalu 24 vyenye eneo la ukubwa wa hekta 65,879.51; na

(e) Wizara itafanya marekebisho ya Sheria nne (4) zinazosimamia mifugo za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na.

19 ya mwaka 2008, Sheria ya Maeneo ya Malisho na Raslimali za Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010, Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo Na. 12 ya Mwaka 2010 ili ziweze kutoa ulinzi wa kutosha kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo na kuweka utaratibu wa kupata maeneo ya wafugaji na kuyasajili.

65. **Mheshimiwa Spika,** ni imani yangu kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itakamilisha mapema tathmini yake na utekelezaji wa mapendekezo ya timu maalum ili kuachia mapema Maeneo Tengefu yaliyokosa sifa yenye ukubwa wa hekta 96,502 na yenye uwezo wa kuhifadhi mifugo 48,251. Pia, tathmini katika maeneo mengine yenye ukubwa wa hekta 5,660,000 nchini ikamilike mapema ili maeneo yaliyokosa sifa yaweze kuongezwa kwa wafugaji.

66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea kufuatilia ujenzi na ukarabati wa malambo na mabwawa uliokuwa umefanyika hapo nyuma yakiwemo mabwawa mawili ya Olyapasei (Kiteto) na Kwamaligwa (Kilindi) pamoja na lambo la Masusu katika Wilaya ya Ngorongoro ambayo yamekamilika. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea na ujenzi wa malambo nane (8) katika Halmashauri ya Wilaya za Ulanga, Rufiji, Busega, Mkuranga, Mwanga, Chato, Meatu na Kilombero. Pia, itaratibu ujenzi wa majosho manane (8) katika sehemu yanakojengwa malambo.

## UDHIBITI WA MAGONJWA YA MIFUGO

67. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake kwa kuzingatia kanuni za biashara hiyo kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) na Shirika la Kimataifa la Biashara (World Trade Organization - WTO). Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo ambapo Kituo cha Kanda ya Kusini Magharibi kilichopo mjini

Sumbawanga kimefanyiwa ukarabati wa jengo la ofisi na kununua vifaa kwa ajili ya kukiwezesha kufanya utambuzi wa magonjwa ya mlipuko.

68. **Mheshimiwa Spika**, Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo umelengwa kutokomezwa duniani ifikapo mwaka 2030 kwa mujibu wa makubaliano ya kikanda na kimataifa yanayoratibu afya ya wanyama. Tanzania imeridhia na itashiriki katika kutekeleza dhamira hii sambamba na kutokomeza Homa ya Mapafu ya Mbuzi na Ndui ya Mbuzi. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi iliendelea kuratibu na kusimamia kampeni za chanjo ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambapo dozi 830,000 zilitumika kuchanja mbuzi na kondoo 702,000 nchini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaratibu upatikanaji na usambazaji dozi 3,800,000 za chanjo katika Wilaya ambazo mifugo yake ipo katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huu.

69. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ilisimamia upatikanaji na kuratibu usambazaji wa dozi 1,020,000 za chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) zilizotumika kuchanja ng'ombe katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Manyara, Mbeya, Pwani, Rukwa na Tanga. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za udhibiti wa ugonjwa huu kwa kushirikiana na wadau wengine kusambaza chanjo kutegemea mwenendo wa ugonjwa.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kufuatilia Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege (HPAI) ndani na nje ya nchi na kuwa ugonjwa huu bado haujaingia nchini pamoja na kuwa ulitokea nchini Uganda. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), imechukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kwa kutoa mafunzo ya utambuzi na ufuatiliaji kwa watalaam na wadau wengine kutoka Wilaya 20 na vituo nane (8) vya Huduma za Mifugo.

Pia, Wizara imeendelea kutoa tahadhari za kisheria ikiwa ni pamoja na kuzuia uingizaji wa kuku na mazao yake usiozingatia taratibu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu kwa kufuatilia mwenendo wa ugonjwa ndani na nje ya nchi.

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018 Wizara kupitia taasisi zake na kwa kushirikiana na sekta binafsi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji wa chanjo ya Mdondo. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine itaendelea kuhamasisha matumizi ya chanjo dhidi ya Mdondo katika maeneo yote nchini. Aidha, ili kuongeza upatikanaji wa chanjo za mifugo za kutosha, Wizara kwa kushirikiana, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na EPZA imehamasisha kampuni binafsi ya 'Hester Biosciences' kutoka India kuja kuwekeza hapa nchini. Taratibu za kuwapatia eneo la Kibaha zimefanyika na ujenzi wa Kiwanda unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018. Kampuni hii itazalisha aina mbalimbali za chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo zitakazouzwa ndani na nje ya nchi.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, matukio ya ugonjwa wa Homa ya Nguruwe yamejitokeza kwenye mikoa ya Dodoma, Iringa, Kagera, Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma ambapo nguruwe 11,485 walikufa kwa ugonjwa huo. Ugonjwa huu unaweza kuzuiwa kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupulizia dawa zenye viini vya kuulia virusi kwenye mabanda na kusimamia sheria ikiwa ni pamoja na kuweka karantini na kuzuia usafirishaji wa nguruwe hai na mazao yake kutoka kwenye eneo lenye ugonjwa huu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine itaendelea kuhamasisha ufugaji bora wa nguruwe kwa kutengeneza mabanda bora, kutoa elimu na kupulizia dawa za kuulia virusi kwenye mabanda. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka zote za Serikali kuanzia

ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa ili kusisimamia sheria inayokataza usafirishaji holela wa nguruwe na mazao yake hususan wakati wa mlipuko wa magonjwa.

### Udhibiti wa Mifugo na Mazao yake kutoka nje ya nchi

73. **Mheshimiwa Spika,** kuanzia tarehe 23 Oktoba, 2017 mpaka tarehe 10 Novemba, 2017, Wizara iliendesha zoezi la kuondoa mifugo ambayo iliingia nchini kutoka nchi jirani kwa ajili ya kutafuta malisho na maji. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia vyombo vya habari iliutaarifu umma kuhusu zoezi la kuondoa mifugo iliyoingizwa nchini kinyume cha sheria na taratibu. Operesheni hii ilitekelezwa katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Ruvuma na Mtwara. Katika operesheni hii jumla ya ng'ombe 11,060 walikamatwa na kutozwa faini na wengine kupigwa mnada na shilingi milioni 271.83 zilikusanywa na kuingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika utaratibu wa kawaida wa usimamizi wa uingizaji wa mifugo na mazao yake nchini, Wizara iliendelea kutekeleza katazo la uingizaji wa ndege na mazao yake kutokana na tishio la uwepo wa ugonjwa wa Mafua Makali ya ndege. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya mayai 11,900 na vifaranga wapatao 9,088 walitaifishwa na kuteketezwa na Serikali kutokana na kuingizwa nchini kinyemela na bila kufuata Sheria na taratibu ambapo pia wahusika wamefikishwa mahakamani.

75. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuimarisha mikakati ya kulinda rasilimali za mifugo na mazao yake kwa kuboresha vituo 36 vya ukaguzi vya mipakani. Pia, Wizara itashirikiana na TRA, TFDA na taasisi nyingine za Serikali kudhibiti uingizaji na utoaji holela wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi inafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni.

## Magonjwa yaenezwayo na Kupe na Mbung'o

76. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi iliratibu upatikanaji na usambazaji wa chanjo ya Ndigana kali na dawa za kuogeshea mifugo, ambapo jumla ya lita 1,387,880.95 za dawa aina mbalimbali za kuogesha mifugo zilinunuliwa na sekta binafsi na kutumika katika mikoa yote nchini. Aidha, wataalam 560 kutoka mikoa ya Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Manyara, Mbeya, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Songwe na Tabora walipata mafunzo ya kutoa chanjo ya Ndigana Kali yaliyotolewa na Makampuni ya *Roanhem International, Dulle Veterinary Center, Vetlife Consultant na Pharmvac Limited*. Jumla ya ng'ombe 88,000 walipata chanjo dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali. Pia, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) umepewa hadhi na ILRI kuwa Kituo mahiri (Centre of Excellency) kwa ajili ya kutoa mafunzo endelevu ya uchanjaji wa Ndigana kali. Wakala huo tayari umeshatoa mafunzo kwa wataalam 79 katika kampasi zake za Madaba Tengeru na Temeke.

77. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na wadau wengine itahamasisha matumizi ya dawa za kuogesha mifugo na kutoa chanjo dhidi ya Ndigana Kali ili kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo. Aidha, LITA itaendelea kutoa mafunzo kwa wachanjaji wa Ndigana kali. Pia, Wizara itaendelea kuratibu upatikanaji wa chanjo ya Ndigana Kali**.**

78. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kupitia dhana ya Afya Moja kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) inaandaa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ugonjwa wa Malale na Nagana kwa Binadamu na Mifugo na kutokomeza mbung'o aenezaye magonjwa hayo. Katika mwaka 2018/ 2019, Wizara itadhibiti Mbung'o na Ndorobo kwa kununua vitendea kazi na kutoa ushauri kuhusu mbinu shirikishi na endelevu katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Manyara, Mara Rukwa na Tabora.

### Magonjwa ya Mifugo yanayoambukiza Binadamu

79. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, magonjwa hatarishi yaambukizwayo binadamu kupitia wanyama yameanza kuongezeka kwa kiwango kikubwa ambayo ni Kichaa cha Mbwa, Kimeta, Homa ya Bonde la Ufa na Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Udhibiti wa magonjwa haya unahitaji dhana ya Afya Moja na utekelezaji wake utahusisha sekta zote zinazohusika. Wadau wa maendeleo wa utekelezaji wa mpango huu ni FAO, WHO, OIE na CDC. Mpango Mkakati wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa hayo ulizinduliwa rasmi na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari, 2018. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa haya.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa kupitia Dhana ya Afya Moja. Aidha, Wizara iliratibu utoaji elimu na uchanjaji wa mbwa 126,000 na paka 13,400, kupitia Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation.* Aidha, katika siku ya Veterinari Duniani ambayo huadhimishwa Jumamosi ya mwisho ya mwezi Aprili kila mwaka FAO ilitoa chanjo ya kichaa cha mbwa dozi 33,700 ambapo kampeni ya Kitaifa ya chanjo hiyo ilizinduliwa mjini Moshi na Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji wa chanjo ya Kichaa cha Mbwa na kutoa elimu kwa wananchi.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Dhana ya Afya Moja imetengeneza Mkakati wa Kufuatilia na Kudhibiti Ugonjwa wa Kimeta kwa Binadamu na Wanyama. Aidha, Wizara ilifuatilia viashiria na mwenendo wa ugonjwa huu katika baadhi ya maeneo ya mwingiliano kati ya wanyama pori na mifugo. Pia, ng'ombe 5,080,500, mbuzi 1,406,000 na kondoo 600,000 walichanjwa katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Mara, Mbeya, Mwanza, Rukwa, Shinyanga na Singida. Katika mwaka 2018/2019,

Wizara kwa kushirikiana na wadau kwa Dhana ya Afya Moja itaendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Kimeta.

82. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kupitia Dhana ya Afya Moja inatekeleza Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa mwaka 2017-2023. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kufuatilia, kuchunguza na kutoa elimu na ushauri wa kitaalam ili kudhibiti ugonjwa huo.

83. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara ilifuatilia viashiria na mwenendo wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ambapo kwa taarifa kutoka taasisi za kimataifa ya "National Aeronautics and Space Administration (NASA)", Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) ilionesha hatari ya kuwepo kwa mlipuko katika msimu huu wa mvua. Aidha, elimu kuhusu udhibiti wa Ugonjwa huu ilitolewa na vipeperushi 1,500 vilisambazwa.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Dhana ya Afya Moja na NASA itaendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa huo na kuchukua tahadhari stahiki.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na FAO imeanzisha mfumo wa kielectronic wa utoaji wa taarifa za magonjwa katika Halmashauri 20 kwa kuwapatia *Smartphone* kwa ajili ya kurahisisha na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji taarifa za magonjwa, katika awamu ya pili Halmashauri nyingine 20 zitaingizwa katika mfumo huu. Aidha, mpango huu utaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Pia, kupitia mfumo huu, vituo vitatu (3) vya Kanda vya uchunguzi wa magonjwa vimepatiwa Kompyuta 11.

85. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imetoa Waraka wa Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo kwa Halmashauri zote

nchini ili kudhibiti magonjwa ya mifugo ambapo kila mfugaji atalazimika kuogesha mifugo yake na kuchanja dhidi ya magonjwa sita (6) ya kipaumbele (Kiambatisho Na. 11**).** Aidha, Wizara itaratibu mahitaji ya chanjo ya kila Halmashauri na kushirikiana na sekta binafsi kuagiza chanjo hizo na mfugaji ambaye hatachanja mifugo yake atachukuliwa hatua za kisheria. Katika kutekeleza Waraka huu Halmashauri zitaandaa sheria ndogo zitakazowezesha kusimamia utekelezaji wa Waraka huu.

## UKAGUZI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE

86. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kushirikiana na Halmashauri katika ukaguzi wa mifugo na mazao yake ili kulinda afya ya wanyama na jamii. Ukaguzi huo umefanyika katika vituo vya mpakani, machinjio na makalo mbalimbali na ng'ombe 604,892, mbuzi 845,960, kondoo 460,730, kuku 2,073,600 na nguruwe 190,070 walikaguliwa kwa ajili ya soko la ndani. Aidha, ng'ombe 1,910, mbuzi 2,751 na kondoo 197 walikaguliwa na kuuzwa nje ya nchi.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia usalama wa chakula kitokanacho na mifugo ili kulinda afya za walaji wa mazao ya mifugo na kukuza biashara ya mazao ya mifugo kimataifa.

## UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI WA MIFUGO

### Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)

87. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia TALIRI imeendelea kuratibu tafiti katika vituo 7 vya TALIRI yaani Kongwa, Mabuki, Mpwapwa, Naliendele, Tanga, West Kilimanjaro na Uyole ambapo jumla ya tafiti 16 zinaendelea. Aidha, TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa inatekeleza miradi ya utafiti kama ifuatavyo:

(i) Kuimarisha upatikanaji wa malisho bora na kuendeleza hifadhi za asili za malisho ya mifugo katika

Halmashauri za Handeni, Kilindi Kilosa, Mvomero, Mufindi, Njombe vijijini Rungwe na Babati Vijijini kwa lengo la kuongeza uzalishaji malisho na kupunguza ufugaji wa kuhamahama. Kazi hizi zinafanywa kwa ushirikiano na COSTECH, ILRI, CIAT, BecA na IFAD;

(ii) Mradi wa kuboresha mbari za kuku wa kiafrika (*African Chicken Genetic Gains* (ACGG)) unaendelea kutekelezwa kwa ushirikiano na ILRI pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Mradi huu unalenga kuboresha kuku wa asili katika kanda tano za kiikolojia nchini ambapo wafugaji 290 (KE=166, ME=124) walishiriki katika mafunzo kwa njia ya majukwaa kwa mwaka huu wa fedha. Tangu mradi uanze, jumla ya kuku 45,154 (Sasso: 32,000, Kuroiler: 11,404 na Black Australorp: 2,500) wamesambazwa katika kanda saba nchini. Aidha, jumla ya wadau 1,651 kutoka Wilaya za Manyoni, Iramba, Bahi, Chamwino, Ifakara na Manispaa ya Morogoro walishirikishwa katika utekelezaji wa mradi pacha wa ACGG wa kilimo mpaka lishe (*Agriculture to Nutrition - ATONU*); na

(iii) Mradi wa kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa (*African Dairy Genetic Gains* -ADGG)) uliendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na ILRI. Katika mradi huu jumla ya wafugaji 22,286 wamepata mafunzo kwa kupitia simu za kiganjani. Pia, jumla ya ng'ombe wa maziwa 37,569 waliwekewa hereni (*ear tags*) zenye Mfumo wa Utambuzi wa Kitaifa (TANLITS) katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Mbeya, Njombe, Songwe na Tanga.

88. **Mheshimiwa Spika**; katika mwaka 2017/2018, Taasisi kwa kushirikiana na AU-IBAR imeendelea na utafiti wa mbuzi weupe aina ya Pare ambapo mbuzi 66 walinunuliwa na kuwekwa kwenye kituo cha TALIRI-West Kilimanjaro kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya ukuaji na uzalishaji.

89. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa kuzalisha ng'ombe bora wa maziwa aina ya *Friesian* umeendelea katika kituo cha TALIRI Uyole ambapo jumla ya ndama 22 (Madume 12 na majike 10) walizaliwa. Aidha, mradi wa

kuzalisha ng'ombe chotara wa maziwa (*Friesian* na Fipa) wenye damu ya *Friesian* (75%) na ng'ombe wenye damu ya Fipa (25%) uliendelea katika kituo hicho ambapo jumla ya ndama 13 (F1 5 na F2 8) wamezaliwa.

90. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, TALIRI imeimarisha mashamba ya mifugo katika vituo vyake saba (7), kuhudumia na kuitunza mifugo iliyopo vituoni. Aina ya mifugo inayofanyiwa tathmini vituoni ni ng'ombe 1,720, mbuzi 1,167, kondoo 274, punda 9 na kuku 1,583. Aidha, jumla ya ng'ombe bora 56 (Mpwapwa, Freisian na Ankole) walisambazwa kwa wafugaji katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Pwani na Tanga.

91. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/2018 Taasisi imezalisha mbegu bora za **malisho** Kiasi cha kilogramu 3,500 (nyasi), kilo 2,500 (mikunde) na kilo 900 (mikunde miti). Aidha, jumla ya marobota (*hay bales*) 20,581 ya malisho yaliyosindikwa. na marobota 6,189 yalisambazwa kwa wafugaji katika Manispaa za Dodoma (2,492), Kinondoni (2,573) na Mbeya (1,124). Vilevile, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Aprili, 2018, TALIRI imesambaza teknolojia 27 za utafiti katika wilaya 41 nchini ambapo vijiji 135 vyenye jumla ya kaya 3,676 zimehusishwa (Kiambatisho Na. 12). Pia, Taasisi imeanzisha miradi minne (4) ya kuzalisha mitamba, kunenepesha mbuzi na uzalishaji wa kuku katika vituo vya Mpwapwa, Kongwa, West Kilimanjaro na Mabuki (Kiambatisho Na. 13).

92. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuiwezesha TALIRI kuendeleza utafiti na uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho ili kuchangia katika kufikia lengo la uchumi wa viwanda na kipato cha kati. Aidha, Wizara kupitia TALIRI itashirikiana na TOSCI kurasimisha mbegu za malisho zinazozalishwa nchini ili kukuza biashara ya mbegu za malisho ndani na nje ya nchi.

93. **Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2017/2018, TALIRI ilitoa mafunzo ya utunzaji wa mifugo kwa wadau 1,991 katika mikoa ya Arusha, Manyara, Morogoro, Dodoma,

Pwani, Mwanza, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Songwe, Shinyanga, Singida na Tanga. Aidha, jumla ya watumishi 30 walihudhuria mafunzo, kati yao 13 walipata mafunzo ya muda mfupi na 17 mafunzo ya muda mrefu ikiwemo ya stashahada (2), Shahada ya Kwanza (5), Shahada ya Uzamili (6) na Shahada ya Uzamivu (4). Pia, TALIRI ilishiriki katika kuonesha na kuelimisha wadau kuhusu teknolojia bora za ufugaji kupitia Maonesho ya Nane Nane katika viwanja vya Maonesho ya Kilimo vya Kanda mbalimbali nchini. Vilevile, watafiti waliandaa na kuwasilisha makala 21 za kisayansi ambapo tisa (9) ziliwasilishwa kwenye majarida na mikutano, warsha na makongamano ndani na nje ya nchi.

94. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuiwezesha TALIRI kutimiza majukumu yake ya kitafiti kwa ushirikiano na Taasisi za kitaifa na Kimataifa kama ifuatavyo:

(i) Kuhudumia mifugo 5,000 (ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na punda) waliopo katika vituo saba nchini;

(ii) Kuibua, kutafiti na kusambaza ng'ombe bora wa nyama 100 katika vituo vya Mpwapwa, Kongwa, Mabuki na West Kilimanjaro;

(iii) Kutafiti na kuzalisha mitamba bora 200 ya ng'ombe wa maziwa katika vituo vinne vya utafiti; na mitamba bora 400 ya ng'ombe wa nyama katika vituo vitatu (3) vya utafiti;

(iv) Kutafiti, kuzalisha na kusambaza mbuzi bora 150 wa maziwa na nyama kwa wafugaji; na vifaranga 5,000 wa nyama na mayai na kusambaza katika kanda saba (7) za kiikolojia nchini;

(v) Kutafiti aina tisa (9) za mbegu bora za malisho, kuzalisha kilo 4,000 za mbegu na kusindika marobota 30,000 ya malisho; na

(vi) Kufanya tafiti za punda 50 na simbilisi *(non-conventional animals*) na kukusanya takwimu kwa ajili ya kuendeleza kosaafu.

## Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)

95. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency – LITA) ilifanya udahili wa wanachuo 2,137, kati ya hao 958 ni wa Stashahada na 1,179 ni wa Astashahada. Wanachuo 958 wa Stashahada wanatarajiwa kuhitimu mafunzo yao mwezi Juni, 2018. Aidha, Wakala imetoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri kwa wafugaji 838 juu ya afya na uzalishaji bora wa mifugo. Vilevile, watumishi 26 wanaendelea na mafunzo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi, katika shahada ya Uzamivu watatu (3), Uzamili wanne (4), Shahada 17, Stashahada mmoja (1), na Astashahada moja (1). Pia, Wataalam wa Afya ya Mifugo 95 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi, walipatiwa mafunzo ya utoaji wa chanjo ya Ndigana Kali (ECF) katika Kampasi za Tengeru, Temeke, Madaba na Mpwapwa; wakufunzi 15 kutoka Kampasi za Wakala walihudhuria kozi ya muda mfupi nchini Kenya juu ya mbinu za kuchanja Ndigana kali.

96. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia LITA imefanya ukarabati wa miundombinu katika Kampasi za Wakala, ili kuwezesha ongezeko la wanachuo na kuboresha mazingira ya kujifunzia. Pia, Pampu moja (1) ya kusukuma maji ilinunuliwa na kutengeneza mfumo wa kusambaza maji katika Kampasi ya Kikulula. Aidha, marobota 19,877 ya hei (hay) yalizalishwa katika Kampasi za Buhuri (6,125) na Tengeru (13,752) kwa matumizi ya Wakala na wafugaji wanaozunguka Kampasi. Pia, mfumo wa kusambaza maji ulifanyiwa matengenezo na matenki ya kuhifadhi na kusambaza maji yalifungwa kwa ajili ya wanachuo katika Kampasi ya Tengeru. Vilevile, vifaa vilinunuliwa ambavyo ni pamoja na magodoro 209 kwa ajili ya Kampasi za Tengeru (100), Buhuri (64), Mabuki (35) na Kikulula (10); vitanda 58 kwa ajili ya Kampasi za Mabuki (26) na Buhuri

(32); meza 64 za wanachuo na viti vyake kwa ajili ya Kampasi ya Buhuri na gari moja (1) ilinunuliwa kwa ajili ya Kampasi ya Kikulula.

97. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaiwezesha LITA kudahili wanachuo 2,700 wa Stashahada na Astashahada. Aidha, Wakala itatoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri kwa wafugaji 1,700 juu ya ufugaji bora wenye tija. Pia, mafunzo ya Menejimenti na Utawala yatatolewa kwa Wakurugenzi wa Kampasi nane (8) za Wakala, pamoja na kuwezesha watumishi 15 kushiriki mikutano ya kitaaluma. Vilevile, mafunzo ya muda mfupi yatatolewa kwa Watumishi 14 kwa lengo la kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na:-

(i) Kukarabati na kuimarisha uendeshaji wa vitengo vya uzalishaji katika Kampasi nane (8) za Wakala;

(ii) Kufanya ukarabati wa mabweni 12 ya wanachuo katika Kampasi za Tengeru (3), Morogoro (3), Mpwapwa (2), Buhuri (2), na Madaba (2) ili kukidhi ongezeko la wanachuo;

(iii) Kukarabati madarasa matatu (3) katika Kampasi za Morogoro (2) na Mpwapwa (1); na

(iv) Kukarabati ukumbi mmoja (1) kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mafunzo katika Kampasi ya Morogoro.

98. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaiwezesha LITA kuchimba visima viwili (2) katika Kampasi za Buhuri (1) na Morogoro (1) kwa ajili ya mahitaji ya wanachuo na uzalishaji wa malisho. Aidha, Kampasi ya Madaba itaunganishwa na gridi ya Umeme wa Taifa ili kupata umeme wa uhakika na mazingira bora ya kujifunzia. Pia, trekta moja (1) litanunuliwa kwa ajili Kampasi ya Kikulula kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Vilevile, magari mawili (2) kwa

ajili ya Kampasi za Mpwapwa (1) na Tengeru (1) yatanunuliwa na kiwanda kimoja (1) cha kuchakata maziwa kitakarabatiwa kwa lengo la kutengeneza bidhaa mbalimbali za maziwa katika Kampasi ya Tengeru na na kuboresha mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya wanachuo na wafugaji.

## Huduma za Ugani wa Mifugo

99. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi ilitoa elimu kwa wadau 5,730 kupitia mafunzo, mikutano ya uhamasishaji na semina zilizokuwa zikiendeshwa wakati wa maonyesho ya Nane Nane na Saba Saba. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau kwa kusambaza vitabu 1,053 vya ufugaji bora, vipeperushi 18,500 na mabango 220. Pia, Wizara kupitia vyombo vya habari ilirusha hewani vipindi 40 vya redio na sita (6) vya luninga, baadhi ya vipindi hivyo vilihusu, teknolojia za hifadhi na uzalishaji wa malisho, Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha kituo cha Maarifa ya Mifugo na Uvuvi cha Lugoba (Bagamoyo) ambapo, kazi ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi inaendelea, kituo hiki kitakapokamilika kitawezesha kutoa elimu kwa wafugaji 11,600 kwa mwaka.

100. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ugani nchini, kusambaza teknolojia sahihi za ufugaji bora na mnyororo wa thamani kupitia, maonesho ya Saba Saba, Nane Nane, kuhamasisha uanzishwaji wa mashamba darasa na mashamba ya mfano katika Halmashauri. Wizara imejiandaa kuboresha mashamba darasa ya malisho bora ya mifugo na kuanzisha mengine nane (8) katika Halmashauri mbalimbali. Pia, Wizara itaendelea kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya radio na 12 vya luninga vya elimu kwa umma kuhusu ufugaji bora na wafugaji 4,000 na watoa huduma za ugani 80 watajengewa uwezo wa uzalishaji katika mnyororo wa thamani.

## UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO

101. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tathmini ya utekelezaji zoezi la kupiga chapa ya moto ng'ombe na punda ilifanyika Mikoa yote ya Tanzania Bara, ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 jumla ya ng'ombe 17,045,944 wamepigwa chapa ikiwa ni asilimia 98.0 ya lengo la kupiga chapa ng'ombe 17,390,090. Vilevile, jumla ya ng'ombe wa maziwa 58,214 wamevishwa hereni ambayo ni asilimia 7.4 kati ya ng'ombe wa maziwa 782,995 wanaotakiwa kuvishwa hereni nchini. Pia, punda 57,797 wamepigwa chapa ikiwa ni asilimia 10.1 ya lengo la kupiga chapa punda 572,357. Pamoja na juhudi za Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vyombo vya habari kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa zoezi hili, bado kuna ng'ombe na punda ambao hawajapigwa chapa. Hali hii ilithibitishwa na timu za Wizara zilizozunguka nchi nzima kuanzia tarehe 15 Februari hadi mwanzoni mwa mwezi Machi, 2018 ili kufanya tathmini, minadani, machungani, mazizini, barabarani na katika mapori ya akiba. Aidha, hali hii ilionyesha kuna udanganyifu mkubwa miongoni mwa watendaji wasio waaminifu wanaopotosha taarifa.

Wizara inapendekeza ifanywe tathmini ya mwisho ya zoezi la chapa ya Kitaifa kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kuhimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe ng'ombe na punda wote waliofikia umri wa miezi sita wanawekewa alama ya chapa. Pia, kila Halmashauri ifanye Tathmini katika maeneo yao husika wajiridhishe kama katika maeneo yao yote kwamba ng'ombe na punda wote wanaostahili kupiga chapa wamepiga chapa na endapo itabainika kuna udanganyifu hatua stahili zitachukuliwa. Aidha, jumla ya wafugaji 1,462,279 wamehamasishwa juu ya Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Tanzania Bara kupitia mikutano ya uhamasishaji iliyoendeshwa na wataalam wa mifugo, Wakuu wa Wilaya na Viongozi wengine. Mwongozo wa utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo ulisambazwa katika mikoa yote. Natoa pongezi kwa

viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri waliosimamia vema utekelezaji wa zoezi hili kwa usahihi.

102. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo nchini ili kuhakikisha ng'ombe na punda wote wanaofikisha umri wa miezi sita (6) na kuendelea wanapigwa chapa. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kusambaza hereni zenye viwango vilivyoidhinishwa zitakazotumika kwa ng'ombe wa maziwa na wanaofugwa kwenye mfumo shadidi. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendesha mafunzo ya matumizi ya rejista ya kieletroniki na kanzidata ya Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo.

## HUDUMA YA MAABARA ZA MIFUGO

### Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency -TVLA)

103. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) katika Taasisi ya Utafiti na Uzalishaji wa Chanjo iliyopo Kibaha imezalisha na kusambaza dozi 28,427,100 za chanjo ya ugonjwa wa Mdondo, dozi 882,100 za chanjo ya ugonjwa wa Kimeta, dozi 128, 600 za chanjo ya ugonjwa wa Chambavu na dozi 625 za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba. Jumla ya shilingi bilioni 1.27 zilipatikana kutokana na mauzo ya chanjo hizo. Uzalishaji wa Chanjo ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa Ng'ombe na chanjo inayokinga kwa pamoja magonjwa ya Kimeta na Chambavu unasubiri majibu kutoka Maabara Kuu ya chanjo barani Afrika ya PANVAC iliyoko nchini Ethiopia ambako sampuli za chanjo hizo zimepelekwa kwa ajili ya kupima ubora wake. Aidha, Wizara ilipata msaada wa chanjo ya Mdondo dozi 2,000,000 kutoka Kampuni ya Hester Biosciences ya India, iliyotumika kwenye kampeni ya chanjo ya Kitaifa iliyozinduliwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Wilayani Mkuranga tarehe 30 Aprili, 2018.

104. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia TVLA imefanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo nchini katika sampuli 15,422 zilizopokelewa. Magonjwa yaliyotambuliwa ni pamoja na Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Kimeta, Kichaa cha Mbwa, Mdondo, Gumboro, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Homa ya Nguruwe, Minyoo na Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Aidha, jumla ya sampuli 1,404 za vyakula vya mifugo na malighafi za kutengenezea vyakula hivyo zilifanyiwa uchambuzi wa viini lishe ambapo upungufu wa protini na nishati ulionekana kati ya asilimia 16-20 ya sampuli hizo. Wafugaji na watengenezaji wa vyakula vya mifugo walipewa ushauri wa namna ya kudhibiti magonjwa hayo na kuboresha vyakula vya mifugo.

105. **Mheshimiwa Spika**, TVLA kupitia vituo vya Kigoma na Tanga vinavyofanya utafiti wa teknolojia za kuangamiza mbun'go waenezao magonjwa ya Nagana na Malale vimeendelea kufanya utafiti wa njia muafaka za kupunguza au kumaliza mbung'o katika maeneo mbalimbali nchini. Utafiti huo pia umejikita katika kuangalia mwenendo wa mbung'o na ndorobo kati ya wanyama pori na wanyama wafugwao na uwezo wao wa kuambukiza wanyama na binadamu. Ili kuendeleza tafiti za kudhibiti mbung'o, maabara imeendelea kuzalisha na kuhifadhi mbung'o wazima na mabuu aina za *G. austeni* wazima 19,895 na mabuu 2,941; *G.m.morstans* wazima 4,092 na mabuu 496 na *G. pallidipes* wazima 3,100 na mabuu 446.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, TVLA itaendelea kufanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama; kufanya uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo na malighafi za kutengenezea vyakula hivyo. Wakala pia unapanga kuzalisha na kusambaza dozi milioni 100 za chanjo ya Mdondo, dozi 1,000,000 za chanjo ya Kimeta, dozi 1,000,000 za chanjo ya Chambavu na dozi 500,000 za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba. Aidha, itakamilisha majaribio na kuanza kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe. Vilevile, Wakala inapanga kuanza majaribio ya kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na chanjo dhidi ya

Kichaa cha Mbwa. TVLA, pia itaendelea kufanya tafiti zinazolenga kuthibiti mbung'o wanaoeneza ugonjwa wa Nagana kwa mifugo na Homa ya Malale kwa binadamu na namna ya kudhibiti au kutokomeza magonjwa mengine ya mifugo.

## USIMAMIZI WA UBORA WA MAZAO, TAALUMA NA HUDUMA ZA VETERINARI

### Bodi ya Nyama

107. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Bodi ya Nyama imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali za kazi za wadau wa tasnia ya nyama. Jumla ya kazi za wadau wa tasnia ya nyama 1,596 (mabucha 1,412, wauzaji wa nyama nje ya nchi 28; waingizaji wa nyama nchini watano (5); wafugaji 88, machinjio 63 na minada mitatu (3) zimekaguliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 za mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Katavi, Morogoro, Mwanza, Shinyanga na Mara. Kati ya hizo, 355 zimekidhi matakwa ya Sheria na kusajiliwa na 948 zimepewa maelekezo kwa ajili ya kuboresha na 169 zimefungiwa kwa kutokidhi matakwa ya Sheria.

108. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuwajengea uwezo watumishi 12 wa Bodi, 20 wa Zoo-sanitary na 85 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 za Ilemela, Nyamagana, Magu, Kwimba na Misungwi; Shinyanga Manispaa, Shinyanga (W), Kishapu, Kahama Mji na Msalala; Manispaa za Ilala, Temeke, Kinondoni, Kigamboni na Ubungo; Manispaa ya Morogoro na Mvomero; Manispaa ya Musoma, Musoma (W), Tarime Mji, Tarime (W), Butiama (W), Rorya (W), Serengeti (W), Bunda Mji na Bunda (W) wanaotekeleza majukumu ya Bodi ya Nyama. Majukumu hayo ni kufanya ukaguzi wa kazi za wadau, kutoa mafunzo ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za kuzingatia wakati wa kuzalisha nyama (Standard Operating Procedures - SOP's), kutumia mfumo wa usajili na kutafuta

masoko kielektroniki pamoja na kusimamia utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Tasnia ya Nyama Na. 10 ya 2006 na Kanuni zake za Mwaka 2011 na 2014. Mafunzo mengine yaliyotolewa ni pamoja na uandishi wa miradi; kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika ununuzi; maadili ya utumishi wa umma na kudhibiti utakatishaji wa fedha.

109. **Mheshimiwa Spika,** Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 imeendelea kuhamasisha ulaji nyama na kutoa mafunzo ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za usafi (SOP's) kwa wadau 469 wa tasnia ya nyama. Pia, imewezesha jumla ya wadau 28 kushiriki katika maonesho mbalimbali ikiwa ni pamoja na maonesho ya Sabasaba (3), Nanenane (5), maonesho ya ndege wafugwao (15) na Tamasha la Nyama Choma (5). Baadhi ya wadau walioshiriki ni *PiMAK, Damari Investment, Abachem Engineering Company, Winning Creative* na *Meat King Distributors*. Bidhaa zilizooneshwa ni pamoja na Bongo Sausage, Smoked Ham, Nyama Okwa zinazozalishwa nchini, vifaa vinavyotumika kukatia nyama katika bucha na mashine za machinjio za kisasa. Aidha, wadau 3,555 walitembelea katika banda la Bodi ya Nyama wakati wa maonesho hayo na kujifunza biashara ya mifugo, nyama na bidhaa zake.

110. **Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kuunda vyama vya wadau ambapo vyama vitatu (3) vya Wafugaji wa Kuku wa Mayai Tanzania (Tanzania Layers Farmers Association - TALFA) na Wafugaji wa Kuku wa Nyama (Tanzania Broiler Farmers Association -TABROFA) na Mtandao wa Vyama 11 vya Wadau wa Tasnia ya Ndege Wafugwao (Poultry Association of Tanzania (PAT) vimeundwa na kusajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Pia, Bodi imeendelea kuimarisha vyama vya wadau vilivyopo kwa kuwezesha Chama cha Wasindikaji wa Nyama (TAMEPA) na Chama cha Wadau wa Mnyororo wa Thamani wa Ng'ombe wa Asili (TANZEBA) kuendesha mikutano yao na kujadili changamoto zilizopo na kuweka mpango kazi wa kutekeleza majukumu ya vyama vyao kwa mujibu wa Katiba zao.

111. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Bodi ya Nyama itaajiri watumishi 10, kutoa mafunzo kwa watumishi wa Bodi kuhusu mfumo wa usajili wa wadau kielektroniki na watumishi 100 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 juu ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za kuzalisha nyama (SOP's). Pia, itahamasisha ulaji wa nyama bora na salama kwa njia mbalimbali, kuandaa, kuendesha maonesho ya Nyama na kushiriki kwenye maonesho ya kitaifa. Aidha, Bodi itatoa mafunzo ya Kilimo Biashara na teknolojia ya uzalishaji wa nyama kwa wadau 2,500 katika mnyororo wa thamani ya nyama ya ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku, kondoo na punda, kuwaunganisha wafugaji na wenye viwanda ili kuwapatia soko la uhakika. Vilevile, Bodi itaendelea kusimamia biashara ya mifugo na nyama katika masoko ya ndani na kufuatilia uingizaji na uuzaji nyama na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Pia, itatambua na kusajili wadau 1,000 wa tasnia ya nyama na vyama vyao na kuimarisha vyama sita (6) vya wadau katika ngazi ya Kitaifa (TAPIFA, PAT, TANZEBA, TAMEPA, CCWT na TALIMETA) ili kuviwezesha kushiriki kikamilifu katika kuendeleza mnyororo wa thamani ya nyama.

**Bodi ya Maziwa**

112. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maziwa imeendelea kusimamia Sheria ya Tasnia ya Maziwa ya mwaka 2004 ili kusimamia shughuli za uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa. Katika mwaka 2017/2018 Bodi iliwajengea uwezo wadau wa maziwa na kutoa mafunzo ya teknolojia za usindikaji na udhibiti wa ubora kwa wasindikaji 15 katika kanda ya Ziwa (6), Kanda ya Mashariki (8) na Nyanda za Juu Kusini (1). Aidha, Bodi imesajili wadau wapya 58 (wazalishaji wa maziwa 11, watoa huduma 1, wasambazaji wa maziwa 2, mashamba makubwa 2, vikundi 5, vituo vya kukusanyia maziwa 2, waingizaji wa maziwa 32, wasindikaji 3) na vyombo 15 vya kusafirishia maziwa. Pia, Bodi imeendelea kudhibiti uingizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi kwa kutoa vibali 622 vya kuingiza maziwa lita (LME) 20,920,537.59 zenye thamani ya shilingi 30,290,485,222 na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazao ya mifugo 19 (Zoosanitary

Inspectors) ili kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa shehena za maziwa katika mipaka yote ya forodha ya Tanzania.

113. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitatu kutoka 2018/19 mpaka 2020/21 wa kuendeleza tasnia ya maziwa. Vilevile, Bodi ya Maziwa na wadau wa tasnia ya Maziwa itaandaa maonesho ya mifugo (Livestock Expo) na wiki ya Uhamasishaji wa Unywaji wa Maziwa itakayofanyika Mkoani Arusha kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 1 Juni, 2018 ikiwa na kauli mbiu inayosema; ''Fungua Fursa katika Sekta ya Mifugo kwa Viwanda na Maendeleo". Kutokana na changamoto inayoikabili Bodi kuhusu usajili wa wadau, Bodi imepitia na kukamilisha Mwongozo wa Ukasimishaji/Ugatuaji baadhi ya majukumu ya Bodi (usajili na ukaguzi) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mwongozo huu unatarajiwa kuongeza kasi ya usajili wa wadau na ukaguzi wa shughuli za maziwa nchini.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa itaendelea kuimarisha na kuongeza vituo 50 vya kukusanyia maziwa katika maeneo yanayozalisha maziwa mengi katika mikoa ya Geita (Bukombe na Chato); Iringa (Mufindi na Mafinga); Mara (Bunda); Mbeya (Rungwe na Busokelo); Morogoro (Mvomero); Njombe (Makete na Ludewa); Pwani (Chalinze na Mkuranga); Rukwa (Kalambo); Ruvuma (Mbinga na Madaba); Simiyu (Meatu); Shinyanga (Kahama) na Tanga (Kilindi).

**Usimamizi wa Viwango vya Huduma ya Afya ya Mifugo na Maadili ya Wataalam**

114. **Mheshimiwa Spika**, viwango vya huduma na maadili ya wataalam wa afya ya mifugo husimamiwa na Baraza la Veterinari Tanzania, lililoanzishwa chini ya Sheria ya Veterinari Na 16 ya mwaka 2003. Katika mwaka 2017/2018, Baraza limefanya kaguzi tano (5) zenye jumla ya siku 70 katika mikoa 13 ya Arusha, Dar-es-Salaam, Geita, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Simiyu, Shinyanga

na Tanga. Katika kaguzi hizi, vituo vya kutoa Huduma ya Afya ya Mifugo 546 vimekaguliwa na wataalam 1,002 wamesajiliwa. Kutokana na kaguzi hizo vituo 20 vimefungwa kwa kutokidhi viwango, wataalam wanne (4) wameonywa kwa kukiuka maadili na wawili (2) kufutiwa usajili. Vilevile, wauzaji 18 wa dawa za mifugo wasiosajiliwa walikamatwa katika minada mbalimbali na kutozwa faini.

115. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Baraza la Veterinari Tanzania limesajili madaktari wa mifugo 48 na kufanya idadi ya waliosajiliwa kufikia 858. Aidha, wataalam wasaidizi wa afya ya mifugo 305 wenye Stashahada na Astashahada waliandikishwa na kuorodheshwa na kufanya idadi ya wataalam wasaidizi walioandikishwa na kuorodheshwa kufikia, 2,881. Pia, wakaguzi wa nyama 50, wataalam wa maabara za veterinari watano (5) na wahimilishaji 21 wamepewa leseni za kutoa huduma hiyo. Hadi sasa, wataalam waliopatiwa leseni wamefikia 704; wakaguzi wa nyama 636; wahimilishaji 34 na wataalam wa maabara 34. Vilevile, vituo 246 vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vimesajiliwa na vyuo viwili (2) vya kutoa mafunzo ya mifugo vya Igabiro (Kagera) na Ukiriguru (Mwanza) vilikaguliwa na kuelekezwa mambo ya kuzingatia kabla ya kuanza kutoa mafunzo hayo.

116. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019**,** Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Veterinari Na.16 ya mwaka 2003 kwa kusajili madaktari wa mifugo 60, vituo vya huduma ya mifugo 400, kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi 1,000, kutoa leseni kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari 210 na kufanya ukaguzi wa maadili na viwango vya utoaji huduma kwa kushirikiana na Halmashauri 184 nchini. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Baraza la Veterinari la Afrika Kusini na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani litawajengea uwezo watendaji wake na wadau wengine kusimamia utoaji wa huduma ya afya ya mifugo nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Jamii ya Chuo

Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Baraza litatoa mafunzo ya kujiendeleza ya miezi mitatu (3) kwa watoa huduma wa afya ya mifugo 300.

## HALI YA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

117. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuhamasisha ujenzi wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama nchini. Katika mwaka 2017/2018 jumla ya viwanda viwili (2) vya HEBO Group kilichopo Dar es Salaam chenye uwezo wa kusindika kuku 7,500 na Kilitan kilichopo Moshi chenye uwezo wa kusindika kuku 4,000 vimejengwa, na viwanda vitano (5) vinaendelea kujengwa. Viwanda hivyo ni vya Manispaa ya Iringa (Iringa); BIMJIANG Company Ltd (Shinyanga); Halmashauri ya Mbeya (Mbeya); Nguru Hills Ranch (Mvomero) na Ruvu (NARCO). Viwanda vya kusindika/ machinjio ya nyama vilivyojengwa nchini kwa sasa vipo 24 (Kiambatisho Na. 14). Pia, Serikali imeendelea kutafuta wawekezaji watakaojenga viwanda vya kusindika nyama vikiwemo Shinyanga na Mbeya. Vilevile, wawekezaji mbalimbali kutoka nje wameonesha nia ya kuwekeza katika ujenzi wa viwanda nchini, hususan wawekezaji kutoka Misri na Korea Kusini.

118. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ujenzi wa viwanda vya kusindika maziwa, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kuimarisha na kujenga viwanda vya kusindika maziwa nchini ambapo kwa sasa, kuna viwanda 82 vya kusindika maziwa, kati ya hivyo, viwanda 76 vinafanya kazi. Katika mwaka 2017/2018 jumla ya viwanda viwili (2) vya Narunyu Dairy (Lindi) chenye uwezo wa kusindika lita 500 kwa siku na Lindi Dairy (Lindi) chenye uwezo wa kusindika maziwa lita 500 kwa siku vimejengwa. Aidha, viwanda viwili (2) vya Tanga Fresh (Tanga) na MilkCom kilichopo Dar es Salaam vimeongeza uwezo wa usindikaji. Pia, viwanda saba (7) vya CHAWAKIM Dairy (Pwani), Galaxy Foods and Bevarage Co. Ltd (Arusha), Gesap Dairy (Kagera), Gonza Milk (Dar es Salaam), Creameries (Kilimanjaro), Asas Dairy (Iringa) na MaltVet Dairy (Pwani) vinaendelea kujengwa au kuongeza uwezo (Kiambatisho Na. 15).

119. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na mifuko ya jamii inajenga kiwanda cha kusindika ngozi katika Gereza la Karanga ambapo kutakuwa na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za ngozi. Aidha, NARCO kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo wa Kiuchumi wa Serikali ya Korea inakamilisha taratibu za awali za ujenzi wa kiwanda cha kusindika ngozi katika machinjio ya kisasa itakayojengwa Ruvu ambayo itakuwa na uwezo wa kuchinja na kuchakata ng'ombe 1,500 na mbuzi/kondoo 2,000 kwa siku na kuzalisha ngozi nyingi. Kiwanda hicho kitakuwa kinatengeneza bidhaa mbalimbali kama vile mikanda, mabegi, viatu na sole za viatu. Kwa sasa, kuna viwanda sita (6) vya ngozi nchini vinavyofanya kazi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuwahamasisha wawekezaji wengi zaidi ili wawekeze kwenye viwanda vya kusindika nyama, maziwa, kuku, punda na nguruwe.

**Uratibu wa Masuala ya Kikanda na Kimataifa kwa Sekta ya Mifugo**

120. **Mheshimiwa Spika,** kupitia sekta ya mifugo, nchi yetu ni mwanachama wa Taasisi mbalimbali za Kikanda na Kimataifa zikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU). Aidha, nchi yetu ni mwanachama wa mashirika na taasisi mbalimbali za Kimataifa yakiwemo Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) na Benki ya Dunia. Katika mwaka 2017/2018, nchi yetu imekuwa ikishiriki kwenye mikutano, makongamano na warsha mbalimbali zenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kusimamia rasilimali za mifugo kama vile uanzishwaji wa Mradi wa Nyama wa pamoja kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri. Aidha, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Abdel Fattah El-sis, Rais wa Misri nchini aliyofanya tarehe 14-15 Agosti, 2017 alipokutana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Misri imeonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya mifugo kwa kuanzisha viwanda vya kusindika nyama.

121. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilishiriki vikao na mikutano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kati vilivyohusu Programu pana ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (Comprehensive Africa Agricultural Development Programme- CAADP) na Mpango wa Afrika wenye lengo la kukuza Uzalishaji wa Kilimo Afrika. Mpango huu unategemea kuleta mabadiliko katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi; kujenga uchumi; kuongeza usalama wa chakula na lishe; kukuza uchumi na kuleta ustawi kwa watu wote Tanzania.

122. **Mheshimiwa Spika,** kupitia FAO na Benki ya Dunia na mashirika mengine Wizara imewezeshwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuridhia na kushiriki kikamilifu katika mpango wa '*Global Health Security Agenda*'. Kwa sasa Dunia inakabiliwa na tatizo la magonjwa tokezi (emerging and re-ermeging disases). Kutokea kwa ugonjwa wa '*Ebola'* nchini Liberia, umebaini umuhimu wa sekta ndani ya nchi na jamii za kimataifa kufanya kazi kwa pamoja zaidi kuliko kila sekta kufanya peke yake.

(b) Dhana ya Afya Moja: Utekelezaji wa mpango huu unahusisha sekta nyingi zikiwemo Mifugo, Afya, Mali Asili na Mazingira. Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, ndiyo inaratibu shughuli zote zenye taswira ya maafa na inazihusisha sekta hizi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Maliasili na Utalii na Wadau wa Maendeleo inatekeleza Mpango Mkakati wa 'Afya Moja' kwa nia ya kutokomeza na kuzuia magonjwa yanayoambukizwa binadamu kupitia kwa wanyama (zoonoses) na athari zingine zinazoathiri wanyama, binadamu na mazingira. Mpango Mkakati huu ulizinduliwa mwezi Februari 2018 jijini Dar-es-Salaam na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

123. **Mheshimiwa Spika**, kupitia dhana ya Afya Moja mafanikio yafuatayo yamepatikana:

(i) Magonjwa matano (5) ya kipaumbele ambayo ni Kichaa cha Mbwa, Homa ya Bonde la Ufa, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Malale na Kimeta yamependekezwa na kuridhiwa;

(ii) Ushiriki wa wadau wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Serikali ya Finland, FAO, WHO na Serikali ya Marekani kupitia taasisi zake za USAID P&R, CDC, DTRA, CBEP wameandaa na kukamilisha mikakati ya ufuatiliaji (Surveillance) na udhibiti (prevention) wa magonjwa hayo matano ya kipaumbele; na

(iii) Mpango kazi wa kitaifa wa kupunguza usugu wa matumizi holela ya dawa za binadamu, wanyama na mimea umeandaliwa na kuzinduliwa rasmi mwezi Oktoba 2017 mjini Dodoma.

**Sensa ya Mifugo Nchini**

124. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II), Wizara imepanga kuimarisha na kuboresha takwimu za sekta ya mifugo na uvuvi nchini kwa kufanya Sensa ya Mifugo kwa mwaka 2018/2019. Sensa ya Mifugo hapa nchini kwa mara ya mwisho ilifanyika mwaka 1984 na kulingana na mwongozo wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), inatakiwa ifanyike kila baada ya miaka kumi.

**C: SEKTA YA UVUVI**

**I: HALI YA SEKTA YA UVUVI**

125. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia 2.2 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2016 na wavuvi na wafugaji samaki wapatao 230,977 walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uvuvi. Aidha, zaidi ya Watanzania milioni 4 wameendelea kupata kipato cha kila siku kwa kushiriki shughuli zinazotegemea kuwepo kwa sekta ya uvuvi ikiwemo kutengeza maboti, kushona nyavu, biashara ya samaki na

mazao yake, wachuuzi na mamalishe. Pia, katika mwaka 2017, Sekta ya Uvuvi imekua kwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na 4.2 ya mwaka 2016 (NBS, 2018).

126. **Mheshimiwa Spika,** taarifa za tafiti za Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na Baraza la Kilimo Tanzania zilizofanyika kwa vipindi tofauti zinaonesha kwamba, kiasi cha samaki kilichopo katika maji yetu ni tani 2,736,248 kwa mtawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria tani 2,143,248, Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000, Maji madogo (maziwa madogo ya kati, mito na mabwawa) tani 30,000 na Maji ya Kitaifa ya Bahari ya Hindi tani 100,000 (Kiambatisho Na. 16).

127. **Mheshimiwa Spika,** idadi ya wavuvi na vyombo vya uvuvi imeendelea kuongezeka kutoka wavuvi 183,800 waliotumia vyombo vya uvuvi 57,291 mwaka 2015 hadi wavuvi 203,529 waliotumia vyombo vya uvuvi 59,338 mwaka 2017. Kiasi kikubwa cha nguvu ya uvuvi kikiwa katika ukanda wa Ziwa Victoria ikifuatiwa na Ukanda wa Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu. Kutokana na nguvu hiyo ya uvuvi, uzalishaji wa samaki kwenye maji asili umeongezeka kutoka tani 362,645 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2015 hadi tani 387,543 zenye thamani ya shilingi trilion 1.74 mwaka 2017 (Kiambatisho Na. 17), sawa na ongezeko la asilimia 6.87.

128. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, kati ya tani za samaki zilizozalishwa mwaka 2017, tani 36,063 na samaki hai wa mapambo 101,110 wenye thamani ya shilingi bilioni 407.21 waliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 10.53 kama ushuru (Kiambatisho Na. 18). Hata hivyo, mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi yameendelea kupungua kutoka tani 40,541 zenye thamani ya shilingi bilioni 542.79 mwaka 2015 hadi tani 36,063 zenye thamani ya shilingi bilioni 407.21 mwaka 2017 (Kiambatisho Na. 19) sawa na upungufu wa asilimia 11.04. Upungufu huo unaweza kuwa umesababishwa na ongezeko la mahitaji ya samaki katika soko la ndani

ambapo ulaji wa samaki kwa mtu kwa mwaka umeongezeka kutoka kilo 8.0 mwaka 2016/2017 hadi kilo 8.6 mwaka 2017/2018 (FAO). Vilevile, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 jumla tani 22,961 zenye thamani ya shilingi bilioni 56.12 zimeingizwa nchini ikilinganishwa na tani 13,919.66 zenye thamani ya shilingi bilioni 26.77 zilizoingizwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 (Kiambatisho Na. 20). Aidha, mauzo ya samaki hai wa mapambo yameendelea kuongeza kutoka samaki 87,630 wenye thamani ya shilingi milioni 373.81 mwaka 2015 hadi samaki 101,110 wenye thamani ya shilingi milioni 678.55 mwaka 2017.

129. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, jumla ya leseni 24 zilitolewa kwa meli 24 za uvuvi ikilinganishwa na leseni 28 zilitolewa kwa meli 28 mwaka 2016/2017. Hata hivyo, idadi hii ya leseni imeshuka kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na leseni 96 zilizotolewa mwaka 2015/2016. Hii imetokana na maboresho ya masharti ya leseni yaliyofanywa mwaka 2016 kwa baadhi ya vifungu vya kanuni ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2009. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi katika Bahari Kuu.

130. **Mheshimiwa Spika,** Ukuzaji Viumbe kwenye Maji umeendelea kuhimizwa na kusimamiwa ikiwa ni pamoja na ufugaji samaki, kambamiti, kilimo cha mwani na ukuzaji wa chaza wa lulu kwa ajili ya lishe, ajira, kipato kwa nchi na kuchangia pato la Taifa. Aidha, kumekuwa na ongezeko la teknolojia za kukuza samaki wengi kwenye ujazo mdogo, hususan vizimba na ufugaji wa kutumia maji kidogo yanayozunguka na kusafishwa. Teknolojia ya ufugaji samaki kwenye vizimba/*cage* (chombo ambacho kimetengenezwa kwa fremu ya chuma, mbao, plastiki, au mianzi na kufanya umbo la mstatili, mraba au duara na kuzungushiwa nyavu kwa lengo la kukuzia samaki) imeanza kutekelezwa kwa kuhusisha sekta binafsi katika ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika mwaka 2017/2018 jumla ya vizimba 315 ambavyo vilizalisha tani 1,260 vimewekwa katika maziwa ya Victoria (187), Nyasa (120) na Tanganyika (8)

ikilinganishwa na vizimba 109 (Ziwa Victoria 63, Ziwa Tanganyika 4, Ziwa Nyasa 42) vilivyowekwa mwaka 2016/2017.

131. **Mheshimiwa Spika,** aidha, ufugaji wa kutumia teknolojia ya maji kidogo yanayozunguka na kusafishwa unaendelea kwenye miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Pia, samaki aina ya perege na kambale wameendelea kufugwa katika mabwawa ambapo mabwawa yameongezeka kutoka 22,702 mwaka 2016/2017 hadi mabwawa 24,302 mwaka 2017/2018. Vilevile, uzalishaji wa vifaranga aina ya kambale na perege umefikia vifaranga 813,969 kutoka vituo vya Serikali (243,569) na sekta binafsi (570,400) na uzalishaji wa vifaranga aina ya kambamiti umefikia vifaranga 12,000,000.

132. **Mheshimiwa Spika,** kilimo cha zao la mwani kinachofanyika katika mwambao wa bahari ya Hindi ni miongoni mwa shughuli za sekta ndogo ya ukuzaji viumbe kwenye maji, ambapo jumla ya tani 1,329.5 zenye thamani ya shilingi milioni 469.8 zimevunwa na kusafirishwa nje ya nchi mwaka 2017/2018 zikilinganishwa na tani 1,197.5 zenye thamani ya shilingi milioni 412 zilizovunwa mwaka 2016/2017. Mwani unaozalishwa nchini unauzwa katika masoko ya nchi za Asia za Ufilipino na Uchina kwa kupitia mawakala kwa bei ya shilingi 500 -700 kwa kilo ya mwani mkavu aina ya *Eucheuma cottonii* na shilingi 300 kwa kilo ya mwani mkavu aina ya *Eucheuma spinosum.* Vilevile, mwani unasindikwa na wadau kwa kutengeneza sabuni za mche, sabuni za maji na shampoo ikiwa ni matokeo ya vikundi 10 vilivyopatiwa mafunzo ya kuongeza thamani kwenye zao hilo. Aidha, jumla ya wadau 5,229 walipata elimu ya ukuzaji viumbe kwenye maji katika mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na wadau 4,146 mwaka 2016/2017 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Njombe, Pwani, Ruvuma, Tabora na Tanga.

133. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na hali halisi iliyoelezwa hapo juu, sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; uvuvi na biashara

haramu ya mazao ya uvuvi, upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na sekta ya uvuvi, ukosefu wa vitotoleshi (hatchery), chakula bora cha samaki wafugwao na masoko yasiyokuwa ya uhakika kwa zao la mwani. Kutokana na changamoto hizi, Wizara ilifanya tathmini mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wa sekta. Tathmini hizo ni pamoja na:-

## TATHMINI YA SEKTA YA UVUVI

### Tathmini kuhusu utendaji kazi wa Sekta ya Uvuvi katika Ziwa Victoria

Tathmini kuhusu utendaji kazi wa Sekta ya Uvuvi katika Ziwa Victoria ilifanyika kuanzia tarehe 12, 2017 hadi 27 Desemba, 2017. Uamuzi wa kuendesha tathmini hii ulitokana na Wizara kwa miaka mingi mfululizo kushindwa kufikia malengo ya kukusanya maduhuli, viwanda vya kuchakata minofu ya samaki kukosa malighafi, na samaki wachanga kuuzwa katika masoko mbalimbali hapa nchini. Kutokana na hali hii, Wizara yangu iliamua kuunda timu ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali na sekta binafsi ili kufanya tathmini kuhusu utendaji wa Sekta ya Uvuvi katika Ziwa Victoria, ambapo mambo makubwa yaliyoibuliwa katika tathmini hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. Viwanda vya kuchakata samaki na mazao yake kupungua kutoka viwanda 13 vilivyokuwepo mwaka 1998 hadi viwanda 8 tu vilivyopo sasa. Kupungua kwa viwanda kumetokana na uhaba wa malighafi ya samaki katika viwanda hivyo;

ii. Wastani wa uzalishaji wa samaki viwandani kupungua kutoka tani 1,065 hadi tani 171 kwa siku hivi sasa, ambapo pia ajira zimepungua kutoka 4,088 na kubaki 2,179 kwa sasa katika viwanda hivyo;

iii. Samaki aina ya Sangara wanaoruhusiwa kuvuliwa kisheria (urefu wa sentimenta 50 hadi 85) kubakia

asilimia 3 tu katika Ziwa Victoria ambapo wale wachanga ni asilimia 96.6 na samaki wazazi ni asilimia 0.4 tu;

iv. Kupungua kwa mauzo ya Sangara nchini kutoka tani 53,675 kwa mwaka 2005 hadi tani 26,045 kwa mwaka 2016 sawa na upungufu wa takribani asilimia 50 katika kipindi cha miaka 10;

v. Samaki aina ya Sangara wanaovuliwa katika maeneo ya mipakani kutoroshwa kwa magendo na kupelekwa katika viwanda vya nchi jirani za Kenya na Uganda ambapo kutokana na utoroshaji katika miaka ya hivi karibuni mauzo ya Sangara ya Tanzania na Kenya yamekuwa yakilingana wakati Tanzania inamiliki asilimia 51 ya Ziwa Victoria na Kenya inamiliki asilimia 6 tu ya Ziwa hilo;

vi. Wapo raia wa kigeni ambao wanajishughulisha na biashara ya samaki ambapo wanakwenda hadi visiwani kukusanya mazao ya uvuvi kinyume cha Sheria na mara nyingine hutumia leseni na vibali vya watanzania, pia leseni moja imekuwa ikitumiwa na wafanyabiashara zaidi ya mmoja. Hali hii imekuwa ikiwapotezea fursa Watanzania na Serikali kukosa mapato;

vii. Uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi imekithiri katika Ziwa Victoria na inakadiriwa kufikia kati ya asilimia 75 hadi 90 ya uvuvi wote ziwani humo, kiwango hiki ni kikubwa zaidi duniani kinachohusisha zana haramu ili kujipatia samaki wengi kwa wakati mmoja. Matumizi ya zana haramu katika uvuvi yanateketeza samaki na mazalia yake kwa wingi;

viii. Halmashauri zinakusanya fedha nyingi zitokanazo na mazao ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Victoria hata hivyo sehemu ya fedha hizo hazitengwi kuendeleza sekta ikiwemo kuendesha doria za kupambana na kudhibiti uvuvi na biashara haramu. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa mwaka 2016/2017 makusanyo yatokanayo na uvuvi yalikuwa milioni 670.56 lakini uvuvi haramu umeshamiri katika maeneo hayo;

ix. Kwa mwaka 2016/2017, mazao ya uvuvi yaliyosafirishwa kwenda nchi jirani ya Zambia na Malawi kupitia mikoa ya Mbeya na Songwe ni kilo 9,020,000 za dagaa na furu. Hata hivyo, takwimu kutoka vituo vya mpakani vya Wizara vya Kasumulo na Tunduma zinaonyesha jumla ya kilo 3,621,100 tu ndizo zilipitishwa na kulipiwa mrabaha, hivyo jumla ya kilo 5,398,900 hazikuonekana kupitishwa kwenye vituo hivyo, hali inayoonyesha mazao hayo yalivushwa kwa magendo na kuikosesha Serikali mapato ya shilingi 982,750,969.20;

x. Katika mpaka wa Sirari (Tanzania na Kenya), jumla ya kilo 1,044,500 za dagaa zilisafirishwa kwenda Kenya kupitia kituo cha Sirari. Hata hivyo, kilo 288,000 tu za dagaa zilionekana kupitishwa na kulipiwa mrabaha. Hivyo, jumla ya kilo 876,500 zilisafirishwa kwa njia za magendo na kuipotezea Serikali mapato ya kiasi cha shilingi 159,547,542;

xi. Imebainika kwamba mawakala wa samaki viwandani na wasafirishaji wa samaki nje ya nchi hukwepa kufanyiwa makadirio na TRA kwa kutokutaja thamani halisi ya mauzo na udanganyifu wa mapato yatokanayo na biashara zao. Aidha, imefahamika kuwa mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 581.5. hayakufanyiwa makadirio ya kodi na TRA katika mwaka wa fedha 2016/2017 na hivyo kuikosesha Serikali mapato; na

xii. Kutokana na kushamiri kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Victoria, mapato ya Serikali yanayokusanywa kutokana na mazao ya uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (MSM) inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 25 kwa sasa.

Kutokana na changamoto hizi, Wizara yangu iliamua kufanya operesheni mbalimbali ili kupambana na uvuvi haramu pamoja na kudhiti upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali, operesheni hiyo kwa jina maarufu "*Operesheni Sangara 2018*"

### (i) Operesheni Sangara 2018

134. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaendesha Operesheni Sangara 2018 kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria, naomba sasa nitoe kwa kifupi matokeo ya Operesheni tangu ianze.

(a) Ukaguzi wa viwanda vyote vya uchakataji wa samaki vinavyofanya kazi ambavyo vinafikia 10 (Mwanza 5, Mara 1, Kagera 2, Dar es Salaam 1 na Tanga 1) ambapo vyote vimekutwa na makosa na kupigwa faini;

(b) Viwanda vitatu (3) vya kutengeneza nyavu na Viwanda vya kuchakata mabondo 12 vyote vimekutwa na makosa na kupigwa faini;

(c) Wavuvi na wafanyabiashara mbalimbali wapatao 2,610 wamefanyiwa ukaguzi na kupatikana na makosa. Aidha, samaki wachanga na wazazi waliovuliwa kwa njia haramu wapatao kilo 136,031 walitaifishwa na kugawiwa taasisi za umma na wananchi. Vilevile, mazao ya uvuvi yakiwemo kayabo kilo 178,244 na mabondo kilo 5,052 yalikamatwa yakiwa yanatoroshwa kwenda nchi jirani ambapo yalitaifishwa na kupigwa mnada;

(d) Ukaguzi wa magari yanayojihusisha na biashara ya samaki yakiwemo malori na mabasi ya abiria ulifanyika ambapo pikipiki 73, magari 119, injini za mitumbwi 494 na mitumbwi 985 ilikamatwa kwa makosa ya kujihusisha na uvuvi haramu;

(e) Jumla ya zana haramu 539,128 (nyavu 529,654 na makokoro 9,474) pamoja na kamba za kuvutia makokoro mita 511,693 zilikamatwa na kuondolewa ziwani na kisha kuteketezwa kwa moto baada ya kupata kibali cha Mahakama. Zana hizi haramu kama zingeendelea kubaki katika Ziwa Victoria, viwanda vingefungwa na shughuli za uvuvi zingekoma;

(f) Jumla ya kiasi cha shilingi 7,029,336,293/= zimekusanywa kutokana na mauzo ya samaki, kayabo na mabondo pamoja na faini katika Operesheni hii. Tangu kuanza kwa operesheni hii, makusanyo ya maduhuli katika ukanda wa Ziwa Victoria yameongezeka kwa asilimia 300. Kwa mfano, makusanyo katika soko la samaki la Kirumba kwa miezi mitatu kabla ya operesheni yalikuwa shilingi milioni 104 (Oktoba, Novemba na Desemba 2017) na baada ya Operesheni kuanza makusanyo yaliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 335.67 (kwa miezi ya Januari, Februari na Machi 2018). Ongezeko hili ni mara tatu ya makusanyo ya awali. Mapato haya yameongezeka licha ya kuwa nyavu nyingi zimeondolewa ziwani;

(g) Jumla ya Viongozi/Watumishi wa Umma wapatao 35 wamepatikana na kujihusisha na uvuvi haramu kwa njia moja ama nyingine wakiwemo Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Maafisa Uvuvi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Watendaji wengine wa Serikali. Kwa mfano, katika Kisiwa cha Lubiri wilayani Muleba kilo 65,000 za kayabo zilizokuwa zimevuliwa kwa njia haramu zilikamatwa huku wakiwepo watendaji na viongozi katika eneo hilo na hawakuwahi kuchukua hatua yoyote. Hii ni kinyume cha katiba ya nchi, sheria na kiapo cha Maadili ya Utumishi wa Umma;

(h) Operesheni ilifanikiwa kumkamata mvuvi haramu maarufu anayemiliki mitumbwi zaidi ya 1,000, katika ukanda wa Ziwa Victoria ambaye alikutwa na nyavu 23,291 na marobota 25 ya nyavu haramu mpya na injini 5 ambapo amefikishwa mahakamani na kufunguliwa mashitaka ya uhujumu uchumi (Economic Crime Case No. 10/2018);

(i) Kiasi cha shilingi 1,625,324,951/= kimetumika kugharamia Operesheni hiyo kulipia matengenezo ya boti, magari, mafuta na posho za watumishi wanaohusika katika operesheni hii;

(j) Wananchi wengi hususan wavuvi, wamesalimisha zana haramu na sasa wameitikia wito wa

kuanza kutumia zana halali na rafiki kwa mazingira. Pia, wananchi wengi wanapongeza operesheni hii kutokana na kuongezeka kwa samaki na kwamba hata samaki wakubwa waliowakosa kwa muda mrefu wameanza kupatikana sasa.

135. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizoainishwa hapo juu kuhusu uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, Wizara yangu imeamua kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuanza mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya kusimamia rasilimali za uvuvi hapa nchini ili kuleta suluhisho la kudumu katika kunusuru rasilimali hizi ambazo kwa sasa zinavunwa kiholela, kutoroshwa nje ya nchi na Serikali kukosa mapato;

(b) Kuweka ulinzi imara na kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato ambayo itapelekea kuongezeka kwa mapato zaidi ya mara 10 ya ilivyo sasa. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, TRA na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kufanya operesheni hadi kuutokomeza uvuvi na biashara haramu;

(c) Kuendelea kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ya kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za uvuvi katika maeneo yao na kuweka miundombinu kwa ajili ya shughuli za uvuvi;

(d) Kuandaa utaratibu wa kuwezesha Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Idara ya Uvuvi) kusimamia Mialo na Masoko ya Kimataifa ya Samaki badala ya Halmashauri kama ilivyo hivi sasa;

(e) Kuendelea kuwachukulia hatua Watendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanaojishughulisha na uvuvi na biashara haramu kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za Utumishi wa Umma;

(f) Kushauri Mamlaka husika kuwachukulia hatua viongozi wa kisiasa na watendaji wa Serikali wanaoshiriki na kufadhili uvuvi haramu; na

(g) Kuishauri TRA ifanye makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi waliokwepa kulipa mapato ya Serikali mwaka 2016/2017 ambapo inakadiriwa kwamba mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 581.5 hayakufanyiwa makadirio na TRA na hivyo kuikosesha mapato Serikali.

### (ii) Operesheni Jodari 2018

136. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kitaifa (Mult Agency Task Team - MATT) cha Kuzuia Uhalifu wa Kimazingira na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa msaada wa Taasisi ya Kimataifa ya *Sea Shepherd Global* inaendesha Operesheni Jodari katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Hindi ambayo itadumu kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 15 Januari hadi Juni, 2018.

Madhumuni ya operesheni hii ni kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu ikiwemo uhaulishaji wa samaki (transhipment) baharini, kutoripoti takwimu sahihi za samaki waliovuliwa, umwagaji wa samaki wasiokusudiwa na kujihusisha na biashara ya mapezi ya papa ambayo inahatarisha juhudi za uhifadhi wa rasilimali za uvuvi pamoja na uchafuzi wa mazingira na kuhakikisha uvuvi unaendana na maazimio ya kikanda ya kupambana na uvuvi haramu (IOTC Port State Measures). Matokeo ya operesheni hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Katika awamu ya kwanza meli tano (5) kati ya 24 zilizopewa leseni ya uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari kuu ya Tanzania (EEZ) zilikaguliwa. Meli hizo zilishusha tani 12.3 za samaki wasiolengwa (by catch) kwenye bandari za hapa nchini, kuuzwa na kuingiza mapato ya jumla shillingi milioni 41.04 (USD 17,860) (Kiambatisho Na.21). Aidha

kati ya meli tano (5) zilizokaguliwa, meli mbili (2) zilipatikana na makosa, meli tatu (3) ziliruhusiwa baada ya kutoonekana na makosa;

(b) Meli ya Buah Naga Na. 1 (Malaysia) ilikamatwa kwa makosa ya kukutwa na mapezi na mikia ya papa 30 bila miili, vikiwa na uzito wa kilo 90. Aidha, Meli haikuwa na Cheti cha Usalama wa Meli na Nahodha alikutwa na bastola aina ya Bereta pamoja na risasi 10 ambayo haikuwa na kibali chochote. Hivyo aliamriwa kulipa faini ya Dola za Kimarekani 350,000 sawa na shilingi milioni 770 ambapo alitakiwa kulipa faini hiyo ndani ya siku saba (7). Hata hivyo, alishindwa kulipa faini na kesi ilipelekwa katika Mahakamani Kuu ya Mtwara;

(c) Meli ya Tai Hong One (China) ilikutwa na makosa ya kuwa na mikia ya papa 44 bila miili, uchafuzi wa mazingira, mabaharia kupewa chakula kilichokwisha muda wake, kufanya njama za kufaulisha mabaharia kutoka meli nyingine za Kampuni hiyo TAI HONG Na. 2, Na. 5, Na. 6, Na. 8 na JI SHENG Na. 2 kuwezesha meli hizo kutoroka na kuzuia ukaguzi na mwangalizi (Obsever) kufanya kazi zake. Pia, meli hii ilifanikiwa kutoroshwa bandarini lakini Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu ilifanikiwa kuitoza faini ya shilingi bilioni moja kwa kufanya kosa hilo; na

(d) Meli 19 zilitoroka bila kukaguliwa, hata hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu iliitoza faini ya kiasi cha shilingi bilioni moja kila meli.

**(iii) Operesheni MATT**

137. **Mheshimiwa Spika,** katika ukanda wa pwani uvuvi haramu wa kutumia mabomu ulikuwa umeshamiri ambapo mabomu yalilipuliwa kila kona. Kutokana na hali hiyo raslimali za uvuvi zilipungua sana katika maeneo hayo kwani mabomu yakilipuliwa huua viumbe vyote vikiwemo mayai, vifaranga na mazalia na kuharibu mfumo mzima wa ikolojia na mazingira ya bahari (bomu moja likipigwa lina uwezo wa kuharibu eneo la mzunguko wa mita kati ya 15-20). Aidha, samaki waliovuliwa kwa mabomu asilimia 75-90

hupotelea kwenye maji, watu wengi wamepoteza maisha na wengine kupata vilema vya maisha, kutishia usalama na maisha ya wananchi na watalii kuogopa kuja nchini wakihofia usalama wao.

138. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kitaifa cha MATT tunaendelea na Operesheni dhidi ya uvuvi haramu katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga ili kudhibiti uvuvi haramu hasa wa mabomu. Operesheni hii itaendelea bila kukoma hadi hapo uvuvi haramu wa mabomu utakapotokomezwa. Matokeo ya operesheni hiyo ni pamoja na mtandao wa walipuaji mabomu umesambaratishwa, kukamatwa kwa mabomu ya milipuko 720, V-6 Explosives vipande 600, detonator 362, mbolea ya Urea kilo 324, mitungi ya gesi 68, vifaa vya kuzamia jozi 252 na Compressors 12. Pia, kutokana na Operesheni hii idadi ya milipuko imepungua kwa asilimia 88 kufikia mwezi Machi, 2018.

139. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya SMARTFish iliwezesha Wizara kupitia MATT kufanya operesheni ya kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu na nyavu zisizoruhusiwa kisheria katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga kuanzia tarehe 15 Machi, 2018 hadi tarehe 31 Machi, 2018. Matokeo ya operesheni ni kukamatwa kwa kilo 928 za kaa hai wachanga chini ya gramu 500, gari 1, "compressor" 2; mitungi ya kuzamia 81; utambi meta 900; "detonator" 1,814; "regulators" 6; miwani ya kuogelea jozi 2; "pressure gauge" 1, makokoro 173, "monofilament" 13, mbolea ya urea kilo 515, vilipuko (explossive gel) 9 na pikipiki 1. Vilevile, watuhumiwa 32 walikamatwa, kesi 13 zilifunguliwa Mahakamani na faini ya shilingi milioni 15.45 zilikusanywa**.** Katika operesheni hii SmartFish imechangia gharama kiasi cha shilingi 114,387,000/=.

140. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendesha doria za kawaida zenye siku kazi 4,113 katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ukanda wa Bahari ya Hindi pamoja na nchi kavu katika maeneo ya viwanja vya Ndege, Bandarini na mipakani. Doria hizo

ziliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zikiwemo makokoro 961, kamba za kokoro mita 800,360, nyavu ndogo za makila 27,271, nyavu za utali 2,381, mitungi ya gesi 114, baruti 4,312, detonators 358, compressors 12, kilo 302 za Urea, regulators 21, vipande vya "boosters" 943, injini za boti 13 na boti 89. Pia, kilo 16,478 za sangara wachanga, kilo 16,557 za dagaa, kilo 140 za kaa, kilo 9 za majongoo bahari, na makombe 104. Kutokana na uhalifu huo, jumla ya watuhumiwa 241 walikamatwa na kesi 21 kufunguliwa mahakamani.

141. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth - SWIOFish) ilifanya semina kuhusu madhara ya uvuvi haramu wa kutumia milipuko kwa wadau 140 wakiwemo mahakimu, viongozi wa dini, madiwani, wapelelezi, waendesha mashtaka, Maafisa Uvuvi katika Halmashauri 14 za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi za Tanga, Mkinga, Pangani, Bagamoyo, Kigamboni, Temeke, Ilala, Kinondoni, Mkuranga, Mafia, Kibiti, Kilwa, Lindi na Mtwara. SWIOFish imechangia kiasi cha shilingi 102,162,000/= kufanikisha mafunzo hayo.

142. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kusimamia na kuimarisha usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya doria za kawaida zenye siku kazi 6,000. Aidha, itawezesha MATT kutekeleza kazi zake kwa kufanya operesheni 12 katika maji bahari na kupanua majukumu ya MATT hadi maji baridi. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu na mafunzo kwa wavuvi na wadau wengine kuhusu madhara ya uvuvi haramu na faida za uvuvi endelevu.

### (b) Tathmini ya kituo cha Kisiju-Pwani na Kimu-Pangani

143. **Mheshimiwa Spika,** tathmini ya kufuatilia uwezekano wa kituo cha zamani cha kupokelea samaki Kisiju-Pwani na kituo cha Kimu-Pangani ilifanyika kuanzia tarehe 8

Machi, 2018 hadi tarehe 12 Machi, 2018 na kuanzia tarehe 23 Novemba, 2017 hadi tarehe 27 Novemba, 2017 mtawalia. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa vituo vya Kisiju-Pwani na Kimu-Pangani vina sifa ya kuwa vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji bahari. Aidha, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati ya kuendeleza vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji vya Kingolwira (Morogoro), Machui (Tanga), Mwamapuli (Tabora) na Ruhila (Ruvuma). Aidha, Kituo cha Ufugaji samaki cha Kingolwira kimewezeshwa kwa kuwekewa mfumo wa maji, kufungiwa vitotoleshi 20 na kuanza uzalishaji unaokadiriwa kufikia vifaranga takriban milioni 15 kwa mwaka. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Ukuzaji Viumbe kwenye Maji kwa kipindi cha mwaka 2018-2025 ambao utapitiwa na wadau kipindi cha 2018/2019 kabla ya kuanza kutekelezwa.

**(c) Ukaguzi wa Ufanisi wa Kazi katika Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

144. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa utendaji kazi (Performance Audit) wa Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2016/2017. Katika vigezo 24 vya kiukaguzi vilivyowekwa vyote vilionyesha udhaifu mkubwa wa kiutendaji na kiutawala. Matokeo ya ukaguzi huo yalibaini mapungufu mbalimbali yakiwemo utoaji wa vibali kiholela, doria hafifu, uratibu na usimamizi dhaifu wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametoa mapendekezo ya kuboresha utendaji kazi wa kitengo. Katika utekelezaji wa mapendekezo hayo, niliamua kuvunja Bodi ya Wadhamini na kumsimamisha kazi Meneja wa Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu, huku mapendekezo mengine yakiendelea kutekelezwa na Wizara yangu.

145. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza maagizo ya kikanda ya usimamizi wa rasilimali

za uvuvi kama yanavyotolewa mara kwa mara. Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Sekta ya Uvuvi wa nchi za Afrika mashariki kilichofanyika tarehe 2 Machi 2018 kilitoa maagizo mbalimbali ya kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa rasilimali ya Sangara kwa nchi hizo yakiwemo:-

(i) Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Taasisi ya LVFO kuendesha operesheni za kuondoa uvuvi haramu katika Ziwa Victoria. Kwa ombi la Wizara yetu nchi hizo zilikubaliana kuchangia fedha kiasi cha Dola za Marekani 600,000 kwa kila nchi ili kuendesha Operesheni Okoa Sangara katika Ziwa Victoria.;

(ii) Nchi hizo zimekubali kufanyia kazi matokeo ya utafiti kwa kuzihuisha Sheria na kanuni za usimamizi wa mazao ya uvuvi katika Ziwa Victoria, pia tumekubaliana kuwa samaki aina ya sangara wavuliwe wakiwa na urefu kati ya sentimita 50 hadi 85 na nyavu za inchi saba (7) kwa uvuvi wa sangara na milimita 10 kwa nyavu za dagaa ili kuruhusu rasilimali hizo kuzaliana; na

(iii) Taasisi za Uvuvi katika nchi wanachama kufanya utafiti wa athari ya nyavu za makila zilizounganishwa (gillnet paneling) kwa uvuvi wa Sangara katika Ziwa Victoria. Kwa upande Tanzania Wizara imeiwezesha TAFIRI kukamilisha utafiti huo. Matokeo ya utafiti huo yataunganishwa na matokeo ya utafiti yaliyofanywa na taasisi ya utafiti nchini Uganda (NaFIRRI) ili kuwa na maamuzi ya pamoja kwa nchi zote tatu (Tanzania, Uganda na Kenya) mwishoni mwa mwezi Mei, 2018 ili kutoa maamuzi ya nyavu zipi ziruhusiwe kwa uvuvi wa Sangara kwa nchi zote tatu.

## II: MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2018/2019

### MAKUSANYO YA MADUHULI

146. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Fungu 64 ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi

19,700,628,051. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2018 kiasi cha shilingi 21,280,222,364.48 kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia 108.02 ikilinganishwa na **shilingi 16,019,668,687/=** zilizokusanywa kuanzia mwezi Julai 2016 hadi tarehe 30 Aprili 2017.

**MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI MWAKA 2018/2019**

147. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 21,534,305,600. Vyanzo vya fedha hizo vitatokana na marekebisho katika ada, tozo na kodi mbalimbali zinazotozwa katika sekta ya uvuvi. Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na:- Leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (Export Licences); Leseni ya uingizaji wa mazao ya uvuvi (Import Royalty); ushuru wa mrabaha (Export Royalty); tozo ya maabara; na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**FEDHA ZILIZOIDHINISHWA**

148. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018 Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi 18,640,171,549/=. Kati ya kiasi hiki, shilingi 16,640,171,549/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 2,000,000,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**MATUMIZI YA BAJETI YA KAWAIDA**

149. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi 16,640,171,549/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi, shilingi 11,541,915,171/= ni mishahara na shilingi 5,098,256,378/= ni Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, jumla ya shilingi 11,471,511,750/= zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia 68.94 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 6,687,703,000/= ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na shilingi 4,783,808,750/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

## MATUMIZI YA BAJETI YA MAENDELEO

150. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2017/ 2018, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha shilingi 2,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, hakuna fedha za ndani za maendeleo zilizotolewa. Aidha, Mradi wa Maendeleo na Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), katika mwaka 2017/2018, mradi ulitengewa kutumia fedha za nje shilingi 8,335,404,000 (Dola za Kimarekani 3,788,820.00). Hadi kufikia Aprili, 2018 mradi huu umetumia jumla ya shilingi 3,699,878,758.90 (Dola za Kimarekani 1,638,564.55), ambayo ni sawa na asilimia 43.2.

## III: MAENEO YA VIPAUMBELE

151. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018 na 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi nchini ilianisha na kutekeleza maeneo ya vipaumbele yaliyohusu utekelezaji wa sekta ya uvuvi. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo**:-**

(i) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu na viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi;

(ii) Kuimarisha, kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi pamoja na kutunza mazingira;

(iii) Kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi;

(iv) Kuhamasisha, kuendeleza na kusimamia ufugaji wa samaki na viumbe wengine kwenye maji;

(v) Kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi; na

(vi) Kufanya Sensa ya Uvuvi.

## IV: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### SERA, SHERIA, MIKAKATI NA PROGRAMU

152. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia uandaaji, mapitio na utekelezaji wa Sera, Mikakati, Sheria, Miongozo, mipango na Programu mbalimbali za kuendeleza Sekta ya Uvuvi Nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha raslimali za uvuvi zinalindwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa njia ambayo ni endelevu kwa faida ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo. Wizara imesambaza kwa wadau nakala 50 za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 na 30 za Fursa za Uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Pia, Serikali imeendelea kusimamia mipango ya kusimamia rasilimali za uvuvi zikiwemo Mpango wa usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji kwa wavuvi wadogo, Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Kambamiti na Mpango wa kusimamia rasilimali ya Pweza pamoja na Mkakati wa Kusimamia Samaki aina ya Jodari.

153. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imetafsiri Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 katika lugha ya Kiswahili ili kuwezesha wadau, hususan wavuvi wadogo kuielewa na hivyo kurahisisha utekelezaji wake. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kutekelezaji Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015 na Sera ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu. Utekelezaji wa mkakati huu utaimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa maendeleo ya sekta. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ambapo kufikia Julai 2018 Shirika litaanza kazi. Kuwepo kwa shirika hili kutawezesha nchi yetu kuwa na meli za kitaifa (National Fleet) kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu ili kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

154. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu itakamilisha Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuboresha Sekta ya Uvuvi na

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Pia, itafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Uvuvi Tanzania (Tanzania Fisheries Master Plan) wa mwaka 2015. Vilevile, Wizara itafufua Shirika la Uvuvi (TAFICO).

155. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za uvuvi ikiwemo Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994, Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na Marekebisho yake ya mwaka 2007 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2016. Pia, kwa kushirikiana na wadau, Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza Sheria za Sekta Mtambuka ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Katika Mwaka 2018/2019, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 ili kupanua maeneo ya hifadhi kwenye maji baridi na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998 na marekebisho yake ya mwaka 2007 na kuandaa kanuni mpya za kutekeleza Sheria mpya ya Uvuvi.

## USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI

156. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia rasilimali za uvuvi katika bahari, maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika, Nyasa pamoja na maziwa ya kati, madogo, mito na mabwawa. Nguvu kubwa ikielekezwa kwenye mavuvi ya kipaumbele kiuchumi na uhakika wa chakula yakiwemo mavuvi ya sangara, dagaa, sato, kambamiti, kambakoche pamoja na pweza. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya wavuvi wadogo 203,529 wanaotumia vyombo vya uvuvi 59,338 walijihusisha moja kwa moja na shughuli za uvuvi nchini katika maji baridi na maji bahari ya Kitaifa. Wavuvi hao waliwezesha kuvunwa kwa tani 387,543 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.74 (Kiambatisho

Na. 22). Aidha, uvuvi kwenye maji baridi ulichangia asilimia 85.76 ya mavuno yote ya samaki nchini na maji bahari asilimia 14.24. Hali ya usimamizi na uvunaji wa samaki kwenye maji yetu ni kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho Na. 23, 24, 25a na 25b.

157. **Mheshimiwa Spika,** kulingana na Sheria na Kanuni za Uvuvi samaki aina ya Sato hawaruhusiwi kusafirisha nje ya nchi ili kulinda soko la ndani na lishe bora kwa wananchi. Aidha, Wizara inafanya mapitio ya kanuni hizo ili kuruhusu samaki aina ya Sato kuuzwa nje ya nchi kuanzia mwezi Julai 2018. Pia, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi samaki aina ya sato wanatakiwa kuvuliwa wakiwa na urefu kuanzia sentimeta 25 ili kuepuka kuvua sato wachanga. Sheria hii inasisitizwa pia katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Masharika kupitia Taasisi ya LVFO ambazo kwa pamoja zimekubaliana samaki aina ya Sato avuliwe akiwa na urefu usiopungua sentimeta 25 ili kuruhusu rasilimali hiyo kuzaliana na kuongezeka.

158. **Mheshimiwa Spika,** samaki wa mapambo ni moja kati ya zao linaloingiza fedha za kigeni kwa Taifa kutokana na ushuru wa mauzo ya samaki hao nje ya nchi. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya samaki 87,630 wenye thamani ya Shilingi bilioni 2.45 waliuzwa na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi milioni 373.81 kama ushuru ikilinganishwa na samaki 45,070 wenye thamani ya shilingi milioni 368.15 walioingiza ushuru wa shilingi miloni 47.80 mwaka 2016 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 48.57. Aidha, idadi ya samaki wa mapambo waliouzwa nje ya Nchi imeongezeka kwa asilimia 124.34 na kufikia samaki 101,110 ambao waliliingizia Taifa jumla ya milioni 95.18 mwaka 2017. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa nguvu ya uvunaji wa rasilimali hii na kupanuka kwa mahitaji ya samaki mapambo katika nchi za Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu uvunaji na biashara ya samaki wa mapambo nchini.

159. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, jumla ya tani 123,970 za dagaa zenye thamani ya shilingi

milioni 557.87 zilivuliwa ikilinganishwa na tani 111,421 zenye thamani ya shilingi milioni 460.92 zilizovuliwa mwaka 2016/2017 ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.26. Ongezeko hili linaweza kuwa limetokana na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi wa dagaa na kupungua kwa samaki wengine ziwani, hususan Sangara ambao hutegemea dagaa kwa chakula. Pia, jumla ya tani 120,212 za dagaa wabichi kutoka Ziwa Victoria ziliuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na tani 106,272 zilizouzwa mwaka 2016/2017 na tani 4,570.11 za dagaa wakavu wenye thamani ya shilingi bilioni 8.26 walisafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 5,149 zilizouzwa mwaka 2016/2017.

160. **Mheshimiwa Spika**, kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa katika Ziwa Victoria chini na Taasisi za Utafiti za Nchi za Kenya Uganda na Tanzania kupitia Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization- LVFO), dagaa katika Ziwa Victoria wanatakiwa kuvuliwa kwa kutumia nyavu zenye macho kuanzia milimita 10. Vilevile, ili kuepuka kuvua dagaa wachanga, wavuvi wanaelekezwa wavue umbali wa zaidi ya Kilomita 2 kutoka ufukweni mwa visiwa au nchi kavu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za uvuvi wa dagaa ili kuwa na uvuvi endelevu wa rasilimali hiyo.

161. **Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa mauzo ya samaki kutoka maji bahari ya Kitaifa kwa baadhi ya aina ya samaki katika mwaka 2017 ni kama ifuatavyo. Kaa hai 1,007,230 wenye thamani ya shilingi bilioni 5.97 walisafirishwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 1.11 kama ushuru ikilinganishwa na kaa hai 272,848 wenye thamani ya shilingi bilioni 8.45 mwaka 2016 zilizoliingizia Taifa jumla ya shilingi milioni 354.99 kama ushuru. Uvunaji wa kaa hai umekuwa ukiongezeka kwa sababu ya kuongezeka kwa mahitaji ya kaa hai katika soko la Asia na hususan nchini China. Aidha, katika mwaka 2017 kambakochi hai 331,310 na waliogandishwa tani 6.44 wote wakiwa na thamani ya shilingi bilioni 1.49 waliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi milioni 330.22 kama ushuru ikilinganishwa na

kambakochi hai 1,051,194 na tani 78.2 za kambakochi waliogandishwa wenye thamani ya shilingi bilioni 120.69 waliouzwa nje nchi mwaka 2016 na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 1.74 kama ushuru.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za uvuvi katika maji ya Kitaifa ya Bahari ya Hindi ili kuwa na uvuvi endelevu wa rasilimali hiyo.

162. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefungua uvuvi wa kambamiti kwa msimu, kila tarehe 01 Aprili hadi tarehe 31 Agosti na kufungwa kila tarehe 01 Septemba hadi tarehe 31 Machi ya kila mwaka kwa wavuvi wote ili kuruhusu kuzaliana. Katika mwaka 2017, meli 12 zilikidhi vigezo vya kufanya uvuvi huo. Hata hivyo, meli moja tu ilifanikiwa kuvua tani 16.61 na wavuvi wadogo waliweza kuvua tani 1.98 za Kambamiti. Katika mwaka 2018, uvuvi huu umefunguliwa kwa wavuvi wote wakubwa na wadogo kuanzia tarehe 01 Aprili 2018 hadi tarehe 31 Agosti na jumla ya meli nane (8) zimekidhi vigezo vya awali vya kuingiza meli za uvuvi kati ya 11 zilizowasilisha maombi. Taratibu za kukagua meli hizo zitafanyika mara baada ya kuwasili kwa meli hizo. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu uvunaji wa samaki kwenye maji ya Kitaifa ya Bahari ya Hindi. Aidha, itaendelea kusimamia na kuratibu uvuvi wa kambamiti, hususan wavuvi wakubwa na kati na kupitia Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi wa kambamiti wa mwaka 2012.

163. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Samaki aina ya Pweza wameendelea kupatikana katika maeneo ya Mafia, Tanga na Mtwara na jumla ya tani 2,121.46 zilivuliwa. Aidha, mwenendo wa uzalishaji wa Pweza umeendelea kushuka kutoka tani 3,395.75 mwaka 2011/2012 hadi tani 2,121.5 mwaka 2017/2018 ambao ni pungufu kwa asilimia 37.52. Pia, biashara ya Pweza inahusisha Pweza waliogandishwa ambapo hadi sasa kuna viwanda vinne (4) vinavyojihusisha na uchakataji wa Pweza vya AlphaKrust (Dar es Salaam), Tanpesca (Mafia), Bahari Food Ltd (Dar es Salaam)

na Kawthar (Dar es Salaam). Viwanda hivi huuza mazao yake katika soko la Nchi za Jumuiya ya Ulaya. Katika mwaka 2017/ 2018, tani 1,102.51 za Pweza zenye thamani ya shilingi bilioni 2.82 ziliuzwa nje na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi milioni 526.87 kama ushuru.

164. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia rasilimali ya Pweza, Wizara imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Pweza (Octopus Fishery Management Plan). Mpango huu umeainisha mipango na mikakati ya kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya Pweza. Katika kutekeleza Mpango huu, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo taasisi ya World Wide Fund (WWF) imehamasisha jamii za wavuvi katika maeneo ya Somanga, Songosongo (Kilwa) na Mafia kutekeleza ufungaji wa hiari wa uvuvi wa Pweza kwa muda kulingana na hali halisi ya uvuvi kwenye mwamba husika. Katika mwaka 2017/2018, Somanga na Songosongo walifunga uvuvi wa Pweza Mwezi Novemba, 2017 na kufungua Mwezi Februari, 2018. Matokeo ya ufungaji huu ni kuongezeka kwa uzito wa Pweza kwa zaidi ya kilo moja ambapo kiwango cha uzito wa juu ilikuwa ni kilo tano kwa Pweza mmoja ikinganishwa na uzito wa Pweza chini ya nusu kilo kwa Pweza katika maeneo ambayo hayajafungwa.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya Pweza na kuhamasisha jamii za wavuvi katika maeneo ya Mkoa wa Tanga, Mtwara na Mafia kutekeleza mpango wa ufungaji wa uvuvi wa Pweza kwa hiari.

**HALI YA UVUVI KATIKA BAHARI KUU**

165. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Mamlaka imeboresha mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za meli na uvuvi wa samaki kwa kuanzisha Kanzidata (Web Based Database) na Kuendelea kukusanya takwimu za uvuvi wa samaki aina ya Jodari na jamii zake unaofanyika katika EEZ. Aidha, Mamlaka imeendelea kukusanya takwimu za uvuvi wa Jodari kwa wavuvi wadogo ambapo jumla ya tani 9 za Jodari zilivuliwa katika Wilaya tano za Mfano (Mtwara Vijijini,

Kilwa, Mafia, Kinondoni, na Tanga jiji,) kwa upande wa Tanzania bara na tani 10 za Jodari zilivuliwa katika Wilaya mbili za Wete-Pemba na Kaskazini "A" Unguja kwa upande wa Zanzibar. Vilevile, Mamlaka iliweka waangalizi wa shughuli za uvuvi katika meli wa tatu (3) katika meli zilizopewa leseni ili kukusanya takwimu na kufanya ulinganifu wa takwimu hizo na zile zinazotumwa na meli hizo ambapo jumla ya tani 2,247.4 za jodari kutoka katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ziliripotiwa kuvuliwa.

166. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ilitoa leseni za uvuvi kwa meli 24 za kuvua katika eneo la Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari ya Tanzania, ambapo katika ya hizo meli 23 zinapeperusha bendara yaTaifa la China na meli moja ina peperusha bendara ya Taifa la Malaysia. Kutokana na leseni hizo shilingi bilioni 1.48 (USD 658,880) zimekusanywa. Pia, meli 23 zenye bendera ya nchi ya China zilitoa ajira kwa Mabaharia wa kitanzania 46. Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na Wadau imefanya doria za kawaida za anga na baharini zenye jumla ya masaa 288 ili kupambana na uvuvi haramu na kufuatilia mienendo ya meli za uvuvi kwenye eneo la Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari ya Tanzania. Doria za anga zilifadhiliwa na Programu ya IOC-SMARTFish na Mradi wa SWIOFish kwa kutumia ndege aina ya Cessna (twin engine) ya Kampuni ya Tan Win Aviation ya Tanzania na ndege aina ya Dornier ya Coast Guard Mauritius. Aidha, doria za baharini zilifanyika kwa kutumia meli ijulikanayo kama Ocean Warriors ya Taasisi ya Kimataifa ya Sea Shephered Global ya Uholanzi.

167. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2018/ 2019, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) itaendelea kufuatilia na kutathmini vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregating Devices-FADs) vilivyowekwa katika maeneo ya Bagamoyo na Nungwi. Aidha, Mamlaka itafanya doria za anga na za baharini zenye jumla ya masaa 144 ili kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu katika EEZ ya Tanzania. Pia, itaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Samaki aina ya Jodari katika Bahari ya Hindi.

## HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU

168. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (Marine Parks and Reserve Unit –MPRU) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za baharini na pwani kupitia Hifadhi tatu (3) na Maeneo Tengefu 15. Katika mwaka 2017/2018, doria zenye siku kazi 420 zilifanyika na kuwezesha kukamatwa na kutaifishwa vyombo vya uvuvi vilivyo kamatwa na kutaifishwa ni pamoja na boti 16, Chupa za kuzamia 11, injini moja (1) na miti ya mikoko 472. Zana haramu zilizokamatwa ni pamoja na makokoro, 18, nyavu za timba (monofilament) 50 na samaki wachanga kilogramu 23. Vilevile, kesi tisa (9) za uvuvi haramu zilifunguliwa mahakamani na jumla ya shilingi milioni 11.79 zilikusanywa kutokana na faini zilizotozwa kwa watuhumiwa kutokana na faini mbalimbali. Doria zote hizo zilifanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wanajamii, Halmashauri za Wilaya, Jeshi la Wananchi (Kikosi cha Wanamaji), Jeshi la Polisi na Kikosi kazi Maalumu cha Kuzuia Uharibifu wa Mazingira (Multi – Agency Task Team - MATT).

169. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizofanywa na MPRU ni pamoja na ushirikishwaji wa jamii zinazoishi ndani ya maeneo ya Hifadhi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za usimamizi na uhifadhi zilizohusisha uperembaji na ufuatiliaji wa hali ya mifumo ikolojia na bioanuwai ya matumbawe, majani bahari, mikoko na samaki katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kutoa taarifa ya hali halisi ya rasilimali na mazingira katika maeneo ya hifadhi. Aidha, MPRU iliendelea kusaidia maendeleo ya vijiji na Halmashauri ndani ya maeneo ya Hifadhi kwa kutoa mgao wa maduhuli yaliyokusanywa kwenye maeneo ya hifadhi hususan Kisiwa cha Mafia. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya shilingi milioni 117.156 zilitengwa na kupelekwa kwenye Halmashauri ya Mafia kwa ajili ya kugharimia shughuli za uhifadhi na miradi ya maendeleo katika vijiji vilivyomo ndani ya Hifadhi.

170. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Kitengo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi

ambayo ni pamoja na usimamizi wa rasilimali za Bahari na Pwani zilizoko katika maeneo yake kwa kufanya doria zenye siku kazi 600. Aidha, Kitengo kitaendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo ya hifadhi na kukamilisha taratibu za kutangaza maeneo ya visiwa vya Ukuza, Nyuni, Fanjove na Simaya kuwa Maeneo Tengefu. Vilevile, Kitengo kitaendelea kutekeleza Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitano (2014 -2019) na Mipango ya Jumla ya Usimamizi wa Rasilimali – (General Management Plans – GMPs) ya maeneo yaliyohifadhiwa.

## UKUZAJI VIUMBE KWENYE MAJI

171. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilikuwa na jukumu la kuendelea kutekeleza Mkakati wa Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji kwa kuimarisha na kuendeleza vituo vitano (5) vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Ruhila (Songea), Mwamapuli (Tabora), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi) na Nyamirembe (Chato) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni 10. Umeme wa 3 "phase" umeingizwa katika kituo cha Kingolwira na mfumo wa maji kwenda katika mabwawa na eneo la kutotoleshea vifaranga vya samaki umekamilika. Aidha, ukarabati wa mabwawa ya kuzalishia samaki umefanyika katika vituo vya Ruhila na Mwamapuli. Pia, vituo vya Luhila, Nyengedi, Mwamapuli na Nyamirembe vimewezeshwa kwa ajili ya kutoa elimu na kutunza samaki wazazi kwa ajili ya kuzalisha vifaranga. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha vituo viwili (2) vya maji bahari vya Machui (Tanga) na Mbegani (Pwani) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni tatu kwa kufunga mfumo wa maji baridi katika jengo la kituo cha Mbegani. Aidha, kituo cha Machui kimewezeshwa kupata chakula cha samaki na vibarua kwa ajili ya kulea samaki wazazi 3,450 (350 urolepis; 800 niloticus; 300 kambamiti na 2,000 mwatiko).

172. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, jumla ya vifaranga vya samaki na kambamiti 15,119,757 vimezalishwa na vituo vya Serikali (243,569) vya Ruhila (176,000) na Kingolwila (67,569) na sekta binafsi (14,876,188) ikilinganishwa na vifaranga 14,119,272 vilivyozalishwa mwaka

2016/2017. Aidha, Sekta Binafsi imezalisha vifaranga 14,924,569 kutoka makampuni ya Eden Agri-Aqua Ltd. Dar es Salaam (500,000) na Safina Big Fish Dar es Salaam (70,400), Ruvu Fish Farm Pwani (650,000), Noni Mkuranga (10,000), J&B Luhanga Bukoba (1,748,631) watu binafsi Mwanza (29,360) na watu binafsi Nyamirembe (31,366) na kusambazwa kwa wafugaji katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani na Tanga. Vilevile, jumla ya vifaranga 12,080,000 vya kambamiti vimezalishwa na Kampuni ya Alphakrust iliyopo Mafia (12,000,000) na Kampuni ya Prawnto Ltd iliyopo Mkuranga (80,000).

173. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuimarisha na kuendeleza vituo vitano (5) vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Ruhila (Songea), Mwamapuli (Tabora), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi) na Nyamirembe (Chato) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni 10. Aidha, itaendeleza vituo viwili (2) vya ufugaji samaki wa maji bahari vya Machui (Tanga) na Mbegani (Pwani) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga milioni 3. Pia, Wizara itawezesha vituo vinne (4) vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Bukoba, Kilimanjaro, Mwanza na Mara kutoa huduma za ugani na itazalisha na kupandikiza vifaranga vya samaki milioni 5 katika malambo na mabwawa ya asili kumi 10 na kwenye skimu tano (5) za umwagiliaji miwa na mpunga.

174. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha ufugaji bora wa viumbe kwenye maji kwa kutumia teknolojia sahihi za ufugaji samaki, ukuzaji wa lulu na ukulima wa mwani. Idadi ya wananchi waliohamasishwa kwa kupatiwa elimu ya ukuzaji viumbe kwenye maji hususan samaki imeongezeka kutoka 4,146 mwaka 2016/2017 hadi wadau 5,229 katika mwaka 2017/2018. Wadau hawa ni kutoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Ruvuma, Lindi, Kagera, Mara, Singida, Shinyanga, Tabora na Kilimanjaro. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha ufugaji mseto wa samaki na kilimo cha mpunga katika Wilaya ya Igunga ambapo Halmashauri kwa kushirikiana na Shirika la “Word Vision” na kituo cha ukuzaji viumbe kwenye maji cha Mwamapuli wameweza kutoa elimu kwa wadau wa ufugaji

samaki 632 na kupandikiza vifaranga 1,000 vya samaki aina ya kambale katika mabwawa mawili (2) ya mfano chini ya Mradi wa "Igunga Eco Village" unaofadhiliwa na Shirika la "Heifer International".

175. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na uhamasishaji wa ukuzaji wa viumbe kwenye maji, idadi ya mabwawa ya ufugaji wa samaki imeongezeka kutoka 22,702 mwaka 2016/2017 hadi 24,302 kwa mwaka 2017/2018. Aidha, uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka tani 1,197.5 za mwani mkavu zenye thamani ya shilingi milioni 412 hadi tani 1,329.5 zenye thamani ya shilingi milioni 469.8 katika maeneo ya Kilwa (420.2), Songosongo (320), Tanga (70) na Lindi (519.3). Pia, kilo 1,016.8 za kaa zimezalishwa na kikundi cha "Mariculture Group" (400) na watu binafsi (616.8) zenye thamani ya shilingi 12,326,800 katika Wilaya ya Pangani Tanga na vipande 180 vya lulu vimevunwa kwenye kijiji cha Mngonji Mtwara na vimeuzwa kwa shillingi 900,000. Vilevile, uzalishaji wa samaki aina ya Perege na Kambale umefikia tani 14,800 ukilinganishwa na tani 11,000 mwaka 2016/2017. Vilevile, uzalishaji wa Kambamiti wanaofugwa na Kampuni ya Alphakrust ya Mafia umefikia tani 371.70.

176. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau 2,400 wa ufugaji samaki kwenye vizimba na kilimo mseto cha samaki na mpunga, itatoa mafunzo kwa mameneja 30 wa mashamba samaki juu ya udhibiti wa magonjwa ya samaki katika mashamba na kufanya kaguzi 200 katika mashamba ya kuzalisha vifaranga na vyakula vya samaki. Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya kuongeza thamani zao la mwani kwa vikundi 20 vya wakulima wa mwani. Pia, itatoa mafunzo ya kutumia teknolojia ya kulima mwani kwenye maji marefu kwa wakulima 25 kutoka vikundi vya Maliwazano na Mkombozi Wilayani Mkinga.

177. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeandaa Rasimu ya mwongozo kwa ajili ya kuendesha maeneo ya kutotolesha vifaranga vya samaki "Hatchery Guidelines" aina ya perege na kambale na kutafsiri

kwa lugha ya kiswahili Mwongozo wa Ukuzaji Viumbe kwenye Maji bahari pamoja na kupitia rasimu ya taarifa ya "Mariculture Scooping Study" iliyowasilishwa na mtaalam mwelekezi chini ya Mradi wa SWIOFish. Aidha, Wizara ilipitia Mpango wa Ufuatiliaji Ubora wa Mazao ya Kambamiti kutoka kwenye mabwawa ya kampuni ya Alphakrust yaliyopo katika Wilaya ya Mafia kwa kuchunguza mabaki ya madini tembo na kemikali na kutafsiri kwa lugha ya kiswahili Mpango Mkakati wa Ufugaji Samaki (National Aquaculture Development Strategy - NADS); ili uweze kutumika na wadau. Pia, Wizara imefanya mkutano na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani juu ya uendelezwaji wa kituo cha uvuvi Kimu-Pangani kwa ajili ya ukuzaji viumbe kwenye maji bahari; na kuanzisha kituo cha Ukuzaji Viumbe Kwenye Maji Simiyu kwa ajili ya kutoa elimu ya ugani.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi itaainisha na kuingiza kwenye ramani na kufanya tathmini ya awali ya mazingira kwa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na maziwa madogo yaliyopo Kanda ya Kaskazini.

178. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara ilishiriki kuandaa Mpango Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Viumbe kwenye Maji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC - Aquatic Animal Health Strategy) wa miaka mitano 2016/2017-2021/2022. Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Viumbe kwenye maji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2016/2017-2021/2022, Wizara ilitoa taarifa kwa umma juu ya tahadhari ya kuwepo kwa ugonjwa wa "*Tilapia Lake Virus*" katika baadhi ya nchi Duniani na Afrika ikiwemo nchi ya Misri na kutoa taarifa kwa wazalishaji wa vifaranga vya samaki na wasimamizi wa mipaka yetu ili kudhibiti uingizwaji holela wa samaki na mazao yake. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeandaa Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti Usugu wa Vimelea vya Magonjwa (The National Action Plan on Antimicrobial Resistance) wa miaka mitano (2017-2022).

179. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itatekeleza Mpango wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Usugu wa Vimelea vya Magonjwa 2017-2022 katika sekta ya uvuvi kwa kukusanya sampuli za samaki katika mashamba ya kufugia samaki 20, viwanda vya kuchakata samaki vitano (5) na sampuli za vyakula vya samaki kwenye viwanda vya kuzalisha vyakula vya samaki (5). Aidha, Wizara itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Viumbe kwenye maji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa miaka mitano 2016/2017-2021/2022 kwa kudhibiti magonjwa ya viumbe wakuzwao kwenye maji yanayovuka mipaka (Transboundary Aquatic Animal Diseases - TAADs) kwa kufanya ufuatiliaji katika vituo thelathini 30 vya mipakani na kufanya mikutano mitano (5) na wadau mbalimbali wa tasnia hii ikiwemo wamiliki wa vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki na wafugaji wa samaki na viumbe wengine wa kwenye maji;

(ii) Kushirikiana na taasisi za utafiti zikiwemo za TAFIRI, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufanya uchunguzi wa visababishi mbalimbali vya magonjwa ukiwemo ugonjwa wa "*Tilapia Lake Virus*"; na

(iii) Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Miaka Mitano wa Kudhibiti Magonjwa ya Viumbe wa Kwenye Maji (The National Aquatic Animal Health Strategy) 2018/2019 – 2023/2024.

## UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI

180. **Mheshimiwa Spika,** uchakataji wa mazao ya uvuvi unahusisha samaki kutoka ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Tanganyika na maji baridi. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya viwanda vikubwa 14 hujishughulisha na uchakataji mazao ya uvuvi katika ukanda wa Pwani (5), Ziwa Victoria (8) na Tanganyika (1) (Kiambatisho Na. 26); na viwanda vidogo 34 vya kuhifadhi samaki hai.

Mazao yanayochakatwa na viwanda hivyo ni pamoja na Pweza, Ngisi, Kaa, Kambamiti na Kambakochi (ukanda wa pwani), Sangara (Ziwa Victoria) na Migebuka (Ziwa Tanganyika). Aidha, kuna maghala 33 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi yaliyokaushwa na maghala 23 ya kuhifadhi mazao yaliyogandishwa.

181. **Mheshimiwa Spika**, viwanda vya kuchakata samaki hufanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji mdogo wa malighafi yaani samaki. Viwanda hivyo vilijengwa vikiwa na uwezo wa kuchakata mazao ya uvuvi wastani wa tani 583 kwa siku, hali halisi ya uchakataji kwa siku moja kwa sasa ni wastani tani 165 ikiwa ni asilimia 28 ya uwezo wake. Hali hii inasababishwa na uhaba wa malighafi (samaki) kwa ajili ya kuchakata. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia uchakataji wa samaki na mazao ya uvuvi kwa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009 kwa kufanya kaguzi 443 kwenye viwanda (351) na maghala (72) ili kuhakiki mifumo ya uzalishaji na uhifadhi ili kulinda uvuvi na afya ya mlaji. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kufuatilia mifumo ya uzalishaji katika viwanda na maghala kwa kufanya kaguzi 200 za kina.

182. **Mheshimiwa Spika**, mialo ya kupokelea mazao ya uvuvi na masoko ya kuuzia mazao hayo ni miundombinu muhimu katika kutunza ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Aidha, ubora wa miundombinu hii hupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa. Upotevu huu kwa sasa unakadiriwa kufikia asilimia 20 hadi 40. Kiwango hiki ni kikubwa na kinaathiri uhakika wa chakula na kipato. Pia, matumizi sahihi ya miundombinu hii husaidia kudhibiti uvuvi na biashara haramu.

183. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya kaguzi 161 kwenye mialo ya kisasa 13 katika ukanda wa Ziwa Victoria (6), ukanda wa Ziwa Tanganyika (4) na ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi (3). Aidha, Wizara imefanya tathmini katika

maeneo ya vijijini 10 vya Marehe na Katembe (Kagera) Kibuyi, Busekela na Kisonya (Mara), Kayenze na Bukima (Mwanza), Chifunfu, Kijiweni na Nyamikoma (Sengerema) ili kutambua changamoto katika usimamizi na uendelezaji wa mialo na masoko ya mazao ya uvuvi, usalama na miundombinu iliyopo.

184. **Mheshimiwa Spika,** masoko ya samaki nchini yamegawanyika katika masoko makubwa na madogo. Masoko makubwa ni pamoja na Kigamboni/Feri (Dar es Salaam), Kirumba (Mwanza), Kasenda (Geita), Kibirizi (Kigoma) na Kasanga (Katavi). Aidha, masoko madogo hujumuisha mialo ya kupokelea samaki. Baadhi ya masoko hayo ni Mwigobero, Busekera na Kisorya (Mara); Magarini (Muleba) na Customs (Kagera); Nyamikoma na Buyorwa (Simiyu) na Nyakaliro (Mwanza), Kilwa (Lindi), Deep Sea (Tanga), Kunduchi na Msasani (Dar es Salaam). Katika mwaka 2017/2018, Wizara, imefanya kaguzi 56 kwenye masoko ya samaki na kaguzi 93 kwenye vyombo vya usafirishaji kwa ajili ya kuhakiki ubora wa masoko na samaki.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufuatilia miundombinu ya mialo na masoko ya uvuvi kwa kufanya kaguzi 200 kuhakiki ubora wa mialo, masoko na mazao yanayozalishwa.

185. **Mheshimiwa Spika,** biashara ya mazao ya uvuvi inahusisha samaki na mazao yake ikiwemo minofu ya Sangara, Kayabo, mabondo, Samaki wakavu, Pweza, Ngisi, Kambamiti, na Kambakochi. Mazao haya huuzwa katika masoko ya ndani, kikanda (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia na Malawi) na kimataifa zikiwemo nchi za Bara la Asia, Ulaya na Amerika. Katika mwaka 2017, Wizara imefanya kaguzi 2,027 za kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya mpakani, Viwanja vya Ndege na Bandarini kabla ya kusafirishwa. Ukaguzi huo umewezesha jumla ya tani 36,063 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 101,110 kukaguliwa na kupewa Hati ya Afya (Health Certificate) ya kusafirishwa nje ya nchi.

Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaimarisha na kuviwezesha vituo vya Ubora na Uthibiti wa mazao kufanya ufuatiliaji kwenye maeneo ya mialo na masoko ya samaki. Aidha, itafanya kaguzi 7,200 za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

186. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Uvuvi - Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2017/2018, wataalam watano (5) wa Maabara walipata mafunzo kuhusu masuala ya shughuli za Maabara. Pia, Maabara iliwezeshwa kufanya uchuguzi wa kimaabara kwa sampuli 1,524 za minofu ya samaki, maji na udongo kubaini uwepo wa vimelea, masalia ya madawa ya mimea, kemikali na madini tembo. Vilevile, Maabara imeendelea kukidhi vigezo vya hati ya umahiri kutoka Taasisi ya Ithibati ya Nchi za SADC (SADCAS) kwa vipimo 13 vya mikrobailojia kwa maji na chakula.

187. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuwezesha Maabara kupata hati ya umahiri upande wa kemikali kwa kuendelea kufanyiwa ukaguzi wa awali katika umahiri wa kupima madini tembo katika maji. Aidha, itafanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli 4,800 za minofu ya samaki, maji, udongo kubaini uwepo wa vimelea haribifu, masalia ya madawa ya mimea, asidi, alikali na madini tembo. Pia, Maabara ya *Harmful Algal Blooms -HABs* ya Dar es Salaam itaaanza kufanya uchunguzi wa sumu kuvu.

## URATIBU WA MASUALA YA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA UVUVI

188. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maji ambayo yanamilikiwa na zaidi ya nchi moja. Maeneo hayo ni pamoja na Ziwa Victoria ambalo linamilikiwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, Ziwa Tanganyika linalomilikiwa

na nchi za Tanzania, Burundi, DR Congo na Zambia, Ziwa Nyasa linalomilikiwa na Nchi za Tanzania, Malawi na Msumbiji na Ukanda wa Bahari ya Hindi. Kupitia mashirikiano hayo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza sheria, miongozo, mikataba, itifaki na taratibu mbalimbali za kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia kwamba samaki hawana mipaka.

189. **Mheshimiwa Spika**, kupitia sekta ya uvuvi, nchi yetu ni mwanachama wa Taasisi mbalimbali za Kikanda zikiwemo Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization- LVFO); Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Authority); Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), *Indian Ocean Tuna commission- IOTC, Indian Ocean Commission- IOC, South Western Indian Ocean Commission (SWIOFC) na International Whalling Commission – IWC.* Aidha, nchi yetu ni mwanachama wa mashirika na taasisi mbalimbali za Kimataifa yakiwemo Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Benki ya Dunia.

190. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, nchi yetu imekuwa ikishiriki kwenye mikutano, makongamano na warsha mbalimbali zenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kusimamia rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kufanya operesheni za pamoja dhidi ya uvuvi haramu usioratibiwa na usiotolewa taarifa (Illegal Unreported and Unregulated Fishing - IUU) katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Aidha, ushirikiano huo umewezesha nchi yetu kushiriki kwenye operesheni mbalimbali kama nilivyoeleza awali.

191. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Norway, NORAD na FAO, mwezi Aprili 2018 nchi yetu ilipata fursa ya kushiriki katika utafiti wa uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kutumia meli ya Utafiti ya *Dr. Fridtjof Nansen* kutoka Norway. Matokeo ya utafiti huu

yanatarajiwa kupatikana baada ya uchambuzi wa takwimu na yatawezesha kufahamu aina, wingi na mtawanyiko wa samaki ambao utasaidia katika kusimamia uvuvi endelevu na kuvutia fursa za uwekezaji. Pia, kupitia Benki ya Dunia, nchi yetu imewezeshwa kutekeleza mradi wa SWIOFish ambao unalenga kuimarisha usimamizi wa uvuvi katika ngazi ya kijamii; kujenga uwezo wa taasisi katika kusimamia rasilimali za uvuvi; na kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi wa rasilmali za uvuvi hususan uvuvi wa Bahari kuu. Vilevile, kupitia mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa, nchi yetu imeingia mikataba ya kulinda na kuhifadhi rasilimali za uvuvi hususani zile zilizopo katika hatari ya kutoweka (endangered species) wakiwemo nguva, majongoo bahari, Nyangumi, Kasa na Dodoji (Sea horse).

192. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda itafanya operesheni dhidi ya uvuvi haramu kupitia Operesheni Okoa Sangara, sensa ya uvuvi na tafiti mbalimbali katika Ziwa Victoria kupitia Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria.

## MIRADI YA SEKTA YA UVUVI NA MICHANGO YAKE KATIKA KUSIMAMIA UVUVI

193. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish)" ambao ni mradi wa kikanda unaotekezwa katika nchi zilizoko Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi kwa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia tarehe 22 Juni 2015 na utakamilika tarehe 30 Mwezi Septemba 2021. Mradi huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia IDA na GEF na unatekelezwa katika nchi za Tanzania, Msumbiji na Comoro. Kwa upande wa Tanzania bara, mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ). Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamamizi madhubuti wa uvuvi

katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kikanda. Malengo mengine ni kujenga uwezo wa nchi katika kusimamia rasilimali za uvuvi; kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi wa rasilmali za uvuvi katika Bahari kuu; kuinua uchumi wa jamii ya watu wa Pwani; na kuinua pato la Taifa kutokana na rasilimali za uvuvi na lishe kwa wananchi. Katika mwaka 2017/2018 Mradi wa SWIOFish umefadhili kazi mbalimbali za uvuvi zikiwemo:-

(i) Kufanya utafiti wa samaki aina za pweza, jodari na jamii zake, samaki wanaoelea, samaki wanaopatikana kwenye matumbawe na kambamiti;

(ii) Kuwezesha doria za kudhibiti uvuvi haramu katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi;

(iii) Kuimarisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa kuipatia vifaa mbalimbali vikiwemo kamera zinazoweza kupiga picha ndani ya maji, maturubai viona mbali (binoculars), Radio Calls na GPS. Pia, kuiwezesha MPRU kutayarisha Mpango wa Biashara wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu;

(iv) Kufanyia marekebisho mfumo wa Taarifa za Uvuvi kulingana na mahitaji ya kitaifa na kikanda Kanzidata ya mazao ya uvuvi;

(v) Kuwezesha mafunzo ya ukusanyaji takwimu kwa BMUs 49 katika Wilaya za Kinondoni, Ilala, Kigamboni, Temeke, Mtwara, Kilwa, Lindi, Tanga, Pangani na Mkinga. Mafunzo hayo yanaendelea pia katika Wilaya za Pangani, Bagamoyo na Lindi;

(vi) Kuchapisha nakala 1,500 za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 na kutafsiri Sera hiyo katika lugha ya Kiswahili;

(vii) Kujenga uwezo kwa watumishi 24 wa sekta ya uvuvi kujiunga na masomo ya Shahada za Uzamili (18) na Shahada za Uzamivu (6);

(viii) Kufanya Sensa ya Uvuvi, kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 1,000 za taarifa ya sensa hiyo iliyofanyika mwaka 2016;

(ix) Kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi ikiwa ni pamoja na usimamizi wa masuala ya uvuvi, ufuatiliaji na tathmini, usimamizi wa fedha, usimamizi wa hatchery na usalama baharini;

(x) Kuwezesha semina kuhusu madhara ya uvuvi haramu hasa wa kutumia mabomu kwa Mahakimu, Waendesha mashtaka, Madiwani na Viongozi wa dini ili wawe chachu ya mabadiliko katika utekelezaji wa majukumu yao katika Halmashauri za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi; na

(xi) Kuwezesha ununuzi wa magari 12 na pikipiki 17 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mradi.

194. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Mradi itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuwezesha TAFIRI kuendelea na tafiti za uvuvi wa pweza, jodari na jamii zake, samaki wanaoelea, samaki wanaopatikana kwenye matumbawe na kambamiti;

(ii) Kuendelea kuwezesha watumishi kuendelea na masomo ya Shahada za Uzamili, Uzamivu na mafunzo ya muda mfupi;

(iii) Kuwezesha jamii za pwani kusimamia rasilimali za uvuvi kupitia Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za uvuvi katika Halmashauri tano zinazotekeleza mradi;

(iv) Kuimarisha shughuli za uhifadhi katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu;

(v) Kuwezesha doria za kudhibiti uvuvi haramu katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

## UWEZESHAJI WA WAVUVI WADOGO NA WAKUZAJI VIUMBE KWENYE MAJI

195. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuwezesha wavuvi wadogo na wakuzaji viumbe kwenye maji kufanya uvuvi na ukuzaji wa tija. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania imewezesha kusambazwa kwa majiko banifu 70 katika vijiji 16 vya uvuvi katika Halmashauri 5 za Kigoma Manispaa, Kigoma, Uvinza, Tanganyika na Nkasi na jumla ya wachakataji wa samaki 480 kutoka Halmashauri hizo walipata mafunzo kuhusu matumizi ya majiko hayo ili kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi. Aidha, majiko banifu 105 yalisambazwa katika mwalo

wa Matema ulioko Ziwa Nyasa na wavuvi 40 walipata mafunzo ya matumizi ya majiko husika.

196. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Mradi wa SWIOFish, imewezesha wavuvi katika Halmashauri za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi zinazotekeleza Mradi kufufua Vikundi 49 vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika Halmashauri za Bagamoyo (9), Lindi (9), Pangani (12), Mkinga (14) na Tanga Jiji (5) kwa kufanya chaguzi na kuweka viongozi wapya. Aidha, Vikundi hivyo vimeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo mafunzo kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi na utawala bora kwa vikundi 36 kutoka Halmashauri za Mkinga (11), Pangani (9), Lindi (6), Jiji la Tanga (4) na Bagamoyo (6).

Pia, wavuvi 760 kutoka Vikundi 19 vilivyopo Halmashauri za Mkinga (14) na Tanga Jiji tano (5) walipata mafunzo kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na kuviwezesha kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi katika eneo husika. Utekelezaji wa Mipango hiyo utawezesha jamii za wavuvi kushiriki kikamilifu katika kusimamia raslimali za uvuvi katika maeneo yao.

197. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mpango wa Ruzuku kwa Wavuvi iliendelea kusambaza injini za boti zilizonunuliwa kupitia mpango wa ruzuku kwa wavuvi katika awamu ya kwanza iliyoanza mwaka 2014/2015. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, injini 46 zilikuwa zimelipiwa na kuchukuliwa na vikundi 33 vya wavuvi vilivyokidhi vigezo. Aidha, injini tatu (3) zimenunuliwa na FETA kwa ajili ya kutoa mafunzo ya usalama kwa wavuvi wadogo na wanachuo na kubaki injini 24 kati ya 73 zilizonunuliwa na Wizara kupiti mpango huo.

## HALI YA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI

198. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya vibali (health certificate)

2,751 vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi vilitolewa, na tani 36,063 za samaki na mazao yake na samaki hai wa mapambo 101,110 walisafirishwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 10.52 kama ushuru. Aidha, sekta binafsi zimeendeea kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, kutengeneza zana za uvuvi na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Hadi sasa, jumla ya viwanda vikubwa 15 na vidogo 34 vya kuchakata mazao ya uvuvi, vitatu (3) vya kutengeneza vyavu, vitatu (3) vya kutengeneza boti na maghala 56 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi vimeanzishwa. Pia, vibali 199 vya kuingiza samaki kutoka nje ya nchi vilitolewa na tani 22,961 zenye thamani ya shilingi bilioni 56 ziliingizwa.

199. **Mheshimiwa Spika,** taratibu za manunuzi za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi wa bahari zimekamilika ambapo Kampuni ya Sering Ingegneria ya Italy kwa kushirikiana na Kampuni ya Kitanzania inayoitwa Doch Tanzania Limited zimefanikiwa katika hatua za awali za kufanya kazi hii. Mkataba wa makubaliano unategemewa kuwekwa saini mwisho wa mwezi Mei, 2018 na kazi hii itatekelezwa kwa muda wa miezi nane (8). Kuwepo kwa bandari ya uvuvi kutawezesha meli zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kushusha samaki, hususan samaki wasiolengwa (by catch), kuwezesha ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki, kutoa ajira, lishe, kipato na kuongeza pato la Taifa.

200. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Shilingi bilioni 45 zinahitajika kwa ajili ya kuanzisha Shirika la Uvuvi Tanzania. Vyanzo vya fedha za kuanzisha TAFICO zinatarajiwa kutoka Serikalini, misaada ya Wahisani, Taasisi za Kifedha na Sekta Binafsi.

201. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewezesha uwekezaji katika ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ambapo jumla ya vizimba 315 vimewekwa katika maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika ikilinganishwa na vizimba

109 mwaka 2016/2017. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi.

## UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI

### Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)

202. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) imetekeleza tafiti mbalimbali ambazo zimesaidia wadau katika kuendeleza sekta ya uvuvi nchini katika kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. Tafiti hizo zilikuwa katika samaki wa maji asili (capture fisheries) na ukuzaji viumbe katika maji (aquaculture). Tafiti zilifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo, maziwa (makuu, kati na madogo), bahari, mito na mabwawa.

203. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, TAFIRI kupitia Mradi wa Kupunguza Uharibifu wa Samaki baada ya Mavuno unaotekelezwa katika Ziwa Tanganyika imeendelea na utafiti wa kupunguza uharibifu wa samaki baada ya mavuno na imefanikiwa kubuni majiko ya kukaushia dagaa na samaki wengine. Malengo ya mradi huu ni kupunguza matumizi ya misitu, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 majiko banifu 70 yamesambazwa katika vijiji/mialo ya uvuvi 16 katika Mikoa ya Kigoma (Kigoma Manispaa, Kigoma, Uvinza), Katavi (Tanganyika) na Rukwa (Nkasi). Majiko mengine 30 yanatarajiwa kusambazwa ili kufikisha idadi ya majiko 100 yaliyoainishwa katika mradi. Vilevile, wachakataji wa samaki 480 katika vijiji 16 wamefundishwa jinsi ya kutumia majiko na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Pia, Maafisa Uvuvi 15 kutoka Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Wilaya za Kigoma, Uvinza, Tanganyika na Nkasi walifundishwa jinsi ya kutumia majiko na jinsi ya kufundisha wachakataji wa samaki katika maeneo yao.

204. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, utafiti wa kuangalia hali ya mazingira ya Ziwa Tanganyika unaendelea. Takwimu zimeendelea kuchukuliwa kutoka boya lililo na "sensor" ambayo hutuma taarifa katika Satelaiti. Uchakataji wa takwimu hizi utafanyika baada ya miaka mitatu ya mradi. Pia, mradi mwingine unaoangalia hali ya maji na mazingira katika ghuba na mito ya Malagarasi na Luiche unaendelea na utatoa taarifa za vijiwe katika maji kila mwezi.

205. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, TAFIRI imetekeleza Mradi wa kupunguza uharibifu wa samaki baada ya mavuno kwa kutumia jiko la kutumia nguvu ya jua. Aidha, TAFIRI imewapatia mafunzo wavuvi na wachakata samaki 40 katika mwalo wa Matema jinsi ya kutengeneza na kutumia majiko hayo ambapo jumla ya majiko 10 yamesambazwa. Lengo ni kusambaza majiko 50 zaidi na hivyo kufikia idadi ya majiko 60. Majiko hayo yamesaidia samaki kutoharibika haraka kutoka mwezi mmoja toka walipovuliwa na kukaushwa mpaka kufikia zaidi ya mwaka mmoja.

206. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, TAFIRI kwa kushirikiana na Wizara ya Maji pamoja na Taasisi ya Jiografia na Limnolojia ya Nanjing, China, wamefanya utafiti kuhusu ubora na unadhifu wa maji katika maziwa makuu na mito inayopita katika miji mikuu (Dar es Salaam, Kigoma, Morogoro Mbeya na Mwanza). Utafiti ulizingatia maeneo makuu matatu, kwa kuzingatia kasi ya ukuaji wa miji na majiji husika. Matokeo ya awali ya utafiti huu yameonyesha maeneo ya kati na kusini mwa ghafu ya Mwanza yamechafuliwa na uwepo wa virutubiso maji (nutrients) hasa fosforasi na naitrojeni ambavyo vinasababisha uwepo wa vimelea maji (*algal bloom*) hivyo kupunguza ubora wa maji hayo. Aidha, TAFIRI imefanya utafiti katika mito na mabwawa na kutoa ushauri wa kufuata ili kuweza kuongeza uwingi wa samaki waliokuwepo, kupungua ama kutoweka kabisa.

207. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI itafanya utafiti na kutoa ushauri kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba (Bwawa la Ikimba) na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga na Simanjiro (Bwawa la Nyumba ya Mungu). Vilevile, TAFIRI itafanya tafiti za kuendelea kujua uwepo, aina na mtawanyiko wa rasilimali za uvuvi katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), Maziwa ya Kati, Maziwa Madogo, mito na mabwawa; na kuainisha rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi, hasa zile ambazo ni muhimu kwa chakula na uchumi kwa wavuvi na Taifa kwa ujumla. Tafiti hizi zitakuwa kwa Bahari ya ndani (territorial sea) na Bahari Kuu (Deep Sea) katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone - EEZ).

208. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Mradi wa kutambua maeneo yenye samaki unafanyika katika maji ya kitaifa (territorial waters) ambapo utaendelezwa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone - EEZ). Utafiti huu unatumia mtambo wa *satellite* uliopo TAFIRI Makao Makuu. Maeneo yenye samaki wengi baharini hutambuliwa na *satellite* kwa kutumia viashiria vya joto na umbijani. Katika awamu ya kwanza ya utafiti huu, vikundi vya wavuvi katika maeneo ya Tanga, Pemba, Nungwi na Mafia kwa kutumia mpango shirikishi (Public Private Partnership - PPP) walipewa GPS na mafunzo ya namna ya kuzitumia. Awamu ya pili wavuvi watapewa mafunzo ya namna ya kuyafikia maeneo ya samaki wengi kwa kutumia "GPS coordinates".

209. **Mheshimiwa Spika,** TAFIRI imeendelea na tafiti za kujua uwingi na biolojia ya Kambamiti na Pweza katika pwani ya Tanzania. Utafiti huu utasaidia kujua muda wa miezi 6 uliowekwa kwa ajili ya kufunga uvuvi ubakie ama ubadilike. Pia, utafiti utasaidia kuainisha nguvu ya uvuvi, na hivyo kutoa ushauri wa jinsi ya kupunguza nguvu hizo kwa ajili ya uvuvi endelevu. Vilevile, utafiti huu utasaidiia kupata ithibati (Certification and Eco-labeling) bidhaa za uvuvi ili kuongeza masoko na thamani. Hii itasaidia wavuvi na kampuni zinazofanya biashara ya pweza wa Tanzania kuwa na masoko zaidi na yenye uhakika na pia kuongezeka kwa

thamani ya pweza na hivyo kipato cha wavuvi na mchango katika pato la Taifa. Aidha, utafiti wa kambamiti unaoendelea utatoa picha halisi ya uvuvi unaofanywa na wavuvi wote.

210. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Kituo cha TAFIRI Mwanza hadi kufikia mwezi Aprili 2018 kimeshazalisha vifaranga 13,159 vya sato na 10,000 vya kambale. Vifaranga hao waliuzwa kwa wafugaji 12 na kikundi cha ufugaji samaki cha watoto waishio kwenye mazingira magumu cha *SOS Children Village* cha Mwanza. Aidha, watafiti wa TAFIRI wakishirikiana na watafiti wa Australia pamoja na wafugaji wa samaki wa Liwale (Lindi) wanaendelea na utafiti wa kuzalisha mbegu bora ya samaki inayofaa kufugwa katika maeneo ya Liwale. Katika mwaka 2018/2019, upanuzi wa mabwawa na ununuzi wa vitotoleshi vipya unatarajia kuongeza uzalishaji hadi kufikia vifaranga 50,000 vya sato na 60,000 vya kambale. Aidha, utafiti wa kuzalisha mbegu bora ya samaki inayofaa kufugwa katika maeneo ya Liwale utaendelea.

211. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, TAFIRI imeendelea na utafiti wa ukuaji wa samaki wa asili aina ya perege (*Oreochromis tanganyicae)* kwenye vizimba katika Ziwa Tanganyika. Utafiti huu ni wa kwanza kwa upande wa Tanzania na umefanyika kwa kushirikiana na Kampuni binafsi ya QP (QP group). Matokeo yameonesha kuwa samaki wamekua kutoka uzito wa gramu 3 hadi ukubwa wa kati ya gramu 100 na 890 (wastani wa gramu 412) na urefu wa sentimeta 33 katika kipindi cha miezi tisa (9).

212. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za ufugaji wa samaki nchini ili kuwa na mbegu bora ya samaki iliyoratibiwa kijenetiki; vyakula bora vya samaki vilivyotokana na malighafi asili inayopatikana katika eneo la wafugaji samaki; teknolojia bora na rahisi ya ufugaji samaki na ufugaji wa vizimba katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, TAFIRI itakarabati mabwawa mawili (2) katika kituo cha Mwanza na kuchimba mabwawa mengine mawili (2) mapya na

kukarabati mabwawa madogo 10 ya kulelea vifaranga (Nursery Ponds). Pia, itaboresha kitotoleshi cha Kituo cha Mwanza kwa kukiwekea miundombinu bora ya kutotolesha vifaranga.

## Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)

213. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Mitaala ya Kozi za Teknolojia ya Uvuvi na Biashara ya mazao ya uvuvi katika ngazi ya *National Technical Award (NTA*) ngazi ya 7 hadi 8. Mitaala hiyo imewasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kupata idhini ya kutumika. Aidha, FETA kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Japan (JICA) wameendelea kutoa mafunzo ya uwekaji vivutio samaki (Fish Aggregating Devices-FADs) katika bahari ya ndani ili kuvutia samaki wanaoishi ukanda wa EEZ kusogea katika maeneo ya karibu ambayo ni rahisi kwa wavuvi wadogo kuwavua.

214. **Mheshimiwa Spika,** FETA imekamilisha asilimia 80 ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu inayohitajika katika utoaji wa mafunzo ya ufugaji samaki katika vituo vya Kigoma, Mikindani (Mtwara) na Gabimori (Rorya). Lengo ni kuviwezesha vyuo vya FETA Mbegani (Bagamoyo) na Nyegezi (Mwanza), vipanue wigo wa utoaji elimu na mafunzo ya uvuvi pamoja na ufugaji samaki kwa wananchi wengi zaidi sambamba na kutoa huduma za ugani kwa wananchi wengi zaidi. Aidha, katika mwaka 2017/2018, jumla ya wanachi 2,745 wamepatiwa mafunzo na huduma za ugani kupitia FETA.

215. **Mheshimiwa Spika,** FETA kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya (EU) imeandaa mpango kazi wa awali ambao utusaidia kujenga uwezo wa kitaasisi wa FETA ili kukabiliana na changamoto ya utoaji wa elimu na mafunzo ya ufugaji samaki kwa kiwango cha kimataifa. Lengo kuu ni kupanua ajira na kuwezesha mazao yatakayozalishwa kutokana na ufugaji samaki yaweze kuuzika katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Programu hiyo itakuwa ni

ya miaka mitatu (2018-2021). Katika mwaka 2017/2018, Wakala ulidahili jumla ya wanachuo 1,040 kwa masomo ya Astashahada (Certificate) na Stashahada (Diploma). Idadi hii ni pungufu kwa asilimia 13 ikilinganishwa na wale 1,196 waliodahiliwa katika mwaka wa 2016/2017. Pamoja na kozi hizo, FETA imetoa mafunzo ya usalama katika maji kwa waendesha boti 358 katika ukanda wa Ziwa Tanganyika na Mwambao wa Bahari. Mafunzo haya yenye ithibati (accreditation) ya SUMATRA yamelenga kupunguza ajali zinazotokea mara kwa mara nchini.

216. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia FETA itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa Astashahada na Stashahada kutoka 1,072 mpaka 1,500 kwa mwaka;

(ii) Kutoa elimu na mafunzo ya uvuvi, uchakataji na ufugaji samaki kwa nadharia na vitendo;

(iii) Kujenga madarasa na kumbi za mihadhara katika Kampasi za Wakala Mikindani (Mtwara), Gabimori (Musoma) na Mwanza South;

(iv) Kujenga maabara nne katika kampasi za Mbegani (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Kibirizi (Kigoma) na Mikindani (Mtwara);

(v) Kuanzisha, kufanya, kuhuisha, kuimarisha na kuendeleza mafunzo na tafiti zitakazowezesha uboreshaji maeneo ya uvuvi kwa kutumia tekinolojia rafiki ya mazingira inayoendana na mahitaji ya sasa ya ufugaji wa samaki badala ya uvuvi wa asili;

(vi) Kuanzisha Kampasi mpya za Kagera na Mbambabay (Nyasa) ili kupanua wigo wa kuwafikia wateja;

(vii) Kununua na kukarabati mashine na mitambo ya kuwezesha utoaji wa elimu na mafunzo ya kisasa ya uvuvi na ufugaji wa samaki; na

(viii) Kuanzisha mtaala mpya wa kufundisha unahodha wa kimataifa na kukithi matakwa ya STCW- 1995.

(ix) Kutengeneza database ya vijana wote waliohitimu kozi mbalimbali katika chuo hicho.

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

217. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutoa Huduma za Ugani kwa kutoa Miongozo mbalimbali inayotumika katika Halmashauri na wadau wengine wanaotoa huduma hii kwa wavuvi na wafugaji wa viumbe kwenye maji. Mahitaji ya wagani kwa sekta ya uvuvi ni wagani 16,000 ikilinganishwa na wagani 750 waliopo ambapo ni pungufu ya wagani 15,250 kati ya wanaohitajika. Aidha, Wizara inaandaa machapisho mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na kuyasambaza kwa wadau kwa lengo la kuhamasisha uvuvi endelevu na ukuzaji bora viumbe kwenye maji.

218. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeshiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba ambapo jumla ya wadau 824 walitembelea mabanda ya uvuvi. Katika maonesho hayo jumla ya vijitabu 150 zikiwemo mwongozo wa ugani na vipeperushi 400 vilitolewa bure kwa wadau mbalimbali wa uvuvi. Aidha, Wizara imeshiriki katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Lindi, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Arusha na Tabora. Katika maonesho hayo Wizara ilitoa elimu kwa wadau 2,234 wa uvuvi na ukuzaji viumbe kwenye maji kuhusu mbinu bora za uvunaji, uchakataji, uhifadhi, ufugaji na biashara ya samaki na mazao yake kupitia maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Lindi, Mbeya, Morogoro Mwanza na Tabora. Vilevile, wavuvi 85 kutoka katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Tanga walipata elimu kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira.

219. **Mheshimiwa Spika**, katika darasa lililoandaliwa kwa ajili ya kutoa elimu ya uvuvi na ufugaji viumbe kwenye maji jumla ya wadau 108 walipatiwa elimu ya uendelezaji wa rasilimali za uvuvi na ufugaji bora wa samaki. Aidha, nakala 50 za Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji na nakala 392 za Mwongozo wa Huduma za Ugani za Uvuvi zilitolewa kwa wadau waliotembelea banda la uvuvi wakati wa maonesho

ya Sabasaba (Dar es Salaam), Nanenane (Lindi na Dodoma) na katika maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani (Geita). Teknolojia mbalimbali za uvuvi zilisambazwa kwa kuandaa vipindi 16 ambavyo vyote vilirushwa na TBC Taifa. Aidha, vipindi sita (6) na Makala moja (1) za luninga viliandaliwa na kurushwa na TBC 1. Vipindi vya radio na luninga vilihusu ulinzi wa rasilimali za uvuvi, ufugaji bora wa samaki (upandikizaji, ulishaji bora wa samaki na uvunaji wenye tija), kilimo cha mwani na uzalishaji wa Chaza wa lulu.

220. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya mabwawa 12 ya kufugia samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni yalitembelewa, hata hivyo, samaki wanaofugwa kwa wingi ni Kambale na Tilapia. Wamiliki wa mabwawa hayo walipewa elimu juu ya ulishaji bora wa samaki na utunzaji bora wa mabwawa ili kuongeza tija. Aidha, wafugaji samaki 20 walitembelewa katika Wilaya za Mvomero na Kilosa na kupewa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki, utunzaji na uchakataji wa samaki na mazao yake mara baada ya kuvunwa. Pia, machapisho mbalimbali yalichapishwa na kugawanywa kwa wadau wa sekta ya uvuvi zikiwemo nakala 250 za mwongozo wa ugani na vipeperushi 2,650.

221. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi 30 vya radio na 10 vya luninga juu ya matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, ufugaji bora wa viumbe kwenye maji, matumizi ya teknolojia sahihi za uzalishaji wa samaki na uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Pia, Wizara itahamasisha na kujenga uelewa kwa wadau wa uvuvi 100 ili wajikite katika uanzishwaji wa shughuli mbadala na hivyo kupunguza nguvu ya uvuvi (fishing pressure) katika maji ya asili. Aidha, Wizara itaendelea kushauriana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitenge nafasi na kuomba kibali cha kuajiri maafisa ugani ili kupunguza pengo la mahitaji ya wagani katika sekta ya uvuvi.

## D: MASUALA YA MTAMBUKA YA MIFUGO NA UVUVI

### Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI

222. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi 482 kupima afya zao kwa hiari na watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU wameendelea kupatiwa huduma ya chakula na lishe. Aidha, Wizara imewaelimisha watumishi 497 kuhusu kuzingatia maadili, nidhamu, haki na wajibu katika utumishi wa Umma. Vilevile, katika kutekeleza agizo la Serikali la kuhamishia Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma, Wizara imewahamisha watumishi 82 katika awamu ya pili na hivyo kufanya idadi ya watumishi waliohamishiwa Dodoma hadi sasa kufikia 207.

223. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/2018 Wizara imeajiri watumishi kumi (**10**) wa kada mbalimbali na watumishi 74 walithibitishwa kazini baada ya kumaliza muda wao wa majaribio. Watumishi 245 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo kuanzia mwezi Novemba 2017. Aidha, Mfumo shirikishi wa Taarifa za Utumshi na Mishahara (HCMIS) na wa Malipo ya Mishahara (GSPP) imesimamiwa ipasavyo.

224. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/2019, Wizara itatekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuelimisha watumishi kuzingatia Sheria Kanuni Taratibu na Miongozo ya kazi katika Utumishi wa Umma. Pia Mkataba wa huduma kwa Mteja utatekelezwa, Dawati la malalamiko na Jinsia litasimamiwa na kuimarishwa pamoja na kutoa mafunzo kwa Watumishi kuhusu Mfumo wa wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS). Vilevile, Mifumo shirikishi wa Taarifa za Utumshi na Mishahara (HCMIS) na Malipo ya Mishahara (GSPP) itasimamiwa kikamilifu ili kuleta matokeo chanya. Aidha, Wizara itajaza nafasi wazi 179, za ajira mpya zikiwemo 82 kada za Uvuvi 86 kada za Mifugo na 11 Kada Mtambuka. Watumishi 343 watapandishwa vyeo kada mbalimbali na watumishi 39 waliokidhi vigezo watathibitishwa kazini. Watumishi wa Wizara wataendelea kuhamasishwa kupima afya zao kwa hiari, na watumishi wanaoishi na VVU na wanaugua UKIMWI wataendelea kupatiwa huduma ya Chakula na lishe. Pia, itawezesha kikao kimoja cha Baraza la Wafanyakazi na majukumu ya vyama vya Wafanyakazi pamoja na kuwezesha michezo na Mabonanza sehemu za kazi ili kuimarisha afya za watumishi.

### Habari Elimu na Mawasiliano

225. **Mheshimiwa spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi. Jumla ya matukio 100 yametangazwa katika vyombo vya habari ikiwemo Sikukuu ya Wakulima (Nanenane), Wiki ya Maziwa na Siku ya Mvuvi Duniani. Vilevile, Wizara kupitia Kitengo cha Habari na Mawasiliano imepokea malalamiko 20 kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha, Wizara imetayarisha na kurusha vipindi vya Redio 20 na Luninga 25 kuhusu Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Pia, imefanya mikutano 35 na waandishi wa habari, imeweza kutangaza ziara 55 za viongozi na kutayarisha Makala za Luninga (Documentary) sita (6) za Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

226. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea kutayarisha na kurusha vipindi 10 vya Redio na vipindi 10 vya Luninga kuhusu Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha Dawati la Malalamiko ili wadau waweze kuwasilisha malalakimo yao na kutatuliwa malalamiko hayo kwa wakati. Pia, Wizara itatangaza ziara mbalimbali 50 za viongozi na matukio muhimu. Vilevile, Wizara itaandaa mikutano 12 na waandishi habari, Makala sita (6) za Luninga (documentary) kuhusu sekta ya mifugo na uvuvi. Vilevile, Tovuti na Blogu zitaendelea kuimarishwa ili kuendelea kusambaza taarifa sahihi na kwa wakati.

### Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

227. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara imejenga, kuimarisha na kusimamia mifumo ya TEHAMA iliyopo katika Wizara ambayo ni *Livestock Revenue Collection System (LRCS), Fisheries Revenue Collection System (FRCS),* Mfumo wa kufuatilia taarifa za magojwa ya milipuko yanayovuka mipaka (Transboundary Animal Diseases Information System (TADINfo), Mfumo wa Utambuzi, Usajili na

Ufuatiliaji wa Mifugo Tanzania (National Livestock Identification and Traceability System -TANLITS), Mfumo wa kukusanya na kutunza takwimu za samaki uitwao Catch Assessment System (CAS), Mfumo wa taarifa za kimaabara (SILAB), Mfumo wa usajili wa wataalam na vituo vya kutoa huduma za mifugo (Livestock Facilities and Professional Registration System - LFPRS) chini ya Baraza la Veterinari Tanzania, Mfumo wa kutuza taarifa za mishahara na kumbukumbu za watumishi (LAWSON) pamoja na Mfumo wa Mawasiliano wa LAN.

Aidha, Wizara imesimika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya mifugo ambao umeunganishwa na mfumo wa Serikali wa GePG (Government Electronic Payment Gateway) katika minada 12 ya upili ya Pugu, Kizota, Mhunze, Nyamatala, Weruweru, Meseran, Themi, Korogwe, Lumecha, Igunga na Ipuli na mnada wa mpakani wa Kirumi. Vilevile, wataalam watatu (3) wameshiriki katika mikutano minne (4) ya kitaaluma. Pia, Wizara imejenga na kuboresha mawasiliano ya mdahalisi (internet) na tovuti ya Wizara.

228. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya uvuvi na kusimika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya mifugo katika minada tisa (9) ya mipakani (Longido,Waso, Mutukula, Murusagamba, Buhigwe, Kasese, Mpemba, Kakonko na Kileo), kujenga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), kukamilisha kujenga mfumo wa taarifa za Bodi ya nyama na kuingiza taarifa za chapa katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Mifugo (TANLITS). Vilevile, kitengo kitafanya utafiti wa maeneo mengine ambayo yatatumia TEHAMA ili kuboresha utendaji kazi na kuongeza tija katika Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuhakikisha vifaa na mifumo ya TEHAMA inafanya kazi, kujenga na kuboresha (LAN na WAN) katika ofisi za Wizara ili kurahisisha mawasiliano ya ofisi za Wizara, Taasisi na wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi, kuwajengea uwezo watumishi na kuwapatia vitendea kazi.

### Hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi

229. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutoa taarifa kwa wafugaji na wavuvi kuhusu upatikanaji wa maji na malisho, hali ya bahari na maziwa na kutoa maelekezo stahiki kwa wafugaji na wavuvi. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) inaendelea na utafiti wa kutambua madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi kwa samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji la Bahari ya Hindi. Takwimu zinazokusanywa ni pamoja na baiolojia ya samaki hao, vimelea maji, viroboto maji, virutubisho, mikondo ya maji, maji kuja juu na fizikia na kemia ya maji. Matokeo ya utafiti huo yatawezesha Serikali kutengeneza mikakati na mipango ya kukabiliana na matatizo ya tabia nchi nchini.

230. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itatoa tahadhari kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa wafugaji na wavuvi na kuhimiza matumizi ya teknolojia zinazozingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwemo matumizi ya boti za fibre glass na ukaushaji wa samaki kwa kutumia jua, chumvi na majiko ya gesi ili kupunguza ukuaji wa miti.

## E: HITIMISHO NA SHUKRANI

231. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanfanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

232. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Israel, Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswis pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO na WHO na mifuko ya kimataifa ya GEF na IFAD kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

233. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

234. **Mheshimiwa Spika**, pia, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Reseach in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer International, Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Security

Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC), Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa sekta za mifugo na uvuvi.

235. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa makatibu wakuu Dkt, Mary S. H. Mashingo, Katibu Mkuu - Mifugo na Dkt. Yohana L. Budeba, Katibu Mkuu – Uvuvi, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kutekeleza majukumu kwa bidiii, juhudi na uhodari wa hali ya juu, endeleeni kuchapa kazi napenda na ninafurahishwa mnavyojitoa kulitumikia Taifa letu **"*Leadership is action not position*".**

236. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani zangu za dhati na pekee kwa wananchi wangu wa Kisesa ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kipaji nilichopewa na mwenyezi mungu kama nilivyowaahidi kuwa "***Sitapumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa".***

237. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijahitimisha hotuba yangu naomba kusisitiza mambo yafuatayo; Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** imejipanga kuleta mageuzi makubwa katika sekta za mifugo na uvuvi tumeamua, tumejipanga na hatutashindwa ***"hakika penye nia pana njia". Hatutakubali kuona rasilimali za uvuvi na mifugo zikitoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulinufaisha Taifa. Aidha, uvuvi na biashara haramu ya mazao ya mifugo na uvuvi havitapata nafasi tena.***

## F: MWISHO MAOMBI YA FEDHA

238. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi **56,455,749,000.00** kama ifuatavyo:-

### Fungu 99: Maendeleo ya Mifugo

239. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **35,362,663,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 99. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **30,362,663,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **5,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**.** Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 30,362,663,000.00**

- Mishahara: Shilingi **20,458,552,000.00;** na
- Matumizi Mengine (OC): Shilingi **9,904,111,000.00.**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 5,000,000,000.00**

- Fedha za Ndani: Shilingi 5,000,000,000; na
- Fedha za Nje: Shilingi - Hakuna

### Fungu 64: Maendeleo ya Uvuvi

240. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara inaomba jumla ya shilingi **21,093,086,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 64. Kati ya fedha hizo, Shilingi **13,966,406,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,126,680,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 13,966,406,000.00**

· Mishahara: Shilingi **8,918,612,000.00;** na
· Matumizi Mengine (OC): Shilingi **5,047,794,000.00.**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 7,126,680,000.00**

· Fedha za Ndani: Shilingi **3,000,000,000.00**, na
· Fedha za Nje : Shilingi **4,126,680,000.00.**

241. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: www.mifugouvuvi.go.tz

242. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na sasa tutamsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Maji, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia afya ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia naomba nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Waislam kote ulimwenguni katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Ramadhani Kareem. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yetu iingie kama ilivyo katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(1) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(2) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(3) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(4) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

(5) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo kumi na moja (11) kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa. Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati katika maeneo ya vipaumbele. Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni pamoja na:-

(a) Kutofanya uwekezaji wa kisasa katika ranchi za Taifa ambao utasaidia wafugaji kujifunza mbinu za ufugaji;

(b) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu;

(c) Uhaba wa Maafisa Ugani wa uvuvi na mifugo ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri;

(d) Mpango mkakati wa kuongeza viwanda vya bidhaa za ngozi, maziwa na nyama hapa nchini ili kupunguza uagizaji wa bidhaa za ngozi nje ya nchi;

(e) Kupunguza tozo nyingi kwenye bidhaa za maziwa ili wawekezaji wasijitoe kwenye sekta ya maziwa;

(f) Kuweka mazingira bora ili kuchochea sekta binafsi kushiriki katika kuwekeza katika sekta ya mifugo na uvuvi; na

(g) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Sekta ya Mifugo - Fungu 99. Fungu 99 liliidhinishiwa jumla ya Sh.29,963,524,000.00. Kati ya fedha hizo, Sh.25,963,524,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.4,000,000,000.00 fedha za ndani ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara kupitia Fungu 99 ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida Sh.21,749,412,823.87 ambayo ni sawa na asilimia 83.8. Kwa upande wa fedha za maendeleo hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyokuwa imetolewa mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi - Fungu 64. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara kupitia Fungu 64 liliidhinishwa jumla ya Sh.16,792,645,829.00. Kati ya fedha hizo Sh.14,792,645,829 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.2,000,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni Sh.7,667,949,400 ambazo ni sawa na 52% na hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni kuhusu mwenendo wa utoaji fedha. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo, fedha za maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli. Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kwa kupitia mafungu yote mawili ilitarajia kukusanya jumla ya Sh.36,105,367,551 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 makusanyo ya maduhuli yalikuwa Sh.26,923,480,109 ambayo ni sawa na asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato ya wastani wa 75% ya malengo ya makadirio ya makusanyo. Kamati imeridhishwa kwa namna ambayo sekta hizi zinakusanywa maduhuli ya Sh.26,923,480,109 kwa kipindi cha nusu mwaka. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na ukweli kwamba, pamoja na makusanyo hayo makubwa, Serikali imeshindwa kuipelekea Wizara fedha yoyote ya maendeleo kiasi cha Sh.6,000,000,000 iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hii inadhihirishwa namna ambavyo sekta hizi hazipewi msukumo katika kukuza pato la Taifa, kuongeza ajira na kuchochea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2017/2018. Msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kufanya ukaguzi wa tathimini halisi ya fedha iliyotumika *(Value for Money).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikuweza kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutokana na miradi ya maendeleo kutopelekewa fedha yeyote na hivyo kulikwamisha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kikatiba wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa bajeti na uchambuzi wa makaridio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchambua malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuifanya Wizara Mifugo na Uvuvi kuwa Wizara kamili ili iweze kujiendesha na kutekeleza shughuli zake rasmi kupitia mafungu mawili tofauti (*Two Separate Votes*) yaani Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 - Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.21,093,086,000. Kati ya fedha hizo, Sh.13,966,406,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.7,126,680,000, ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli, Wizara imepanga kukusanya jumla ya Sh.50,525,670,000 zitakazopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Mifugo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.35,362,663,000. Kati ya fedha hizo, Sh.30,362,663,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.5,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya Sh.105,556,392,250 zitakazopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya utekelezaji wa vipaumbele kwa sekta ya mifugo na uvuvi. Fedha zinazoombwa zinapanga kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Kamati imepitia, kuchambua na kutathmini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019 na kuridhishwa nayo. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha iliyotengwa kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele ilivyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara kupitia mafungu yote mawili inaombwa kuidhinishiwa Sh.12,126,680,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikilinganishwa na maombi ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo iliidhinishiwa kiasi cha Sh.6,000,000,000, maombi ambayo ni ongezeko la asilimia 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kupita Mafungu yote imekadiria kukusanya Sh.156,082,062,250 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.36,105,367,551 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kiasi hiki ni ongezeko la makadirio ya makusanyo ya asilimia 76.87. Kamati inaipongeza Serikali kwa dhamira ya kuinua Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kuongeza kiasi cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza ni vyema Serikali ikatoa kiasi cha fedha zinazoombwa kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo tisa (9) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Uwekezaji Mdogo katika Sekta ya Uvuvi. Sekta ya Uvuvi ni moja ya sekta inayochangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kuuza samaki ndani na nje ya nchi hivyo husaidia nchi kupata fedha za kigeni. Aidha, sekta ya uvuvi ina mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe bora, na kipato. Hata hivyo, maendeleo katika sekta hii si mazuri sana kutokana na

sababu mbalimbali ikiwemo bajeti ndogo inayotengwa na kutolewa isiyokidhi mahitaji na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara imetengewa kiasi cha shilingi 7,126,680,000.00 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha zilizotengwa ni kidogo na hazitoshi kutekeleza hata kipaumbele kimoja cha Wizara ambacho kinahusu kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu ambao unahitaji uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa bandari ya uvuvi, miundombinu ya kuhudumia meli za uvuvi, gharama kubwa za kuendesha doria za anga na baharini. Kamati inashauri Serikali kupanga na kutoa fedha za maendeleo kadri ya mipango ya vipaumbele ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Usioridhisha. Upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za Uvuvi. Kwa mfano; kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 64 - Uvuvi ilitengewa Sh.2,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa fedha usioridhisha umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika sekta ya uvuvi hivyo kusababisha kushuka kwa mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa kutoka wastani wa asilimia mbili, mwaka 2015 hadi asilimia 1.5, mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango wa uvuvi katika kuwapatia wananchi ajira, lishe bora, kipato na Pato la Taifa; Kamati inashauri Serikali kuimarisha utoaji fedha kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi kama zinavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Udhibiti wa Uvuvi Haramu. Kwa muda mrefu Tanzania imeendelea kukabiliwa

na changamoto ya uvuvi haramu, ambayo imesababisha kupungua kwa wingi wa rasilimali za uvuvi na kuathiri upatikanaji wa lishe bora, kipato, ajira na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yanayoambatana na uvuvi haramu yamesababisha Serikali kuchukua hatua madhubuti za kupambana na uvuvi haramu ikiwa ni pamoja na Operesheni Sangara iliyoanza kutekelezwa mwaka 2018 kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia sumu, mabomu, baruti na zana zingine haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali ili kuweza kuwa na uvuvi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo. Hata hivyo, Kamati imepokea malalamiko kutoka kwa wavuvi kwa namna Opereshion Sangara, 2018 ilivyotekelezwa, haikuzingatia misingi ya haki za binadamu kwani imegubikwa na vitisho, ubabe na viashiria vya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala yanayolalamikiwa ni pamoja na kuchomwa kambi za wavuvi, nyavu na mitumbwi, kutaifisha nyenzo na mali nyingine za wavuvi. Kufuatia malalamiko hayo Kamati inaamini kuwa, ni vyema Serikali ikafanya tathmini ya utekelezaji wa Operesheni Sangara, 2018 na kurekebisha kasoro zote zilizobainika ili kuweka misingi ya namna bora zaidi ya kutekeleza operesheni za aina hii bila ya kuleta athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali ili kukomesha uvuvi haramu ni vyema jitihada kubwa zikaelekezwa kwenye kudhibiti utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Ufugaji wa Viumbe Kwenye Maji na Ukuzaji wa Samaki katika Vizimba *(Aquaculture).* Tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba ifikapo mwaka 2030 Afrika itakabiliwa na uhaba mkubwa wa samaki kwa kiasi cha upungufu wa tani milioni 1.8. Upungufu huu

unatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ulaji wa samaki kutokana na virutubisho vyake muhimu kwa mwili wa binadamu, uvuvi uliopitiliza na matumizi ya zana haramu za uvuvi yanayosababisha pamoja na mambo mengine kuharibu mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa viumbe kwenye maji na ukuzaji wa samaki katika vizimba ndiyo njia mbadala ya kuongeza uzalishaji wa samaki hivyo kuwezesha upatikanaji wa samaki endelevu. Hata hivyo, ufugaji wa samaki kwenye vizimba unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa Maafisa Ugani, ukosefu wa elimu na mitaji, pamoja na ukosefu wa teknolojia na nyenzo za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia changamoto hizo, Kamati ina maoni kuwa ni vyema Serikali ikatambua fursa zilizopo kwenye ufugaji wa samaki kwenye vizimba kwa kuweka na kutekeleza mipango itakayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Mabadiliko Kuhusu Taratibu za Uingizaji na Usambazaji Samaki hapa Nchini. Mahitaji ya ulaji wa samaki nchini ni makubwa kuliko samaki wanaoweza kuvuliwa ambao ni tani 350,000 kwa mwaka. Kwa sasa kuna namna mbili zinazoweza kusaidia upungufu huo. Namna moja ni kwamba; kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba na namna nyingine ni kwa kuagiza samaki kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba bado haujawa wa uhakika na wa kutegemewa, upungufu uliopo unafidiwa kwa kiasi kikubwa na uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi ambao huuzwa kwa bei nafuu kuliko samaki wanaopatikana nchini. Hii imesababisha kupungua kwa soko la samaki wa ndani na hivyo kuikosesha Serikali na wavuvi mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto hiyo Serikali imeanzisha tozo ya *dollar* 0.25 kwa

kila kilo ya samaki ili kupunguza uagizwaji wa samaki kutoka nje ya nchi ambao hawapatikani hapa nchini. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuongeza mapato ya ndani na kuwasaidia wavuvi kunufaika na rasilimali za uvuzi zilizopo nchini, Kamati inaamini na kushauri kuwa, ongezeko la tozo iliyoongezwa imesababisha wafanyabiashara wengi wa samaki kushindwa kuagiza samaki kutoka nje kwani imewalazimu wauze kwa bei ya juu na wananchi hawamudu na hivyo kusababisha upungufu wa samaki kwa walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati kuweka kipindi cha mpito cha utekelezaji wa tozo iliyoanzishwa, ili wakati wa kipindi cha mpito Serikali kwa kutumia wataalam wake iwe inaweza kupunguza gharama za tozo na hivyo kuweka kiwango ambacho hakitaathiri mapato ya Serikali lakini pia hakitazorotesha ushiriki wa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Bajeti Ndogo ya Sekta ya Mifugo Isiyowiana na Mchango wa Sekta Hiyo Katika Pato la Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo. Pamoja na takwimu za wingi wa mifugo iliyopo bajeti ndogo inayotengwa kwenye sekta hii ni dhahiri kwamba haiwezi kuleta kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Sekta ya Mifugo, iwe na manufaa kwa Taifa na wafugaji ni muhimu kwa Serikali kutenga bajeti ya kutosha, kuwekeza katika miundombinu, kutoa elimu ya ufugaji bora na wa kisasa pamoja na kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji nyama, maziwa na ngozi. Ujenzi wa viwanda hivi, utasaidia kuongeza thamani ya rasilimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Uwekezaji katika Ranchi za Taifa. Ranchi za Taifa ni rasilimali muhimu ambazo endapo zitatumika vizuri, zitaweza kuongeza Pato la Taifa kwa wafugaji. Tanzania ina jumla ya ranchi 13 zenye ukubwa wa jumla ya hekta 623,856, katika mikoa 10 nchini.

Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa hali ya uwekezaji uliopo katika ranchi za Taifa hauendani na rasilimali zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ranchi hizo kutotumika ipasavyo, wananchi waishio karibu na maeneo ya ranchi hizo, wamekuwa wakiingiza mifugo yao ndani ya ranchi hizo kwa ajili ya kupata malisho na kusababisha migogoro isiyokuwa ya lazima. Ili kuondokana na changamoto hii Kamati inashauri Serikali kurejesha ranchi zote walizopewa wawekezaji wakashindwa kuziendeleza ili Serikali iweze kuziendeleza na kuzitumia kwa ajili ya malisho na kwa wafugaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Uwekezaji Mdogo katika Tasnia ya Maziwa. Takwimu zinaonesha Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi na tano zinazoongoza kwa idadi kubwa ya ng'ombe duniani, inashika nafasi ya tisa (9) kwa wingi wa ng'ombe wa kisasa na wa kienyeji na ni ya tatu barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Pamoja na kuwa na idadi kubwa ya mifugo katika uzalishaji wa maziwa, Tanzania haimo katika nafasi kumi na tano (15) za nchi zinazozalisha maziwa kwa wingi, hali hiyo inatokana na kuwa na idadi ndogo ya ngo'mbe wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina viwanda vikubwa vya usindikaji wa maziwa visivyozidi vitano ambavyo vina uwezo wa kuchakata bidhaa za maziwa zenye uhai wa muda mrefu. Viwanda vya usindikaji maziwa vilivyopo nchini vinahitaji lita lita 700,000 za maziwa ili kukidhi mahitaji ya viwanda hivyo kila siku, wakati usindikaji uliopo ni lita 200,000 tu na hivyo kusababisha upungufu wa lita 500,000 ambao hufidiwa kwa kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi na kuigharimu Serikali zaidi ya shilingi bilioni mia moja sitini na tano kwa mwaka na kuvifanya viwanda hivyo vya ndani kushindwa kuhimili ushindani wa maziwa ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya ndani vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ya ushindani mkubwa wa maziwa yanayoagizwa kutoka

nje ya nchi ambayo yanawekewa dawa ili yasiharibike, tozo za kodi mbalimbali, kununua maziwa yasiyo na ubora kutokana na ufugaji usiokuwa na tija, ukosefu wa chakula bora na malisho, miundombinu mibovu, upotevu na uharibifu wa maziwa kabla ya kufikishwa viwandani na baadaye kukosa soko. Pia kukosekana kwa vituo vya ukusanyaji wa maziwa pindi yanapozalishwa kwa kuwa vituo havina vifaa vya kisasa vya kuhifadhi maziwa pindi yazalishwapo na kufikishwa viwandani au kabla ya kumfikia mlaji, hivyo kukwamisha ukuaji wa sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutathmini idadi ya tozo zilizopo katika sekta ya maziwa ili kuzipunguza na kuzitafutia wawekezaji kabla ya kujua na kupanua ukubwa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Binafsi ni wadau muhimu katika kukuza sekta na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi na kwa kufanya hivyo, imekuwa ikichangia katika Pato la Taifa, kutoa ajira na soko la uhakika katika mazao ya mifugo. Pamoja na changamoto, mchango wa sekta binafsi kwa Taifa, changamoto mbalimbali zimekuwa zikikwamisha ushiriki wake katika njia za uzalishaji mali. Aidha, sekta hii itaweza kushiriki na kutoa mchango wake kikamilifu. Serikali haina budi kuweka mazingira mazuri kibiashara yatakayowezesha uwekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika ustawi wa sekta, Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto hizi, kwa kuongeza kasi ya kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Luhaga J.

Mpina; na Naibu Waziri Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega; Katibu Mkuu Yohana Budeba; na Katibu Mkuu Maria Mashingo pamoja na Wataalam wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati inachambua na kujadili bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili (2) ambayo ni Fungu 64- Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 –Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MASWALA MBALIMBALI

### 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo kumi na moja (11) yafuatayo:-

a) Umuhimu wa fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati;

b) Umuhimu wa Tafiti katika sekta ya mifugo na uvuvi ili kuongeza tija katika uzalishaji;

c) Umuhimu wa kuwa na Maafisa Ugani wa kutosha nchinzima, ili kueneza na kusimamia teknolojia za kisasa katika sekta za mifugo na uvuvi;

d) Umuhimu wa sekta za mifugo na uvuvi katika kukuza na kuendeleza sekta ya viwanda nchini;

e) Kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji wa maeneo ya Mifugo na watumiaji wengine wa ardhi ili kukabiliana na migogoro ya ardhi;

f) Kufanya tathmini kwenye mazao ya Mifugo na Uvuvi ili kubaini tozo zisizo za lazima na kuzifuta ili kumuondolea mfugaji na mvuvi makato yasiyostahili ambayo yamekuwa kero za muda mrefu;

g) Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuviwezesha na kuvilinda viwanda vya ndani vya nyama, samaki, ngozi na maziwa, ili viweze kuzalisha kwa wingi na kuondokana na uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje ya nchi**;**

h) Udhibiti wa Uvuvi haramu na biashara ya utoroshwaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi;

i) Umuhimu wa kuimarisha doria katika Bahari Kuu;

j) Kuongeza kasi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi; na

k) Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya mifugo na uvuvi sanjari na uhakika wa masoko.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa. Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati katika maeneo ya vipaumbele.

Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni pamoja na:-

a) Kutofanya uwekezaji wa kisasa katika ranchi za Taifa ambao utasaidia wafugaji kujifunza mbinu za ufugaji;

b) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu;

c) Uhaba wa Maafisa ugani wa uvuvi na mifugo ikilinganishwa na mahitaji ya wataalamu hao katika Halmashauri;

d) Mpango mkakati wa kuongeza viwanda vya bidhaa za ngozi, maziwa na nyama hapa nchini ili kupunguza uagizaji wa bidhaa za ngozi nje ya nchi;

e) Kupunguza tozo nyingi kwenye bidhaa za maziwa ili wawekezaji wasijitoe kwenye sekta ya maziwa;

f) Kuweka mazingira bora ili kuchochea sekta binafsi kushiriki katika kuwekeza katika sekta ya mifugo na uvuvi;

g) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi;

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Machi, 2018 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2018.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.2.1 Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

#### a) SEKTA YA MIFUGO - FUNGU 99

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha **2017/2018** Wizara kupitia Fungu 99 iliidhinishiwa jumla ya shilingi

**29,963,524,000.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **25,963,524,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **4,000,000,000.00** fedha za ndani ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara kupitia Fungu 99 ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi **21,749,412,823.87** ambayo ni sawa na **asilimia 83.8**. Kwa upande wa fedha za maendeleo hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyokuwa imetolewa.

## b) SEKTA YA UVUVI - FUNGU 64

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia fungu 64 liliidhinishwa jumla ya shilingi **16,792,645,829.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **14,792,645,829** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **2,000,000,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni shilingi **7,667,949,400** ambazo ni sawa na **asilimia 52** na hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa.

## c) Maoni kuhusu mwenendo wa utoaji fedha

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo, fedha za maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu.

## d) Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kwa kupitia mafungu yote mawili (Uvuvi 64 na Mifugo 99) ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi **36,105,367,551:00** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 makusanyo ya maduhuli yalikuwa shilingi **26,923,480,109:00** ambayo ni sawa na **asilimia 75**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato ya wastani wa asilimia **75%** ya malengo ya makadirio ya makusanyo. Kamati imeridhishwa kwa namna ambayo sekta hizi zinakusanywa maduhuli ya shilingi **26,923,480,109:00** kwa kipindi cha nusu mwaka, hata hivyo Kamati imesikitishwa na ukweli kwamba, pamoja na makusanyo hayo Serikali imeshindwa kuipelekea Wizara fedha yoyote ya maendeleo kiasi cha shilingi **6,000,000,000** iliyoidhinishwa na Bunge katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** hii inadhihirishwa namna ambavyo Serikali haitilii manani umuhimu wa sekta hizi katika kukuza pato la Taifa, kuongeza ajira, na kuchochea uchumi wa viwanda.

## 2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kufanya ukaguzi wa tathimini halisi ya fedha iliyotumika (*Value for Money*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuweza kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kutokana na miradi ya maendeleo kutopelekewa fedha yeyote. Na hivyo kulikwamisha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kikatiba wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli zinazotekelezwa na Wizara kupitia program na miradi mbalimbali ambayo ilipata fedha katika miaka ya nyuma katika Mkoa wa Kigoma ambapo Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA),Kampasi ya Kibirizi – Kigoma ambayo ni moja ya vituo vya mafunzo ya elimu ya uvuvi vilivyo chini ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi-

FETA ambavyo vinawajibu wa kutoa elimu na mafunzo ya muda mrefu ya uvuvi na ufugaji viumbe kwenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilibaini changamoto kubwa zinazoikabili Kampasi ya Kibirizi kuwa ni ufinyu wa rasilimali fedha ,uhaba wa vitendea kazi na upungufu wa watumishi ukilinganisha na mahitaji halisi. Kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali ili kukabiliana na changamoto ya maafisa ugani ni muhimu ikawezesha vyuo vya uvuvi kifedha ili kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuzalisha wataalam wa uvuvi.

## 2.4 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 22-23 Machi, 2018 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019, Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/ 2019 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa 2025.

## 2.5 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kuchambua malengo ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuifanya Wizara Mifugo na Uvuvi kuwa Wizara kamili ili iweze kujiendesha na kutekeleza shughuli zake rasmi kupitia mafungu mawili tofauti (*Two Separate Votes*) yaani Fungu 64 (sekta ya uvuvi) na Fungu 99( sekta ya Mifugo).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 64 na

Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **56,455,749,000.** Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi **156,082,062,250.**

### 2.5.1 FUNGU 64: SEKTA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 Wizara kupitia fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **21,093,086,000**. Kati ya fedha hizo, shilingi **13,966,406,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **7,126,680,000,** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi **50,525,670,000** zitakazopatikana kutokana na mapato yatokanayo na ushuru wa soko, leseni za kuvua na kusafirisha samaki na mazao yake na ushuru wa mrahaba.

### 2.5.2 FUNGU 99: MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **35,362,663,000.** Kati ya fedha hizo, shilingi **30,362,663,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **5,000,000,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi **105,556,392,250** zitakazopatikana kutokana na leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi (*Exporty Duty License fees*), ada mbalimbali, ushuru wa soko, mauzo ya chanjo na kodi za pango la nyumba za Serikali na mauzo ya zabuni.

## 2.6 MALENGO YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELE KWA SEKTA YA MIFUNGO NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa zimepanga kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara.

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi malengo yatakayotekelezwa ni pamoja na:-

a) Kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi;

b) Kuimarisha, kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi pamoja na kutunza mazingira;

c) Kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi;

d) Kuhamasisha, kuendeleza na kusimamia ufugaji wa samaki na viumbe wengine kwenye maji;

e) Kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi; na

f) Kufanya sensa ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya Mifugo, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

a) Kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kutenga maeneo ya malisho;

b) Kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo;

c) Kuimarisha huduma za utafiti, ugani na mafunzo ya uzalishaji bora wa mifugo ili kupata bidhaa za mifugo zenye ubora (nyama, ngozi na maziwa);

d) Kuimarisha vituo vya uhimilishaji Kitaifa na Kikanda;

e) Kuboresha masoko ya miundombinu ya uzalishaji mifugo na kuongeza thamani bidhaa za mifugo;

f) Kuimarisha tasnia ya nyama na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa;

g) Kuimarisha tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo; na

h) Kufanya sensa ya mifugo.

## 2.7 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019 na kuridhishwa nayo. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha iliyotengwa kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele ilivyojiwekea kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake, imebaini kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa fedha za miradi ya maendeleo na makusanyo ya maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hatua hii inadhihirisha kuwa Serikali imejipanga na imeanza kutambua umuhimu wa kuwezesha sekta za uvuvi na mifugo kwa lengo la kuchangia pato la Taifa, ajira na lishe.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara kupitia mafungu yote mawili fungu 64 na fungu 99 inaombwa kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 12,126,680,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikilinganishwa na maombi ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 6,000,000,000**. Maombi haya ni ongezeko la **asilimi 51**. Aidha, kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2018 Wizara kupita mafungu yote imekadiria kukusanya **shilling 156,082,062,250** ikilinganishwa na makadirio ya **shlingi 36,105,367,551** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kiasi hiki ni ongezeko la makadirio ya makusanyo ya **asilimia 76.87**. Kamati inaipongeza Serikali kwa dhamira ya kuinua sekta za mifugo na uvuvi kwa kuongeza kiasi cha fedha zinazopangwa na kiasi cha maduhuli kinachotarajiwa kukusanywa. Kamati inasisitiza kuwa, kupanga ni jambo moja, hivyo ni vema Serikali ikatekeleza dhamira hii kwa kutoa kiasi cha fedha zinazoombwa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuongeza mchango wa sekta katika pato la wadau na serikali kwa ujumla.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo tisa (9) yafuatayo:-

### 1. UWEKEZAJI MDOGO KATIKA SEKTA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uvuvi ni moja ya sekta inayochangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kuuza samaki ndani na nje ya nchi hivyo husaidia nchi kupata fedha za kigeni. Aidha, Sekta ya Uvuvi ina mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe bora, na kipato. Hata hivyo, maendeleo katika sekta hii si mazuri sana kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo bajeti ndogo inayotengwa na kutolewa isiyokidhi mahitaji na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya uvuvi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ndogo inayotengwa na isiyokidhi mahitaji inajidhihirisha katika bajeti iliyowasilishwa na Serikali ikiwianishwa na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kwa mfano; kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara imetengewa **shilingi 7,126,680,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha zilizotengwa ni kidogo na hazitoshi kutekeleza hata kipaumbele kimoja cha Wizara ambacho kinahusu kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu ambao unahitaji uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa bandari ya uvuvi, miundombinu ya kuhudumia meli za uvuvi, gharama kubwa za kuendesha doria za anga na baharini.

### 2. MTIRIRIKO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO USIORIDHISHA

**Mheshimiwa Spika,** upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na

kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za Uvuvi. Kwa mfano; kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 64- Uvuvi ilitengewa **shilingi 2,000,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ilihusu Maendeleo ya Uvuvi na Ukuzaji viumbe kwenye maji, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa fedha usioridhisha umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika sekta ya uvuvi ambapo takwimu zinaonyesha mchango wa sekta ya uvuvi kwenye Pato la Taifa umekuwa wa kusuasua na usioridhisha ambapo kwa Mwaka 2016 uvuvi ulichangia Pato la Taifa kwa wastani wa **asilimia 2**, ambapo mwaka 2015 mchango wa uvuvi kwenye Pato la Taifa ulikuwa **asilimia 1.5,** mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa utaendelea kuwa mdogo endapo Serikali haitachukua hatua madhubuti za kuinua sekta hii.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo huu unaashiria kwamba:-

- Uvuvi si moja ya vipaumbele vya Serikali;

- Serikali haitambui umuhimu wa sekta za uvuvi katika ustawi wa sekta zingine; na

- Serikali haitambui mchango wa sekta ya uvuvi kwenye maisha ya kila siku ya wananchi ambapo zaidi ya watu milioni 4 wanaendesha maisha yao kwa kutegemea shughuli za uvuvi ikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, na utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa kutambua mchango wa uvuvi katika kuwapatia wananchi ajira, lishe bora, kipato na Pato la Taifa inaishauri Serikali kuimarisha utoaji fedha kwa ajili ya sekta ya uvuvi kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

## 3. UDHIBITI WA UVUVI HARAMU

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu Tanzania imeendelea kukabiliwa na changamoto ya uvuvi haramu, ambayo imepelekea kupungua kwa wingi wa rasilimali za uvuvi na kuathiri upatikanaji wa lishe bora, kipato, ajira na Pato la Taifa. Baadhi ya madhara ya uvuvi haramu ni pamoja na kusababisha upungufu mkubwa wa samaki, uharibifu wa matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki na kuharibu ikolojia ya viumbe wa majini.

**Mheshimiwa Spika,** madhara yanayoambatana na uvuvi haramu yamepelekea Serikali kuchukua hatua madhubuti za kupambana na uvuvi haramu ikiwa ni pamoja na Operesheni Sangara iliyoanza kutekelezwa mwaka 2018 kwa lengo la kudhibiti uvuvi wa kutumia sumu, mabomu, baruti na zana zingine haramu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali ili kuweza kuwa na uvuvi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo. Hata hivyo, Kamati imepokea malalamiko kutoka kwa wavuvi kuhusu namna Opereshion Sangara, 2018 ilivyotekelezwa kuwa ilikiuka misingi ya haki za binadamu kwani utekelezaji wake umegubikwa na vitisho, ubabe na viashiria vya rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya masuala yanayolalamikiwa ni pamoja na kuchomwa kambi za wavuvi, nyavu na mitumbi, kuitaifishwa nyenzo za uvuvi, na mali nyingine za wavuvi. Kufuatia malalamiko hayo Kamati inamaoni kuwa, ni vyema Serikali ikafanya tathimi ya utekelezaji wa Operesheni Sangara, 2018 na kurekebisha kasoro zitakazobainika ili kuweka misingi ya namna bora zaidi ya kutekeleza operesheni za aina hii bila ya kuleta athari kwa wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ili kukomesha uvuvi haramu ni vyema jitihada kubwa zikaelekezwa kwenye kudhibiti utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu pia kwa Serikali kushirikisha nchi jirani za Kenya na Uganda hasa kwa kuzingatiwa kuwa Ziwa Viktoria linatumiwa pia na nchi hizo kwa lengo la kuhifadhi rasilimali katika Ziwa Viktoria kwa pamoja.

## 4. UFUGAJI WA VIUMBE KWENYE MAJI NA UKUZAJI WA SAMAKI KATIKA VIZIMBA (AQUACULTURE)

**Mheshimiwa Spika,** tafiti mbalimbali zinaonyesha ifikapo mwaka 2030 Afrika itakabiliwa na uhaba mkubwa wa samaki kwa kiasi cha upungufu wa **tani milioni 1.8** upungufu huu unatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ulaji wa samaki kutokana na virutubisho vyake muhimu kwa mwili wa binadamu, uvuvi uliopitiliza/uliokithiri (*Overfishing*) na matumizi ya zana haramu za uvuvi yanayopelekea pamoja na mambo mengine kuharibu mazalia ya samaki.

**Mheshimiwa Spika,** ufugaji wa viumbe kwenye maji na ukuzaji wa samaki katika vizimba ndio njia mbadala ya kuongeza uzalishaji wa samaki hivyo kuwezesha upatikanaji wa samaki endelevu. Hata hivyo, ufugaji wa samaki kwenye vizimba unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa maafisa ugani, ukosefu wa elimu na mitaji, pamoja na ukosefu wa teknolojia na nyenzo za kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizo, Kamati ina maoni kuwa ni vyema Serikali ikatambua fursa zilizopo kwenye ufugaji wa samaki kwenye vizimba kwa kuweka na kutekeleza mipango itakayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kilimo/ ufugaji wa samaki. Aidha, ni vyema Serikali ikatambua kuwa ufugaji wa viumbe kwenye maji hususan kwenye mabwawa ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ili ufugaji wa viumbe kwenye maji usaidie kukabili uhaba wa samaki uliopo ni lazima ufanyike baharini, kwenye maziwa na mito, hivyo mipango ya Wizara ni lazima ijielekeze kwenye maeneo hayo.

## 5. MABADILIKO KUHUSU TARATIBU ZA UINGIZAJI NA USAMBAZAJI SAMAKI NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya ulaji wa samaki nchini ni makubwa kuliko samaki wanaoweza kuvuliwa ambao ni **tani 350,000** kwa mwaka**,** kwa sasa kuna namna mbili zinazoweza kusaidia upungufu huo. Kwanza ni kwa kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba na namna nyingine ni kwa kuagiza samaki kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba bado haujawa wa uhakika na kutegemewa, upungufu uliopo unafidiwa kwa kiasi kikubwa na uagizaji wa Samaki kutoka nje ya nchi ambao huuzwa kwa bei nafuu kuliko samaki wanaopatikana nchini na hivyo wananchi wengi kumudu gharama zake. Kufuatia uagizaji huu wa samaki kutoka nje ya nchi na kwa kuwa wanauzwa kwa bei nafuu kumepelekea kupungua kwa soko la samaki wa ndani na hivyo kuikosesha Serikali na wavuvi mapato.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto hiyo Serikali imeanzisha tozo ya **usd 0.25** kama mrabaha kwa kila kilo ya samaki ili kupunguza uagizwaji wa samaki kutoka nje ya nchi ambao hupatikana nchini. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuongeza mapato ya ndani na kuwasaidia wavuvi kunufaika na rasilimali za uvuzi zilizopo nchini, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

a) Kufanya tahimini ya ongezeko la tozo iliyoongezwa ambayo imepelekea wafanyabiashara wengi wa samaki kushindwa kuagiza samaki kutoka nje kutokana na wananchi kushindwa kumudu bei ya samaki hao. Kamati inaamini kushindwa kwa wafanya biashara kuagiza samaki kutoka nje kutaongeza upungufu wa samaki wa ndani na hivyo kupanda kwa bei;

b) Kuongeza tozo ya uagizaji samaki kutoka nje sio suluhisho la uhaba wa samaki uliopo nchini, Kamati inaishauri

Serikali badala ya kuongeza tozo ya samaki ijikite katika kuongeza uzalishaji kwa kuhamasisha wananchi pamoja na kuwezesha wavuvi kufanya ufugaji wa samaki ambao utasaidia upatikanaji wa samaki wengi na hivyo wafanyabiasha kushindwa kuagiza samaki kutoka nje ambao si wazuri kama samaki wa ndani;

c) Ni vyema Serikali ikawa na kipindi cha mpito cha utekelezaji wa tozo iliyoanzishwa, Aidha wakati wa kipindi cha mpito Serikali kwa kutumia wataalam wake inaweza kupunguza gharama za tozo hiyo na kuweka kiwango ambacho hakitaathiri mapato ya Serikali lakini pia hakitazorotesha ushiriki wa sekta binafsi.

## 6. BAJETI NDOGO YA SEKTA YA MIFUGO ISIYOWIANA NA MCHANGO WA SEKTA HIYO KATIKA PATO LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo inayojumuisha ng'ombe **milioni 25.8**, mbuzi **milioni 17.1,** kondoo **milioni 9.2,** nguruwe **milioni 2.67** na kuku **milioni 42**. Pamoja na takwimu za wingi wa mifugo iliyopo, kwa bajeti ndogo ya Serikali ambayo imekuwa ikitengwa ni dhahiri kwamba haiwezi kuleta kuleta tija katika pato la wafugaji na uchumi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mukutadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika miundombinu ya mifugo, kutoa elimu ya ufugaji bora na wa kisasa pamoja na kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji nyama, maziwa na ngozi. Ujenzi wa viwanda hivi, vitasaidia kuongeza thamani ya rasilimali hizo.

## 7. UWEKEZAJI KATIKA RANCHI ZA TAIFA

**Mheshimiwa Spika**, Ranchi za Taifa ni rasilimali muhimu na fursa muhimu katika kuchangia pato la Taifa na uchumi wa wafugaji. Tanzania ina jumla ya Ranchi **13** zenye ukubwa wa jumla ya hekta **627,856,** katika mikoa **10** chini.

Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa hali ya uwekezaji uliopo katika Ranchi za Taifa haukidhi na hauendani na fursa ya ukubwa wa rasilimali zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matumizi kidogo ya maeneo ya ranchi, wananchi waishio karibu na ranchi hizi wamekua wakivamia na kulisha mifugo yao na kusababisha migogoro isiyokuwa ya lazma. Ili kuondokana na changamoto hii Kamati inashauri ranchi zote walizopewa wawekezaji na kushindwa kuziendeleza zirudishwe Serikalini ili Serikali iweze kuziendeleza kwa kuziboresha zitumike kama maeneo ya malisho kwa wafugaji waishio pembezoni mwa ranchi hizo, mara baada ya uboreshaji utakaofanyika ranchi hizo zitumike kama shamba darasa ambalo litasaidia wafugaji wengi kujifunza mbinu za ufugaji bora na kuachana na ufugaji wa kuhamahama kwenda kutafuta malisho.

## 8. UWEKEZAJI MDOGO KATIKA TASNIA YA MAZIWA

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu za mwaka 2015 zilizotolewa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) zinaonyesha Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi na tano (15) zinazoongoza kwa idadi kubwa ya ng'ombe duniani, inashika nafasi ya tisa (9) kwa wingi wa ng'ombe wa kisasa na wa kienyeji na ni ya tatu barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan . Pamoja na kuwa na idadi kubwa ya mifugo katika uzalishaji wa maziwa, Tanzania haimo katika nafasi kumi na tano (15) za nchi zinazozalisha maziwa kwa wingi, hali hiyo inatokana na kuwa na idadi ndogo ya ngo'mbe wa kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina viwanda vikubwa vya usindikaji maziwa visivyopungua vitano ambavyo vina uwezo wa kuchakata bidhaa za maziwa zenye uhai mrefu zaidi. Viwanda vya usindikaji maziwa vilivyopo nchini vinahitaji lita **lita 700,000** za maziwa ili kukidhi mahitaji ya viwanda ya kila siku, wakati usindikaji uliopo ni **lita 200,000** tu na hivyo kusababisha upungufu wa **lita 500,000** ambazo hufidiwa kwa kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi na hivyo kuigharimu Serikali zaidi ya shilingi **bilioni 165** kwa mwaka

na kudidimiza ukuaji wa viwanda vya ndani huku viwanda vya nje vikinufaika na soko lililopo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** gharama kubwa inayoingiwa na Serikali kuagiza maziwa nje ya nchi inatokana na uwekezaji mdogo kwenye sekta hiyo, Aidha viwanda vya usindikaji maziwa vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ya ushindani mkubwa wa maziwa yanayoagizwa kutoka nje ya nchi ambayo yanawekewa dawa ili yasiharibike, tozo za kodi mbalimbali, kununua maziwa yasiyo na ubora kutokana na ufugaji usiokuwa na tija, ukosefu wa chakula bora na malisho, miundombinu mibovu, upotevu na uharibifu wa maziwa kabla ya kufikishwa viwandani na baadae sokoni, kukosekana kwa vituo vya ukusanyaji wa maziwa pindi yanapozalishwa kwa kuwa vituo havina vifaa vya kisasa vya kuhifadhia maziwa pindi yazalishwapo na kufikishwa kiwandani au kabla ya kumfikia mlaji.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hii na nyingine nyingi zimekuwa zikikwamisha ukuaji wa sekta, hivyo Kamati inashauri ni vyema Serikali ikaangalia tozo upya msululu wa tozo za kodi mbalimbali sekta hii ili kuvutia wawekezaji wapya kuja na uwekezaji na upanuzi mkubwa wa viwanda ili kusaidia kuongeza pato la Taifa katika sekta na kufikia azma ya Tanzania ya Viwanda.

Aidha, ni vyema Serikali ikashirikiana na viwanda kutatua changamoto na kero mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa wafugaji ili wafuge kisasa pamoja na kuzingatia kanuni za ufugaji bora ,kuwa na mbegu bora zenye uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa cha maziwa, kutatua migogoro iliyopo kati ya wakulima na wafugaji na kuongeza bajeti katika sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuanzisha viwanda vya usindikaji maziwa kila kanda Kama ilivyokuwa siku za nyuma. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha vituo vya kutosha vya kukusanyia maziwa kwani uchache wa vituo hivi au kutokuwepo kabisa kwa vituo katika baadhi ya maeneo yanapozalishwa maziwa kwa wingi

imekuwa ni taabu kwa wafanyabiashra wa viwanda vya kuchakata maziwa na wafugaji pia kwani hupelekea kupata hasara ya maziwa kuganda au kuharibika kutokana na ukosefu wa vifaa duni vya kupozea maziwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya usindikaji maziwa pamoja na kuinua viwanda vya ndani, Kamati inaishauri Serikali na taasisi zake kuacha matumizi ya maziwa yanayoagizwa kutoka nje ya nchi na kutumia maziwa yanayozalishwa nchini kama ambavyo imefanyika na kufanikiwa kwenye samani za ofisi za Serikali ambapo samani zote za ofisi za Serikali zinatengenezwa nchini tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi**.** Kamati inaamini kwa kufanya hivi kutawezesha ukuaji wa viwanda vya ndani, kuongeza mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la Taifa, kuimarisha kipato cha mfugaji na familia pamoja na kuimarisha afya itakayotokana na lishe bora**.**

## 9. KUWEKA MAZINGIRA BORA ILI KUCHOCHEA SEKTA BINAFSI KUSHIRIKI KUWEKEZA KATIKA MNYORORO WA THAMANI KWA MAZAO YA MIFUGO NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** sekta binafsi ni wadau muhimu katika kukuza sekta na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi na kwa kufanya hivyo, imekuwa ikichangia katika pato la Taifa, kutoa ajira na soko la uhakika kwa wakulima nchini. Pamoja na mchango wa sekta binafsi kwa Taifa, changamoto mbalimbali zimekuwa zikikwamisha ushiriki wake katika njia za uzalishaji mali. Aidha, ili sekta hii iweze kushiriki na kutoa mchango wake kikamilifu, Serikali hainabudi kuwawekea mazingira mazuri kibiashara yatakayowezesha uwekezaji wenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake imebaini kuwepo malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta binafsi wanaojihusisha kwa namna moja au ingine na mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi. Msingi wa malalamiko yaliyopo ni kutokuwepo mazingira wezeshi ya kuwekeza katika sekta ya kuongeza

thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi kwa faida. Kwa ujumla malalamiko yao yanajikita katika kuwepo changamoto ikiwa ni pamoja na:-

a) Kuwepo mamlaka nyingi za Serikali za udhibiti unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji. Kwa mfano Mamlaka ya udhibiti ubora wa chakula na dawa (TFDA), Shirika la viwango nchini (TBS) na Idara ya Afya, Taasisi hizi zinahusika na usalama na ubora wa bidhaa nchini, zimekuwa na muingiliano wa majukumu unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa kiwanda;

b) Ushindani usio wa haki unaosababishwa na bidhaa kutoka nje na zisizo na ubora kusababisha kukosa masoko ya uhakika ya bidhaa za ndani;

c) Tozo nyingi kwa baadhi ya bidhaa, mfano wasindikaji wa maziwa wanakabiliwa na changamoto ya tozo za ladha za maziwa, vifungashio na leseni za usajili;

d) Ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini unaopelekea ugumu wa wakulima kufikisha bidhaa katika masoko au viwanda kwa muda unaostahili, na

e) Ukosefu wa umeme wa uhakika kwa ajili ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika ustawi wa sekta, Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto hizi, kwa kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora yasiyo na urasimu yatakayowezesha na kuvutia sekta binafsi. Kamati inaamini Mipango mbalimbali iliyowekwa na Serikali itatekelezwa kwa ufanisi endapo sekta binafsi itashiriki kikamilifu.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga J. Mpina, (Mb), na Naibu Waziri Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb), Katibu Mkuu - Uvuvi Dkt. Yohana Budeba na Katibu Mkuu - Mifugo Dkt. Maria Mashingo pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa , Mb | Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3.Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | Mjumbe |
| 4.Mhe.Eng. Edwin A. Ngonyani , Mb | “ |
| 5.Mhe. Justine Joseph Monko, Mb | “ |
| 6.Mhe. Deo Kasenyenda Sanga , Mb | “ |
| 7.Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb | “ |
| 8.Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | “ |
| 9.Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | “ |
| 10.Mhe. Haroon Mullah Pirmohamed, Mb | “ |
| 11.Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | “ |
| 12.Mhe. Lucy Saimon Magereli , Mb | “ |
| 13.Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb | “ |
| 14.Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | “ |
| 15.Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | “ |
| 16.Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | “ |
| 17.Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb | “ |
| 18.Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb | “ |
| 19.Mhe. Haji Khatibu Khai, Mb | “ |
| 20.Mhe. Sikudhani Yasin Chikambo, Mb | “ |
| 21.Mhe. Mbaraka Salim Bawazir, Mb | “ |
| 22.Mhe. Juma Ali Juma, Mb | “ |
| 23.Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | “ |
| 24.Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | “ |
| 25.Mhe. Mattar Alli Salum, Mb | “ |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Martha Chassama, Ndg. Virgil Mtui na Ndg Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
17 MEI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimepokea majina ya wachangiaji. Kama ulivyo utaratibu wetu, tutaanza na Mheshimiwa Julius Kalanga, atachangia dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Susane Maselle, dakika tano halafu Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ambayo nitapata taabu kidogo kulingana na mazingira yenyewe ya sekta kwa sababu nina maslahi nayo mapana kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitapata taabu kwa sababu Mawaziri wlaiopo katika Wizara hii wote ni vijana na ni marafiki zangu ambao tunafahamiana kwa muda mrefu lakini ambao kwa kweli katika Wizara hii wameshindwa kabisa kabisa kuonesha ujana wao katika Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu kuna makundi makubwa manne; kuna kundi la wafanyakazi, wakulima, wafugaji na kuna wavuvi. Kama Serikali inatafuta ugomvi kwa makundi haya yote manne hii Serikali inategemea ku-*survive* kwa mazingira gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitatu mfululizo hawajapandisha mishahara ya watumishi, miaka mitatu mfululizo wameshindwa kupeleka mbolea kwa wakulima, miaka mitatu mfululizo wameshindwa kutuletea hata shilingi ya wafugaji. Mheshimiwa Waziri, wanategemea nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Serikali ni kwenda kuomba ridhaa kwa wananchi wakipewa wanakusanya kodi kwa niaba ya wananchi, wanapeleka huduma. Wao wanakusanya, hawatuletei huduma. Mkataba wetu kwa maana ya wananchi na Serikali tunakutana wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana wakaona ng'ombe kama chakula, wakaona kama kitoweo wanavyoenda kunywa maziwa pale, wakala nyama, wakala samaki, wakala kuku, wakala mayai, wakashiba mkaja hapa wakaendelea. Sisi ni uchumi! Sisi ni maisha yetu! Mheshimiwa Waziri anakubalije kumeza dhambi hii? Anakusanya bilioni ishirini na sita kutoka kwetu halafu anaandika kwenye bajeti yake hajapeleka hata shilingi. Kama binadamu, yeye anajisikiaje? Huu ni unyang'anyi uliohalalishwa na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Mheshimiwa Waziri, anatuletea bajeti, ndugu yangu, rafiki yangu kweli? Halafu amekusanya bilioni ishirini na sita, wameshindwa hata kutupa shilingi 100, kweli Mheshimiwa Waziri? Wafugaji wa nchi hii tumewakosea nini Serikali? Wizara zote wamepelekewa kidogo, sisi hata shilingi hawajatuletea, fadhila wanazotupa ni kutunyang'anya ng'ombe, fadhila wanazotupa ni kutunyang'anya samaki, nyavu, kutufilisi halafu kweli? Hata basi wangekuwa wanatunyang'anya, lakini wangeturudishia

hata sehemu basi, kwa nini Wizara hii inyimwe fedha kuliko Wizara zote katika nchi yetu? Tumewakosea nini tuwaombe radhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka yote ya nchi hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Serikali haijawahi kupeleka ruzuku; kilimo ina ruzuku, sisi hatuna! Sisi tunataka watutengenezee mazingira tufuge, lakini kweli wanakusanya hela, wanatunyang'anya hela kwa nguvu halafu hawaturudishii hata kidogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Mheshimiwa Waziri anajua ambayo imefanyiwa marekebisho ya tatu mwaka 1983 na 1997, imeeleza changamoto nne za wafugaji. Moja, ilizungumza habari ya ukosefu wa mikopo na mitaji ikazungumza habari ya magonjwa, ikazungumza habari ya ardhi, malisho ya maji na maeneo mengine ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 13 baadaye serikali hii imeshindwa kutatua hata tatizo moja ambalo sera hii imeainisha kwenye kitabu cha Serikali. Wanahitaji miaka mingapi kutusaidia malisho na wanahitaji miaka mingapi kutusaidia majosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anasema amepeleka *zero,* kwetu sisi, tunataka watuwezeshe tu. Hii sera wametunga wenyewe, maeneo mengine inasema kabisa kwamba, matatizo haya yametokea kwa sabahu maeneo ya wafugaji yamevamiwa na wakulima na maeneo mengine yamevamiwa na uwekezaji wa *National Parks,* lakini *ranch* za Taifa wamewapa watu hawataki kuwarejesha wala hawataki kuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana katika nchi yetu kwa mujibu wa takwimu *60 hectors million* ni kwa sababu maeneo yanafaa kwa ajili ya nyanda za malisho ya mifugo. Mpaka leo kwenye ramani ya nchi hii miaka 50 ya uhuru hakuna mahali hata pamoja kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2010 iliyotangaza rasmi maeneo ya nyanda za

malisho ya wafugaji, lakini wanayo sheria, hawatekelezi sheria wanatunyanyasa, hawatutengei maeneo ya malisho ya mifugo, tukiingia kwenye hifadhi wanatuuwa, tukiingia kwenye *parks* wanatuuwa, tukiingia kwenye maeneo ya mapori wanatuuwa, wanatunyang'anya ng'ombe wetu wanauza, sisi twende wapi? Watueleze leo? Tumepata soko Kenya, juzi wameenda wamezuia tusiuze, hawana masoko tupeleke wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mahali pa kulisha, hakuna maji, hakuna dawa, hakuna ruzuku wanayotuletea. Tunataka kuuza, tumekosa masoko ndani tumepata masoko nje wanataka kutu-*charge* kodi kwa lipi walilowekeza? Kwa nini wanataka kuvuna pasipo kupanda? Kwa nini wao wanataka kuvuna pasipo kupanda? Wamewekeza nini kwenye mifugo wanatukamata kila siku? Wametuletea nini? Wanasema wasipeleke nje, tupe masoko basi; hakuna haki pasipo wajibu. Wizara wajibu wao ni nini katika hili wanalotu-*charge* kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji wa fedha. Mwaka 2015/2016, walitenga shilingi bilioni nne hawakupeleka hata shilingi moja. Mwaka 2016/2017 walitenga bilioni nne hawakupeleka hata shilingi, mwaka jana bilioni nne hawakupeleka hata shilingi, miaka mitatu mfululizo, hivi wanafikiri sisi tunaishije? Wanatutaka nini wafugaji wa nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wamebaki kukusanya kodi na kutupiga na kutunyang'anya ng'ombe, lakini wao hawatuchangii chochote. Natamani wafugaji wa nchi hii siku moja, wiki moja tu wawanyime maziwa, wawanyime nyama, mayai, samaki, kama hawajafa humu ndani, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utitiri wa kodi katika sekta ya mifugo. Hii Mheshimiwa Waziri naomba atuambie leo, mtu akitaka kuwa na *Export License* ya Mifugo anatakiwa kulipa Sh.2,500,000/=, lakini wakati huo huo anatakiwa kujisajili kwenye Bodi ya Nyama Sh.100,000/=,

lakini wakati huo huo anatakiwa alipe *Movement Permit* Sh.2,500/= kwa kila ng'ombe. Akipeleka pale Namanga anatakiwa kulipa Sh.20,000/= kwa kila ng'ombe, anatakiwa kulipa *Market Fee* Sh.5,000/= kwa kila ng'ombe, anatakiwa kulipa Sh.2,000/= mpaka Sh.3,000/= ya hela za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe mmoja tu akisimama wao wanachukua Sh.50,000/= hawajachangia chochote, hawajafanya chochote, wanadai hizo fedha. Kama mtu ana *Transport License* ya Mifugo anapeleka Kenya kwa nini wana-*charge* ng'ombe mmoja mmoja tena fedha? Kama sio wizi ni nini huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu ana *Permit* ya kusafirisha mifugo kwa nini wanatu-*charge* Sh.20,000/= kule Namanga? Tumewakosea nini sisi wafugaji wa nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunafuga kwa tabu, sisi tunachunga, sisi tunaondoka asubuhi umekunywa uji unarudi saa 12.00 jioni. Tunateseka sisi kutafuta malisho, tunateseka kutafuta maji, badala ya kutuonea huruma wanatu-*charge* hata kile kidogo tunachotafuta. Hii sio *fair,* linaniumiza kwa sababu linanigusa. Kwa nini wanatuwekea tozo hizi? Kwa nini wameondoa tozo nyingine kwenye mazao mengine yote mifugo wameacha? Kwa nini watu-*charge* mara kumi kumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina leseni ya kupeleka ng'ombe Nairobi nimepata soko, unaenda kunizuia tena pale unani-*charge* Sh.20,000/= kila ng'ombe, nimekukosea nini? Kwa nini unatu-*charge* hiyo 20,000/=? Atuambie Waziri hizi tozo atapunguza lini, mbona kwingine wanapunguza? Au wana lengo la kuua mifugo? Waue basi tubaki hatuna, kwa sababu, huu ni unyang'anyi wa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapata hasara katika sekta ya mifugo; nchi yetu ni nchi ya tatu Afrika kwa

upatikanaji wa ng'ombe, lakini Mheshimiwa Waziri anajua tunapoteza zaidi ya bilioni mia moja ishirini kwa sababu ya uingizaji wa maziwa nchini, tunapoteza zaidi ya shilingi bilioni saba kwa sababu ya uingizaji wa nyama nchini. Tunapoteza zaidi ya bilioni hamsini na saba kwa sababu ya upelekaji wa ngozi nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni aibu gani Taifa linaloongoza kwa mifugo tunaongoza kuingiza nyama na maziwa na hii mifugo yote tunapeleka sisi Kenya wana-*process* wanatuletea sisi, kwa nini? Hivi hawajisikii aibu tunapoteza rasilimali za Taifa kwa mazingira ambayo Serikali inapaswa tu kuweka viwanda ili tuuze ndani humu? *(Makofi)* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wameshindwa kujenga viwanda, hakuna muunganiko kati ya viwanda na mifugo, tukipeleka nje wanatu-*charge* wanasema tusitoroshe, tutatorosha tu. Tutatorosha tu na naamini mpaka watengeneze barabara ya kuzunguka mipaka hii, ili wazuie ng'ombe tumeshauza wengi sana. Watutengenezee mazingira rafiki ndani ya nchi ili wafugaji wapate masoko wauze nchini. Wasitembelee migongo yetu kwa sababu wao wameshindwa kutimiza majukumu yenu, wajenge mazingira rafiki. Tunaomba watuambie hizo tozo wataziondoa wakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali, moja, wafugaji watengewe maeneo yao na yalindwe kisheria; *Ranch* za Taifa ambazo wawekezaji wameshindwa kuendeleza watupatie tuendeleze sisi, hata tukilipia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, watuondolee tu kodi kwenye dawa za uogeshaji wa mifugo na chanjo za mifugo, sisi tutanunua, lakini waondoe kodi ili na sisi tuweze kuendesha wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mapori ya akiba yatolewe yarejeshwe kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Suzan Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mheshimiwa Catherine Ruge ajiandae.

**MHE. SUSAN P. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hatukatai wala hatupingi *Operation Uvuvi Haramu,* lakini tunapinga *operation* hii inavyoendeshwa. *Operation* hii inaendeshwa bila kufuata weledi, wavuvi wetu wamekuwa wakiombwa rushwa kutokana na hii *operation,* utakuta mvuvi anaombwa rushwa ya mpaka milioni ishirini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu ni watu wa chini sana, unaenda unamwomba rushwa ya milioni ishirini, wakikataa wanakamata nyavu zao hata kama ni halali kwa uvuvi, wanaenda kuzichoma. Huu ni uonevu wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu wamekuwa wakionewa sana, wanalipishwa *fine* ambazo haziko kwenye Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003. Mtu analipishwa *fine* mpaka milioni hamsini. Huyu ni mvuvi wa hali ya chini, unategemea afanye nini? Matokeo yake wanaenda wanauza mpaka rasilimali zao, wanauza nyumba zao, wengine mpaka wamekufa kwa *pressure* kwa sababu ya hizi *fine. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua sheria hii inafanyiwa marekebisho na Wizara, lakini naomba sana Wizara inapofanya marekebisho haya iwahusishe wavuvi ambao ni wadau na ambao wataitumia hii sheria kuliko wao kukaa wenyewe na kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Wizara inaogopa kukutana na hawa watu? Kuna shida gani? Ni vizuri Wizara ikawashirikisha; *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wizara imetoa tangazo la hii *operation* ya kukamata nyavu ambazo si halali, lakini vile vile imezuia nyavu halali kuingia nchini. Kuna nyavu ambazo zimezuiliwa mipakani, sasa wanataka hawa watu watumie kitu gani? Hii sekta imeajiri zaidi ya watu milioni nne, sasa mnataka wafanye shughuli hii kwa kutuimia vifaa gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wamezuia lakini sioni Wizara ikiweka mkakati wa kuweza kuwasaidia hawa wavuvi kwa kuwapatia vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuvua. Wamekuwa wakivua kwa kutumia nyavu zisizokuwa halali kwa sababu hawana vifaa na Serikali nimeona kwamba, haina makakati wowote wa kupeleka pesa kwenye hii Wizara kwa ajili ya kutatua haya matatizo ya wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hakuna elimu ambayo inatokewa kwa hawa wavuvi. Wavuvi wengi wamezaliwa wakakuta wazazi wao wanafanya shughuli hii ya uvuvi, kwa hiyo wakaingia tu kwenye hii shughuli na kuanza kuvua, hawajui hata sheria zipi ambazo zinatakuwa kuwaongoza, na Wizara imekaa tu, inatangaza *operation* bila hata kutoa elimu kwa hawa watu, ili waweze kujua ni nini wanatakiwa wafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu viwanda. Hakuna viwanda vya kutosha vya kuchakata samaki. Tungeomba Wizara ije itueleze ina mkakati gani wa kuongeza viwanda kwa ajili ya kuchakata samaki kwa sababu, viwanda vilivyopo ni vichache na haviendani na mahitaji ya samaki wanaopatikana. Vile vile pia wametangaza *Operation Number* 3 ambayo wamesema kwamba kutakuwa na mahakama ambazo zinatembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Mahakama itakuwa inafanya kazi gani, kwa sababu wamesema kwamba watakuwa wanaenda moja kwa moja kwa wavuvi wakiwakamata wanawahukumu hapo hapo; hawa wavuvi wataweza kujitetea wakati gani? Kwa sababu hawatakuwa na muda wa kuweza kutafuta watu wa kuwatetea. Wamesema kwamba, watakuwa wanaenda wanatoa hukumu hapo hapo, hiyo si sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwamba Bunge liunde tume ambayo itaweza kufuatilia hizi *operation;* kwa sababu kumekuwa na matamko. Tangu matamko yametoka watu wamefanya kama mradi wa kujipatia pesa, kila mmoja anakuja na la kwakwe mpaka wavuvi wamekuwa hawaishi kwa raha. Tukumbuke kwamba hawa ni watu wanyonge na wamesema kwamba Serikali yao inasimamia watu wanyonge. Watu wanyonge ndio hawa wavuvi wetu, sasa wanataka wasimamie watu gani? Naomba kwenye hilo tuweze kulisimamia kabisa kwa sababu hizi *operation* zinaumiza wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu mifugo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Agness Mathew Marwa dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Ruge dakika 10, Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili nichangie Wizara hii kwa sababu na mimi pia ni mvuvi. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwatetea Watanzania na kuwajali Watanzania na hasa Watanzania masikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuchaguliwa katika Wizara hii. Kipekee zaidi nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii na Wataalam wake kwa kuwasababishia Watanzania umaskini uliokithiri na hasa Watanzania wafugaji, narudia. Nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na wataalam wake kwa kuwasababishia wavuvi wa Tanzania umaskini uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na mengine nianze kwa kuishauri Serikali. Kutokana na mapato waliyofanya na hasa yale waliyofanya baadhi yao ya unyang'anyi kwa wavuvi hawa niiombe Serikali sasa imuagize *CAG* aende akakague hizo pesa walizowanyang'anya hawa wavuvi ili iweze kufanya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili niishauri pia Serikali kwamba kutokana na kwamba, tuna matatizo mengi sana ya maji, elimu na mambo mengine Wizara hii safari hii kwa bajeti hii isipewe pesa, hiyo pesa iende kwenye elimu na mambo mengine, kwa sababu pesa waliyokusanya, ukisema uwaongezee pesa nyingine ni kwa ajili ya kusafiri na kwenda kuwapiga mabomu ndani ya bahari na ndani ya ziwa wavuvi na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kabisa Mheshimiwa Mpina ananisikia na narudia tena kumwambia Mheshimiwa Mpina ameingizwa chaka na Waziri Mkuu wake.

**MBUNGE FULANI:** Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameingizwa chaka na Katibu Mkuu wake pamoja na hawa wasaidizi wake, kwa nini, Katibu Mkuu, yeye ni Mtaalam wa mambo haya na ndiyo maana amechaguliwa kuwa Katibu kwa sababu yeye kasomea. Hata kama Waziri hajasomea mambo haya ya uvuvi basi Katibu Mkuu na wataalam wake wanaelewa; lakini kwa nini wanafanya vitu bila kuangalia shida au matatizo yanayowapata wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ndio wapiga kura wetu, hawa ndio wapiga kura wa Mheshimiwa Magufuli. Naamini kabisa hata Mheshimiwa Dkt. Magufuli jinsi alivyo *active* Mheshimiwa Rais wetu akinisikia leo atatuma tume haraka sana iende kuangalia haya mambo, kwa sababu hiki tunachokilalamikia hata Mheshimiwa Rais wakati mwingine haelewi ni nini kinachoendelea huko ziwani. Ni kama wakati ule wa *operation* ya bomoa bomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa *operation* ya bomoa bomoa kuna watu walivyosikia tu bomoa bomoa wakaingia na wengine ambao hata hawakuwa wanafanya au wanabomoa kihalali wakaanza kubomoa hovyo hovyo. Hata hivyo Mheshimiwa Rais kwa sababu ya kuwajali Watanzania, aliposikia vizuri na aliposikiliza kwamba watu hawa wanaonewa aliendа kuangalia na kweli sasa watu hawaonewi tena. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Rais hili suala alichukulie kwa umakini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe Bunge lako Tukufu liunde kamati kwa ajili ya uchunguzi wa haya masuala ya uvuvi ili kusudi tuwasaidie wavuvi hawa. Wanaumia, wanaumizwa sana, kwa sababu kuna baadhi yao wanachomewa nyumba, wanachomewa nyavu, lakini bila sababu za msingi. Tunakubali kwamba sheria zipo na sheria zenyewe tulizitunga sisi wenyewe, lakini wanapitiliza sasa wanavuka wanaenda nje ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niiombe sana Serikali iliangalie hili suala kwa umuhimu zaidi; kwa sababu kuna mambo mengine yanatokea kwa mfano Mheshimiwa Waziri leo amesema kwamba milipuko imepungua kwa wavuvi haramu. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Waziri milipuko imepungua kwa wavuvi haramu, lakini milipuko imeongezeka kwa wale wataalam wake wale wanaokwenda kule kwenye *operation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao sasa ndio kabla hawajaenda kuwakamata wavuvi wanaanza kulipua mabomu. Hivi lengo lao ni kwenda kuwakamata au lengo

lao ni kuwauwa wananchi? Hali ngumu Mheshimiwa Waziri, wananchi wana maisha magumu, kwa hiyo wananchi wengi sasa hivi wana ugonjwa wa *pressure,* sukari; hivi wanaposikia yale mabomu wanajisikiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya masuala yananiuma sana kwa sababu na mimi nimetokea kwa wavuvi, hawa wavuvi wanapata shida. Wavuvi wa nchi hii, fikiria ukianzia Zanzibar, Dar-es-Salaam, Mara na sehemu nyingine, huu ni uonevu unaopitiliza. Hebu Serikali ichukue hatua za lazima waende wakasaidiwe, waende wakaangaliwe, kwa sababu haya mambo yanayofanywa ni mambo ambayo ni ya uonevu tena uonevu uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri Mpina, anaona hii Wizara hawezi kuitendea haki Mheshimiwa Mpina amwambie tu Mheshimiwa Rais atoke ili kusudi amchague mvuvi kabisa aende akaangalie haya mambo anaelewa uvuvi. Wakinichagua hata mimi ambaye sijasomea hayo mambo kwa sababu, nilikuwa mvuvi naweza, kuliko hawa wataalam wanadanganya, wanakudanganya... *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:**...mimi najua wanamwingiza chaka, Mheshimiwa Mpina ni mtendaji mzuri, lakini wanamwingiza chaka kuna mambo mengine alitakiwa, kwa mfano... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa, kuna Taarifa huku. Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe Taarifa muongeaji kwamba, haya anayolalamikia ni matokeo ya *operation. Operation* mara nyingi inakumba waliopo na wasiokuwepo. Kama kwa

mfano, ilivyotokea kwenye *Operation* Tokomeza walikumbwa waliokuwepo na wasio kuwepo, lakini baadaye ikaundwa tume wale ambao walipembuliwa wale ambao wamekumbwa bila makosa watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimpe taarifa mwongeaji kwamba, acha *operation* iendelee, wale ambao watakuwa hawana mataizo watalipwa fidia. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa, unaikubali taarifa hiyo?

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hii taarifa siipokei kwa sababu huyu Mzanzibari ni mtani wangu, kwa hiyo naona anafanya bla-bla Bungeni tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, ulikuwa umesimama muda, unampa Mheshimiwa Kuchauka au unampa yupi taarifa?

Mheshimiwa Agness Mathew Marwa kuna Taarifa nyingine hapa.

**TAARIFA**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa Taarifa ya *Operation Tokomeza* iliyofanyika wakati Bunge hili limeanza, Bunge hili hili lilikataa kwamba wananchi wale walioathirika na *operation* tokomeza wasilipwe tena upande huu mkaitika kwa sauti kubwa hapana. Kwa hiyo natoa hiyo taarifa tusidanganye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu na yeye ni kati ya watu waliochanganyikiwa kukiwa kuna suala la umoja kama hili la Watanzania wote hapaswi kuongea mambo kama hayo. Ndiyo maana kipindi kile walikuwa wanatoka Bungeni wanashindwa kuongea vitu vya maana. Sasa tunawahakikishia Wabunge wa CCM tunawatetea wananchi na wanajua, pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tozo...

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha kanuni iliyovunjwa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** 64

**NAIBU SPIKA:** Wapi? 64 ngapi iliyovunjwa?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio nakuja huko, 64 (1)(a) ambayo inasema Mbunge anayezungumza hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge anayezungumza Mheshimiwa Agnes pamoja na kuzungumza kwa hisia kali na kulia lakini amezungumza maneno ambayo kidogo hayana ukweli na yanadhalilisha jina la Waziri Mkuu au cheo cha Waziri Mkuu. Kwa sababu amesema hapa kwamba Mheshimiwa Mpina yale anayoyafanya ametumwa au ameingizwa chaka na Waziri Mkuu. Kwa hiyo tunaomba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Amesema kwamba ametu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha unaongea na mimi na mimi nimeshakusikia.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba ametumwa na Waziri Mkuu yaani yale anayoyafanya ameingizwa chaka na Waziri Mkuu. Kwa hiyo naomba kwa kutumia kanuni hizi kwamba anamuingiza Waziri Mkuu kwenye mambo ambayo hahusiki nayo, naomba afute kauli.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Maftaha ametupa taarifa kwamba Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa anavunja kanuni ya 64 (1) (a) kwamba hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa alikusudia kusema Katibu Mkuu akasema Waziri Mkuu na amerekebisha hapa wakati akiendelea na mchango wake. Kwa hiyo Mheshimiwa Maftaha alirekebisha Mheshimiwa Mathew Marwa kwamba alikusudia kusema Katibu Mkuu na si Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru narudia tena ni kweli nakushukuru sana kwa sababu nilikusudia kusema Katibu Mkuu na si Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kwa mfano bei za nyavu zile nyavu zinazohitajika kuvuliwa dagaa au samaki zilikuwa kati ya Sh.16,000/= lakini sasa hivi zimefika Sh.45,000/=. Pia kuna maboya ambayo kwa *bundle* ilikuwa ni Sh.30,000/= lakini sasa ni Sh.130,000/=. Kwa hiyo inaonesha ni jinsi gani haya mambo sasa yanavyokuwa ni magumu kwa hawa wavuvi. Wanachomewa vitu vyao, lakini pia bado wanapewa, wanawekewa tozo nyingi zisizokuwa na sababu au na maana. Pia kuna gharama nyingine ambazo kwa kweli zinakuwa ngumu sana kwa wavuvi na hasa wale wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kama hii leseni kweli aliitoa yeye kwa huyu mfanyabiashara ambaye ni mmoja tu anayetoa na kuuza

nyavu hizi; yule Mhindi ambaye yuko Arusha, Mheshimiwa Waziri akaongee naye sasa arekebishe hizi bei kwa sababu hizi bei zinawaumiza hawa wananchi. Kwa hiyo itabidi waendelee angalau kutumia zile, watatumia hata vile vyandarua ambavyo wanapewa wajawazito na watoto wadogo kwa sababu inakuwa ni ngumu sasa kuzinunua ni bei ghali. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hili suala aliangalie ili kusudi hawa wananchi waweze ku-*afford* kununua hizi nyavu kwa ajili ya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni mtoto wa mkulima na ni mchapakazi. Mheshimiwa Waziri hili suala la uvuvi na hasa hawa wanaotoza ushuru kwenye magari au wanaotoza ushuru hawa samaki hata yeye mwenyewe anaweza tu akaliangalia hili suala, kwa sababu kwa mfano kuna vibambala. Mheshimiwa Waziri vibambala wale huwa ni samaki wakubwa ambao ni wale Sangara wakubwa kidogo huwa wanataka kuwa kama *reject,* samaki ambao si *fresh* sana lakini ni samaki ambao hawaingii kiwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wale wananchi wanatengeneza vibambala, si samaki wadogo. Sasa Mheshimiwa Waziri kama hata hawa samaki vibambala wanakamatwa na wanatozwa ushuru anategemea nini , kwamba sasa tutakula nini. Au wananchi hawa wafanyabiashara, maana hivyo vibambala wanaouza wengi wao ni wale wamama wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri afuatilie haya masuala kwa ukaribu kama nilivyoshauri, kwamba iundwe kamati maalum toka Bungeni ili iende ikasimamie na kushughulikia haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi kuna gari ilikamatwa la kuku. Kuku wana ushuru, hapo Singida. Kuku wamekatiwa ushuru, kutoka tu kituo kimoja kwenda kituo kingine wanataka ushuru mwingine, kutoka kituo kimoja tena kwenda kingine wanataka ushuru mwingine. Mheshimiwa Waziri hivi kweli hata kama ndiyo *operation* hii ni *operation*

chukua pesa au *operation* tokomeza? Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili suala aliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lile la hawa hawa wafanyabiashara wenye mitumbwi. Kwenye mtumbwi anakuwepo *boss* na wafanyakazi wake. Kwa mfano anakuwepo *boss* mwenye mitumbwi na wafanyakazi wanaopanda mle kwenye boti wanaokwenda kuvua wanakuwa watano hadi kumi. Sasa kila mmoja anatakiwa awe na leseni, *boss* awe na leseni, wale 10 ambao pia ni wavuvi wake wanatakiwa kila mmoja awe na leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Mheshimiwa Waziri katika mazingira haya inakuwaje? Ni kwamba sasa hata kama, mimi siamini kama Mheshimiwa Rais kweli atakubaliana na hili suala kwamba kila mwananchi, hata yule ambaye anaajiriwa aende akakatiwe leseni. Hiyo leseni yeye anaifanyia kazi gani wakati *boss* wake ana leseni? Au siku hizi labda kuna leseni za vibarua ili uajiriwe lazima uwe na leseni ndipo uajiriwe. Hata kazi za kuvua samaki, hata kazi za kuuza dagaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ndivyo basi tunatakiwa hata sisi tuwe na leseni. Mheshimiwa Spika anatakiwa awe na leseni, wewe Naibu unatakiwa uwe na leseni, sisi Wabunge tunatakiwa tuwe tuna leseni ili kusudi ndipo tuingie bungeni. Kwahiyo mimi niiombe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Catherine Ruge atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama Taifa tuna-*set trend* ya kuwa, sekta hii ya Mifugo na Uvuvi haijaliwi na Serikali ya CCM. Kwa nini nasema hivi; tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani hakuna hata asilimia moja ya Bajeti ya Maendeleo iliyoweza kupelekwa kwenye sekta hii. Sekta ya uvuvi pekee inatoa ajira kwa Watanzania milioni tano, hii ni sawa na asilimia 10 ya wananchi wote wa Tanzania. Pia watu milioni nne wanajishughulisha moja kwa moja na shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 7.8 ya sekta ya mifugo na uvuvi inachangia Pato la Taifa. Asilimia 5.9 ikiwa inatoka kwenye sekta ya mifugo na asilimia 1.9 ikiwa inatoka kwenye sekta ya uvuvi. Takwimu hizi zinatoka kwenye *quarterly bulletin* za *BOT 2017*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sekta hii ya mifugo na uvuvi inachangia zaidi ya sekta ya madini kwenye Pato la Taifa, ambapo sekta ya madini inachangia asilimia 4.8 tu; lakini nasikitika kwamba sekta hii imepuuzwa na imeshindwa kabisa kupewa kipaumbele na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *take it from me*, tukiamua kuwekeza kwenye sekta hii ya mifugo na uvuvi na tukaweza kufikia asilimia 10 tu kuchangia kwenye Pato la Taifa nawaambia nchi hii itakimbia. *Solution* hapa ni ku-*double* tu uzalishaji na kuangalia vipaumbele vyetu ni vipi. Je, *return* ya *investment* ya ku-*invest* kwenye ndege ni kubwa kuliko *return* ya *investment* ya kuwekeza kwenye sekta ambayo asilimia 50 ya kaya inategemea sekta ya mifugo na uvuvi? Kwa hiyo kupanga ni kuchagua, tuamue tunachagua wanyonge ambao ni zaidi ya asilimia 90 ya Taifa hili au tunachagua asilimia tano ya watu wachache ambao wana uwezo wa kupanda ndege? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna ng'ombe zaidi ya milioni 28 lakini ukiangalia Botswana na Ethiopia wanafanya vizuri kuliko sisi. Hebu tukae tujiulize shida ni nini? Maldives,

Mauritius uchumi wao unaendeshwa kwa uvuvi, sisi tuna tatizo gani wakati samaki wao wanakuja kwenye maji yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii kwa mwaka mmoja tu imeweza kukusanya maduhuli ya bilioni 26.9; naomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze ni kwa nini sekta hii imeshindwa kupata pesa za maendeleo hata asilimia 10 basi wakati imeweza kukusanya kwa mwaka mmoja tu *75 percent* ya malengo ya Wizara? Kwa kweli inasikitisha sana; yaani inaonesha tuna chuki, Serikali hii ina chuki kwa wafugaji, ina chuki kwa wavuvi. Hebu tuache hiyo chuki ili tuweze kuwainua wafugaji na wavuvi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia viwanda vya ndani vinavyotokana na sekta ya mifugo na uvuvi. Ningependa nianze na kiwanda cha maziwa. Viwanda vyetu vya ndani vina uwezo wa kutengeneza lita milioni 276.6 kwa mwaka, lakini sasa hivi vina uwezo wa kutengeneza lita milioni 56.3 ambayo ni sawa na asilimia 20 tu ya *operating capacity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo viwanda vyetu vya maziwa vina-*operate under capacity* kwa asilimia 80. Vile vile kinachoshangaza bado wafanyabiashara wa nchi hii wa maziwa na bidhaa nyingine kama *cheese, butter* wanaagiza bidhaa kutoka nje. Naomba Mheshimiwa Waziri akija atuambie, ni kwa nini viwanda vyetu vya ndani vya maziwa vina-*operate under capacity for eighty percent (80%) yet* tunaagiza bidhaa za maziwa kutoka nje na tunapoteza kama Taifa *almost* bilioni mia moja ishirini kwa kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya nyama vina uwezo wa kusindika nyama kwa tani 626,922 kwa mwaka, lakini maajabu sasa hivi viwanda vyetu vya nyama vya nchi hii vinatengeneza au vinasindika nyama kwa tani elfu themanini na moja, elfu ishirini na mbili sawa na asilimia 13. Tuna-*operate under capacity* kwa asilimia 87 na bado tunaagiza nyama kutoka nje kila mwaka. Kutokana na

taarifa za Wizara 2016/2017 tumeagiza nyama kutoka nje kwa kutumia dola milioni saba na bado tunasema Tanzania ya Viwanda; hivi kweli tuna nia ya dhati ya kuwekeza kwenye viwanda vyetu vya ndani au viwanda tunavyovizungumzia ni viwanda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye viwanda vya samaki. Nchi yetu ina uwezo wa ku-*process* tani 700,000 kwa mwaka, lakini sasa hivi *capacity* ni tani 350,000 tuna-*operate* kwa asilimia 50 tu na asilimia 50 bado tunaagiza kutoka nje. Ningependa kupata majibu yanayoridhisha kutokana na *production capacity* ya viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hii hotuba ya Wizara, hotuba haiko *solution oriented,* haitoi *solution* kwa matatizo yetu. Ukisoma maneno mengi tunafanya tathmini, tumewatuma wataalam, tutajitahidi, tuta-*make sure*, tutafanya nini. Ukiangalia ukurasa wa 38, 39 na 40 kuonesha jinsi yeye na wataalam wake Mheshimiwa Waziri ambavyo hamko makini unasema kuhusu *NARCO* na *NICO* kwamba, naomba nianze kusoma ukurasa wa thelathini na tisa (39):-

*"NARCO haikupata gawio lolote kwa kipindi cha miaka 10 na kwa kuwa hakuna maendeleo yoyote yanayofanyika kwa mujibu wa mkataba wa mipango na biashara na hivyo kutofikia malengo na matarajio ya Serikali, hivyo ili kukamilisha taarifa ya uchambuzi wa mkataba na kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi Msajili wa Hazina anaelekezwa kufanya ukaguzi maalum (Special Financial Audit) katika kampuni ya nyama iliyopo Dodoma".*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nikusaidie Mheshimiwa Waziri, Msajili kazi yake siyo kufanya *audit*. *Audit* inafanywa na *Control and Auditor General* ndiye mwenye *mandate* ya kufanya ukaguzi kwenye Taifa hili, Msajili kazi yake ni kuangalia mali, kwa hiyo aende aka-*review* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia suala la tozo mbalimbali na manyanyaso yanayofanywa kwa wafugaji. Mimi natoka Mkoa wa Mara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo imeshagonga, ahsante sana. Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Hadija Hassan Aboud atafuatia.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema aliyonipatia, Muumbaji wa Mbingu na Nchi na vyote vilivyomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kumteua Mfugaji Mheshimiwa Mpina kuwa Waziri wa Wizara hii na kwa kumteua Mheshimiwa Naibu wake ambaye pia ni Mvuvi. Amewateua kwa makusudi maalum akijua kwamba wanajua changamoto za wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwa hiyo wavuvi na wafugaji wana matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Waziri aliyepo na Naibu wake kwa sababu wanaijua sekta hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa haraka sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri na jinsi sekta ya mifugo ilivyochangia Pato la Taifa na nimefadhaika na kuhuzunika nilivyosoma taarifa hii jinsi sekta ya mifugo ambayo imetufanya kuwa nchi ya tatu Afrika kwa wingi wa mifugo lakini ikachangia kiasi kidogo sana katika Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana hatuko makini, inawezekana hatujajali sana sekta hii ya mifugo na uvuvi, kiasi kwamba tungekuwa *serious* katika sekta hii tungefanya vizuri na sekta ya mifugo ingechangia kama sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri ukusara wa 25 amesema Wizara ilikusanya bilioni 10.5 tu na kutochangia ipasavyo katika pato la Taifa na wakaorodhesha sababu huku, wakasema zaidi ya asilimia 20 ya maziwa yanaagizwa kutoka nje. Wakasema usafirishaji holela wa ngozi ndani na nje ya nchi, uingizaji mkubwa wa bidhaa za ngozi kutoka nje, kuwepo dawa bandia. Naamini tuna watalaam na naamini wataalam wetu kazi yao ni kusimamia sekta waliyoisomea na waliyopewa kuidhibiti. Nilikuwa na matumaini kwamba wasingeruhusu haya yote yakatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata kigugumizi kuona kwamba sekta ya mifugo inachangia kiasi kidogo namna hiyo. Siyo mwaka huu tu, miaka yote ya nyuma sekta ya mifugo inachangia kidogo sana pato la Taifa. Tumepoteza bilioni 263.95 kwa sababu ya kutosimamia/kutodhibiti sekta ya mifugo na hii iko katika ukurasa wa 28 wa hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita vijijini akinamama na vijana wanatembeza maziwa, hawana pa kupeleka kwa sababu hatuna viwanda vya maziwa; viwanda vya maziwa ni vinne tu nchi hii yenye ng'ombe wengi. Havitoshelezi kununua maziwa ya nchi nzima, lakini kama hatuwezi, hatuna viwanda vya kutosheleza tutafute namna ya kusindika haya maziwa yakauzwa nje ya nchi kuliko kutumia *Lactogen* (maziwa ya kopo) kwa watoto wetu, maofisini na hata mahotelini wakati tuna ng'ombe zaidi ya milioni 20, hatufaidiki na ufugaji tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji waliopo hawafaidiki na ufugaji kwa sababu hawana namna ya kuuza ng'ombe, hawana namna ya kusafirisha ng'ombe nje ya nchi na hata utaratibu wa dawa za mifugo haueleweki. Wafugaji wananunua hawajui kwamba je, hii ni dawa halisi au dawa hii siyo dawa halisi, mradi kaikuta dukani kama ina jina bandia hajui kwa sababu hata Maafisa Ugani tulionao hawatoshelezi. Hatuna Maafisa Ugani wanaotosheleza mahitaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafirishaji wa ngozi, hatuna viwanda vya ngozi ndiyo maana tunanunua viatu kutoka China na Kenya, nje ya nchi hatuna viwanda vya ngozi. Viwanda vya ngozi hatuna, viwanda vya maziwa vinne tu, viwanda vya nyama sijui ni vingapi hata ile cha Shinyanga nadhani imeshasimama, Tanganyika *Packers* ndiyo tulishasahau; kuna nini katika kuanzisha viwanda vya mifugo hapa nchini?(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa/ nashindwa kujua tatizo lipo wapi. Mwaka huu au mwaka wa fedha unaoisha Wizara ya Mifugo walipiga chapa ng'ombe wakapata bilioni 14; kazi ndogo kweli lakini walipata bilioni 14. Hizi bilioni 14 hawajarudisha kwa wafugaji, hawajachimba malambo, wafugaji wanahangaika kipindi cha kiangazi, lakini kwa chapa tu wamepata bilioni 14. Wafugaji hawana malambo wakati wa kiangazi wanahama huku na kule, Wizara iwasaidie wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo chetu cha *LITI* kipo Mpwapwa, kile chuo kilishasahaulika siku nyingi, mabweni yamechakaa, hakuna vifaa vya maabara, mabweni yamechakaa, madarasa yamechakaa, bajeti ni finyu lakini wanafunzi Tanzania nzima wanakwenda pale kujifunza. Nimwombe Mheshimiwa Waziri akikumbuke Chuo cha *LITI. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja tena, wavuvi wameonewa sana katika nchi hii. Nyavu inchi nne na inchi tano ni haramu, timba na kokoro ni haramu, nyavu inchi sita na saba kama ina macho 78 ni haramu, lakini kama ina macho 26 ni halali. Wavuvi wamechomewa nyavu zao waliokopa wengine wamekufa; wamekufa kwa sababu wanatozwa faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unashikwa na samaki, samaki hao wakati wavuvi wanakwenda ziwani/baharini, Afisa Uvuvi amekagua nyavu lakini wanapotoka kuvua samaki wanakamatwa, nyavu zinachomwa na faini

anatozwa milioni 25 au milioni 50 alipe ndani ya masaa 24. hivi ni nani nayeweza kuwa na milioni 50 kwa siku, akiweka pesa yake tayari tu kwa ajili ya kulipa faini kwa sababu ya nyavu ambazo Afisa Uvuvi amezikagua na Mkurugenzi wa Uvuvi alipitisha lakini bado nyavu zikachomwa. Watu wamekufa; Kanda ya Ziwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa watu wamekufa, Rukwa watu wamekufa kwa mambo ambayo Serikali ingeweza ikakaa na wavuvi na wakaelewana na wavuvi wakapata elimu hiyo na wasirudie makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako waliochomewa kimakosa, hawa waliowachomea kimakosa wanawafanyaje? Nyumba zao zimeuzwa walikopa benki, wanawafanyaje? Tunaambiwa nyama ina *cholesterol* tule samaki, Dodoma sasa hivi unaweza kutafuta samaki mabucha 20 usipate samaki kwa sababu ya matatizo yaliyopo kwenye maziwa na bahari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mwanza kuna mtu mmoja tu anaitwa Naipich ndiye ameruhusiwa kutengeneza nyavu, hivi yeye peke yake anaweza kutengeneza nyavu za Tanzania nzima? Hivi dagaa anavuliwa kwenye nyavu ya aina gani, kule Ziwa Viktoria kuna samaki wanaitwa Furu, Furu hakui hata ukimfuga miaka 20 yupo vilevile anavuliwa kwenye nyavu za aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwafanye wavuvi wakajiona kwamba wao sio Watanzania, tusiwafanye wavuvi wakatuchuki... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Ranchi zetu pia hazijatumika vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Stanslaus Mabula kama muda utaruhusu atachangia Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa mchana huu kupata nafasi kuzungumza kidogo juu ya habari ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwanza kuzungumza juu ya habari ya mifugo ambayo Mwanza peke yake tuna kiwanda cha *Tanneries.* Moja ya viwanda vya mazao ya mifugo ambavyo kwa sasa havifanyi kazi na vipo ni pamoja na Kiwanda cha Nyama Shinyanga, Mwanza *Tanneries* na Kiwanda cha Maziwa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikuzungumza habari ya Mwanza *Tanneries* na nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wangu wa Mwanza Comrade John Mongela kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha kiwanda hiki kinarudi mikononi mwa Serikali. Miaka mingi kiwanda hiki watu wamekuwa wanapokezana tu hati na kuchukua fedha kwenye mabenki bila utaratibu wowote ili hali kiwanda kikiwa ni mali halali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Mifugo kwa sababu yupo hapa wachukue jitihada na juhudi za haraka kuhakikisha viwanda hivi kwa kuwa vimerudi Serikalini vinapata wadau na vianze kufanya kazi haraka kwa sababu ndiyo malengo ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kuhakikisha viwanda vinafanya kazi kwa maana ya Serikali ya viwanda na ajira zinapatikana kwa wingi. Pasi kufanya hivyo tutakuwa bado hatutimizi malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015 - 2020 kuwasaidia Watanzania wengi na vijana kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye oparesheni Sangara. Operesheni Sangara, nitajikita hapo zaidi kwa sababu Sangara anapatikana katika Ziwa Viktoria peke yake. Ni ukweli usiopingika hakuna hata mtu mmoja

miongoni mwetu anayepingana na zoezi zima la uvuvi haramu. Hata hivyo, nataka tu nijiulize mambo machache; tunapozungumzia uvuvi haramu leo lazima kuna watu ambao wanajulikana na shughuli yao kubwa ni uvuvi haramu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka tu nijue na Wizara inisaidie kujua sana. Sangara hawa tunaowazungumza leo miaka ya nyuma ukija Dodoma hapa kwa kina Mzee Lubeleje walikuwa wanaletewa mapanki na vichwa. Leo Sangara huyu analiwa karibu nchi nzima akiwa nyama kama vile alivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kujua leo tunapozungumza uvuvi haramu na zana haramu tunazozizungumza ni zipi? Tunazungumzia kokoro, timba, baruti, sumu au nyavu za inchi nne, sita na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri kuna vitu viwili hapa, kuna wizara na kila wizara inapokwenda kwenye operesheni aidha inapotoka liko kundi lingine la uvuvi wa operesheni kutoka kwenye Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wamenyanyasika sana, wako watu wanatumia jina la operesheni Mpina kwa sababu tu wakisikia Mpina ameingia wanatetemeka na wanatumia nafasi hii kuwaumiza sana wavuvi hawa kupitia jina lako. Natambua kazi inayofanywa na Wizara lakini yapo maeneo inawezekana wameyaacha wazi sana, wavuvi hawa wananyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano, nyavu ya macho 26, hii siyo haramu imeruhusiwa lakini wataalam wanajua na hata wao ukiwauliza nyavu hii tafsiri yake inavua kwenye maji madogo. Sasa kama inavua kwenye maji ya kina kifupi, nyavu hii ya macho ya macho 26 kwa nini isiende kutetekeza hicho kizazi tunachokitegemea, ombi langu turudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri alituma timu ya utafiti kutoka *TAFIRI* ikafanya kazi kubwa sana na wavuvi hawa. Chama cha Wavuvi wamezunguka takribani siku 14, wamekaa ziwani, wameangalia madhara ya nyavu yenye matundu 78 na matundu 52 na kujua tatizo lipo wapi, wameleta ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akiifanyia kazi vizuri ripoti hii itamsaidia na nyavu hizi zenye matundu 78 wanazoziita haramu na hapa mimi huwa najiuliza nyavu hii ina matundu 78, ukiipunguza mara mbili ukatoa moja ukatoa mbili inabaki 26 inakuwa siyo haramu, haramu haiwezi kuwa halali hata ukiigeuza vipi. Tuweke utaratibu mzuri ambao Wizara mnafanya na leo najikita sana kwenye kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza tunayoiona leo nataka niwaambie haijajengwa na dhahabu na kitu kingine chochote, imejengwa na wavuvi hawa. Ukichukua ajira, ajira ya wavuvi wanaotega, wavuvi wamiliki wenye mitumbwi, ukachukua na ajira zilizopo kwenye viwanda, hawa wategaji na wavuvi wa kawaida ni wengi kuliko ajira za kwenye viwanda. Kwa hiyo, hii ni sehemu nyingine ya kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri tusimame sana, gharama za uvuvi zimepelekea wachuuzi wa bidhaa za uvuvi zimekwenda juu. Leo imeongelewa hapa boya moja la Sh.200 sasa hivi linauzwa Sh.400, lakini ukizungumza kamba iliyokuwa inauzwa laki moja na nusu, leo ipo mpaka laki mbili na themanini. Ni kwa sababu watu wajanja wachache wanatumia mwanya huo wa operesheni kujinufaisha wao na kuumiza wavuvi. Lawama zote zinazopigwa leo zinarudi kwenye Serikali ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nataka niombe Mheshimiwa Waziri ashughulike na watu ambao hawataki kututendea mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa unaonesha kabisa kwamba ziko aina ya nyavu hazina

madhara kama zitatumika kuanzia kwenye maji ya kina kirefu na maeneo mengine kwa sababu nyavu hizo zinaonekana zinawasaidia watu hawa. Ukirudi leo ukizungumzia masuala ya faini ambayo watu wengi kweli wamepigwa faini na nimekuwa najiuliza, akitoka Mheshimiwa Waziri, kinaenda chombo kingine kinakwenda kufanya operesheni ya Wilaya na hiki ndicho kinachokwenda na ubabe wa hali ya juu, haujawahi kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitoe mfano, mtu ameenda kwenye kisiwa kimoja Goziba au Ilubwa kule akaenda kuvua amekaa kule siku 16 anasubiri samaki, ameondoka na barafu kutoka kwenye kiwanda Mwanza, amesafiri siku nzima kesho yake amefika ameanza kusubiri kununua samaki. Siku anarudi na samaki wake ameweka barafu, ile barafu kwa pale juu kadri ya siku alivyokaa inaanza kuyeyuka kushuka chini polepole, akikutana na Afisa Uvuvi kule ziwani anamwambia mbona barafu hakuna samaki ameonekana mgongo, anapigwa faini na anapewa masaa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu hawamtakii mema Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya. Naamini kazi hii ikifanywa kwa weledi mzuri na *style* nzuri baada ya miezi michache ijayo Mwanza tunazungumza dhahabu ya pamba itakuwa Ziwa Viktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi unawezaje kumpiga faini mtu ambaye unaona tu mgogo wa samaki umeelea juu, kwa sababu barafu imeyeyuka. Mtu huyu akifika kiwandani hakuna Sangara anayeoza, akifika kwa mwenye kiwanda, mwenye kiwanda atachukua samaki anaowataka. Wale wengine ndiyo maana wanatengeneza kayabo, wanakwenda kuuzwa nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaombe sana Maafisa wa Uvuvi wawe wanaangalia na wao ni wataalam wanajua misingi thabiti ya jambo hili kubwa wanalolifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuchangia, Mji wa Mwanza biashara zake zote, kwa mfano leo dizeli haiuzwi, petroli haiuzwi kwa kiwango hicho kwa sababu wenye mahitaji haya ni hawa hawa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri na jambo lingine kubwa tufanye mkakati kama Wizara na Serikali, tumekuwa tukifanya sana huko na tumesikia asubuhi hapa masuala ya bahari kuu vinatafutwa vifaa vya uvuvi na kadha wa kadha kwenye bahari kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa amejibu vizuri, lakini hebu tujiulize wavuvi wa Kanda ya Ziwa wanapokwenda ziwani kuvua wanatumia fikra zao, wanabuni, wanahisi sehemu fulani leo kunaweza kuwa na samaki wengine wanaweza kuwa wanafuata mwezi, wanahisi au wanaweza kuwa wanabashiri ni wapi samaki watapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yake Waziri, Mheshimiwa Mpina itengeneze sasa utaratibu, ifikirie mpango thabiti wa kuwasaidia wavuvi wa Kanda ya Ziwa ili na wao wawe na vifaa; wanapokwenda kule kwenye maji wawe na uhakika nakwenda na nyavu yenye matundu kadhaa, ninapokwenda kutupa nyavu ndani ya masaa sita nitakuwa nimepata samaki ninaowahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wavuvi hawa anaweza kuwasha boti kutoka kwenye kisiwa akafika mpaka ziwani, akaishia kilo mbili amechoma mafuta ya gharama akarudi akakutana na operesheni hata zile kilo mbili akanyang'anywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, yeye bado kijana ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi hii na akabaki kwenye historia kukumbukwa kwenye Taifa hili... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula muda wako umekwisha lakini nakuongezea dakika moja umalizie. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hivi tunavyokwenda Wizara inaweza ikatusaidia sana kuhakikisha wavuvi na wafugaji katika Taifa hili wanabaki salama, lakini anaanzsiha vitu ambavyo vitakuwa na historia kubwa, vitamjenga ataacha *legacy* kwa wavuvi hawa. Mheshimiwa Waziri asimamie watendaji wasiokuwa waaminifu wanaendelea mpaka kesho. Leo wanasema ukifika kwenda kukamata operesheni kabla hujakamatwa umeona boti, unatupa kwanza bomu na hii imetokea na taarifa ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tusimame kwenye misingi ya kulisaidia Taifa hili. Narudia tena miezi michache ijayo Ziwa Viktoria itakuwa na dhahabu ya pamba kama hatutawanyanyasa watu hawa na kupora mitaji yao kwa namna ambavyo inatupelekea kubaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Nitayataja majina machache ya wachangiaji wetu wa mchana. Mheshimiwa Khadija Hassan Abood, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Costantine Kanyasu, Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Maftah Nachuma na Mheshimiwa Nuru Bafadhil hawa ndio ambao nawataja kwa sasa tutaanza nao, lakini yapo majina zaidi ya wachangajiaji.

Waheshimiwa wabunge mambo mawili ya kikanuni kuhusu staha ndani ya Bunge. Mheshimiwa Mbunge Kanuni zinakutaka unaponyanyuka mahali pako kwenda sehemu nyingine kutoka sehemu yako kwa heshima, watu siku hizi

wanazunguka tu, anasimama anaenda, anatoka huko anarudi. Inabidi aidha ukunje goti ndiyo kanuni zetu zinavyosema ama uiname kwa kichwa ndiyo kanuni zetu zinavyosema. *(Makofi)*

Lingine Waheshimiwa Wabunge ili tusifike mahali tukaanza kurudishana hapa katikati kwenye Siwa watoka pande zote msikatishe hapa, kama upo mbele zunguka viti vya nyuma ili usikatishe hapa katikati, wanaokatisha hapa ni hawa wahudumu wa humu ndani.

Kwa hiyo, nawakumbusha tu hilo Waheshimiwa Wabunge. Kuna Mbunge ananionesha kuhusu mavazi, hilo tutazungumza siku nyingine.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi atafuatia, halafu Mheshimiwa Constantine Kanyasu ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha tunapata uvuvi endelevu na pia tunaliongezea Taifa fedha za kigeni kupitia Sekta hizi za Ufugaji na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ufugaji na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa sababu ni sekta ambayo kwanza pia inatupa usalama wa chakula ndani ya nchi; lakini pili, inaongeza ajira; tatu, inaongeza pato la Taifa, lakini pia

inatupa lishe bora. Ni vyema sasa Serikali ikaona kuna haja ya kuongeza msukumo zaidi katika sekta hizi ili kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Sekta ya ufugaji, wafugaji wanahitaji mipango bora ya malisho na maji, wanatakiwa wapewe elimu juu ya uvunaji wa maji ya mvua ili waweze kujenga mabwawa na malambo kwa ajili ya kulishia mifugo yao. Natumai wafugaji wakipewa elimu hii wataweza kuchukua baadhi ya mifugo na kuwekeza katika sekta hii ya upatikanaji wa maji na malisho; pia kunatakiwa wafugaji na wavuvi waendelee kupewa elimu ya juu ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelekea kwenye bidhaa za ngozi, kuna bidhaa nyingi za ngozi ambazo hazitumiki, na badala yake zinakaa zinapotea. Nawashauri Serikali, kwa vile viwanda ambavyo sasa hivi vinachakata ngozi, ile ngozi ya ziada ambayo haitumiki ni bora kukatengenezwa mazingira rahisi ili ngozi zile zikauzwa badala ya kubaki na kuwa hazifai au kuharibika au kuoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Maziwa; sekta hii ina changamoto nyingi kwa wawekezaji wa viwanda vya maziwa. Changamoto pia inamkuta hata yule mzalishaji mdogo wa maziwa kwa sababu maziwa mengi yanaharibika njiani kutokana na miundombinu ambayo siyo rafiki kwa mkulima wa maziwa na tukizingatia kwamba bidhaa hi ya maziwa haichukui muda kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale wazalishaji wadogo wa maziwa wanapokwenda kupeleka maziwa kiwandani hawana vyombo vya kupooza maziwa hayo ili yachukue muda mrefu yawafikie viwandani na watumiaji wengine. Ni vyema sasa tukahamasisha, au Serikali ikatafuta mpango wa vipoozeo vya maziwa kuwapa hawa wakakopa kwa kupitia mabenki, kwa kupitia vikundi mbalimbali, waweze kupata vipoozeo vya maziwa ili maziwa yao yakae muda mrefu na yamfikie mtumiaji bila kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria za uvuvi, sheria hizi wavuvi wengi hawazifahamu, hizo sera hawazifahamu. Kwa hiyo ni vyema sasa wavuvi wetu wakaelekezwa juu ya sheria, sera na kanuni mbalimbali za uvuvi kwa sababu inaelekea kuna baadhi ya sheria zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza ambazo wavuvi wetu hawazifahamu. Kwa hiyo, naipongeza Wizara kwa kutafsiri hii sheria kwa lugha ya Kiswahili ambayo itakuwa ni lugha nyepesi kwa wavuvi wetu kuweza kuifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachotakiwa baada ya tafsiri hiyo, zishushwe chini sasa kwa wavuvi wenyewe ili wazifahamu na wapewe mafunzo elekezi ya kufahamu sheria hizo na sera za uvuvi. Tukiwafundisha kanuni na sera za uvuvi kutapunguza huo uvuvi haramu tunaoupiga vita. Sisi sote tunajua kwamba uvuvi haramu ni janga la Taifa, linaharibu mazingira, linaharibu mazao yetu ya samaki na mazao mengine ya baharini. Sasa ni vyema wavuvi wetu wakapewa elimu zaidi ya kufahamu sheria, kanuni, vitu gani vinafaa kwa uvuvi na vitu gani havifai, nyavu ziwe na ukubwa gani, elimu hii iendelee kutolewa mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiki Kiwanda cha *Sunflag* ambacho kinazalisha nyavu inaelekea nyavu zake hazina ubora. Kwa sababu wavuvi wakitumia mara moja au mara mbili nyavu zimeshavurugika, zimeshakatika, hivyo tunamtia hasara mvuvi mdogo maskini ambaye amejichuma pesa zake ndogondogo akaweza kununua nyavu. Sasa tuangalie upatikanaji wa nyavu bora na vivulio bora vya samaki ili tusimuongezee mzigo mvuvi wetu mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea samaki, mvuvi amevua kwa bahati mbaya, kuna masikitiko na malalamiko, samaki ambaye hahitajiki kwa wakati ule, samaki ni samaki ndani ya bahari, unapopitisha nyavu anaweza akaingia na mwingine ambaye hahitajiki. Basi jambo lile lisichukuliwe kwamba yule mvuvi kafanya makusudi akalipishwa faini, akachomewa nyavu, akachomewa vyombo. Kwa hiyo hili

suala linatakiwa lichukuliwe kwa umakini wake na kujua katika bahari kuna vitu vingi na vitu hivyo vinaweza vikajichomeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la mipaka ya leseni za uvuvi, wale wavuvi wanatakiwa waelezwe leseni zile wanazokata zinatumia mipaka gani. Kwa sababu bahari haina mipaka, imeanzia Zanzibar, Kilwa, Dar es Salaam, Kimbiji, inazunguka, na mvuvi anataka kutafuta samaki ili asipoteze muda wa kukaa kutwa kucha nzima baharini bila ya samaki, kwa hiyo hizi leseni zinazotoka hebu zitolewe kwa ufafanuzi ili wavuvi waelewe mipaka yao ya kuvua ni ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, kwa sababu wakienda eneo lingine wanatozwa faini wanaambiwa wakate leseni nyingine. Sasa hizi leseni zimegawiwa kwa viwango gani, au akate leseni ya aina gani ili aweze kuvua sehemu yoyote ya Tanzania? Hili linatakiwa lifanyiwe kazi na wavuvi wetu waelezwe ili kuepusha hizo kasoro ndogondogo zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kutengeneza huo mfumo wa kuzalisha samaki ambao sasa wavuvi wetu watajua wapi samaki wapo na watavua kwa wingi gani. Kwa hiyo, hili nalipongeza, ni jambo zuri na linatakiwa liwe endelevu kwa wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali na Wizara kwa kutaka kuifufua na kuiboresha *TAFICO. TAFICO* ikifufuliwa na ikiboreshwa ikawekewa miundombinu na mitaji, itaweza kufanya kazi za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zana bora za uvuvi, zana bora za uvuvi kwa wavuvi wetu zinahitajika kwa sababu wataepuka kubahatisha kuvua. Kazi ya uvuvi ni ngumu na inahitaji uvumilivu wa hali ya juu. Wavuvi wanapokwenda baharini ukaona upepo unavuma huna uhakika kama mvuvi atarudi au harudi, atakuwa salama au hawi salama, atapotelea wapi. Tumeshuhudia Tanzania tunapokea wavuvi kutoka Comoro wengi tu ambao wamepotea baharini siku

saba, siku nane na Watanzania wanapotea kuelekea nchi nyingine. Kwa hiyo, hii kazi ni ngumu, siyo kazi rahisi, inataka ujasiri. Kwa hiyo, ni vyema wavuvi wetu sasa tukawaendeleza ili wapate zana bora za uvuvi za kujua wapi samaki wapo, kwa ukubwa gani, kwa wingi gani, kwa kina gani cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu, naomba Serikali imalize hii michakato ya ujenzi wa bandari za uvuvi na ununuzi wa meli ya uvuvi. Kwenye uvuvi wa bahari kuu hakuna haja ya kuwekeza, Mwenyezi Mungu ameshawalea mwenyewe samaki, ameshawakuza sasa hivi kazi yetu sisi wanadamu ni kwenda kuwavua. Kwenye uvuvi wa bahari kuu kuna samaki wengi ambao nchi za duniani wanafaidika na uvuvi huu. Tutaweza kuongeza Pato letu la Taifa na tutaweza kutengeneza miundombinu mingi kupitia uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikiendelea kwenye uvuvi huu wa bahari kuu, kuna mgao wa fedha, mgao huu unahusu Serikali mbili. Naomba usicheleweshwe, ugawiwe kwa maeneo yote Bara na Zanzibar, ili Sekta ya Uvuvi iweze kusonga mbele badala ya kubakia tu hazipelekwi. Kwa sababu kuna miundombinu mingi ya kupanua Sekta ya Uvuvi bado hatujafikia na tunahitaji mapato ya kutosha ili tuwekeze kwenye Sekta hii ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara, lakini pia nakipongeza Chuo kile cha Uvuvi cha Kigoma. Bila kutumia senti hata moja ya Serikali wameweza kufufua chuo kile kwa fedha zao wenyewe, wamejibinya, wameweza kufufua kile chuo na kuongeza wanafunzi wa kusomea mambo ya uvuvi. Hapa nataka nishauri Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija, muda wako umekwisha.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae kama atakuwa hajafika basi Mheshimiwa Nuru Bafadhili ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara muhimu kabisa kwetu sisi tunaotoka kandokando ya ziwa, lakini pia maeneo ambayo kwa sasa kilio cha wananchi ni kwa kweli unyang'anyi mkubwa unaoendelea kufanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kusikitika kidogo, kuna bahati mbaya kwamba tunazungumza hapa kwa nguvu kubwa sana tukiwa tunazungumza maoni ambayo tunaamini waliotutuma ndiyo tunaleta, lakini majibu mepesi yanayokuja ni kwamba tumekamata Wabunge, tumekamata Madiwani ndiyo maana wanalalamika. Kama ziko kumbukumbu za Mbunge aliyewahi kukamatwa anavua samaki au na zana haramu, tungeomba sana leo wakati Waziri anahitimisha aseme ni Mbunge gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hili linatia woga watu kuchangia kwa kuogopa kutuhumiwa na wengine wanaamini kila anayesema anasema kwa sababu ana maslahi. Kauli hii ilienda mbali zaidi, Mheshimiwa Waziri alikuwa na kikao na viongozi 260 akiandaa Operesheni yake ya Sangara awamu ya tatu. Kauli walizozitoa viongozi aliokuwa nao ni kwamba wanasiasa wanapotosha zoezi hili kwa sababu wana maslahi binafsi na kwa maana nyepesi wanasiasa ni sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuliweka vizuri hili, kwanza ni vizuri sana akaweka kumbukumbu hizi sawa; anawazungumzia wanasiasa wapi wanaopotosha? Kwa sababu tunayoyazungumza sisi tunayazungumza kwa sababu tunayafahamu. Hata hivyo, ni vizuri sana pia viongozi wenzetu

huko waliko kwa kuwa tunazungumza kuwawakilisha wananchi, wakafahamu kwamba sisi tunapokuja hapa tunakuja tumetumwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa kuchangia; kwanza nianze na suala la operesheni ambayo inaendelea hivi sasa. Tulizungumza hapa na tukaomba mwongozo na tatizo kubwa halikuwa kupinga operesheni ya wavuvi haramu. Naomba niweke kumbukumbu vizuri; naunga mkono operesheni ya kupambana na uvuvi haramu, naunga mkono operesheni ya kupambana na zana haramu, naunga mkono dhamira ya Serikali ya kuongeza kipato kinachotokana na uvuvi na mifugo, yote ninaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, unapotaka kufanya operesheni lazima uiwekee mipaa, lakini pawe na ile *sense of humanity,* kwamba ninaokwenda ku-*deal* nao ni binadamu. Tunao wavuvi kule ziwani, niliuliza swali na halijawahi kujibiwa mpaka leo. Unapotumia nyavu ziwani ya inchi sita iliyoruhusiwa na Serikali ambayo siyo zana haramu, ukaenda nayo ziwani ikiwa *single* ina uwezo wa kukamata samaki wanaozidi sentimita 50 na wanaopungua sentimita 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na watu wake wote wanakiri kwamba nyavu hiyo kwa kawaida *ratio* inaweza ikawa mpaka *ten percent* ya nyavu ambazo ziko *under size.* Ni kwa nini operesheni ya Mheshimiwa Waziri inaendelea kukamata watu hata wenye samaki wawili? Kwa nini inaendelea kupiga watu faini ya mamilioni ya shilingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye sheria, sheria zote za mambo ya uvuvi ambazo zipo kwenye Sheria ya Mwaka 2003 na *regulations* zake, zinazungumzia faini na ziko *very clear.* Hata hivyo, kwa sababu operesheni ililenga kukusanya pesa, ililenga kwenda kuhakikisha kwamba watu wanatoka barabarani, mtu anapigwa faini mpaka ya milioni 50 kwa kosa la kukutwa na samaki 10, 15 kwenye mtumbwi, na operesheni hii inalenga wavuvi wakubwa peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza wanakwenda kwenye mwalo wanaangalia mvuvi mwenye mitumbwi zaidi ya 30, wakifika wanamkamata, wakimkamata wanam-*detain* kwenye gari tangu asubuhi mpaka jioni yuko chini ya ulinzi. Wanamwambia faini ni milioni 20 wanatembea naye, akikosa wanamweka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye wanasema wewe bila kuleta milioni 20 tutakufungulia kesi ya uhujumu. Watu wanakwenda kuuza nyumba, wanakwenda kuuza ng'ombe. Kwa nini tunafanya hivi kama tuna nia njema na operesheni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliposema maneno haya, majibu yaliyotoka mepesi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri anasema ni kwamba nikiondoa hiyo *exemption* ya *ten percent* zoezi zima la operesheni halina maana. Maana yake ni nini kama wataalam wake wamekiri kuna kasoro na lazima iwepo, kwa nini anasema akiondoa haina maana; maana yake ni kwamba lengo la Mheshimiwa Waziri ni kufilisi watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua nyavu ya dagaa ukaenda nayo ziwani leo, ukizungusha ile nyavu ya dagaa utapata sangara, utapata furu na sangara utakaowapata ni wadogo wadogo na watakufa kabla hujawatoa ziwani. Nataka kujua Mheshimiwa Waziri, anawapeleka wapi hao samaki? Kwa sababu hao samaki atakapovua lazima waje na kokoro na dagaa, unawapeleka wapi? Wavuvi wote wa dagaa sasa hivi wanaogopa kuvua samaki, tulikuwa tunanunua kisado cha dagaa Sh.2,500, sasa kimepanda mpaka Sh.15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niikumbushe Serikali, pamoja na lengo la kutafuta pesa kwenye samaki, samaki ni chakula kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa. Yaani kwa sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa, samaki ni chakula namba moja. Wewe unapofikiria mapato ya nje, fikiria kwanza watu ambao wanafaidika na samaki hao. Kinachoendelea katika zoezi hili ni uonezi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la nyavu; hivi tunavyozungumza, nyavu hakuna madukani. Nyavu za dagaa *license* amepewa mtu mmoja, yuko Arusha, alikuwa anatengeneza neti za mbu, anatengeneza nyavu za dagaa, matokeo yake nyavu ikiingia ziwani miezi miwili imepasuka. Wavuvi wameacha kununua nyavu za Tanzania wananunua nyavu za magendo kutoka Kenya na Uganda, Serikali inakula hasara. Waziri amezuia nyavu zisiingie Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyavu za sangara; nilizungumza hapa wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, wafanyabiashara wamelipia nyavu tangu mwezi wa kwanza ziko bandarini, wanaomba kibali nyavu ziingie Tanzania. Wengine wamelipia na ushuru miezi miwili, Waziri hasemi kwa nini anazuia, hasemi ataruhusu lini, watu wanaenda kupigwa *storage.* Hebu tuwaambie Watanzania tunataka nini hapa kwenye nyavu, nyavu zile Mheshimiwa Waziri anazozitaka ziko bandarini hataki ziingie kwenye soko. Tunataka watu wavulie nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nafahamu na elimu yangu ndogo ya uchumi inaniambia ukitengeneza mazingira ya kupunguza *supply* kwenye soko ukasababisha *demand* ambayo haitarajiwi, bei ya nyavu itapanda na matokeo yake watu hawatanunua; ndiyo elimu yangu ya uchumi inavyoniambia. Sasa matokeo yake ni kwamba nyavu imepanda kutoka Sh.16,000 mpaka Sh.45,000 *piece* moja. Hiyo ambayo imepanda vifaa vyake vimepanda mara nne zaidi kwa sababu wanaoleta wote mali zao zimezuiliwa mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka Mheshimiwa Waziri aniambie, anazuia kwa maslahi ya nani? Sielewi. Kwa sababu kama anataka ku-*control,* apeleke mtu akakague kontena, kama anataka kuzuia atangazie watu wasilete nyavu. Watu wamelipa kodi wanamwomba kibali hataki, wanamwambia hiki, hataki, anataka nini, aseme. Kwa sababu ni rahisi sana kuwatangazia Watanzania wasiingize nyavu kutoka nje

tunategemea viwanda vya ndani, watu hawataleta. Sasa hasemi chochote, amekaa kimya, watu wanakula hasara, nyavu ziwani hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hapa, nyavu sasa watu wanaanza kuendea nje ya nchi kwa sababu wanaona kuna urasimu; tunakula hasara. Kwa nini hili linatokea; tunamlinda nani? Kwa sababu lengo ni kulinda viwanda vya ndani, wakati huu viwanda vya ndani havina uwezo lazima uvuvi uendelee. Hiki ninachokizungumza ninavyo vielelezo; Mheshimiwa Waziri nimemwomba zaidi ya mara tatu hataki kusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, tulifanya semina akasema amezuia mitungi ya gesi na yenyewe ni uvuvi haramu. Kwenye uvuvi wa bahari, tulipozuia *trolling* tuliruhusu wavuvi waende zaidi ya mita 50 *deep, deep sea* ya mita 50 kwa pumzi ya kawaida lazima utumie mitungi ya gesi. Hii inatusaidia sana kwa sababu uvuvi pekee siyo majongoo bahari. Kama lengo ni ku-*control* majongoo bahari, tungeweka mfumo wa kuweka *season fishing* kwenye maeneo unasema kuanzia sehemu hii mpaka sehemu hii tutavua kwa miezi mitatu, kuanzia hapa tutavua kwa miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapofanya *burning totally* wale wanaotumia mitungi hawaendi tu kwenye majongoo bahari, kuna uvuvi ambao ni *selective* ndani bahari. Hii mitungi watu wanaitumia kuzamia chini, maana yake ni nini sasa, tunajielekeza kwenye kufikiri kwa jambo moja tu kwamba wavuvi wote wa mitungi wanakwenda kwenye majongoo bahari. Pia kuzuia kabisa wala sio *economically*, sio kitu ambacho nafkiri ni sawa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu kengele zilishagonga, nimekuongeza dakika hapo, lakini naona bado hujamaliza hoja yako, sasa dakika moja malizia.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza siungi mkono hoja kabisa, lakini namtaka Mheshimiwa Waziri kwa nia njema kabisa atakapokuja hapa aturidhishe na mateso makubwa wanayopata wavuvi wa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi dakika tano, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha dakika tano, watafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Bafadhili.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa dakika tano hizi kwangu ni chache sana lakini nitajitahidi niweze kuwasilisha ujumbe wangu. Uchumi wa Taifa kwa ujumla wake unategemea sana uchumi wa mtu mmoja mmoja na Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo ni Wizara muhimu sana *specifically* kwenye eneo la uvuvi linachangia asilimia 2.2 ya pato la Taifa, lakini sioni kama Taifa tunaweka umuhimu kwenye uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa napitia, kwa mfano nilipitia mwongozo wa maandilizi ya mpango wa bajeti 2018/2019, sioni eneo lolote ambalo mpango huu unagusa eneo la uvuvi, kidogo imenisikitisha sana. Hata hivyo, uvuvi kwa ujumla wake kwa mfano kwenye eneo la Kanda la Ziwa ni siasa, ni maisha na ni kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikiongelea kwa mfano operesheni sangara, Mheshimiwa Kanyasu ameongea vizuri sana kinachofanyika kwenye Kanda ya Ziwa hususani operesheni sangara ni unyanyasaji, ni uonevu, ni dhuluma, inafanyika dhidi ya wavuvi. Matendo wanayofanyiwa si mambo ambayo yanapaswa kuendekezwa wala kuyakubali katika Taifa hili. Watu wanafilisiwa, wanapoteza maisha wanafanyiwa vitendo vya ajabu sana ambavyo vinatia simanzi na huzuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia kwamba hii Sekta ya Uvuvi, kwa mfano, watu takribani milioni nne

wanategemea uvuvi na *implication* yake ni nini hata wale wanaotegemea watu hawa zaidi ya watu milioni tano, milioni kumi wanategemea sekta hii ya Uvuvi. Kwa hiyo, unapovuruga Sekta hii ya Uvuvi wananchi zaidi ya milioni kumi ambao ni zaidi ya asilimia 20 ya wananchi wa Taifa hili wanaathirika na mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye ushauri kwa sababu hatuwezi kuendelea kufanya haya wananchi wanaathirika, leo asubuhi tumeahirisha Bunge hapa na toka nje napigiwa na wavuvi kutoka Ukerewe. Kwa sababu Operesheni Sangara sasa kuna watu ama ni wahuni tu au namna gani wanatumia njia hii kuwabughudhi watu kule. Wameenda kule kwa sababu walichomewa nyavu zao wametafuta rasilimali pesa wakanunua nyavu nyingine zinazotakiwa, wameenda watu tena leo wanataka kuwachomea zile nyavu kwamba siyo halali, sasa maisha gani watu wataishi katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niende tu kwenye ushauri; la kwanza nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini sijaona sehemu yoyote ambayo kuna eneo la mafunzo kwa wavuvi wetu, kwa sababu haiwezekani kwenda kuwaadhibu tu wavuvi hata kama ni mtoto huwezi kwenda kumuadhibu kabla ya kumwonesha ni kitu gani anapaswa afanye. Sasa tunatakiwa tutoe elimu kwa wavuvi wetu, tujue kwamba hawa ni wavuvi na shughuli zao ni uvuvi. Sasa ni uvuvi gani sasa wanatakiwa waufanye, ni wajibu wetu kama Serikali kutoa elimu hii lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuna marekebisho ya sheria namba 22 ya mwaka 2003, kwenye hotuba wameonyesha iko kwenye mchakato, kwenye hatua nzuri, lakini je, sheria hii wakati wa kufanya marekebisho wadau wameshirikishwa kwa kiasi gani. Kwa sababu moja kati ya malalamiko ni kwamba tumekuwa tunatunga sheria na kufanya marekebisho, lakini hatuwahusishi wadau kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo ni kwamba, tunatunga sheria za upande mmoja bila wadau kushiriki na kutoa changamoto na mtazamo wao juu ya yale ambayo tunayatunga. Kwa hiyo, niombe kwamba sheria hii au marekebisho haya yatakapokuwa yanaletwa tujiridhishe kwamba wadau hasa wavuvi wameshirikishwa katika mabadiliko ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ni juu ya nyavu. Tumezuia nyavu hizi walizokuwa wanatumia kwamba ni nyavu haramu, sasa hizi nyavu zinazopaswa kutumika ziko wapi? Kwa sababu wavuvi hawana nyavu hizi, wale ambao walikuwa wanaagiza nyavu hizi wamezuiliwa kuingiza nyavu hizi, sasa nini kitakachotumika na wale waliopewa jukumu ya kutengeneza nyavu hizi walikuwa wanatengeneza vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nyavu zinazotumika sasa hivi kwa mfano za dagaa watu wanatumia ndani ya mwezi mmoja nyavu zile zimeharibika, inabidi wanunue nyavu nyingine, ni gharama kubwa kwa wavuvi wetu hawa ambao kwanza tumewatia umaskini kwa kuwachomea nyavu zao, halafu inabidi watafute rasilimali pesa nyingine kununua nyavu nyingine. Kwa hiyo, kama hatuna uwezo wa kuzalisha nyavu hapa nchini turuhusu nyavu kutoka nje ziweze kuingizwa nchini ili wavuvi waweze kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa Mheshimiwa Waziri niombe, wadau wangu Ukerewe sisi tunavua samaki aina nyingi. Kuna samaki aina ya gogogo kwetu maarufu kama ngere ni samaki maalum na muhimu sana wanavuliwa kwa msimu, watuambie wanavuliwa kwa nyavu *size* gani na wale wanapatikana kwa msimu. Msimu wake ni kuanzia mwezi huu kuendelea mpaka mwezi wa Nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, watafiti wa Mheshimiwa Waziri inawezekana hawajui kwamba samaki hawa wanapatikana kwa msimu, lakini wale wanatakiwa sasa ndio

waanze kuvuliwa. Kwa hiyo, tunaomba sasa watuambie tunavua kwa nyavu *size* gani ili wananchi waweze kupata, lakini...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda umekwisha.

Mheshimiwa Waziri uzuri Wataalam wako wako hapa, mengine nadhani wanaweza kuanza kuyafanyia kazi sasa hivi ili baadaye utakapokuja kutoa majibu yawepo tayari. Mheshimiwa Nuru Bafadhili, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Khatib Kai...

**MHE. MARWA R. CHACHA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ulinitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuata. Ulitajwa lakini ulikuwa hujaingia Bungeni Mheshimiwa.

*(Hapa Mheshimiwa Ryoba Chacha alikuwa akibishana na Naibu Spika)*

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona ukiingia kutoka kule usibishane nami, nimekuona wakati ukiingia pale. Mheshimiwa Nuru Bafadhili.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijachangia chochote nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa kwa siku ya leo. Kwanza napenda kutoa pongezi kwa Serikali kudhibiti uvuvi haramu. Kwa sababu uvuvi haramu sina maana ya nyavu tu, uvuvi haramu ni wale pia wanaotumia mabomu. Vijana wetu wanaathirika kwa kutumia mabomu, kuna wengine wamekuwa ni vipofu, kuna wengine wamekuwa ni viwete hawana miguu, wengine hawana mikono na wengine wanapoteza maisha kutokana na mabomu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mabomu haya yanaharibu matumbawe ambayo ndiyo nyumba za kuzalia samaki. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kudhibiti hali hiyo na tunaiomba Serikali iendelee na hili zoezi kwa sababu tunao vijana na ushahidi upo wapo tayari wamepoteza hali yao ya kuona kutokana na mabomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kuhusu hizi nyavu; kwa kweli wavuvi siyo wanaotengeneza nyavu, wavuvi wananunua. Sasa ilitakiwa wale wanaouza nyavu wazuiliwe kuuza zile nyavu ambazo hazistahili kwa ajili ya kuvulia samaki, badala ya kumwadhibu mvuvi ambaye yeye anakwenda kununua kwa ajili ya kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wana maneno wanasema unapofagia unaanzia kufagia pale miguuni kwako kwenda mbele. Sasa ninachosema sisi Mwenyezi Mungu ametupa bahari, Mungu ametupa maziwa na Mwenyezi Mungu ameweza kutupa mito. Kwa hiyo, tuna samaki wengi sana, sasa kabla hatujanunua samaki kutoka nje kwenye makopo, kwenye *super markets* ni lazima sisi tutumie samaki wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki wetu ni wazuri sana, kwanza unapokula samaki unakuwa una akili, mtu yoyote anayetumia samaki anakuwa na akili nzuri sana. Vilevile samaki ni chakula kizuri hata kama huna chakula chochote cha kula lakini unaweza ku-*survive* kwa kula samaki. Kwa hiyo, tujitahidi kula tuweze kula samaki wetu ambao wanavuliwa hapahapa, tuone fahari kutumia samaki wetu kuliko kununua samaki ambao wanatoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wenzangu nadhani walikwishasema kuhusu leseni hizi ambapo mvuvi anakata leseni, mwenye chombo anakata leseni, msaidizi anakata leseni. Sasa hizo leseni zimekuwa nyingi kabisa kiasi ambacho wanalalamika hawapati faida. Matokeo yake wanapokwenda kwenye bahari kuu kule samaki wanauzwa hukohuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama Tanga sisi tumepakana na Kenya. Kwa hiyo, samaki wanapopatikana pale wanauzwa mvuvi anarudi hivihivi anakwambia sikupata chochote. Kwa hiyo, tunapoteza mapato kwa ajili ya nchi yetu, hivyo, tuhakikishe hizi leseni zinapungua ili kuwapungizia wavuvi adha ya kupata kiasi kidogo katika hela zao wanazozipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna viwanda vya samaki kwenye Mikoa ya Kanda ya Ziwa lakini sisi watu wa Pwani hatuna viwanda vya kuchakata samaki. Sasa Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini Serikali itafanya mpango wa kutujengea viwanda ambavyo tunaweza tukachakata samaki, kwa sababu tuna samaki wengi sana, tuna jodari, changu, kolekole, ngisi, pweza na wengineo. Pia tunajua pweza anawasaidia sana akinamama wazazi wakati wanapokuwa wamejifungua wanapata maziwa na akinababa pia wanasaidiwa na hao pweza, wenyewe wanajua jinsi gani wanavyowasaidia hao pweza. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu ufugaji. Nadhani hapa ufugaji una matatizo kwa watu wanaoishi katika maeneo ya Miji. Kwa mfano, katika Jiji la Tanga watu wanajitahidi wanafuga ng'ombe katika nyumba zao, lakini inakuja amri kutoka Halmashauri ya Jiji kwamba atakayeonekana anafuga ng'ombe ndani ya nyumba yake atachukuliwa hatua. Sasa hiyo inamvunja moyo mtu ambaye anataka kufanya ujasiriamali wa ufugaji. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe inaandaa utaratibu vilevile wale wafugaji wafuge kwa amani badala kwa kunyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mifugo inayotembea tembea barabani sasa mifugo hii hatujui ina wenyewe au haina wenyewe ile ndiyo mifugo ambayo inayotakiwa idhibitiwe ili isiweze kuzunguka barabarani wakati mwingine inagongwa na gari, wakati mwingine inasababisha ajali kwa watu, kwa hiyo mifugo ile inatakiwa iangaliwe. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana muda wako umekwisha, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, atafuatia na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mheshimiwa Mwita Waitara ajiandae.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu siku ya leo kuweza kunifikisha katika Bunge hili Tukufu na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu. Pia niwatakie rehema Waislam wote ambao wamekabiliwa na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni sekta ambayo imekuwa ikibeba Watanzania wengi ambao wamekuwa wakijiajiri wenyewe ambapo Serikali imeshindwa kuwaajiri. Hata hivyo, pamoja na kujiajiri wenyewe Serikali imekuwa ikiwakwamisha kwa visingizio ambavyo wakati mwingine havina msingi wowote. Mwaka 1995 Serikali ilipiga marufuku uvuvi wa kokoro. Mwaka huohuo Serikali ikapitisha sheria ya *ring net* kuvua katika bahari kuu ambayo itakuwa ni kuanzia mita 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mita 50 za *deep sea* ni mita kubwa sana ni tofauti na uvuvi wa kokoro ambao wamekuwa wakivua maji ya kina kidogo. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa Serikali ambayo imepitisha sheria ya kwamba uvuvi wa *ring net* wavue kuanzia mita 50 wamekuwa wakiwazuia wavuvi hawa wa *ring net* kutumia chupa za *oxygen* ambazo zinaweza zikawawezesha kutumia upepo wa *oxygen* ili kuwasaidia katika uvuvi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi wa *ring net* ni uvuvi ambao hauna madhara yoyote. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kwa sababu uvuvi wa *ring net* hauna madhaa yoyote, lakini kupitia Wizara yake imepiga marufuku uvuvi wa *ring net* kwa sababu ambazo hazina msingi, kwa hivyo kama kuna matatizo yoyote au kama kuna tatizo lolote

ambalo wameliona Wizara kwamba uvuvi wa *ring net* kwa kutumia chupa kuna matatizo, basi namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze ni matatizo gani ambayo yanasababishwa na chupa ambazo wanaweza kutumia wavuvi wa *ring net. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mheshimiwa Waziri akiwa hapa Bungeni akijibu swali la Mheshimiwa Maryam Msabaha ambaye alitaka kujua ni kero ngapi za Muungano hadi sasa zimetatuliwa. Mheshimiwa Waziri ambaye wakati huo alikuwa Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira alisema kwamba kati ya kero za Muungano ambazo zimetatuliwa moja ni uvuvi katika ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi karibuni tu wavuvi wangu wapatao 54 wakitokea nchini Kenya kwenye dago walikutana na meli ambayo inafanya *patrol* ya uvuvi haramu na ugaidi baada ya kupatikana wavuvi hao walisimamishwa wakaulizwa maswali na wakajibu na masuala waliyouliziwa ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi ni nani, mnatoka wapi na mnakwenda wapi? Wavuvi hawa walijibu sisi ni Watanzania na ni wavuvi na tunatoka Dagoni Kenya. Hata hivyo, meli ile ambayo inafanya *patrol* ya uvuvi haramu na ugaidi ilitaka kujiridhisha kwamba kweli ninyi ni Watanzania na mnatoka Kenya. Wavuvi wale walitoa *passport* zao wakaonesha, lakini hiyo haikuwanusuru. Kwa masikitiko makubwa sana wavuvi hawa wakiwa maeneo ya Pemba kabisa, lakini waliambiwa watoke kwenye chombo chao na waliingizwa kwenye meli wakapelekwa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana kutoka Pemba na Tanga ni mbali sana, lakini hata hivyo wavuvi hawa waliwaomba kwamba ikiwa tunaomba kwa sababu tuko Pemba na vyombo vya ulinzi ni Muungano tunawaomba basi kama kuna tatizo, kama tumevunja sheria mtukabidhi vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo viko huko kama tumevunja sheria tuchukuliwe hatua. Pamoja na hayo,

lakini walipelekwa Tanga wakiwa wamechoka sana na wakaenda wakadhalilishwa pale, zaidi ya wiki nzima wako Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara kwa kweli alinipa ushirikiano, tulisaidiana na kuhakiksha kwamba wavuvi wale hawabambikiziwi kesi nyingine. Kwa kweli nchi hii kama kuna watu ambao wamekuwa wakionewa ni wafugaji na wavuvi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haji Khatib Kai muda wako umekwisha, lakini naona ulikuwa unaeleza kesi mahususi hapo, kama kesi hiyo haijamalizwa, basi Mheshimiwa Mtolea uwe unakua mtulivu. Kama hiyo kesi haijafanyiwa kazi nadhani tukishamaliza Bunge hapa unaweza kuwaona Mawaziri ili waweze kulifanyia kazi. Kwa sababu kama watu bado wako Tanga ni jambo la kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Muftaha Nachuma ajiandae wote ni dakika tano tano.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, ni moja ya Wizara hewa. Katika Wizara hewa ambazo zimewahi kuundwa ni hii na nina sababu. Nenda ukurasa wa nane wa hotuba walitengewa *development* bilioni nne, ukisoma pale anasema hadi kufika mwezi Aprili 2018 hakuna fedha iliyokuwa imetolewa, yaani maana yake sifuri, walipewa sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajua mimi ni Mwalimu, ukisahihisha ukamwekea mtoto sifuri, maana yake hewa, hakuna kitu. Sasa najiuliza kwa nini waliamua kutoa hii Wizara iliyokuwa pamoja na kilimo ili iwe peke yake! Sasa nimejua kwamba ilikuwa ni kutafutia washikaji ulaji, haikuwa na maana yoyote. Kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi huwezi kutenga fedha za maendeleo maana yake ni nini? Wabunge

wote mko hapa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba hawataki kusikia biashara ya wafugaji, hawataki kusikia habari ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niwaeleze wafugaji, Serikali hii ya CCM haina mpango na nyie. Hivi *can you imagine* wafugaji wanaoteseka nchi hii, kwa wale wafugaji ambao wako kandokando ya hifadhi na mapori ya akiba, ng'ombe akikanyaga hifadhini, ng'ombe mmoja laki moja ndiyo Sheria inasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa mfugaji mmoja kutoka Jimboni kwangu Serengeti, ng'ombe 300 wote wamepigwa mnada amebaki maskini. Ng'ombe akikanyaga hifadhini laki moja, tembo akila heka tano shamba la mahindi mtu anapewa laki moja, hii ndiyo Serikali ya CCM. Tembo akila shamba la hekari tano, laki moja; ng'ombe akikanyaga tu pale hifadhini akakamatwa, ng'ombe mmoja *fine* laki moja, hutaki kulipa wanapiga mnada Mahakamani, hiyo ndiyo Serikali ya CCM. Kwa hiyo, hii Wizara kazi yenu ni nini? Kama hamuwezi kutetea wafugaji wa nchi hii kazi yenu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wanateseka, unajua tumekaa hapa kuna watu wanakula nyama tu hawajui tabu ambayo wafugaji wanakula. Utakwenda pale *canteen* utakuta kuna Wabunge wanakula hata hajui ng'ombe anavyofugwa, lakini ukimkuta anavyopinga ng'ombe humu. Wafugaji wetu wanapata shida, sasa nilikuwa naangalia kwenye ule ukurasa sijui watafanya nini mwaka huu, watatoa wapi hela? Ulega atatoa wapi hela? Haya wanayosema watafanya hela watatoa wapi? Kama mwaka uliopita wameshindwa kupewa hata mia, afadhali waje hata naweza kuwafadhili, kama Magufuli ameshindwa kuwapa hela, waje nitawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uvuvi ni balaa, yaani Ulega na Mpina wanataka wananchi wa Kanda ya Ziwa wale nini? Tulizoea kula dagaa, kula samaki sasa hivi hawataki kabisa na mitego yote, nyavu zote wamechoma

na kuteketeza. Hata zile ambazo ziko kwa mujibu wa Sheria walikuwa wameigiza, ziko pale mpakani Sirari Mpina amezikataa. Akija hapa atuambie kwanini zile nyavu ambazo ziko pale mpakani amezikataa. Nataka majibu leo toka kwa Mpina, kama hatatupa majibu, mimi nitakamata shilingi yake na Wabunge wote wa Kanda ya Ziwa tutamsulubu kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka majibu, kwa nini nyavu za wafanyabisahara zile ambazo ziko pale Sirari amezikataa ambazo ziko kwa mujibu wa sheria. Sasa hivi dagaa wameadimika Kanda ya Ziwa hakuna dagaa, hakuna samaki. Nilikwenda pale naulizia samaki wananiambia elfu 30, samaki mmoja shilingi elfu 30. Hivi Mheshimiwa Mpina anatoka Kanda ya Ziwa au anatokea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli niwaombe Wabunge wa CCM kama wataunga mkono hoja, uchumi wa Kanda ya Ziwa ni samaki, uchumi wa Kanda ya Ziwa ni ng'ombe, ng'ombe wamepigwa mnada wamekwisha, samaki nao hawataki, sasa wanataka wafanye nini, wakaibe? Mheshimiwa Mpina wakaibe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kimsingi nashangaa Wizara hii, hivi kazi yao ni nini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Ryoba Chacha. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwa Kanuni zetu humu ndani tukiwa tunatajana majina inabidi uweke neno 'Mheshimiwa' labda kama unamwita kwa cheo chake unaweza kusahau neno 'Mheshimiwa' ukimwita jina kila mtu humu ndani ni Mheshimiwa, Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Mpina. Mheshimiwa Mwita Waitara

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Haya majina ya Waheshimiwa haya yanatuvimbisha vichwa wakati mwingine, kuna watu wakiitwa jina inawezekana ukapata ujumbe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri alikuja Ukonga katika mnada wa Pugu na akajionea hali ya shida iliyopo na ugomvi wa mnada ule na wananchi wanaozunguka eneo lile Mtaa wa Banguro. Nimeona kwenye ukurasa wa 40 amelizungumzia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Eneo la Banguro ni kweli kwamba Wizara yake ina hati ya mwaka 1939, lakini vilevile wananchi wenyewe walipewa hati ya Kijiji na Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa nchi hii, Julius Kambarage Nyerere ya mwaka 1976 na wamejenga shule, wana zahanati, shughuli za maendeleo zinaendelea katika eneo lile. Kuna hekari 4,800 na wameshachukua hekari hizo zote karibu 4,162 anazo 108. Alipozunguka alikuwa anaoneshwa *beacons* ambazo ziko kwenye Miji ya watu na huduma za Kijamii.

Mheshimiwa N aibu Spika, ushari wangu ni kwamba, kwa kuwa wananchi walipewa hati na Serikali na hati ya kwanza ni ya mwaka 1939, hati ya pili ya mwaka 1976, *automatically* hii hati ya mwisho imefuta ile ya kwanza na ndiyo maana wamefanya shughuli za kimaendeleo, kuna zahanati pale wanajenga, shule ipo na watu wanaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeshauri kwa sababu kuna hekari zilizobaki 108, kama alivyosema abaki na hizi kwa maana ya kuimarisha, lakini ikimpendeza sasa hivi ule mnada uko mjini, kuna maeneo hata hapa Ruvu makubwa tu, mapori makubwa ng'ombe wanahitaji maji, wanahitaji majosho, wanahitaji mabwawa, wanahitaji huduma mbalimbali katika eneo hilo, kule Dar es Salaam anapaswa alete tu nyama, hawa ng'ombe wanaweza wakatoka kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri hataki kwenda Ruvu, pale Zingiziwa tuna hekari 70, ni nje ya Mji, anaweza akapeleka hiyo huduma katika eneo lile. Kwa sasa wananchi wale kwa kweli wamepata sintofahamu, hawafanyi shughuli za kimaendeleo, wanaambiwa watafukuzwa kesho, watabomolewa kesho, kwa hiyo,

natarajia katika mazungumzo yake na kwa sababu aliunda timu itakuwa imemshauri vizuri kwamba wale wananchi kwa sababu walipewa na Serikali na wana leseni za makazi, wengine wana hati miliki kama alivyojionea. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kauli yake itoke ili wapate amani katika maisha yao, waweze kujiendeleza, wasikae kwa wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Pugu *Station* wananchi wamevunjiwa nyumba kutoka Gongo la Mboto, kuja Ukonga, kuja Pugu mpaka Pugu *Station.* Tena sasa inakuja hofu tena ya mnada wa Pugu, kwa kweli hawawatendei haki wale wananchi. Ni muhimu ili watu wafanye shughuli za kimaendeleo na za kiuchumi wapate fursa na kauli ya Serikali ili waweze ku-*settle* na wajiendeleze. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mradi ule aliuona, katika eneo lile hakuna hata uzio, ndiyo maana kuna ugomvi kati ya wananchi na Wizara ya Mifugo na kuna malalamiko. Pale wanahitaji maji, wanahitaji uzio, ng'ombe wanaokufa juzi ameona wamekamatwa. Nilimwambia siku ile ng'ombe wanaokufa kwanza kuna tundu la kuchomwa ile mifugo ili wateketezwe, lile limeharibika na ile ya kuchimbia ile mifugo haipo, hivyo wanatupwa kule bondeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakitupwa kule bondeni, watu wanazunguka, wanachukua mizoga, wanachinja, wanaingia mtaani, watu wanakula mizoga iliyokufa, ile ambayo wamekamata juzi ni michache. Ukweli ni kwamba ng'ombe wanakufa na watu wanakula vibudu pale kwa sababu hiyo. Kwa hiyo nadhani hilo nalo Mheshimiwa Waziri alishughulikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kule Dar es Salaam tuna machinjio mbili, ile ya Vingunguti lakini na ile ya Mazizini. Mazizini ni machinjio ya mtu binafsi kwa hiyo hata Halmashauri inashindwa kuiboresha. Kwa hiyo, wananchi wa Mazizini wanapata shida, kuna maji machafu nilishamwambia na Mheshimiwa Naibu Waziri anajua. Maji yote ya ng'ombe wanaochinjwa pale, damu zote zinaingia mtaani. Kwa hiyo, ile sehemu wakati wote wa majira ya

mwaka ni kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Tumewaambia, tumelalamika mara nyingi walishughulikie, kama wanachukua kodi, waboreshe maeneo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara hawa wa ng'ombe wanalalamika wana leseni mbili; kuna leseni ya kutoka kwenye mnada na akifika tena machinjioni analipa tena leseni nyingine. Bahati mbaya wale wafanyabiashara wanazuiliwa kuonana na viongozi yaani umoja wao, viongozi hawakutani nao ili wawaambie kero zao. Wanazuia hata ng'ombe ambao wanachinjwa hawajui idadi, wanadhulumiwa. Wanasema wale Madaktari, machinjio yote hata hii ya Kizota hapa Dodoma na nyingine Dar es Salaam, ng'ombe wanaochinjwa wale jamaa wanasema wanaibiwa nyama kwa sababu hawawezi kuhakiki. Kwa hiyo, hili nalo naomba Mheshimiwa Waziri alishughulikie lipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na shida mwenzangu amezungumza hapa asubuhi kwamba, ukihamisha mfugo kutoka eneo moja kwenda lingine unalipa kodi, hizi kodi si ndiyo Rais alisema kwamba ni Rais wa wanyonge ataziondoa, kulipwe kodi moja ambayo inaeleweka, leseni iwe moja, waiunganishe ili kuondoa usumbufu na kuondoa mianya ya rushwa na kuwasumbuasumbua watu. Vikodi kodi vingi vingi hivi kila mahali watu kwa kuwa wajanja wameingiza mikono yao na wafanyabiashara kimsingi hawanufaiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri kwa kweli ni mtu wa Kanda ya Ziwa na mimi nimeolea kule Nyakabindi kule Bariadi, yeye ni mfugaji, ni mkulima, kwa kweli siyo haki wakulima wa nchi hii, yaani mkulima analia, mvuvi analia na nyama tunaitaka. Haiwezekani wameendesha operesheni nyingi zimewaumiza watu sana. Operesheni Tokomeza walikuwa wanachukua ng'ombe, wanachukua miti wanawachomeka kule nyuma mpaka mtu anatoka utumbo, ni *very unfair* Mheshimiwa Waziri, siyo sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawa wanazunguka nchi nzima yaani Mmasai akionekana mahali ni kama mnyama, Msukuma watu wanatuchukia. Wameleta ugomvi kati ya wafugaji na wakulima. Watenge maeneo, ng'ombe apewe heshima yake, watengewe maeneo ya wafugaji ili tuondoe ugomvi kati ya wakulima na wafugaji. Nilitarajia Waziri aje na hiyo suluhu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Ahsante sana Mheshimiwa Mwita. Mheshimiwa Maftah Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala,* lakini niwashukuru vile vile wananchi wangu wa Mtwara ambao leo hii wameniagiza kwa mara nyingine tena nimweleze Mheshimiwa Mpina kwamba kijana aliyeuawa na kikosi kazi chake ambacho alikiunda yeye cha kushughulikia uvuvi haramu katika Operesheni ya *MATT* ambayo inafanyika kwenye Bahari ya Hindi kuanzia kule Mtwara mpaka kule Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha salamu hizi kwa niaba ya wananchi wa Mtwara, wameniagiza nimweleze Mheshimiwa Waziri ile roho iliyoondoka, iliyopotea, kijana Abdillah Abdulrahman ambaye alipigwa risasi kisogoni kwake akiwa anatafuta kitoweo. Tunaomba kauli ya Serikali kwa sababu mpaka leo Serikali iko kimya na Wizara hii ndiyo iliyounda ile Tume ya Kushughulikia Uvuvi Haramu na huyu kijana alikuwa hafanyi uvuvi haramu. Tunaomba tamko na kauli ya Serikali kutoka Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nikiwa nasoma, nilisoma jiografia na historia, niliweza kusoma kwamba maelezo ya zamani ya vitabu vyote vimeandika kwamba Miji ya zamani Miji yote Tanzania na duniani kote

ilikuwa inaanzishwa kutokana na mambo kadhaa. Jambo la kwanza, ni uwepo wa *water bodies* yaani vile vyanzo vya maji. Kwa hiyo, wananchi wengi wamejenga katika maeneo mbalimbali ambako maji yanapatikana kwa lengo kuu moja au mawili:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kutumia yale maji kwa ajili ya kuweza kujipatia chakula chao kwa kufanya uvuvi ambao tunasema *subsistence kind of fishing* ili waweze kuvua, waweze kutumia wale samaki kwa ajili ya kula. Hawa wananchi wamejenga kwenye vyanzo hivi vya maji waweze kupata wale samaki wanapokwenda kuvua mwisho wa siku waweze kupata pesa, wakiuza waweze kuendesha maisha yao, waweze kujenga nyumba, waweze kusomesha, waweze kufanya mambo mengi ya maendeleo. Nilikuwa nasoma mambo haya wakati nasoma historia wakati nikiwa sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, watu wengine wamejenga maeneo mbalimbali kwa sababu tu ya kufuata barabara. Sasa mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Mtwara Mjini ni miongoni mwa wananchi ambao tulijenga Mtwara, tuliamua kuishi Mtwara tangu mababu na mababu kwa sababu ya kufuata bahari ambayo ndiyo ilikuwa inatunufaisha kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunasikitika sana kwamba oparesheni hizi zinazoendesha (Operesheni *MATT*) na Operesheni Jodari) ambazo zinafanyika kwenye bahari kuu kwamba wananchi wanakatazwa kuvua samaki, wananchi wanakatazwa kwa maana nyingine wasile samaki wao ambao Mwenyezi Mungu amewapa na wao wameenda kujenga kwenye maeneo yale ili waweze kunufaika na samaki kwa kisingizo kwamba ni uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote na Wabunge wengine wamezungumza hapa kwamba hakuna anayetaka wanachi wafanye uvuvi haramu, la hasha, hata pale Mtwara mwaka 2008 wananchi walikamatwa wengi sana ambao

walikuwa wanatumia uvuvi wa mabomu na sisi tulifurahia sana kwa sababu samaki waliendelea kupatikana na wananchi tulikuwa tuna-*enjoy* samaki, tuna-*enjoy* matunda aliyotupa Mwenyezi Mungu. Sasa wanavyosema kwamba eti kila nyavu ni nyavu haramu, hawa wananchi wa kawaida ambao Serikali hii haijawapa vifaa maalum vya kuvulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka 2008 tukiwa Chuo Kikuu pale tuliweza kuletewa samaki wa Magufuli wakati ule, tuliweza kula wale samaki zaidi ya mwezi mzima pale Chuo Kikuu kwa sababu walikamata meli moja tu ya Wachina waliokuwa wanavua wale samaki, wakaikamata, wale samaki tuligawiwa Vyuo vyote Dar es Salaam pale. Tuliweza kula mwezi mzima mpaka tukawachoka, hiyo ni meli moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu Serikali haijawapa vifaa, wanavua kwa nyavu za kawaida halafu wanakwenda kuwakamata, wanawaambia mnavua uvuvi haramu, wakale wapi? Waishi vipi? Wananchi hawa wanaishi kwenye maeneo ya bahari, wafanye kazi gani? Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali ihakikishe ya kwamba inaleta vifaa vya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mtwara nimeshaandika sana, nimezungumza sana ndani ya Bunge hili kwamba wananchi wangu wamejiunga katika vikundi vidogo vidogo wanahitaji boti, wanahitaji zana za kisasa za kuvulia Serikali ituletee waweze kukopa wale wavuvi mwisho wa siku waweze kufanya uvuvi ambao hawaitwi uvuvi haramu, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itekeleze hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, pale Mtwara kuna Chuo cha Uvuvi ambacho kimejengwa, huu ni zaidi ya mwaka wa saba hakijaanza kutumika, wanafunzi hawajaanza kusoma, zaidi ya miaka saba lile jengo lipo tu, lipo baharini kabisa pale Mikindani, ninapoishi mimi, bahari iko hapa kile Chuo kipo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji sasa hiki Chuo kianze kufanya kazi, wanafunzi wafundishwe, waweze kusoma, mwisho wa siku tusifanye uvuvi haramu lakini Serikali haitekelezi, haitupi haya, mwisho wa siku wanakuja kutukamata kwa yale ambayo tunafanya, wanasema kwamba eti hatuvui sawasawa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Vedasto Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Niende moja kwa moja kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi hasa katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa kila nikipata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii, kilio changu ni kuhusiana na suala zima la mazingira wezeshi, mazingira ambayo yanaweza kuwafanya wafugaji wafanye shughuli zao na hii nikiwa na maana kwamba Serikali imefanya maamuzi ya kupeleka mifugo Mkoa wa Lindi na hasa Wilaya ya Kilwa, lakini mpaka hivi ninavyozungumza hakuna chochote kimefanyika kuhusiana na miundiombinu ambayo ingeweza au itaweza kuwasaidia wafugaji wale kufanya shughuli zao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapori yote ya Kilwa sasa yamevamiwa na mifugo, lakini hakuna bwawa, hakuna josho kwa hiyo wafugaji wale wanafanya shughuli zao kiholela. Nichukue nafasi hii kuishauri Wizara, naomba mjenge mabwawa na majosho Kilwa ili basi mifugo ile iweze kustawi kama ambavyo tumekusudia. Kwa hali iliyopo sasa ni ugomvi tu baina ya wenyeji wakulima na ndugu zetu wafugaji. Kama ambavyo wanafahamu, sisi watu wa Kilwa hatufugi sisi kazi yetu ni kuvua, kazi yetu kulima, tukiona ng'ombe watoto

wanakimbia ndiyo kwanza tumeanza kuona ng'ombe, sasa wameleta kwa maelfu bila kipimo, wanatupa shida, tunapata tabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii labda mimi naeleza kwa hisia nyepesi nyepesi Mheshimiwa Ulega anafahamu, alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, anafahamu ninachokizungumza, ni mashaka. Kwa hiyo, tunaomba hatuna shida na wafugaji lakini andaeni sasa miundombinu ili sisi basi tufanye shughuli zetu kama wavuvi, kama wakulima na wafugaji wafanye shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la zoezi la upigaji chapa, kuna zoezi hili linaendelea na kusudio lake lilikuwa sasa kuweza kutengenisha wapi sasa wanatakiwa wawepo wafugaji na eneo gani wakulima wataendelea kuwepo na kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni tajiri wa mapori na ardhi ambayo unaweza ukafanya shughuli za kilimo ipasavyo na shughuli za ufugaji, lakini katika hali ya kushangaza, katika program hii, wakulima na wafugaji wanachanganywa na ili kuondokana na hili ndiyo likaja wazo sasa la kupiga chapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili la kupiga chapa linaendeshwa kwa urasimu mkubwa. Tunashindwa kuelewa. Kwa mfano, Lindi tuna Selou, tuna mapori ambayo hayana kazi, lakini wafugaji hawa wanakuja kung'ang'ania kukaa katika maeneo ya wakulima, haieleweki tatizo ni nini. Naishauri Wizara wafugaji wawaweke tofauti na wakulima, tuna maeneo mengi katika vijiji vyetu, wafugaji hawa wanaweza wakafanya shughuli zao tofauti kabisa na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la maendeleo ya uvuvi. Kwangu Kilwa ni wavuvi lakini mpaka sasa ukimuuliza mvuvi ni lini alisaidiwa na Serikali hakuna siku ambayo mvuvi alisaidiwa na Serikali na Serikali haijakuja na *program* yoyote ya kuwasaidia wavuvi.

Naishauri Serikali iwaangalie wavuvi kama ambavyo inawaangalia wafugaji na wakulima. Wavuvi nao waangaliwe, wapewe vifaa vya kisasa, wawezeshwe kwenda kuvua kwenye kina kirefu cha maji ili waweze kupata tija katika shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa, wavuvi wale wanafanya shughuli zao kienyeji na sasa hivi hizi operesheni za ndugu yangu Mheshimiwa Mpina kwamba kila siku anakuja na programu mpya, inawadidimiza kabisa wavuvi wetu. Kwa hiyo, naomba Serikali ije na programu maalum ya kufanya ustawi kwa wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote wanaweza kuwa mashahidi. Leo ukisafiri kwenda Mikoa ya Kusini, sehemu ambayo unaweza kwenda ukasimama ukapata samaki wazuri ni maeneo ya Somanga. Somanga ile ambayo tunapata samaki, lakini hakuna Soko la Samaki. Tasi na changu wananunua kienyeji, hakuna Soko la Samaki. Hii inaonesha namna gani ambavyo Wizara haijapanga kuwasaidia wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, Mheshimiwa Ulega alikuwa Kilwa pale, basi na ndugu zangu wale wa Somanga pawepo na soko ambalo sasa Waheshimiwa wakipita, watapata samaki wa kupaka na wali wa nazi, mambo yanaenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu ya muda, naomba tu niende moja kwa moja kwa kusema kwamba kwa upande wa mifugo kusema kweli Wizara wala Serikali haijafanya chochote kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia katika kitabu chetu kwamba fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji, yaani ni kituko kabisa. Kwa hiyo, tunadhani Serikali ina changamoto kubwa, ione ni kwa kiasi gani, inahitaji ijipange kuhakikisha kwamba inawasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la mbegu bora. Mifugo mingi ya Tanzania pamoja na kwamba Tanzania ni nchi ya tatu, tuna ile mifugo ambayo ni aina ya zebu. Kwa hiyo, tunaifuga kwa muda mrefu lakini tija yake ni ndogo. Kwa hiyo, ushauri wangu, hebu Serikali iangalie kupitia hizi *ranch* zake iweze kuzalisha ng'ombe bora wa mbegu na iweze kusambaza kwa gharama nafuu. Tunadhani kwa namna hiyo, itaweza kuwasaidia Watanzania wengi waweze kufuga kwa tija kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu ushauri, kwa sababu sisi mojawapo ya kazi yetu ni kushauri, ukiangalia hata *ranch* zetu za Serikali zote tulizonazo, nenda Kongwa na hizo za *NARCO,* zote zimekufa. Yaani ni kwamba zile *ranch* hazina tija. Ni vizuri wale Mameneja wa Ranchi zile badala ya kuteua tu kwamba tunadhani fulani ni mwaminifu tumkabidhi *ranch,* Mheshimiwa Waziri atangaze nani anaweza kusimamia? Naamini atapata watalaam wazuri wanaoweza kusimamia na wakaziendesha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani *ranch* inaweza kubeba ng'ombe 16,000, unaipatia ng'ombe 4,000. Tafsiri yake ni kwamba tunawasaidia tu wale Mameneja pamoja na wale wahusika walioko kule, lakini hazina manufaa yoyote na hata sisi hatuwezi kujifunza kupitia zile ranchi. Kwa hiyo, huo ndio ushauri wangu kwa upande wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uvuvi, yawezekana nikatofautiana kidogo na wenzangu. Binafsi napongeza suala la ukomeshaji wa uvuvi haramu, kwa sababu gani? Maana wanasema penye ukweli lazima tuseme ukweli kwa sababu tunahitaji kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwangu Musoma Mjini, baada ya zoezi la kukomesha uvuvi haramu kuendelea kwa muda, leo ukienda pale ukimwuliza kila mmoja anakubali kwamba sasa samaki wameongezeka. Kwa hiyo, hilo ni jukumu ambalo tuna kila sababu ya kupongeza kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Waziri, kuna yule ambaye ni *DC* wangu wa pale mjini, anasaidia sana suala la uvuvi haramu. Nimefanya mikutano mingi, wale wale waliokuwa wanachukia wakati ule wakisema wanakandamizwa, leo kila mmoja anakubali kwamba kweli samaki wanapatikana. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na haya mafanikio, yako matatizo na changamoto ambazo lazima tujipange tuone namna ya kuzimaliza. Ile timu ya Mheshimiwa Waziri inayofanya kazi ile, wako wengine wanafanya kazi kwa uaminifu, lakini wengine wanatumia nafasi zile kuwaumiza wale wavuvi pamoja na wale raia wa kule. Shida iliyoko pale, wakati mwingine naweza kuita ile timu, kama ilivyokuwa Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na mimi tumewasiliana mara nyingi. Moja, unakuta labda wale watu wanapofanya operesheni zao, wakikuta tu kwenye ile gari labda hawana ile koleo ya *plastic,* anaambiwa faini shilingi milioni moja hadi shilingi milioni tatu, wakati vile vitu ni vya kuelimishana tu. Mtu yule hana *gumboot* anapigwa faini ya shilingi milioni moja hadi shilingi milioni tatu. Kwa yule mvuvi wa kawaida anayefanya biashara hiyo, maana yake ni kwamba tunamfilisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimekwenda kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na wafanyabiashara wa Musoma wanaosafirisha samaki. Wote tunafahamu, samaki wote tunaokula huku hatuna magari yenye *refrigerated system* yanayoweza kusafirisha samaki. Wanaweka kwenye *Fusso,* wanafunga kwenye maboksi wanasafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale samaki wakiwa kule Musoma, kabla ya hawajaondoka, wanaenda pale kwenye Kituo cha Uvuvi, ndipo wanapakilia, wanakaguliwa. Wanapofika Singida, hatuna *storage system.* Ile *Fusso* inafunguliwa, wanacheki *box* moja moja, zinakutwa kilogram tatu kwenye tani 14. Wakikuta kilogram tatu wanapiga faini shilingi milioni sita. Hivi hiyo ni tokomeza au ni kuendeleza uvuvi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi, bahati nzuri mimi na Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukiwasiliana na kusema kweli mambo mengine amekuwa akiyamaliza. Nitoe mifano kwa machache ambayo tumewasiliana na tuone namna ya kuyarekebisha ili mambo yaende. Hili gari moja walipofungua pale Singida wakakuta hakuna kilogram tatu, ni *under size* walipigwa faini ya shilingi milioni sita. Waliponiambia, nikazungumza na Mheshimiwa Waziri. Akaniambia hiyo gari kama ina kilogram tatu peke yake hebu iachieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watu walionesha kiburi wakasema wanarudi ku-*check* upya. Badala ya ile *sampling* waka-*check* upya. Kwenye kilogram 14, maana yake ile kazi waliifanya kwa siku mbili. Tafsiri yake ni kwamba hilo gari siyo *refrigerated.* Kwa hiyo, matokeo yake wale samaki wote walifika Dar es Salaam sokoni wakiwa wameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi walipo-*check* tena kila *box,* wakapata kama kilogram 30 zikiwa ni *under size.* Ile faini ikarushwa kutoka shilingi milioni sita mpaka shilingi milioni 20. Hivi tunategemea hiyo ni Operesheni Tokemeza au hiyo ni kusaidia kumaliza tatizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali, ihakikishe kwamba samaki wanapatikana, lakini lazima tuangalie namna ya utendaji wa kazi unavyofanyika. Kibaya zaidi, wale watu wakisikia tu kwamba Mheshimiwa Waziri kaambiwa jambo, kalalamikiwa hapo ndipo wanakuja zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili, maana ni vizuri tukaenda kwa mifano. Ilitokea kwa mtu mmoja, kwa kawaida wale wanaofanya biashara ya kununua samaki, akinunua samaki anapaswa awe na watu wengine nadhani kama wanne hivi. Kwa bahati mbaya wakati anakata leseni akalipia wale watu wote lakini jina likaandikwa la kampuni yake peke yake. Walipomshika mtu wake wakati yeye hayupo, matokeo yake akapigwa faini. Kwa bahati nzuri nilimweleza Mheshimiwa Waziri na akafuatilia. Hapo sasa ndiyo wakasema wanamtafuta na mwenye mzigo naye wanataka wampige faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema kwamba ukiangalia zoezi lenyewe ni nzuri, lakini kwa maana ya kwamba tunategemea kama sisi watu wa Musoma pale tuna viwanda visivyopungua vinne vya samaki ambavyo vyote vimekufa. Hata hivyo, leo furaha yangu ni kuona kwamba viwanda sasa vinachipuka kwa maana vinafunguliwa na samaki wanapatikana. Sasa kupatikana kwa samaki huku lazima kuendane na kuwapa watu wetu elimu kuliko hiki kinachofanyika sasa, badala ya kuwaendeleza badala yake tunawamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine hata zile nyavu tunapozishika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajua; tunashika nyavu haramu, zile nyavu tuna haki ya kuziteketeza. Sasa hebu tuelezwe, ile boti, zile *engine,* tuna haja gani ya kuziharibu? Maana yake ni kwamba unachoma ile boti, tafsiri yake ni kwamba unataka yule mtu afilisike. Kwa hiyo, huyo mtu unapotaka afilisike, sasa kesho ataendeshaje maisha yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kazi nzuri ambayo ndugu zetu wanaifanya, lakini hebu waone namna gani wanaweza wakaifanya kwa uzuri zaidi. Ushauri wangu, ni vizuri kwenye ile timu watu wengi wakahusika mle; watu wa usalama, Polisi na wenyewe wakawemo mle. Ule mchanganyiko tunadhani utasaidia kuwafanya watu wawe na mbinu nzuri za kufanya ile Operasheni ambayo kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**TAARIFA**

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, kuna taarifa.

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anazindua Operesheni Sangara, awamu ya tatu ameanzisha Mahakama inayotembea, lakini katika Mahakama hiyo Hakimu anaenda kusikiliza kesi, analipwa posho yake na ya anayemfanyia kazi. Maana yake atakuwa na Hakimu, Polisi na Afisa Usalama anaowalipa posho ili wakasikilize kesi ya mvuvi. Inawezekanaje akamtendea haki wakati anayewalipa posho yupo? Nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi ulikuwa umeshagongewa kengele. Nakupa dakika moja umalizie na useme kama hiyo taarifa unaipokea.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa naipokea kwa maana kwamba, Mheshimiwa Waziri ajue sasa kwamba hizo ni changamoto ambazo anahitaji kuzirekebisha kwa haraka, *otherwise* badala ya huu uvuvi kutusaidia, basi utaendelea kuwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nami naunga mkono hoja, lakini hayo yote yarekebishwe ili mambo mazuri yaendelee kufanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Manyinyi. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Sekta hii ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uwe na mifugo na ufugaji wa kisasa ni lazima elimu itumike na hii elimu inatolewa na Afisa Ugani. Afisa Ugani ni watu muhimu sana. Kwa upande wa uvuvi kuna uhaba wa Afisa Ugani. Wanaohitajika ni 16,000 lakini waliopo ni 750 tu. Kwa hiyo, kuna Afisa Ugani 15,250. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa upande wa mifugo na wenyewe kuna uhaba na hata hao waliopo, hawafanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, nashauri Wizara kwa kushirikiana pamoja na TAMISEMI iangalie jinsi ya kuwapa mwongozo na utaratibu hawa Afisa Ugani wa Uvuvi na hasa wa Mifugo waliopo waweze kufanya kazi kwa kujituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mpaka sasa hivi ninapoongea, hawawatembelei wakulima na hasa Maafisa Ugani wa Mifugo. Inabidi uwaite ndiyo waje wakutembelee. Siyo kama zamani walivyokuwa wanajituma. Kwa hiyo nashauri Serikali iangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sekta nyingine ambayo huwa haiongelewi sana, nayo ni ufugaji wa kuku wa kienyeji. Nikisema ufugaji wa kuku wa kienyeji, napenda sana nimpe pongezi rafiki yangu Profesa Salome Mtayoba kwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi. Hongera sana kwa upande wa ufugaji. Ufugaji wa kuku wa kienyeji ni kitu kizuri sana kwa sababu unanufaisha sana familia kwa kuinua kipato na kuwapa ajira ya mara moja vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba licha ya Wizara kuona inaweka msisitizo, lakini naona kuwa msisitizo uwe zaidi na zaidi kuhusu hawa akinamama pamoja na vijana, pamoja na familia tuweze kuinua kipato, tuweze kuinua lishe. Sasa hivi tumefikia 32% ya Watanzania wengi

hasa watoto ambao ni wadumavu *(malnutrition).* Kwa hiyo, kwa upande wa lishe, lazima tukazanie kwenye upande wa kilimo hasa ufugaji wa kuku wa kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni ufugaji wa samaki kwenye upande wa mabwawa *(fish ponds* au *aquaculture).* Elimu hii haijaenea sana kwa wakulima au wafugaji. Hiki kilimo cha mabwawa ni rahisi sana kufanyika hata nyumbani kwako. Mahali popote unaweza ukafanya ili mradi una maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuinua ufugaji wa samaki ambao hauna shida kukamatwa nyavu na kupigwa mabomu, naona Wizara ihimize kilimo cha uvuvi wa samaki kwenye mabwawa, kwa kifupi ni *fish ponds,* ambayo unaweza ukaenda wewe mwenyewe, hata mwanamke mwenyewe ukachukua samaki wako ukaja ukapika mara moja, watoto wako wakapata lishe na familia nzima ikapata lishe na kupandisha kipato. Kwa hiyo, nauliza upande wa Serikali, mkakati mkubwa sana waliouweka kwenye upande wa ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ukoje? Naomba utiliwe mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee migogoro ya wafugaji pamoja na wakulima. Kwa upande wa Mkoa wa Morogoro, hii bado ipo, hatuwezi kusema imekwisha. Imetulia kidogo kwa sababu sasa hivi kuna mvua, majani yanapatikana, malisho yanapatikana, ndiyo sababu imetulia. Ukienda kilosa kwenye Kijiji cha Mabwegere bado kuna matatizo ya wafugaji pamoja na wakulima. Akinamama hawapati raha kwenda kulima, kama mnavyojua wakulima wengi, zaidi ya asilimia 70 wanaotoa chakula ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana waliangalie hilo. Dawa yenyewe iliyopo ni matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, tuendelee kupima ardhi kusudi watu waweze kupata ardhi yao na waweze kuona ni wapi pa kulishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni elimu ya malisho. Jambo lingine ambalo linaweza likaondoa migogoro ya

wafugaji pamoja na wakulima ni Elimu ya Malisho. Elimu ya Malisho bado haijaenea sana. Naomba sana wawahimize hao wafugaji na hii inawezekana wakiipata hii elimu hata kuhama hama kwa hawa wafugaji kutaacha, kwa sababu wataweza kustawisha malisho yao na wataweza kuyatumia wakati wowote na inaweza ikasaidia hata wakati wa kiangazi kwa sababu watatengeneza *hay* ambayo wanaweza kulisha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo, kama tulivyoona, kwa msimu wa mwaka 2017/2018 kwa upande wa mifugo iliinidhishwa shilingi bilioni nne na kwa upande wa uvuvi shilingi bilioni sita. Mpaka Machi mwaka huu 2018, hakuna hela yoyote ya maendeleo ambayo ilikuwa imeshatolewa. Sasa kama hela za maendeleo hazitolewi, miradi itaendeleaje au itafanyikaje? Kwa hiyo, naomba kama tunaidhinisha hela humu Bungeni, tujitahidi Hazina pamoja na Serikali kwa ujumla hela ziweze kutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvuvi haramu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine sekunde 30.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naongea uvuvi haramu. Naomba Serikali iangalie hiyo sheria kusudi wavuvi waache kupiga kelele na waache kuonewa. Tutumie sheria kuwanusuru hawa wavuvi waweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni muhimu sana, inatoa ajira... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga na Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nami pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na afya kuweza kukutana leo. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri leo asubuhi, lakini nilikuwa nataka nianze tu na ushauri mdogo tu kwake. Hii Wizara haitakiwi kuendeshwa kwa *operations.* Naomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji, wafahamu kabisa kwamba Wizara hii haitakiwi kuendeshwa kwa operesheni kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni zipo katika vikosi vya jeshi na kwenye *theater* za mahospitali. Kule ndiyo kuna operesheni. Wamefanya operesheni ya kwanza na ya pili, inatosha. Watoe elimu sasa, wasijikite kwenye operesheni kila siku, itakuwa kila siku kazi yao wanaifanya kama *fire brigade* sasa. Kazi yao ni kuzima moto tu. Waende wakatoe elimu. Nitatoa mfano mdogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la mitungi ya gesi limezungumzwa sana hapa. Mimi natokea Mafia, mwaka huu peke yake nimeshapoteza wavuvi zaidi ya watatu, wamekufa. Wamepiga marufuku kokoro, wameruhusu *ring net* ambapo watu wanakwenda katika kina kirefu cha mita 50, wakati huo unatarajia mvuvi aende aka-*dive* mita 50 chini bila ya kutumia mtungi wa gesi. Maana yake una-*condemn to death,* hakuna tafsiri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa upande mwingine wanasababisha vifo kwa hawa wavuvi wetu. Sasa wanapokuja na hoja kama hizi za kusema kwamba wavuvi wasitumie mitungi ya gesi, mita 50 sijui wenzetu waliokuwa kwenye *comfort zone,* kwenye viti vyenu vya kuzunguka huko na Watendaji Maofisini sijui kama hawa wataalam wanakwenda kwa wavuvi na kuongea nao. Bahati nzuri kuna Chama cha Wavuvi na Wawakilishi wao, wapo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwa Mheshimiwa Waziri hebu wapate nafasi waende wakaongee na hao wavuvi wawaambie anayekwenda kuchukua

majongoo kule chini ni nani na anayekwenda kuvua ni nani? Haiwezekani kosa la mmoja wakawahukumu wavuvi wote. Siyo sawa kabisa. Kama kuna dereva ameendesha gari akiwa amelewa, huwezi kufungia leseni za madereva wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inashangaza sana kama kuna wavuvi wanatumia mitungi ya gesi, wanafanya *diving,* wakifika chini kule wanachukua yale majongoo bahari, wa-*deal* na hao tu, wasiwazuie wote. Matokeo yake sasa tunapoteza watu na wavuvi wanafariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la hifadhi ya bahari nimekuwa nikilizungumza sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ameanza vizuri sana, ametuletea mtendaji mpya pale, nami natarajia kwamba tutakwenda vizuri, lakini lazima zile changamoto ambazo amezikuta pale azifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu ya Mafia na Mheshimiwa Ulega anafahamu, alikuja Mafia. Tunasisitiza siku zote, kanuni zao zinatuumiza kule Mafia. Leo Mafia, Halmashauri yangu inakufa. Hifadhi ya bahari, taasisi yenye *staff* wasiozidi 15 wanakusanya zaidi ya shilingi bilioni moja kutokana na maduhuli. Sisi Halmashauri ya Mafia ambao ndiyo Serikali, tunakusanya shilingi milioni 600. Ile Halmashauri inakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaambia siku zote, wabadilishe ile kanuni, sisi tunataka asilimia 10 tu ya maduhuli yale. Nami naamini amekuja mtendaji mpya na pia Waziri mpya pale, wakae wabadilishe hii kanuni. Haiwezekani sisi Halmashauri ambao tunaendesha mambo mengi tupate asilimia 10 tu halafu Hifadhi ya Bahari ambayo *staffing* yake haizidi watu 15, wanachukua pesa chungu nzima. Kwa hiyo natarajia Mheshimiwa Waziri angalau mara hii kilio hiki watakisikia, wakabadilishe kanuni. Suala ni kanuni tu, wala siyo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka jana naongea na Mkurugenzi wangu ananiambia mapato ya Halmashauri ya

Mafia mwaka wa fedha unaisha mwezi ujao yako chini ya asilimia 47 na Waziri Mkuu bahati mbaya leo hayupo, lakini alishasema Halmashauri yoyote yenye kukusanya chini ya asilimia 80 inafutwa. Kwa hiyo, Halmashauri ya Mafia inakwenda kufutwa kwa sababu tu Hifadhi ya Bahari imechukua vyanzo vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami katika kuongezea hili, nataka nisisitize, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yupo hapa, yale maduhuli yakusanywe na *TRA* inakuwaje sisi pale tuko watu wawili; kuna Hifadhi ya Bahari na kuna Halmashauri ya Mafia, lakini Hifadhi ya Bahari ndiyo wanakusanya halafu wanatoa gharama. Kwenye gharama mle sijui wanaweka *night*, safari, wanaweka maposho makali makali, halafu wakija wakitoa sasa wanasema tumepata shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka chanzo hiki Mheshimiwa Waziri wa Fedha akichukue, *TRA* waende wakasimamie makusanyo ya maduhuli yanatokana na watalii kule Mafia. Hapo ndiyo itakuwa salama. Vinginevyo, tunaibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri leo asubuhi alikuwa akijibu swali hapa akawa anapata taabu kidogo katika kuelezea hawa samaki. Mimi sifahamu sana kuhusu samaki wa maziwani huko; furu, sijui nembe na gogo; sifahamu sana kuhusu hawa samaki. Ila kule baharini kuna misusa, ngawala na kuna samaki wadogo wadogo. Sasa tunaomba watupe tafsiri, tunawavua kwa nyavu zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali asubuhi alisema hapa kwamba hawa samaki wengi; nembe, sijui gogo ni samaki wapya waliokuja ziwani. Kwa hiyo, sheria ilianza halafu baadaye samaki ndiyo wakaja wakahamia. Sasa kama samaki walikutwa na sheria, kwa nini wameanza operesheni wakati wakijua hawa samaki walikuja baada ya sheria? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbaraka muda wako umekwisha. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Hilaly na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naomba niliambie Bunge na Watanzania kwa ujumla kwamba kwa mujibu wa maandiko matakatifu, samaki hazijaweza kutosha Ziwa Victoria wala baharini. Kwa sababu Yesu alipokuwa akitembea kule Galilaya, aliwakuta akina Petro na ndugu zake wametupa jarife, wamechoka, wamekosa samaki, akawauliza, kwa nini mmechoka? Wakasema, tumekesha tunavuta, lakini hatujapata samaki. Akafanya miujiza yeye mwenyewe, ndipo wakavuta wakapata samaki. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Biblia, samaki baharini, samaki ziwani hawajawahi kutosha. Hilo lazima Bunge lijue na Taifa kwa ujumla lijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri iliyokuwa imeanzishwa na Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni nzuri sana kwa sababu uchafu ulikuwa umeshakithiri katika maziwa yetu. Tatizo ni moja tu kwamba badala ya kudhibiti uvuvi haramu, watu wanaonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani leo tunazungumza uvuvi haramu, mtu unamkuta ana sangara mmoja wa sentimita 52 au wa sentimita 86 ambaye amempata tu kwa sababu nyavu hizi zinanasa samaki yeyote bila kubagua wakati mwingine. Huyu samaki wa sentimita 86, ukimkuta naye mmoja, unamkamata, unamwambia uhujumu uchumi, faini yake shilingi milioni 10, faini yake ni shilingi milioni 20, unategemea kwamba tunawasaidia wavuvi? Hatuwasaidii hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana Wizara hii haijapewa fedha za maendeleo miaka mingi, ndiyo maana sasa inatafuta fedha za faini ziwe fedha za maendeleo. Haiwezekani jambo hili *brother,* haiwezekani. Ni vizuri Serikali tukaiwezesha Wizara hii ikapata fedha za kutosha kuendesha Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusema kwamba ni Serikali hii ndiyo itakayomaliza uvuvi haramu, lakini siyo kwa staili hii. Kwanza wamefanya kazi kubwa. Wavuvi wale wakubwa sasa hivi hakuna anayevua haramu, yaliyobaki ni makokoro ambayo wameshindwa kuyadhibiti kwisha. Hata hivyo, najiuliza sana kwamba tukienda kwa *style* hii tutamaliza uvuvi haramu?

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Dau kwamba ni muda muafaka wa kutoa elimu sasa kwa wavuvi ili tuwe na uvuvi endelevu. La sivyo, tutamaliza gharama bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *task force* ambazo ziko kule zinaendesha operesheni, ofisi zao ni *Guest House*. Hivi hakuna Ofisi za Serikali? Majengo ya Wakuu wa Wilaya yana nini? Wao ofisi zao zimegeuka kuwa *Guest House,* ni sawa sawa? Watueleze! Kwa sababu hata Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya hatambuliki na operesheni hizi, ni sawasawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hata faini hizi wanakataa kuingiziwa benki, wanataka uwapelekee *cash,* wakati mwingine unalipa kwa *M-Pesa*, ni sahihi? Ushahidi tunao. Yawezekana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu hamjui, lakini Watendaji wenu wanaofanya operesheni kule wana-*sabotage* Serikali. Haiwezekani hii *brother!* Lazima tukubaliane kwamba operesheni hii siyo msaada sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti umefanyika *TAFIRI* na wavuvi, ripoti ipo ya madhara ya macho 26 na madhara ya macho 78. Kuna madhara gani? Mapendeklezo ambayo

tunajua sisi ni kwamba macho 78 hayana madhara yoyote kwa uvuvi wa Ziwa Victoria. Tunawasitisha wavuvi wetu wa nchi hii, Kenya inavua macho 78, Uganda inavua macho 78, hivi tunawasaidia Watanzania? Yawezekana Mheshimiwa Waziri hajui vizuri, kazi yake inaweza kuharibiwa na watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi nchi jirani tunaamini kwamba kuna sheria ambazo zinashabihiana: Je, tumeshindwa kuwa na sheria moja ambayo inaweza kuwezesha uvuvi endelevu kwa nchi zote hizi tatu ambazo tunatumia ziwa letu na bahari nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kiwanda cha Nyavu cha Arusha. Kiwanda hiki kilikuwa kinatengeza vyandarua, lakini kiwanda hiki kimegeuzwa kuwa kinatengeza nyavu. Wavuvi hawa wanasema, *material* yale ya vyandarua hayadumu kwenye maji kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wanachukua miezi sita nyavu hizo zote zinaisha, tunawatia umaskini. Naomba wataalam wawashauri vizuri Mawaziri, ni *material* yapi yanayofaa kutengenezwa nyavu za kuvua katika Ziwa Victoria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mifugo. Mifugo inakamatwa kwenye hifadhi. Inapokamatwa inapelekwa Mahakamani, wafugaji wakishinda kesi, hawarudishiwi mifugo yao. Tunawasaidia? Kama Mahakama imesema mifugo hii irudishwe kwa wenyewe, hairudishwi tunawasaidia? Itafutwe njia ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wengine mtu alikuwa amekamatiwa ng'ombe zake 260, anarudishiwa 76, wengine wamekufa. Ni sahihi? Tunataka wanapokamatwa ng'ombe wa wafugaji wetu, watunzwe, walishwe mpaka ambapo kesi itafikia muda wake wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la ufugaji, kuna na viwanda. Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga ni

kiwanda ambacho kiko eneo zuri na kubwa, lina uwezo kabisa la kufugwa ng'ombe na kuchakata ng'ombe, lakini kiwanda hiki kimesimama. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, ifanye mkakati wa haraka kuweza kufufua kiwanda hiki pamoja na kiwanda cha maziwa kilichopo Utegi na kiwanda cha ngozi kilichopo Mwanza ili kusaidia mazao haya ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende haraka haraka, dakika moja tu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu dakika moja, kuna mifugo inakamatwa inapotoka Minadani, wanataka ipakiliwe kwenye malori; ng'ombe watatu au wanne, hata mahali pa kupakia huko kwenye Minada ya Serikali hatujatengeneza. Tunawapiga faini bure hawa wafugaji. Hata wanapopeleka maeneo ya kwenda kupakilia, wamekaribia na gari wanaliona, ile *task force.* Wanawakamata wanawatoza faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hili namwomba sana Mheshimiwa Waziri hata kama alikuwa halijui, alifuatilie watamharibia sifa na heshima ambayo alikuwa ameanza nayo vizuri. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Nagu na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia jioni ya leo. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kwa kuteua Majaji ili kesi zisiwe na mlundikano kwenye Mahakama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la wafugaji. Wafugaji wetu wameteseka sana hususan wanaoishi maeneo ya kando kando ya hifadhi. Mheshimiwa Rais alipoteua Majaji na Majaji hawa wanafanya kazi nzuri sana na kiapo chao walichoapa watatoa hukumu kulingana na mazingira ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wilaya yangu ya Itilima kuna wafugaji walikuwa wamehukumiwa na mifugo yao ikataifishwa; ng'ombe 339 lakini Mahakama Kuu ikaamuru ng'ombe wale waachiwe na wale watuhumiwa waachiwe, lakini cha ajabu mpaka leo wale ng'ombe hawajaachiwa lakini watuhumiwa walishaachiwa. Sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana angetueleza yeye kama msimamizi wa wafugaji, anatusaidiaje wafugaji ambao tunaendelea kuhangaika, lakini kabisa azma ya Serikali Awamu ya Tano ni kuhakikisha inakomboa wanyonge na hususan mambo haya yapo kisheria na Kimahakama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hotuba yake alisema baada ya mamlaka kumruhusu vibali vya Kimahakama aliweza kuteketeza nyavu, lakini sasa baaadhi ya vyombo vyetu, Mahakama imeamuru ng'ombe warudishwe lakini bado wamezuiliwa na mpaka sasa na ng'ombe wanaendelea kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atusaidie, ni kwa nini mambo haya yanaendelea katika maeneo yetu hususan kwa

wakulima na Serikali ya Awamu ya Tano ni ya wanyonge na wakumbuke ng'ombe hawa ni wa wafugaji maskini lakini ndio matajiri wakubwa ambao wanatuwezesha humu ndani sisi sote tukiamka asubuhi tunakunywa supu, tukiamka asubuhi tunataka nyama, maziwa na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisema, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumza katika suala zima la ng'ombe. Mheshimiwa Waziri anaelewa kabisa kwamba maeneo yetu bado hatujawa na miundombinu mizuri katika minada yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa, mnunuzi amenunua ng'ombe wake watano na tunafahamu kabisa wafugaji wetu au wakulima wetu anaweza akauza mazao yake anaamua kwenda kununua ng'ombe au ametoka machimboni akanunua ng'ombe wake hata 10, 20. Akikutana na wale jamaa, anaambiwa huruhusiwi kuswaga ng'ombe zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii wangetusaidia sana kuweka miundombinu katika maeneo yenu mazuri. Nia ni ya dhati na kazi zao wanazofanya ni nzuri sana, wanalinda rasilimali zetu za nchi lakini namwomba Mheshimiwa Waziri achukue huu ushauri akaufanyie kazi ili kusudi tuondokane na adha hizi ambazo zimejitokeza katika meneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mipango yake mizuri aliyoilekeza katika ukurasa wa 15 na 12 kuhakikisha Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga, kinarudishwa na kinafanya kazi katika maeneo yetu. Hongera sana, hiyo akiifanya litakuwa jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo, atusaidie katika eneo liliko Maswa Shishiu ekari 10,240 hazina kazi. Sasa hiyo ni sehemu mojawapo ya kutatua baadhi ya changamoto za wafugaji. Ikiwezekana maeneo haya basi tuwape wafugaji waweze kulifanyia kazi kuliko eneo lipo

tangu tupate uhuru lakini halina kazi, yanazidi kupoteza muda. Tukiwapa Watanzania na wafugaji wataweza kutusaidia sana kuongeza kipato cha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Amebeba dhamana mpaka ya kuhakikisha analinda rasilimali na mapato ya nchi yaweze kuongezeka. Ushauri wangu ni kwamba wavuvi wamelalamika lakini wanatoa mchango kwa kuunga hoja zake anazozileta, lakini sasa kwenye suala zima la upatikanaji wa vitendea kazi, kiwanda cha Arusha kinaonekana kimezidiwa. Baada ya mwezi mmoja au miwili zile nyavu zinaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni jambo jema sana Mheshimiwa Waziri akalichukua na kulifanyia kazi. Kuna Kontena za watu ziko bandarini ambazo tayari zimeshaingia hapa nchini. wangetumia ule utaratibu wa kawaida wakazifanyia uchunguzi, hawa wavuvi wakapatiwa zana hizo wakaendelea kufanya kazi yao kubwa na nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua kampeni yake Jangwani, alisema anataka nchi ya viwanda, lakini pia anataka Watanzania wasipate shida. Uzuri Mheshimiwa Waziri amepewa dhamana hii ya kusimamia. Naomba sana pamoja na waatalam waliangalie kwa mapana zaidi ili kusudi wakulima na wafugaji waendelee kufanikiwa katika kutimiza azma ya Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nampongeza Katibu Mkuu. Tena bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amepewa Katibu Mkuu mwanamama na mwanaume. Kwa hiyo, una sehemu kabisa nzuri za kulelewa vizuri na akafanya kazi yake vizuri sana na kuhakikisha Watanzania wanapiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa naMheshimiwa Mattar Ali Salum, ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika sekta yangu hii iliyo muhimu sana lakini haijulikani kama ni muhimu. Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu Wataalamu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii ya Waziri kutoka mwanzo ili muda ukiniishia, nisionekane kwamba siungi mkono jitihada za Serikali. Hata hivyo, napenda kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo na samaki inaangaliwa kama ni mali ya mtu mmoja mmoja, lakini kwa ukweli ni rasilimali muhimu ya Taifa. Siyo mali ya mtu mmoja mmoja ila ni rasilimali ya Taifa. Ningependa kusema kwamba, Tanzania ni nchi ya pili kwa wingi wa mifugo. Tanzania ni nchi yenye maziwa mengi na kwa hiyo, ni nchi yenye samaki wengi. Kwa hiyo, tuna bahati kubwa ya kuwa na rasilimali hii ambayo ikisimamiwa na wote na wanaohusika, nchi itanufaika na hii hali ya umaskini ni rahisi kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu tuna ng'ombe milioni 30, tuna mbuzi milioni 18 na kondoo zaidi ya milioni tano. Utaona jinsi nchi ilivyokuwa na rasilimali kubwa kutokana na mifugo hii. Mwaka 2017 tumezalisha nyama tani laki sita na zaidi; tumekamua maziwa lita bilioni 2.4. Sekta hii imekua kwa asilimia 2.8, ingepaswa ikue kwa asilimia zaidi na kuchangia pato la Taifa kwa asilimia 6.9. Uchangiaji huu ni mkubwa kuliko hata Sekta ya Madini. Hata hivyo utaona kwamba macho mengi yanaangalia madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini kwa mwaka 2017 imechangia pato la Taifa kwa asilimia 3.5. Inasikitisha kuona kwamba fedha za maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni

nne lakini pamoja na kutenga fedha hizo senti hata moja haikutolewa kwenye sekta hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna namna ya kuikimbia sekta hii, nani ambaye haitaji protini? Nani ambaye hahitaji maziwa? Mtoto gani anayekua bila ya maziwa? Wafugaji ni wachache lakini mahitaji kutoka kwa wafugaji ni makubwa na ni ya watu wote. Naomba tuone hii. Hatua hii ya kutokutoa fedha ya maendeleo, inaonesha kwamba hatuipi sekta hii umuhimu unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sekta hii Serikali imekusanya shilingi bilioni 16 na zaidi. Utaeleza vipi? Kwa nini fedha ya maendeleo haijatolewa jamani kama siyo wa kutotoa umuhimu kwenye sekta hii? Inaonesha kwamba hatuipi umuhimu stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ina migogoro mingi; wakulima na wafugaji, hifadhi na wafugaji, hata wale wenye maeneo ya madini wana migogoro na wafugaji. Migogoro hii inatatuliwa kwa kusimamia sheria bila kuwa na moyo wa ubinadamu. Nasema hivyo kwa nini? Kwa sababu naamini wale wanaotekeleza, pengine azma ya Serikali ni nzuri, lakini wale wanaotekeleza hawana nia nzuri, wana nia mbaya au ovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia ilivyofilisi watu. Ng'ombe waliochukuliwa kwenye hifadhi, ama wamekufa, ama wameuzwa bila kushirikisha wafugaji. Wamewafilisi wafugaji. Angalia jinsi inavyogombanisha wakulima na wafugaji katika kusimamia sheria hii. Angalia jinsi ambavyo tunapunguza amani kati ya Serikali na watu wake. Kwa hiyo, naomba sana nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba jamani *operation* hizi ziendeshwe; nami siko *against* au sipingi lakini lazima kuwe na moyo wa ubinadamu kuona kwamba ng'ombe ni rasilimali ya Taifa na wale wanaochukuliwa ng'ombe wanaumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, badala ya kufilisi au badala ya watu kufa, tutumie sheria hii ili

tuwasaidie wafugaji. Tuone kwamba fedha hizi zinazotumika kwenye *operation* zinapelekwa kwenye malambo, madawa ya tiba na chanjo. Ionekane kwamba hata wanapopigwa chapa siyo kuharibu ngozi au alama isionekane. Tukichukua hatua zinazostahili, tutakuwa tumewasaidia wafugaji. Ilivyo hapa sasa hivi wafugaji wanaona hawapo kwenye nchi yao, wanaona kwamba wapo porini kama wanyama wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu ambalo nataka niliseme, kwa nini kila Wizara isitenge eneo la wakulima na wafugaji? Hizi fedha za kwenda kwenye *operation* zingetumika kuwa na matumizi bora ya ardhi ili wafugaji wajue kwetu ni hapa na wakulima wajue kwetu ni hapa, lakini katika kufanya shughuli zao watakuwa wanashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tukifanya hivyo na sisi tuko nyuma ya Mheshimiwa Waziri. Nayasema hayo siyo kuonesha *weakness* yake, nataka nimshauri ili tushirikiane tuweze kutunza rasilimali hii iongezeke, iweze kunufaisha watu mmoja mmoja na inufaishe Taifa letu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA.** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, shukurani.

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningekuwa na muda mrefu, ningesema na watu wa Hanang ambao ni watu wafugaji, wameonewa swagaswaga na kwenye mapori mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mattar Ali Salum, dakika zilizobaki atamalizia Mheshimiwa George Lubeleje.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzito walioifanya katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tu kwa haraka haraka huwezi kujua kazi wanayoifanya Waheshimiwa hawa wawili. Leo hii kwa mfano nchi nzima kuwe hakuna nyama nchi nzima, hakuna maziwa, hakuna samaki utaona umuhimu wa Wizara hii. Wizara hii ni nyeti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Wizara hii pia inachangia kwenye Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa kuliko Wizara nyingine nyingi. Kwa masikitiko makubwa, wanapelekewa bajeti ndogo. Ukiona kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri, wamekusanya sana kwenye maduhuli. Sasa yale makusanyo waliyokuwa wanakusanya kwenye maduhuli, mengine yangekuwa yanarudi kwenye bajeti zao ili ziwasaidie kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Wizara hii imetoka kwenye utaratibu wa kufanya *identification* ya ng'ombe walioko hapa nchini kwa kuwapiga chapa. Tuna ng'ombe takriban milioni 29 na kila mchangiaji alikuwa anatoa shilingi 500/=. Kwa hesabu ya haraka haraka tu, wamekusanya karibu shilingi bilioni 14. Tujiulize ni kiasi gani cha pesa kinarudi kwa ajili ya kusaidia kwenye sekta hiyo ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, *collection* inayopatikana katika maeneo yao, tungetengeneza utaratibu wa kuhakikisha fedha zinarudi kwa ajili ya kuwasaida wakulima pamoja na wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo pekee ambalo linatoa ajira kwa urahisi ni eneo la uvuvi. Una-*invest* mara moja lakini una uhakika wa kufanya miaka yote katika eneo hili. Wizara inatakiwa itambue hilo; na kuwa karibu sana na kuwashirikisha sana katika kazi zao sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibi Spika, miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa na Wabunge wengi ni mahusiano kati ya Wizara, pamoja na sekta binafsi. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri alione hili *gap* alipunguze. Kuna watu wanataka wakae, wazungumze pamoja kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni eneo la tasnia ya maziwa. Tuna viwanda vikubwa vitano katika nchi hii. Tuna takwimu ya ng'ombe milioni 29 ambao nimezungumza. Kwa masikitiko sana, asilimia 85 ya maziwa yanayotumika hapa nchini yanatoka nje ya nchi. Sasa tujiulize, huu wingi wa ng'ombe unasaidia nini katika tasnia ya maziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaogopa ku-*invest* katika eneo hii kwa sababu ya tozo mbalimbali zilizopo ambazo hazina tija kwa watu wetu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, zile tozo ambazo hazina tija, tuziondoe kusudi watu waweze kujiunga katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni ku-*protect* viwanda vya ndani. Wewe ni shahidi maofisi yote ya Serikali yanatumia maziwa kutoka nje. Ukienda kwenye ofisi yoyote hapa au majumbani utakuta *Nido* au *Lactogen* kutoka nchi za nje. Kwa nini tusitumie maziwa ya ndani? Kwa utaratibu huu, tunaendelea kuvidhoofisha viwanda vya ndani badala ya kuvisaidia. Kwa hiyo, ifike wakati tuweke *ban* kama tulivyoweka *ban* kwenye *furniture* kwamba sasa ni marufuku kuagiza maziwa nje, tutumie maziwa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mattar Ali Salum.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Niendeleze hapa alipoacha kaka yangu Mheshimiwa Mgimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakuwa na mikakati thabiti ndani ya Wizara hii na kama tutaishauri Serikali vizuri, itasikia tunavyosema Waheshimiwa Wabunge. Jambo la kwanza kwenye tasnia ya maziwa, lazima Wizara zetu yaweze kutumika maziwa ambayo tunazalisha nchini kwetu. Tunaweza tukai-*promote* sekta hii ikawa inafanya kazi vizuri kuliko kitu chochote, lakini sisi wenyewe ndani yetu tunaanza kutumia maziwa ya kuagiza nje. Hivi sekta hii itakua lini? Naomba sana Serikali tubadilishe utumiaji wa maziwa, twende katika utumiaji wa maziwa tunayozalisha ndani sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ukiangalia bajeti ambayo ilikuwa imepangwa kutolewa katika Wizara hii, jambo la kusikitisha sana, bajeti hii haijaenda, haina hata kitu kimoja. Hawa Mawaziri wanachapa kazi vizuri, naamini wana jitihada sana ya kufanya kazi. Nawashukuru sana hawa Mawaziri, lakini kutokana na bajeti ambayo iko hapa, waliyopewa hawa, basi haiwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni uvuvi wa Bahari Kuu ambao nauzungumzia kwa kina. Nchi yetu tukitaka tuendelee, tufike mahali halisi tunapopataka pasipo kuangalia madini, basi tuangalie kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Tukisimamia uvuvi wa Bahari Kuu tunaweza kufika mahali pazuri kuliko kuangalia madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, baada ya macho kuangalia katika madini, basi tuangalie hapa kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Tukifanya kazi, tukipaimarisha vizuri katika uvuvi wa Bahari Kuu, haya matatizo ya uvuvi haramu na matatizo sijui ya maziwa, yote yataondoka. Nami kaka yangu Mheshimiwa Ulega namshauri kila siku, hebu twendeni kwenye uvuvi wa Bahari Kuu, tuangalieni, kuna nini? Sijui tumelogwa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumesema katika Kamati tukilalamika kuhusu ununuaji wa meli na ujengaji wa gati. Ndani ya hotuba zetu hizi hatujaona mahali palipo na mkakati rasmi kwamba sasa tunaenda kuwekeza

kwenye Bahari Kuu. Uchumi wa Bahari Kuu, wenzetu waliokuja kuwekeza ndani ya nchi yetu hii wanapata mafanikio makubwa, sisi tunabakia katika tozo ya leseni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara hii na Serikali iweze kusimamia uvuvi wa Bahari Kuu, kuhakikisha tunakwenda mahali pazuri. Naamini tukisimamia kidhati kwenye Bahari Kuu, basi tutakwenda tunapopataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nigusie suala la ufugaji, bado hatujatoa elimu na bado hatujaamua kusimamia katika suala la ufugaji. Tukiangalia hata mifugo yetu, bado hatuna ng'ombe wanaoridhisha. Angalau ng'ombe unayemkamua maziwa umpe malisho bora. Kikitokea kiangazi kidogo tunashuhudia ng'ombe wanaokufa ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tumekwenda ziara kuangalia ng'ombe, wanapukutika njiani kama majani. Tujipange katika suala la ufugaji.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde thelathini Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Dakika hapana, sekunde 30.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ahsante. Tuwawezeshe wafugaji wetu, tuwape mikopo ya ng'ombe wa kisasa, tuwaelimishe ufugaji wa kisasa ili tupate maziwa mengi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Lubeleje, dakika mbili.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja moja tu. Wilaya ya Mpwapwa ina taasisi mbili za mifugo. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Chuo cha Mifugo. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ndiyo Makao Makuu ya nchi nzima katika utafiti wa mifugo. Taasisi hii ina ng'ombe zaidi ya 800, lakini hawana vitendea kazi. Wana mashamba ya kulima majani kwa ajili ya mifugo, wana trekta moja na limechakaa na wana *Lorry* moja, nalo limechakaa. Sasa ili ng'ombe wapate chakula, watalima yale mashamba kwa majembe ya mkono? Kwa hiyo, naomba ile taasisi ipewe fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Chuo cha Mifugo, mwaka 1995 yale mabweni tulitaka tuyachukue sisi Halmashauri tuyakarabati iwe Shule ya Sekondari lakini Wizar ikayawahi. Sasa yamechakaa tena. Itolewe bajeti ya kutosha mabweni yakarabatiwe na ile Taasisi ya Mifugo ya Mafunzo iongezewe bajeti na ile maabara iongezewe vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi0*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje kwa kutumalizia mchango wetu wa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la wageni tulionao Bungeni jioni hii, nitaanza na wageni walioko jukwaa la Spika.

Wageni wangu watatu ambao ni Waandishi wa Habari kutoka Mkoani Mbeya. Wa kwanza ni Ndugu Boldion Kalulunga ambaye ni Mwandishi wa Gazeti la Mtanzania. Mwingine ni Ndugu Haroub Kabwe ambaye yeye ni Mmiliki wa *Haroub TV Online* na mwingine ni Ndugu Emmanuel Lengwa, yeye ni Mwandishi wa *ITV*. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wawili wa Mheshimiwa *Eng*. Atashasta Nditiye ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano; na hawa ni Viongozi wa Chama cha Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam (UWADA)

ambao ni Mwenyekiti wa UWADA; Ndugu Kismat Dalah na Makamu wake Ndugu Athumani Chingu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa wanaotoka Vikundi vya Wavuvi wa Ziwa Victoria Kisiwani Mafia na Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Sijaona James. Karibuni sana wavuvi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi niliombwa Mwongozo mfupi kabisa na Mheshimiwa Khatib Haji na nilisema nitautoa mchana.

Leo katika Kikao cha Thelathini na Moja cha Mkutano wa Kumi na Moja baada ya kipindi cha Maswali na Majibu niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliyetoa maelezo kuwa wakati Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi akiuliza swali la msingi Na. 263, alitoa maelezo ya uongo na ya kupotosha Bunge kuhusu Meli ya Wachina iliyokamatwa na Serikali wakati Mheshimiwa Rais akiwa Waziri wa Wizara iliyokuwa inashughulikia uvuvi wakati huo.

Waheshimiwa Wabunge, madai ya Mheshimiwa Khatib Said Haji ni kwamba maelezo ya majibu ya muuliza swali ya Mheshimiwa Amina Makilagi kwamba Serikali ililipata tija kutokana na kukamatwa kwa meli hiyo siyo sahihi, ni uongo na ya kupotosha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nilielekeza kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge kuona Mheshimiwa Amina Makilagi alisemaje ili niweze kutoa Mwongozo.

Pia nilitoa maelezo ya awali kuwa kanuni kuhusu madai ya Mbunge kupotosha Bunge tunazifahamu, hivyo niahidi kutoa Mwongozo wangu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu Kutokusema Uongo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka utaratibu kuhusu kutokusema uongo Bungeni. Fasili ya (3) ya kanuni tajwa inalekeza kuwa

Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka kuhusu utaratibu. Baada ya kuruhusiwa na Spika ataeleza kuwa Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Khatib Said Haji hakuzingatia kanuni tajwa bali alitumia kanuni ya 68(7) inayohusu Mwongozo wa Spika na siyo kanuni inayohusu kusema uongo Bungeni. Ili Kiti kiweze kutamka Mbunge kuthibitisha ukweli kuhusu jambo analodai ni la uongo, ilitakiwa Mbunge husika kutumia kanuni ya 63 ili taratibu ziweze kuweka ukweli bayana ili iweze kuzingatiwa.

Hivyo basi, kwa kuwa suala hili halikuzingatia kanuni, Kiti hakitachukua hatua yoyote katika Mwongozo ulioombwa na mchango wa Mheshimiwa Makilagi unabaki kama ulivyo. Huo ndiyo Mwongozo wangu, umetolewa leo tarehe 17 Mei, 2018. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya ijumaa, tarehe 18 Mei, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.00 ioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 18 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*